**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 23 Mei, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo zilizowasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:**

Hotuba ya Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMEIR – (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED – (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirka kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

### HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA MHESHIMIWA STEPHEN MASATO WASIRA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo inayohusu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu linapokea na kujadili na hotuba hii ikiwa ya mwisho chini ya Serikali ya Awamu ya Nne, baada ya miaka kumi ya uongozi wa Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Ingawa miaka kumi si kipindi kirefu sana kwa maendeleo lakini Watanzania walio wengi na wenye nia njema watakubaliana na mimi kuwa miaka kumi ya Awamu ya Nne imekuwa ya mafanikio makubwa na ya kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio makubwa yamepatikana katika nyanja za uchumi, huduma za jamii hususan elimu na afya, bila kusahau miundombinu ya barabara ambayo pia imechangia sana katika ukuzaji wa kilimo. Naungana na Watanzania kumpongeza kwa dhati Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa mafanikio hayo makubwa ya maendeleo yaliyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu binafsi nitoe shukrani zangu za pekee kwa imani ya Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwangu katika kipindi chote cha miaka kumi. Amenishirikisha katika Serikali yake katika Wizara mbalimbali zikiwemo Wizara ya Maji; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika mara tatu; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu). Katika kipindi hicho, amefanya mabadiliko mara nyingi na kila

alipofanya mabadiliko, alinipa fursa ya kuendelea kulitumikia Taifa letu katika nafasi ya Uwaziri. Kwa vile hii ni hotuba yangu ya mwisho kabla ya uchaguzi ujao, natumia nafasi hii kumtakia kila la kheri na maisha marefu baada ya kustaafu kwa heshima kubwa mwishoni mwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza kwa namna ya pekee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa msukumo wa kuendeleza sekta ya kilimo. Msukumo huo umedhihirika katika shughuli zake kwa kutoa maelekezo ya moja kwa moja katika utekelezaji kupitia Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa katika sekta ya kilimo ili kuongeza uwekezaji na kukuza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal ambaye pamoja na majukumu yake makubwa, amekuwa akitenga muda wa kutosha kufuatilia maendeleo ya sekta ya kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kupambana na umaskini. Katika nyakati tofauti amekuwa akisisitiza kilimo hifadhi kinachozingatia utunzaji wa mazingira kwa maendeleo ya kilimo endelevu. Aidha, amekuwa akisisitiza mageuzi ya kilimo kwa kutilia mkazo zaidi upatikanaji na matumizi sahihi ya pembejeo, zana za kilimo za kisasa, elimu kwa wakulima, upatikanaji wa masoko, uongezaji wa thamani kwa mazao ya kilimo na umuhimu wa kuwekeza katika utafiti ili kupata teknolojia bora zinazoendana na mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia nitumie fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa juhudi zake za kuendeleza kilimo kupitia azma ya dhana ya Kilimo Kwanza. Aidha, nampongeza kwa hotuba yake katika Bunge hili ambayo imetoa maelezo na maelekezo kuhusu maendeleo ya sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itakavyokumbukwa, Mheshimiwa Rais alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri na kufanya uteuzi wa Wabunge wawili wapya. Napenda kuwapongeza kwanza Mheshimiwa George Boniface Simbachawene na Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama kwa kuteuliwa na kupandishwa cheo kuwa Waziri wa Nishati na Madini na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) mtawalia, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Mheshimiwa Charles Mwijage kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge Innocent Sebba na Dkt. Grace Khwaya Puja kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili. Nawaahidi ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015, Bunge lako Tukufu lilipata msiba wa kuondokewa na Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi. Wote tutamkumbuka marehemu kwa umahiri wake katika fani yake ya sanaa. Msiba huo ni mkubwa siyo tu kwa familia bali

kwa Bunge lako na Watanzania wote. Natumia nafasi hii kwa mara nyingine, kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa familia ya marehemu na kuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wegine wa Bunge kwa uongozi wenu mzuri, siyo tu katika kikao hiki, bali katika kipindi chote cha uhai wa Bunge hili. Mmekabiliana na changamoto nyingi na kuzishinda, mnastahili pongezi zetu za dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo chini ya uongozi wa Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo, kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ya mwaka 2014/2015 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2015/2016. Napenda kulihakikishia Bunge hili kwamba Wizara yangu imezingatia maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati hiyo kuhusiana na mpango wa kilimo na bajeti iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu, nawashukuru sana wananchi wa Bunda kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Pamoja na shughuli nyingi, nimewatumikia kwa moyo na nguvu zangu zote na mimi sitaki kujisemea nitawaacha wao waseme kwa niaba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie hali ya kilimo na ushirika. Kilimo kinaendelea kuwa sekta muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa kinatoa ajira kwa asilimia 75 ya Watanzania na kinachangia zaidi ya asilimia 100 ya chakula kinachopatikana nchini kwa miaka yenye mvua za kutosha. Katika mwaka 2014, sekta ya kilimo ilichangia asilimia 28.9 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 31.2 mwaka 2013. Sekta ndogo ya mazao ilichangia asilimia 16.2; mifugo asilimia 7.4; misitu asilimia 3.1 na uvuvi asilimia 2.2. Kwa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea shughuli za kilimo katika maeneo yao, kilimo ndio sekta inayochangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato la Taifa kwa mwaka 2014/2015 kwa shughuli za msingi za kiuchumi zinazojumuisha kilimo cha mazao, mifugo, misitu na uvuvi limekua kwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na asilimia 3.2 ya mwaka 2013. Katika ukuaji huo, mchango wa mazao ulikuwa asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 3.5 ya mwaka 2013. Uzalishaji wa mazao ya nafaka uliongezeka kutoka tani milioni 7.8 mwaka 2013 hadi tani milioni 9.8 mwaka 2014 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 26. Aidha, uzalishaji wa mahindi uliongezeka kutoka tani milioni 5.3 mwaka 2013 hadi tani milioni 6.7 mwaka 2014 sawa na ongezeko la

asilimia 27. Uzalishaji wa mchele uliongezeka kutoka tani milioni 1.3 mwaka 2013 hadi tani milioni 1.7 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo nafaka ulikuwa tani milioni 6.2 ikilinganishwa na tani milioni 6.8 kwa mwaka 2013. Uzalishaji wa mazao ya chakula ya nafaka na yasiyo ya nafaka katika mwaka 2014 ni jumla ya tani milioni 16 milioni, uzalishaji huo wa mazao ya chakula ukilinganishwa na mahitaji ya tani 12.8 ya chakula na matumizi mengineyo katika mwaka 2014/2015, unaonesha kuwepo kwa ziada ya tani milioni 3.2 za chakula. Ongezeko hilo limetokana na kuwepo kwa mvua za kutosha na juhudi za Serikali za kuboresha uzalishaji kwa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima, limeleta utoshelevu wa chakula nchini kwa kiwango cha asilimia 125. Kilimo cha umwagiliaji kimechangia asilimia 24 katika utoshelevu huo. Aidha, utoshelevu huo ulichangia kushuka kwa bei ya vyakula na hivyo kuchangia katika kupunguza mfumuko wa bei za bidhaa kutoka asilimia 6.1 Machi, 2014 hadi 4.5 Aprili, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya chakula na uzalishaji wa mazao ya chakula. Hali ya chakula mwaka 2014/2015, imeendelea kuwa nzuri kutokana na mavuno ya kutosha na ziada yaliyopatikana msimu wa kilimo wa 2013/2014. Tathmini ya uzalishaji iliyofanyika mwezi Agosti, 2014 nchini ilibaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2013/2014 ulikuwa tani 16,015,238 za mazao ya chakula zikiwemo tani 9,829,540 za nafaka na tani 6,186,698 za mazao yasiyo ya nafaka. Kiasi hicho cha chakula kikilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani 12,765,879 katika mwaka 2014/201, kilionesha kuwepo kwa ziada ya tani 3,247,359 za chakula. Kutokana na hali hiyo, Taifa lilijitosheleza kwa chakula kwa asilimia 125 ambapo mikoa 23 kati ya 25 ya Tanzania Bara ilibainika kuwa na viwango vya ama ya ziada ama utoshelevu. Tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe iliyofanyika mwezi Januari 2015, ilibaini kuwepo kwa jumla ya watu 424,136 waliokuwa na upungufu wa chakula na walihitaji tani 9,917 za chakula cha msaada na hatua ya kukabiliana na upungufu huo zinaendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa kilimo wa 2014/2015, maeneo yanayopata mvua za vuli miezi ya Oktoba hadi Desemba yalipata mvua juu ya wastani, wastani na chini ya wastani. Maeneo machache katika Mikoa ya Arusha na Morogoro yalipata mvua za juu ya wastani. Mikoa ya Kagera, Mara, Shinyanga, Mwanza, Manyara, Kilimanjaro na Tanga yalipata mvua za wastani zenye mtawanyiko mbaya. Aidha, maeneo ya Dar es Salaam, Pwani, Same na Moshi yalipata mvua chini ya wastani. Kwa ujumla mvua hizo za vuli zilichelewa kuanza na kuisha mapema na hivyo kuathiri ukuaji wa mazao. Hali hiyo inaashiria kupungua kwa mchango wa vuli katika uzalishaji wa chakula msimu wa 2014/2015 na upatikanaji wa chakula katika mwaka 2015/2016. Kawaida, mvua za vuli huchangia takriban asilimia 27 ya chakula chote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua za msimu zilinyesha kwa mtawanyiko mzuri katika Mikoa 15 na hazikunyesha kwa mtawanyiko mzuri katika Mikoa 10. Vilevile kulingana na utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa, mvua za msimu na za masika zilitarajiwa kuisha katika wiki ya mwisho ya mwezi Machi na wiki ya kwanza ya mwezi Mei ambayo ni mapema kuliko kawaida. Baadhi ya Mikoa ya Kanda ya Kati ya Dodoma na Singida imekwishaathirika kwa kukatika mapema kwa mvua na hivyo kuathiri mazao kwa kiasi kikubwa. Tathmini ya awali ya hali ya mazao ya chakula msimu wa 2014/2015, imeonesha kuwepo upungufu wa chakula katika Mikoa ya Singida, Simiyu, Dodoma, Geita, Mara, Lindi, Tabora, Mwanza, Manyara na Shinyanga. Utabiri wa kina wa hali ya chakula nchini kwa mwaka 2015/2016 utafanyika mwishoni mwa mwezi Mei hadi mwezi Juni, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) ulianza msimu wa ununuzi tarehe 1 Julai, 2014 ukiwa na akiba ya tani 189,493,694 za nafaka. Ununuzi wa nafaka uliofanywa na *NFRA* katika msimu wa 2014/2015 ulikuwa tani 305,424,118 na akiba ya nafaka katika maghala ya *NFRA* hadi tarehe 14 Mei 2015 ni jumla ya tani 422,285,705. Aidha, hadi kufikia mwezi Desemba 2014, Serikali ilikuwa inadaiwa na wakulima kiasi cha shilingi bilioni 89.157. Kati ya mwezi Januari na Mei 2015, Serikali kupitia *NFRA* imelipa wakulima jumla ya shilingi bilioni 77 na bado inadaiwa Shilingi bilioni 12 ambazo Serikali inaahidi kuzilipa wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya umwagiliaji. Eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji hapa nchini limefikia hekta 461,326 ambapo tija kwa zao la mpunga imeongezeka kutoka tani 1.8 hadi mbili (2) kwa hekta mwaka 2006/2007 hadi kufikia tani nne (4) hadi tano (5) kwa hekta mwaka 2014/2015. Uzalishaji wa mazao ya chakula kupitia kilimo cha umwagiliaji ulikuwa tani 3,141,237.34 sawa na asilimia 24.6 ya mahitaji ya chakula kufikia Desemba 2014. Kiwango hicho kinakaribia lengo la Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya asilimia 25 ya mahitaji ya chakula kutokana na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ushirika. Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Mageuzi ya Modenaizesheni ya Ushirika kwa madhumuni ya kuimarisha ushirika nchini. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kisekta, Mamlaka za Tawala na Serikali za Mitaa imeendelea kuhimiza na kukuza maedeleo halisi na endelevu ya vyama vya ushirika kwa kuongeza mwamko wa umma, vijana na makundi mengine katika jamii kujiunga na kuazisha vyama vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilihakiki vyama vya ushirika kwa lengo la kubaini uwepo na uhai wa vyama. Zoezi hilo limebaini kuwa hadi Machi 2015, idadi ya vyama hai vya ushirika ni 7,888 ikilinganishwa na vyama 9,604 Machi 2014. Kati ya vyama 7,888, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)*

ni 3,865, vyama vya ushirika vya aina nyingine (kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, madini, nyumba) ni 3,973, benki za ushirika mbili na vyama vikuu 48. Aidha, wanachama wa vyama vya ushirika ni 2,390,593 kati yao wanachama 919,992 ni wa *SACCOS* ambao wanamiliki hisa, akiba na amana zenye thamani ya shilingi bilioni 534 ukilinganisha na shilingi bilioni 451 mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika wa Mazao vimeendelea kuwapatia wakulima masoko ya mazao. Katika msimu wa 2014/2015, vyama hivi viliweza kukusanya na kuuza mazao yenye thamani ya shilingi bilioni 44 ukilinganisha na shilingi bilioni 37.1 kwa mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 20.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato na matumizi ya fedha katika kipindi cha 2014/2015. Makusanyo ya maduhuli. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2014/2015, ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi 3,229,010,000 kupitia Fungu 43, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 30 April, 2015, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 2,730,909,095.09 sawa na asilimia 84.6 ya makadirio. Wizara inaendelea kukusanya maduhuli hayo kwa lengo la kufikia asilimia 100 iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizoidhinishwa. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 5 ilitengewa jumla ya shilingi 383,187,544,389. Kati ya fedha hizo, shilingi 295,264,754,389 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 87,922,790,000 ni fedha za maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, shilingi 46,945,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 40,977,790,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 22 Aprili, 2015, shilingi 40,982,880,943 za maendeleo sawa na asilimia 46.26 ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewawa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali za maendeleo.

Aidha, shilingi 205,008,914,502 sawa na asilimia 69.4 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa zimetolewa. Fedha za matumizi ya kawaida zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa nafaka ya hifadhi ya chakula ya Taifa, madeni ya ruzuku ya pembejeo na mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi zake, madeni ya huduma mbalimbali ya miaka ya nyuma, ruzuku ya mashirika ya ndani, Mfuko wa Pembejeo, chakula cha wanafunzi katika vyuo vya kilimo, udhibiti wa visumbufu vya mimea na uendeshaji wa Wizara na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na kutumika umeonyeshwa katika aya ya 28 hadi 32 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo kwa mwaka 2014/2015. Katika kufikia lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo, Wizara ilisimamia upatikanaji wa pembejeo za kilimo; uzalishaji wa mbegu na miche;

utoaji ruzuku ya pembejeo za kilimo; udhibiti wa ubora wa mbolea, mbegu na madawa; utafiti wa huduma za ugani; ukaguzi wa viuatilifu vya mazao na mbegu; kuainisha mashamba makubwa kwa ajili ya uwekezaji na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na mafunzo kwa wakulima kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na miradi mingine ya kisekta. Aidha, upatikanaji wa masoko, uongezaji wa thamani ya mazao na ajira kwa vijana ni baadhi ya vipaumbele vinavyotiliwa mkazo. Utekelezaji wa vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa pembejezo za kilimo. Makadirio ya mahitaji ya mbolea kwa mwaka 2014/2015 yalikuwa tani 485,000 na kufikia Aprili 2015, jumla ya tani 342,798 za mbolea zilipatikana na kusambazwa Mikoani sawa na asilimia 70.7 ya mahitaji. Aidha, upatikanaji wa mbegu bora ulifikia tani 36,410.46 sawa na asilimia 60.7 ya mahitaji halisi ya mbegu bora ya tani 60,000. Kati ya mbegu hizo, tani 21,407.29 zimezalishwa nchini na tani 15,003.167 zimeagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku ya pembejeo. Mpango wa ruzuku kwa mwaka 2014/2015, ulilenga kutoa ruzuku ya riba ya mikopo ya pembejeo za kilimo kwa vikundi vya wakulima na vyama vya ushirika kupitia taasisi za fedha. Vikundi 4,990 vilivyosajiliwa kisheria vyenye kaya 974,000 vilitambuliwa. Hadi mwezi Machi, 2015 vikundi vilivyokidhi masharti ya kukopesheka ni 712 kupitia benki za *NMB, CRDB* na Benki za Wananchi. Benki ya *NMB* imetoa mikopo kwa vikundi vya wakulima 281 vyenye wanachama 28,700 na Benki ya *CRDB* ilitoa mikopo kwa vikundi 247 vyenye wanachama 24,700. Benki za Wanachi zimetoa mikopo kwa vikundi vya wakulima 188 vyenye jumla ya wanachama 3,315. Changamoto iliyojitokeza katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa mwaka 214/2015 ni kukosekana kwa mtandao wa benki katika nchi nzima na wakulima wengi kutokuwa katika vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto zilizojitokeza katika msimu uliopita kwa wakulima wengi kukosa pembejeo ya ruzuku, Serikali katika mwaka 2015/2016 itarejesha utaratibu wa matumizi ya vocha kwa mazao ya mahindi na mpunga. Serikali itachangia asilimia 50 ya gharama za pembejeo kwa lengo la kutoa ruzuku ya tani 99,923 za mbolea na tani 10,270.86 za mbegu bora za mahindi na mpunga zitakazonufaisha kaya 999,926 au 1,000,000. Hata hivyo, kiasi hicho cha pembejeo zenye ruzuku ni kidogo kulinganishwa na mahitaji ya wakulima kutokana na ufinyu wa bajeti inayotolewa na Serikali. Maelezo ya kina yanaonekana aya ya 37 hadi 42 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa ubora wa pembejeo. Wizara ilidhibiti ubora wa mbolea, mbegu na viuatilifu kwa kukagua mshamba, mipaka, maghala, maduka na viwanda. Hadi mwezi Aprili, 2015 tani 342,798 za mbolea zilikaguliwa wakati wa kuingizwa nchini. Aidha, Wizara pia ilikagua hekta 12,425

za mashamba yaliyozalishwa mbegu katika madaraja mbalimbali ambapo hekta 12,418.4, sawa asilimia 99.9 zilikidhi viwango vya ubora wa mashamba ya kuzalisha mbegu. Wizara kupitia Sheria ya Taasisi ya Udhibiti ilichukua hatua ya kusitisha leseni kwa wafanyabiashara wa mbolea na viuatilifu waliobainika kuingiza na kuuza mbolea zisizokidhi viwango vya ubora na kuamuliwa kuziondoa sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Pembejeo, itafanya majaribio ya aina mpya za mbegu 100, itakagua hekta 14,000 za mashamba ya kuzalisha mbegu, kuthibitisha ubora wa mbegu, kukagua mbegu zitakazoingizwa kutoka nje, kukagua na kusajili viuatilifu na kudhibiti ubora wa mbolea. Maelezo ya kina kuhusu udhibiti na ubora wa pembejeo yanapatikana katika aya ya 43 hadi 49 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara. Katika mwaka 2014/2015, uzalishaji wa mazao makuu ya asili ya biashara ulikuwa tani 937,060.2 ikilinganishwa na tani 897,028 mwaka 2013/2014 sawa na ongezeko la asilimia 4.46. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za Serikali na wakulima zilizolenga kuongeza uzalishaji, kupunguza kero za wazalishaji na kuzijengea uwezo taasisi zinazosimamia uendelezaji wa mazao. Pamoja na ongezeko hilo, kumekuwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kwenye Bodi za Mazao ambao umeathiri usimamizi na hivyo kutofikia malengo ya ukuaji wa tasnia husika. Katika mwaka 2015/2016, matarajio ya uzalishaji wa mazao makuu ya asili ya biashara ni tani 1, 034,016. Ili kufikia lengo hilo, Bodi za mazao zitaendelea kusimamia na kuhamasisha wadau wa mazao hayo kuongeza tija, uzalishaji na ubora wa mazao na kuongeza matumizi ya pembejeo na miche bora, kuhamasisha uanzishaji wa viwanda na usindikaji, kuboresha ujendaji wa mifuko ya wakfu na kuendeleza mazao husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sukari. Mahitaji ya sukari nchini ni wastani wa tani 420,000 kwa matumizi ya nyumbani na tani 170,000 kwa matumizi ya viwandani kwa mwaka. Uzalishaji wa sukari msimu 2014/2015, ulifikia tani 304,007 ukilinganisha na tani 294,300 msimu wa 2013/2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.3. Uzalishaji kwa kila kiwanda umeonyeshwa kwenye kiambatisho na. 1 ukurasa wa 97 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu wa sukari uliopo nchini, Serikali imeidhinisha uagizaji wa tani 100,000 za sukari ya matumizi ya nyumbani ili kuziba pengo la mahitaji kwa msimu wa 2014/2015. Kati ya kiasi hicho tani 88,940.25 zitaagizwa kutoka nje na tani 11,000 ambazo ni *transit sugar* zitatumika nchini kuziba pengo la sukari baada ya kutozwa ushuru stahiki. Aidha, tani 182,765 za sukari ya matumizi ya viwandani ziliidhinishwa kuingizwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Sukari imetoa leseni kwa makampuni 25 kuingiza sukari nchini, kati ya mwezi Machi na Mei ambapo sukari hiyo inalipiwa Kodi ya Ongezeko la Thamani ya asilimia 18 na ushuru wa forodha kwa asilimia 50. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2015 tani 23,000 za sukari ya matumizi ya nyumbani zimeingizwa na tani 51,799 zimeagizwa. Aidha, tani 97,000 za sukari ya matumizi ya viwandani zimeingizwa nchini sawa na asilimia 53 ya kiasi kilichoidhinishwa. Maelezo ya kina ya kila zao yameonyeshwa katika aya ya 50 hadi 73 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao ya bustani na mbegu. Uzalishaji wa mazao ya bustani umeongeza kutoka tani milioni 5.4 mwaka 2013/2014 hadi tani milioni 5.64 mwaka 2014/2015. Ongezeko hilo lilitokana na uzalishaji wa mazao ya bustani katika skimu za umwagiliaji. Aidha, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta umeongezeka kutoka tani milioni 5.5 mwaka 2013/2014 hadi 5.9 mwaka 2014 kutokana na kuimarika kwa ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ndogo ya mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na *TAHA* itaendelea kusimamia uendeshwaji wa majengo ya kuhifadhia mazao ya bustani; kuunganisha wakulima na taasisi za fedha ili kupata mikopo yenye gharama nafuu; kuunganisha na masoko wakulima 1,015 na kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mazao ya bustani. Aidha, *TAHA* itatoa mafunzo kwa wazalishaji 10,000 wa mazao ya bustani na Maafisa Ugani 65 pamoja na kusambaza taarifa za masoko na dondoo muhimu za mazao ya bustani 3,500. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora za mazao ya mafuta na kuhamasisha usindikaji. Maelezo ya kina ya mazao ya bustani na mbegu za mafuta yanapatikana aya ya 75 hadi 79 katika kitabu cha hutuba kilichogawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji. Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kutekeleza miradi ya umwagiliaji kupitia mfumo wa *BRN* ambapo skimu 19 zenye hekta 9531 zimekarabatiwa na kunufaisha wakulima 69,981. Vilevile, Wizara iliendelea na ujenzi wa skimu ya Itete yenye hekta 1000 na wanufaika 5000 ambapo hadi kufikia Machi, 2015, ujenzi wa skimu hiyo ulikuwa umefikia asilimia 75. Kupitia mfuko wa kuendeleza umwagiliaji ngazi ya Wilaya, *DIDF*, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, iliendelea na usimamizi wa ujenzi wa skimu za umwagiliaji 45 zenye hekta 11,140 na wanufaika 55,700 ambapo hadi Machi, 2015 ujenzi ulifikia asilimia 46. Aidha, ukarabati wa skimu 15 za umwagiliaji zenye eneo la hekta 4,186 unaogharamiwa kupitia Mfuko wa Pamoja wa Serikali ya Tanzania na Japan umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kuendeleza kuboresha skimu 78 katika mfumo

wa *BRN* kwa kufanya mapito ya usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni na kujenga skimu 58. Kukarabati na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 20. Wizara pia itaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu kwenye skimu 20 yaani 10 za za *DASIP* na 10 za kimkakati na mabwawa madogo ya Lwango (Mbarali), Dongobesh (Mbulu) na Inala (Tabora).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara kwa kushirikiana na *USAID*, kupitia Mradi wa *Feed the Future* itaendelea kukakarabati skimu ya umwagiliaji ya Dakawa yenye hekta 2,000 na kujenga hekta nyingine 500. Vilevile kupitia mradi wa *PHRD,* skimu 20 za umwagiliaji zenye hekta 15,431 zitaendelezwa kwa kuzingatia mnyororo wa thamani ya mazao ya mpunga. Maelezo ya kina yanapatikana katika aya ya 86 hadi 95 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zana za kilimo na Mfuko wa Taifa wa Pembejeo. Wizara imehamasisha sekta binafsi kuingiza nchini zana bora za kilimo. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Disemba, 2014, matrekta makubwa 1,212 na matrekta mkono 393 yameingizwa nchini. Aidha, Wizara imenunua na kusambaza *combine harvesters* za kuvuna mpunga 64, mashine za kupura mpunga 36 na mashine za kukata mpunga 16 katika skimu 14 za umwagiliaji kwenye Halmashauri za Wilaya 12. Wizara kupita Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo, ilitoa mikopo ya matrekta mapya 94 na pembejeo mbalimbali za kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuongeza upatikanaji wa matrekta na matumizi zana bora za kilimo nchini na kununua na kusimika mashine za kusindika mpunga katika skimu 14 za umwagiliaji. Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo itaendelea kutoa mikopo mipya ya zana za pembejeo za kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya mazungumzo na Serikalii ya Poland kwa ajili ya kupata mkopo wa kuanzisha kiwanda cha kuunganisha matrekta na zana za kilimo nchini. Hatua iliyofikiwa ni utayarishaji wa makubaliano ya awali uliofanywa na SUMAJKT kwa niaba ya Serikali na *Pol-Mot Holdings S.A.* inayomiliki kampuni ya Ursus kwa niaba ya Serikali ya Poland. Serikali itaendelea kufuatilia upatikanaji wa mkopo huo. Aya ya 96 hadi 103 katika kitabu cha hotuba inatoa maelezo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa visumbufu vya mazao. Wizara imeendelea kudhibiti visumbufu vya milipuko katika maeneo yaliyovamiwa na nzige, panya na kwelea kwelea na visumbufu vipya. Aidha, elimu imetolewa kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu na udhibiti husishi kwa kutumia teknolojia zilizopo katika taasisi za utafiti, taasisi zisizokuwa za kiserikali na miradi mbalimbali. Vilevile Wizara imeendelea kukagua mazao yanayoingia nchini na yanayotoka nje ya nchi na kutoa elimu kwa wakaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara itatathmini vituo 40 vya ukaguzi mipakani ili kudhibiti mazao yanayosafirishwa na yanayoingia nchini. Pia itadhibiti milipuko ya nzige, kwelea kwelea, panya, viwavijeshi na magonjwa ya mimea. Wizara itaandaa na kueneza teknolojia ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ugani. Wizara imeimarisha utoaji huduma za ugani na kuboresha uenezaji wa teknolojia za kilimo kwa kutumia mbinu shirikishi jamii katika kilimo, ikiwa ni pamoja na matumizi ya Shamba Darasa ambapo wakulima hujifunza kwa vitendo kanuni za kilimo bora. Wizara pia ilitoa mafunzo ya kilimo bora kwa mazao ya mpunga, muhogo na ngano kwa wakulima wawezasha 2,075 na Maafisa Ugani 568 ili waweze kufundisha wakulima wengine katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI itaendelea kusambaza teknolojia za matokeo ya utafiti wa kilimo kwa wakulima kwa kutumia Mashamba Darasa 20,000 yenye wakulima laki tano na Maonesho ya Nane Nane, Siku ya Ushirika na Siku ya Chakula Duniani, zahanati za kilimo, redio, sinema, runinga na vituo vya rasilimali ya kilimo vya Kata. Wizara itajenga uwezo wa vyuo vya wakulima vya Inyala, Ichenga, Bihawana na Mkindo kwa kuvipatia vitendea kazi bora ambavyo vitatoa mafunzo kwa Maafisa Ugani wa wakulima na wakulima wawezeshaji.s

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwa 2014/2015, Wizara imeendelea kuratibu maombi ya kibali cha ajira za Maafisa Ugani na wataalam wa kilimo na umwagiliaji, ikiwa utekelezaji wa mkakati wa Serikali wa kuwa na Afisa wa Ugani mmoja katika kila kijiji ifikapo mwaka 2015. Hadi Mei 2015, idadi ya Maafisa Ugani katika kata na vijiji ni 10,089 ikilinganishwa na mahitaji ya Maafisa Ugani 15,853. Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI itaendelea kuratibu ajira ya watumishi 5,000 wa fani mbalimbali kulingana na upatikanaji wa kibali cha ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti. Katika mwaka 2014/2015, Wizara iliidhinisha aina mpya 48 za mbegu za mazao zikiwemo mahindi (4), ngano (3), mbaazi (4), kunde (2), muhogo (4), ufuta (1), korosho (24), miwa (5) na pamba (1). Aina hizi za mbegu zimegunduliwa kutoka vituo vya utafiti vya Wizara vya Uyole, Ilonga, Kibaha na Naliendele. Vilevile Wizara iliidhinisha aina mpya 17 za mbegu zilizogunduliwa na sekta binafsi zikiwemo za mtamba (2), mahindi (21) na tumbaku (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 201/2016, Wizara itandelea na utafiti wa kugundua aina tano mpya za mbegu, njia ya kudhibiti magonjwa ya

wadudu waharibifu wa mazao na kuzisambaza kwa wadau. Aidha, Wizara itazalisha tani 10 za mbegu mama kwa mazao ya nafaka, mikunde, mboga na mbegu za mafuta na pingili milioni mbili za mazao jamii ya mizizi. Wizara pia itatathmini na kusambaza miche ya mbegu za mazao ya mboga na matunda yenye thamani kubwa ikiwemo nyanya, maembe, kakao na matofaa na maparachichi katika kanda ya ikolojia inayofaa kwa kilimo cha mazao hayo. Vilevile, Wizara itaendelea kurekebisha mapendekezo ya matumizi bora ya mbolea kwa mazao ya mpunga na mahindi na kurekebisha ramani za udogo kwa matumizi ya wakulima na wawekezaji. Maelezo ya kina kuhusu huduma za utafiti wa mazao yanapatikana aya ya 104 hadi 139 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba ya kilimo cha biashara na mazao ya mpunga na miwa. Katika kutekeleza mfumo wa *BRN*, jumla ya mashamba makubwa 25 yakiwemo 16 ya zao la miwa na tisa ya mazao ya mpunga yenye jumla ya hekta 350,000 yalibainishwa. Hadi kufikia mwezi Aprili, mashamba makubwa ya Mkurazi, Kitengule, Bagamoyo na Lukulo yenye jumla ya hekta 114,000 yamehakikiwa na kupewa hati. Aidha mashamba ya Bagamoyo, Lukulo na Kitengule yamepata wawekezaji. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imehakiki hekta 43,000 za mashamba ya wakulima wadogo na kuandaa hati miliki za kimila 1,513 kwa wakulima wanaozunguka mashamba ya Lukulo na Ngalamila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015/2016, Wizara itahamasisha uwekezaji katika kilimo cha biashara katika mashamba manne ya Mvuha na Kisaki (Morogoro Vijijini), Tawi, Muhoro, Mkongo (Rufiji), Muhurunga (Mtwara Vijijini) Kasulu (Kasulu) na Kumsenga (Kibondo). Wizara pia itakamilisha mapendekezo ya sheria ya mwongozo wa kulinda rasilimali za kilimo kwa kupima na kuchora ramani za mashamba 12 ya wawekezaji.

Aidha, Wizara kupitia RUBADA itaainisha na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kutenga hekta 10,000 katika kongani ya Rudewa na Rufiji na kuandaa hati za hakimiliki kwa wakulima wadogo. Aidha, Wizara itaendelea kupima na kuweka mipaka katika maeneo yanayomilikiwa na Wizara vikiwemo vituo vya utafiti, vyuo vya mafunzo, mashamba ya mbegu na bustani za Serikali, kuongeza upatikanaji wa masoko…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umebakiwa na dakika mbili tu, omba fedha, nenda ukurasa wa 94.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika yote ambayo yanatusaidia. Aidha, nampa pongezi sana Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki na kumtakia kila la kheri na kumpongeza Katibu Mkuu Bi. Sophia Kaduma na wasaidizi wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha. Katika mwaka 2015/2016, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05, inaomba jumla ya Sh.353,150,873,000 kama ifuatavyo:-

Fungu 43, jumla ya Sh.290,744,623,000 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Sh.249,751,550,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.40,993,073,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 24, kiasi cha Sh.7,627,990,000 kinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 05, jumla ya Sh.54,778,260,000 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Sh.383,686,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.54,394,574,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA MHESHIMIWA STEPHEN MASATO WASIRA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Maji na Mifugo inayohusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka 2015/2016.

**2.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Bunge lako Tukufu linapokea na kujadili hoja hii ikiwa ya mwisho chini ya Serikali ya awamu ya nne, baada ya miaka kumi ya uongozi wa Rais Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete ingawa miaka kumi si kipindi kirefu sana kwa maendeleo. Watanzania walio wengi na wenye nia njema, watakubaliana na mimi kuwa miaka kumi ya awamu ya nne imekuwa ya mafanikio makubwa na ya kujivunia. Mafanikio makubwa yamepatikana katika nyanja za uchumi, huduma za jamii hususan elimu na afya, bila kusahau miundombinu ya barabara ambayo pia imechangia kukuza uchumi wa kilimo.

Naungana na Watanzania kumpongeza kwa dhati Rais Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwa mafanikio hayo makubwa ya maendeleo yaliyopatikana.

**3.** ***Mheshimiwa Spika***, niruhusu binafsi nitoe shukrani zangu za pekee kwa imani ya Rais Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwangu katika kipindi chote cha miaka kumi, amenishirikisha katika Serikali yake katika Wizara mbalimbali zikiwemo Wizara ya Maji; Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika mara tatu; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu. Katika kipindi hicho, amefanya mabadiliko mara nyingi na kila alipofanya mabadiliko, alinipa fursa ya kuendelea kulitumikia Taifa letu katika nafasi ya uwaziri. Kwa vile hii ni hotuba yangu ya mwisho kabla ya uchaguzi ujao, natumia nafasi hii kumtakia kila la kheri na maisha marefu, baada ya kustaafu kwa heshima kubwa mwishoni mwa mwaka huu.

**4.** Aidha, nampongeza kwa namna ya pekee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa msukumo wa kuendeleza Sekta ya Kilimo. Msukumo huo umedhihirika katika shughuli zake kwa kutoa maelekezo ya moja kwa moja katika utekelezaji kupitia Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) katika Sekta ya Kilimo, ili kuongeza uwekezaji na kukuza kilimo.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal ambaye pamoja na majukumu yake makubwa, amekuwa akitenga muda wa kutosha kufuatilia Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kupambana na umaskini. Katika nyakati tofauti amekuwa akisisitiza kilimo hifadhi kinachozingatia utunzaji wa mazingira, kwa maendeleo ya kilimo endelevu. Aidha, amekuwa akisisitiza mageuzi ya kilimo kwa kutilia mkazo zaidi upatikanaji na matumizi sahihi ya pembejeo, zana za kilimo za kisasa, elimu kwa wakulima, upatikanaji wa masoko, uongezaji wa thamani kwa mazao ya kilimo na umuhimu wa kuwekeza katika utafiti ili kupata teknolojia bora zinazoendana na mazingira ya nchi yetu.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** niruhusu pia nitumie fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) kwa juhudi zake za kuendeleza kilimo kupitia azma ya dhana ya Kilimo Kwanza. Aidha, nampongeza kwa hotuba yake katika Bunge hili ambayo imetoa maelezo na maelekezo kuhusu maendeleo ya Sekta ya Kilimo.

**7.** ***Mheshimiwa Spika***, kama itakavyokumbukwa, Mhe. Rais alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri na kufanya uteuzi wa Wabunge wawili wapya. Napenda kuwapongeza Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb) na Mhe. Jenista Joachim Mhagama (Mb) kwa kuteuliwa na kupandishwa cheo kuwa Waziri wa Nishati na Madini, na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Uratibu na Bunge mtawalia, Mhe. Anne Kilango Malecela (Mb) kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Mhe. Charles Mwijage (Mb)

kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge Innocent Sebba (Mb) na Dkt. Grace Khwaya Puja (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili. Nawaahidi ushirikiano.

**8.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2015 Bunge lako Tukufu lilipata msiba wa kuondokewa na Mhe. Kapteni John Damiano Komba (Mb) aliyekuwa mbunge wa Mbinga Magharibi, wote tutamkumbuka marehemu kwa umahiri wake katika fani yake ya sanaa. Msiba huo ni mkubwa siyo tu kwa familia bali kwa Bunge lako na Watanzania wote. Natumia nafasi hii kwa mara nyingine, kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa familia ya marehemu. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu wako na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu mzuri, siyo tu katika kikao hiki, bali katika kipindi chote cha uhai wa Bunge hili. Mmekabiliana na changamoto nyingi na kuzishinda, mnastahili pongezi zetu za dhati.

**10.*Mheshimiwa Spika*,** sina budi kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Maji na Mifugo chini ya uongozi wa Mhe. Prof. Peter Mahammud Msolla Mbunge wa Kilolo, kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ya mwaka 2014/2015 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2015/2016. Napenda kulihakikishia Bunge hili kwamba Wizara yangu imezingatia maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati hiyo kuhusiana na mpango wa kilimo na bajeti iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu.

**11.*Mheshimiwa Spika*,** mwisho siyo kwa umuhimu, nawashukuru sana wananchi wa Bunda kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa pamoja na shughuli nyingi, nimewatumikia kwa moyo na nguvu zangu zote. Sitaki kuwasemea kwa hili.

## 2.0 HALI YA KILIMO NA USHIRIKA

### 2.1 Hali ya Kilimo

**12.*Mheshimiwa Spika***, kilimo kinaendelea kuwa Sekta muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa kinatoa ajira kwa asilimia 75 ya Watanzania na kinachangia zaidi ya asilimia 100 ya chakula kinachopatikana nchini kwa miaka yenye mvua za kutosha. Katika mwaka 2014 Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 28.9 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 31.2 mwaka 2013. Sekta ndogo ya mazao ilichangia asilimia 16.2; mifugo asilimia 7.4; misitu asilimia 3.1; na uvuvi asilimia 2.2. Kwa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea shughuli za kilimo katika maeneo yao, kilimo ndio Sekta inayochangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza umaskini.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** pato la Taifa kwa mwaka 2014/2015 kwa shughuli za msingi za kiuchumi zinazojumuisha kilimo cha mazao, mifugo, misitu na uvuvi limekua kwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na asilimia 3.2 ya mwaka 2013. Katika ukuaji huo, mchango wa mazao ulikuwa asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 3.5 ya mwaka 2013. Uzalishaji wa mazao ya nafaka uliongezeka kutoka tani milioni 7.8 mwaka 2013 hadi tani milioni 9.8 mwaka 2014 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 26. Aidha, uzalishaji wa mahindi uliongezeka kutoka tani milioni 5.3 mwaka 2013 hadi tani milioni 6.7 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 27. Uzalishaji wa mchele uliongezeka kutoka tani milioni 1.3 mwaka 2013 hadi tani milioni 1.7 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 25.

**14.** Vilevile, uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo nafaka ulikuwa tani milioni 6.2 ikilinganishwa na tani milioni 6.8 kwa mwaka 2013. Uzalishaji wa mazao ya chakula ya nafaka na yasiyo ya nafaka katika mwaka 2014 ni tani milioni 16.0. Uzalishaji huo wa mazao ya chakula ukilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 12.8 ya chakula na matumizi mengineyo katika mwaka 2014/2015 unaonesha kuwepo kwa ziada ya tani milioni 3.2 za chakula. Ongezeko hilo ambalo limetokana na kuwepo kwa mvua za kutosha na juhudi za Serikali za kuboresha uzalishaji kwa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima, limeleta utoshelevu wa chakula nchini kwa kiwango cha asilimia 125. Kilimo cha umwagiliaji kimechangia asilimia 24 katika utoshelevu huo. Aidha, utoshelevu huo ulichangia kushuka kwa bei za vyakula na hivyo kuchangia katika kupunguza mfumuko wa bei za bidhaa kutoka asilimia 6.1 Machi, 2014 hadi 4.5 Aprili, 2015.

### 2.1.1 Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Asili ya Biashara

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 uzalishaji wa mazao makuu ya asili ya biashara ulikuwa tani 937,060.2 ikilinganishwa na tani 897,028 zilizozalishwa katika mwaka 2013/2014. Ongezeko hili la asilimia 4.46 limetokana na juhudi za Serikali na wakulima zilizolenga kuongeza uzalishaji. Pamoja na ongezeko hilo kumekuwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kwenye Bodi za Mazao ambao umeathiri usimamizi na hivyo kutofikia malengo ya ukuaji wa tasnia husika.

**16.** Ufanisi uliopatikana ni pamoja na kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya Chai (tani 33,500 hadi 35,500), Pareto (tani 7,000 hadi 7,600), Tumbaku (tani 100,000 hadi 113,600), Korosho (tani 130,124 hadi 200,000), Mkonge (tani 37,291 hadi 40,000) na Sukari (tani 294,300 hadi 300,230). Aidha, mazao ya Pamba na Kahawa yamezalishwa kwa kiwango cha chini ikilinganishwa na uzalishaji wa mwaka 2013/2014, ambapo uzalishaji wa zao la pamba umeshuka kutoka tani 245,831 hadi 203,313 na kahawa kutoka tani 48,982 hadi 40,759.2.

**17.*Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani milioni 5.40 mwaka 2013/2014 hadi tani milioni 5.64 mwaka 2014/2015. Ongezeko hilo lilitokana na uzalishaji wa mazao ya bustani katika skimu za umwagiliaji. Aidha, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta umeongezeka kutoka tani milioni 5.55 mwaka 2013/2014 hadi tani milioni 5.93 mwaka 2014/2015 kutokana na kuimarika kwa Sekta Binafsi katika uzalishaji wa alizeti katika mikoa ya Singida, Manyara na Dodoma; karanga katika mikoa ya Tabora, Morogoro na Singida; ufuta katika mikoa ya Lindi na Mtwara; na mawese katika mkoa wa Kigoma na kuifanya sekta hiyo kuendelea kukua.

### 2.1.2 Hali ya Chakula na Uzalishaji wa Mazao ya Chakula

**18.*Mheshimiwa Spika,*** hali ya chakula mwaka 2014/2015 imeendelea kuwa nzuri kutokana na mavuno ya kutosha na ziada yaliyopatikana msimu wa kilimo wa 2013/2014. Tathmini ya uzalishaji iliyofanyika mwezi Agosti 2014 nchini ilibaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2013/2014 ulikuwa tani 16,015,238 za mazao ya chakula zikiwemo tani 9,828,540 za nafaka na tani 6,186,698 za mazao yasiyo ya nafaka. Kiasi hicho cha chakula kikilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani 12,767,879 katika mwaka 2014/2015 kilionesha kuwepo kwa ziada ya tani 3,247,359 za chakula. Kutokana na hali hiyo, Taifa lilijitosheleza kwa chakula kwa asilimia 125 ambapo mikoa 23 kati ya 25 ya Tanzania Bara ilibainika kuwa na viwango vya ama ziada au utoshelevu. Tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe iliyofanyika mwezi Januari 2015 ilibaini kuwepo kwa jumla ya watu 424,136 waliokuwa na upungufu wa chakula na walihitaji tani 9,917 za chakula cha msaada na hatua za kukabiliana na upungufu huo zinaendelea kuchukuliwa.

**19.*Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa kilimo wa 2014/2015 maeneo yanayopata mvua za vuli miezi ya Oktoba hadi Desemba yalipata mvua juu ya wastani, wastani na chini ya wastani. Maeneo machache katika mikoa ya Arusha na Morogoro yalipata mvua za juu ya wastani. Mikoa ya Kagera, Mara, Shinyanga, Mwanza, Manyara, Kilimanjaro na Tanga yalipata mvua za wastani zenye mtawanyiko mbaya. Aidha, maeneo ya Dar es Salaam, Pwani, Same na Moshi yalipata mvua chini ya wastani. Kwa ujumla mvua hizo za vuli zilichelewa kuanza na kuisha mapema na hivyo kuathiri ukuaji wa mazao. Hali hiyo inaashiria kupungua kwa mchango wa vuli katika uzalishaji wa chakula msimu wa 2014/2015 na upatikanaji wa chakula katika mwaka 2015/2016. Kawaida, mvua za vuli huchangia takriban asilimia 27 ya chakula.

**20.*Mheshimiwa Spika,*** mvua za msimu zilinyesha kwa mtawanyiko mzuri katika mikoa 15 na hazikunyesha kwa mtawanyiko mzuri katika mikoa 10. Vilevile kulingana na utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa mvua za msimu na za masika zilitarajiwa kuisha katika wiki ya mwisho ya mwezi Machi na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2015 ambapo ni mapema kuliko kawaida. Baadhi ya mikoa ya

Kanda ya Kati ya Dodoma na Singida imekwisha athirika kwa kukatika mapema kwa mvua na hivyo kuathiri mazao kwa kiasi kikubwa. Tathmini ya awali ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula msimu wa 2014/2015 imeonesha kuwepo kwa upungufu wa chakula katika mikoa ya Singida, Simiyu, Dodoma, Geita, Mara, Lindi, Tabora, Mwanza, Manyara na Shinyanga. Utabiri wa kina wa hali ya chakula nchini kwa mwaka 2015/2016 utafanyika mwishoni mwa mwezi Mei hadi mwezi Juni, 2015.

**21.*Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulianza msimu wa ununuzi tarehe 1 Julai 2014 ukiwa na akiba ya tani 189,493.694 za nafaka. Ununuzi wa nafaka uliofanywa na NFRA katika msimu wa 2014/2015 ulikuwa tani 305,424.118 za nafaka zikiwemo tani 296,810.575 za mahindi, tani 4,673.913 za mtama na tani 3,939.630 za mpunga. Aidha, akiba ya nafaka katika maghala ya NFRA hadi tarehe 14 Mei 2015 ni jumla ya tani 422,285.705 zikiwemo tani 413,165.804 za mahindi, tani 5,180.271 za mtama na tani 3,939.630 za mpunga. Aidha, hadi kufikia mwezi Desemba 2014 Serikali ilikuwa inadaiwa na wakulima kiasi cha Shilingi bilioni 89.157. Kati ya mwezi Januari na Mei 2015, Serikali kupitia NFRA imelipa wakulima jumla ya Shilingi bilioni 77 na bado inadaiwa Shilingi bilioni 12. Serikali inaendelea na jitihada za kulipa madeni yaliyobaki.

### 2.2 Hali ya Umwagiliaji

**22.*Mheshimiwa Spika,*** eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji hapa nchini limefikia hekta 461,326 ambapo tija kwa zao la mpunga imeongezeka kutoka tani 1.8 hadi 2.0 kwa hekta mwaka 2006/2007 hadi kufikia tani 4.0 hadi 5.0 kwa hekta mwaka 2014/2015. Hadi kufikia Desemba 2014 uzalishaji wa mazao ya chakula kupitia kilimo cha umwagiliaji ulikuwa tani 3,141,237.34 sawa na asilimia 24.6 ya mahitaji ya chakula nchini, kiwango ambacho kinakaribia lengo la Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya asilimia 25 ya mahitaji ya chakula yatokane na kilimo cha umwagiliaji.

### 2.3 Hali ya Ushirika

**23.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika kwa madhumuni ya kuimarisha ushirika nchini. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeendelea kuhimiza na kukuza maendeleo halisi na endelevu ya vyama vya ushirika kwa kuongeza mwamko wa umma, vijana na makundi mengineyo katika jamii kujiunga na kuanzisha vyama vya ushirika.

**24.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kufanya uhakiki wa vyama vyote vya ushirika vilivyopo nchini kwa lengo la kubaini uwepo na uhai wa vyama hivyo ili kuwezesha Serikali kuratibu mchango wa ushirika katika uchumi na

maendeleo ya Taifa na pia kuwezesha ushirika kuingizwa katika mipango ya maendeleo ya Taifa kupitia sekta husika. Zoezi la uhakiki wa vyama vya ushirika lililofanyika mwaka 2014/2015 limebaini kuwa hadi kufikia Machi 2015, idadi ya Vyama hai vya Ushirika ni 7,888 ikilinganishwa na vyama 9,604 Machi 2014. Kati ya vyama 7,888, vyama vya ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ni 3,865, vyama vya ushirika vya aina nyingine (kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, madini, nyumba) ni 3,973, Benki za ushirika mbili na Vyama Vikuu vya Ushirika 48. Hadi kufikia Machi 2015 jumla ya wanachama wa vyama vya ushirika ni 2,390,593 kati yao wanachama wa SACCOS ni 919,992 ambao wanamiliki hisa, akiba na amana zenye thamani ya Shilingi bilioni 534 mwezi Machi 2015 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 451 mwaka 2014.

***25.Mheshimiwa Spika,*** vyama vya ushirika wa Mazao *(Agricultural Marketing Cooperative Societies – AMCOS*) vimeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuwapatia wakulima masoko ya mazao, hususan mazao makuu ya korosho, kahawa, tumbaku na pamba. Katika msimu wa 2014/2015 Vyama hivi viliweza kukusanya na kuuza mazao yenye thamani ya shilingi bilioni 44.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 37.1 kwa mwaka 2013/2014. Hili ni ongezeko la asilimia 20.5. Uzalishaji wa maziwa kupitia ushirika uliongezeka kutoka lita 775,000 hadi lita 1,075,000 katika kipindi hicho. Wafugaji hao waliweza kujiingizia kipato kutoka takriban Shilingi 426,250,000 mwaka 2013/2014 hadi Shilingi 752,500,000 mwaka 2014/2015.

***26.Mheshimiwa Spika,*** ushirika umeendelea kuchangia katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa watendaji 31,552 wa vyama vya ushirika na hivyo kuchangia katika jitihada za Taifa za kupunguza ukosefu wa ajira rasmi. Vilevile ushirika umewezesha wanachama zaidi ya 50,000 kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) katika mwaka 2014/2015. Wanachama hao waliweza kupata mikopo ya riba nafuu, mafao ya matibabu na malipo ya uzeeni.

## 3.0 MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA KIPINDI CHA 2014/2015

### 3.1 Makusanyo ya Maduhuli

***27.Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka 2014/2015 ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi 3,229,010,000 kupitia Fungu 43, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015 Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi 2,730,909,095.09 sawa na asilimia 84.6 ya makadirio. Wizara inaendelea kukusanya maduhuli hayo.

### 3.2 Fedha Zilizoidhinishwa

**28.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilitengewa jumla ya Shilingi 383,187,544,389 ambapo Shilingi 342,147,611,389 ni Fungu 43, Shilingi 6,631,913,000 ni Fungu 24 na Shilingi 34,408,020,000 ni Fungu 05. Kati ya fedha hizo, Shilingi 295,264,754,389 ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo Shilingi 288,157,841,389 ni Fungu 43, Shilingi 6,631,913,000 ni Fungu 24 na Shilingi 475,000,000 ni Fungu 05. Aidha, jumla ya Shilingi 87,922,790,000 ni fedha za maendeleo zikiwemo Shilingi 53,989,770,000 za Fungu 43 na Shilingi 33,933,020,000 za Fungu 05.

### 3.3 Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo

**29.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2014/2015, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilitengewa jumla ya Shilingi 53,989,770,000 kupitia Fungu 43 na Shilingi 33,933,020,000 kupitia Fungu 05 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 46,945,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 40,977,790,000 ni fedha za nje. Programu na miradi iliyotekelezwa ni:

i)Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme – ASDP*);
ii)Programu ya Kilimo ya Kuendeleza Tija na Uzalishaji katika Mashariki mwa Afrika *(Eastern Africa Agricultural Productivity Programme- EAAPP);*

iii)Mradi wa *Japan Policy and Human Resources Development – PHRD;* na

iv)Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT)*.

**30.*Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 22 Aprili 2015 Shilingi 40,982,880,943 zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo sawa na asilimia 46.26 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Shilingi 31,528,164,943 ni kutoka Fungu 43 na Shillingi 9,454,716,000 ni kutoka Fungu 05.

### 3.4 Matumizi ya Bajeti ya Kawaida

**31.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi 295,264,754,389. Fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Wizara, ununuzi wa nafaka, ruzuku ya pembejeo, michango kwa mashirika ya nje, ruzuku kwa mashirika ya ndani, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, ununuzi wa viuatilifu, chakula cha wanafunzi na uendeshaji wa Tume za Ushirika na Umwagiliaji.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 22 Aprili 2015 jumla ya Shilingi 205,008,914,502 zimetolewa sawa na asilimia 69.43 ya fedha zilizoidhinishwa. Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa nafaka ya hifadhi ya chakula cha Taifa (Shilingi 102,229,136,060), madeni ya ruzuku ya pembejeo (Shilingi 47,095,159,818), mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi (Shilingi 30,328,651,850), madeni ya huduma mbalimbali ya miaka ya nyuma (Shilingi 9,586,933,388.68), ruzuku ya mashirika ya ndani (Shilingi 5,190,252,018), Mfuko wa Pembejeo (Shilingi 1,304,190,991), Chakula cha wanafunzi katika vyuo vya kilimo (Shilingi 1,197,666,312.8), Udhibiti wa visumbufu vya mimea (Shilingi 125,000,000) na fedha zilizotumika kwa ajili ya uendeshaji wa Wizara na Taasisi (Shilingi 7,951,924,064).

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2014/2015 NA MPANGO WA MWAKA 2015/2016

### 4.1 MALENGO

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2014/2015, umezingatia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now – BRN*) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Malengo hayo yalitekelezwa kupitia ASDP, Programu ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika na SAGCOT.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufanikisha majukumu yake, Wizara imetekeleza Malengo Mkakati nane (8) kupitia Fungu 43, 24 na 05 katika Idara, Vitengo, Asasi na Taasisi za Wizara. Malengo Mkakati hayo ni:

i) Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo;

ii) Kuwezesha Upatikanaji wa Masoko ya Bidhaa za Kilimo;

iii) Kuwezesha Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo;

iv) Kuwezesha na Kuimarisha Ushirika na Asasi za Wananchi katika Kilimo na Sekta nyingine za Kiuchumi;

v) Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji, Uhifadhi, Uchambuzi na Usambazaji wa Takwimu;

vi) Kusimamia Sera na Sheria katika Sekta ya Kilimo;

vii) Kuboresha Uwezo wa Wizara wa kutoa Huduma; na

viii) Kuzingatia Masuala Mtambuka katika Kilimo.

### 4.2 Utekelezaji wa Malengo Mkakati kwa Mwaka 2014/2015 na Mpango wa Mwaka 2015/2016

**35.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kutekeleza majukumu yake mbalimbali, ambayo yamewezesha kuinua Sekta ya kilimo na hivyo kuchangia katika pato la Taifa kwa asilimia 31.7 mwaka 2014. Aidha, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia malengo Mkakati nane ambayo imejiwekea. Utekelezaji wa Malengo Mkakati hayo ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.1 Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo

**36.*Mheshimiwa Spika,*** katika kufikia lengo la kuongeza uzalishaji na tija, Wizara ilisimamia upatikanaji wa pembejeo za kilimo; uzalishaji wa mbegu na miche bora; utoaji ruzuku ya pembejeo za kilimo; udhibiti wa ubora wa mbolea, mbegu na madawa; utafiti; huduma za ugani; ukaguzi wa viuatilifu vya mazao na mbegu; kuainisha mashamba makubwa kwa ajili ya uwekezaji na mafunzo kwa wakulima kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo; na miradi mingine ya kisekta kama ifuatavyo:-

***Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo***

**37.*Mheshimiwa Spika,*** makadirio ya mahitaji ya mbolea kwa mwaka 2014/2015 yalikuwa tani 485,000 na kufikia Aprili 2015, jumla ya tani 342,798 za mbolea zilipatikana na kusambazwa mikoani sawa na asilimia 70.7 ya mahitaji. Aidha, upatikanaji wa mbegu bora ulifikia tani 36,410.46 sawa na asilimia 60.7 ya mahitaji halisi ya mbegu bora ya tani 60,000. Kati ya mbegu hizo tani 21,407.29 zimezalishwa nchini ambapo asilimia 81.3 ni mbegu za mahindi na asilimia 6.7 ni mbegu za mpunga na tani 15,003.17 zimeagizwa kutoka nje ya nchi. Muhtasari wa upatikanaji wa mbegu bora kwa mwaka 2014/2015 umeoneshwa kwenye **Jedwali Na 1.**

**Jedwali Na 1: Mchanganuo wa upatikanaji wa mbegu bora kwa mwaka 2014/2015 (Tani)**

| Aina ya Mbegu | Mahitaji | Uzalishaji | Uagizaji kutoka nje | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 28,160 | 17,411.61 | 12,879.16 | 30,290.77 |
| Mpunga | 13,860 | 1,444.68 | 0.02 | 1,444.70 |
| Mtama | 10,840 | 651.89 | 2.23 | 654.12 |
| Shayiri | 1,000 | 200.00 | 280 | 480.00 |
| Alizeti | 1,820 | 297.75 | 1095.91 | 1,393.66 |
| Maharagwe | 1,000 | 196.90 | 204.405 | 401.31 |
| Ngano | 500 | 64.94 | 0 | 64.94 |
| Ufuta | 250 | 36.40 | 0 | 36.40 |
| Mboga | 1,500 | 689.68 | 511.43047 | 1,201.11 |
| Njegere | 50 | 2.44 | 0 | 2.44 |
| Kunde | 125 | 15.97 | 0 | 15.97 |
| Mbaazi | 100 | 60.03 | 0 | 60.03 |
| Maharagwe Soya | 100 | 0 | 30 | 30.00 |
| Karanga | 100 | 0 | 0.01 | 0.01 |
| Viazi Mviringo | 595 | 335.00 | 0 | 335.00 |
| **Jumla** | **60,000** | **21,407.29** | **15,003.167** | **36,410.46** |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika*

***Uzalishaji wa Mbegu na Miche Bora***

**38.*Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa tunapata mbegu bora za kutosha hapa nchini, Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) umezalisha tani 3,154 za mbegu bora za nafaka, mikunde, na mboga katika mwaka 2014/2015. Aidha, ASA imeendelea kushirikiana na Sekta Binafsi yakiwemo makampuni ya kizalendo ya *Suba Agro Trading & Engineering Company Limited* na *Meru Agro Tours & Consultants Limited* na kuzalisha tani 2,234 za mbegu bora za nafaka katika shamba la mbegu la Mbozi. Aidha, ASA imezalisha vipando bora vya muhogo 9,980,531 na miche bora ya matunda 75,791. ASA imehamasisha vijana kuingia kwenye Kilimo kwa makubaliano na kampuni ya vijana ya RABICAN, ambapo wamepatiwa ekari 500 za shamba la mbegu la Bugaga (Kasulu) kwa ajili ya kuzalisha mbegu na mazao ya biashara. Vilevile wakulima wadogo walizalisha mbegu za daraja la kuazimiwa *(Quality Declared Seed-QDS)* jumla ya tani 627.15 za nafaka, mikunde, mbegu za mafuta na mboga. Makampuni mengine ya mbegu yalizalisha jumla ya tani 15,440.6 zilizochangia katika upatikanaji wa mbegu bora.

**39.*Mheshimiwa Spika,*** ASA imejenga miundombinu ya umwagiliaji katika eneo la eka 500 katika shamba la mbegu la Kilangali (Kilosa) kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu za mpunga. Aidha, ASA imejenga na kukarabati maghala mawili na kufunga mitambo mipya miwili ya kisasa ya kusindika mbegu. Katika mwaka 2015/2016 ASA itazalisha tani 2,990 za mbegu bora za nafaka, mikunde na mboga; pingili 12,000,000 za muhogo; na miche bora 80,000 ya matunda katika mashamba yake. Vilevile, ASA itaendelea kushirikiana na JKT, Jeshi la Magereza na Sekta binafsi katika kuzalisha pingili za muhogo, miche bora ya matunda, tani 4,100 za mbegu bora za nafaka, alizeti na soya. ASA pia

itazalisha tani 351 za mbegu bora za mahindi kwa kushirikiana na *Clinton Development Foundation (CDF)*.

***Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo***

**40.*Mheshimiwa Spika,*** mpango wa ruzuku kwa mwaka 2014/2015 ulilenga kutoa ruzuku ya riba ya mikopo ya pembejeo za kilimo kwa Vikundi vya Wakulima na vyama vya ushirika kupitia Taasisi za Fedha. Vikundi 4,990 vilivyosajiliwa kisheria vyenye kaya 974,030 vilitambuliwa. Hadi mwezi Machi 2015 jumla ya vikundi vilivyokidhi masharti ya kukopesheka ni 712 kupitia benki za NMB, CRDB na benki za wananchi. Benki ya NMB imetoa mikopo kwa jumla ya vyama vya ushirika vya Msingi na Vikundi vya Wakulima 281 vyenye wanachama 28,700. Aidha, Benki ya CRDB ilitoa mikopo kwa Vikundi na vyama vya ushirika 247 vyenye wanachama 24,700 katika mikoa ya Tabora (145), Kigoma (35), Shinyanga (Kahama 16), Mbeya (Chunya 16), Katavi (Mpanda 6), Ruvuma (12), Iringa (5), na Singida (12). Vile vile benki za wananchi za Mbinga, Njombe, Mufindi, Kagera na Tandahimba zimetoa mikopo kwa Vikundi vya Wakulima 184 vyenye jumla ya wanachama 3,315. Shilingi 1,308,779,475 zimetolewa kwa wakulima kwa ajili ya mikopo ya pembejeo za kilimo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na 2.** Changamoto iliyojitokeza ni kukosekana kwa mtandao wa benki katika nchi nzima  na wakulima wengi kutokuwa katika vikundi.

**Jedwali Na 2: Vikundi na Wanachama Waliokopeshwa na Benki za Wananchi**

| Benki | Vikundi | Wanachama | Thamani ya Mikopo (TZS) |
|---|---|---|---|
| Mbinga | 28 | 400 | 78,119,175 |
| Njombe | 56 | 594 | 125,392,500 |
| Mufindi | 25 | 374 | 45,307,800 |
| Kagera | 26 | 1,560 | 585,710,000 |
| Tandahimba | 26 | 387 | 474,250,000 |
| **Jumla** | **184** | **3,315** | **1,308,779,475** |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika*

**41.*Mheshimiwa Spika,*** kutokana na changamoto zilizojitokeza katika msimu uliopita kwa wakulima wengi kukosa pembejeo ya ruzuku, Serikali katika mwaka 2015/2016 itarejesha utaratibu wa matumizi ya vocha kwa mazao ya mahindi na mpunga. Serikali itachangia asilimia 50 ya gharama za pembejeo kwa lengo la kutoa ruzuku ya tani 99,923 za mbolea na tani 10,270.86 za mbegu bora za mahindi na mpunga zitakazonufaisha kaya 999,926. Hata hivyo, kiasi hicho cha pembejeo zenye ruzuku ni kidogo kulingana na mahitaji ya wakulima kutokana na ufinyu wa bajeti inayotolewa na Serikali.

**42.*Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya uzalishaji wa miche bora ya chai na ya kahawa. Hadi kufikia Aprili 2015, jumla ya miche bora

ya kahawa 1,014,671 ilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima wa Moshi, Mbinga, Bukoba na Tarime sawa na asilimia 20.3 ya lengo la kuzalisha miche 5,000,000. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA) wamezalisha miche 1,000,000 ya chai. Vilevile Wizara itatoa ruzuku ya mbegu bora za mtama na alizeti kwa maeneo kame na yale yanayopata mvua za wastani. Ruzuku zingine zitakazotolewa ni pamoja na miche bora ya chai na kahawa, mbegu za pamba na madawa ya pamba na korosho.

***Udhibiti wa Ubora wa Mbolea***

**43.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kudhibiti ubora wa mbolea kwa ajili ya matumizi bila kusababisha madhara kwa watumiaji na mazingira. Hadi mwezi Aprili 2015 jumla ya tani 342,798 za mbolea zilikaguliwa wakati wa kuingizwa nchini. Wizara pia ilikagua maduka na maghala ya mbolea katika mikoa ya Dar es salaam, Mbeya, Njombe, Arusha na Ruvuma. Wizara kupitia Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009 ilichukua hatua za kusitisha leseni kwa wafanyabiashara waliobainika kuingiza na kuuza mbolea zisizokidhi viwango na kuamriwa kuziondoa sokoni mbolea hizo.

**44.** Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya utunzaji, usambazaji na uuzaji wa mbolea kwa mawakala 240 (Mbeya 67, Njombe 61, Mwanza 66, Mara 7, Simiyu 13, Shinyanga 4, Geita 14, Tabora 5 na Kigoma 3). Vilevile Wizara imesajili mawakala 220 katika mwaka 2014/2015 na kuwa na jumla ya mawakala 854. Ili kukabiliana na uingizwaji wa mbolea zisizokidhi viwango vya ubora, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania imesaini mikataba na makampuni ya kimataifa ya SGS, *Intertek International (T) Limited* na *Bureau Veritas* kuhakikisha mbolea kabla ya kuingizwa nchini inapimwa ubora wake. Vilevile Wizara imekamilisha muundo wa TFRA na kuidhinishwa na Mamlaka husika kwa utekelezaji. Katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kudhibiti ubora wa mbolea nchini.

***Udhibiti wa Ubora wa Mbegu***

**45.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TOSCI ilifanya majaribio ya ubora wa mbegu mpya aina 74 ambapo aina 65 zilikidhi viwango. Wizara pia ilikagua hekta 12,425 za mashamba yaliyozalisha mbegu katika madaraja mbalimbali ambapo hekta 12,418.4 sawa na asilimia 99.9 zilikidhi viwango vya ubora wa mashamba ya kuzalisha mbegu. Aidha, Wizara kupitia TOSCI ilisimamia udhibiti wa ubora wa mbegu kwa kuchukua sampuli 1,394 zilizowakilisha tani 6,427 za mbegu mbalimbali za mazao kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya maabara. Vipimo vya maabara vilionyesha kuwa asilimia 98.8 ya sampuli zilikidhi viwango vya maabara ikiwemo usafi na uotaji.

**46.*Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na mbegu zisizokidhi viwango vya ubora na kuhakiki ubora wa mbegu zinazouzwa, Wizara ilikagua maduka ya mbegu 105 ambapo maduka matano yalibainika kuuza mbegu ambazo uotaji wake haukukidhi viwango vya uotaji na hivyo kuzuiliwa kuuzwa kwa wakulima. Wizara pia katika ziara za ukaguzi wa maduka ilitumia fursa ya kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutumia mbegu bora na jinsi ya kutambua mbegu zisizokidhi viwango vya ubora. Vilevile Wizara iliandaa maandiko rasmi na kuyawasilisha kwenye Sekretarieti za Mashirika ya Kimataifa yanayohakiki Viwango vya Ubora wa Mbegu ili kuwezesha Tanzania kupata ithibati ili mbegu zinazozalishwa nchini ziweze kutambulika kimataifa.

**47.*Mheshimiwa Spika,*** katika kuijengea uwezo TOSCI, Wizara imeajiri maafisa 30 na kuhamisha maafisa wawili (2) kutoka Wizarani. Vilevile maabara za TOSCI ziliboreshwa kupitia mradi wa EAAPP kwa kupatiwa vifaa vya kisasa. Aidha, maafisa wanne (4) wa Taasisi walihudhuria mafunzo ya utaalamu wa mbegu ili kudhibiti ubora wa mbegu. TOSCI imeendesha mafunzo mbalimbali kwa wazalishaji wadogo wa mbegu pamoja na wasimamizi wao kwa ufadhili wa mashirika yasiyo ya kiserikali.

**48.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itafanya majaribio ya aina mpya za mbegu 100. Vilevile, Wizara itakagua hekta 14,000 za mashamba ya kuzalisha mbegu na kuthibitisha ubora wa tani 8,000 za mbegu na kukagua tani 20,000 za mbegu zitakazoingizwa kutoka nje. Aidha, Wizara itatekeleza utaratibu wa kuweka lebo katika mifuko ya mbegu ili kukabiliana na wimbi la mbegu zisizokidhi viwango na kukidhi vigezo vya uanachama wa OECD. Wizara pia itaendelea na hatua za kujiunga na ISTA na OECD.

***Udhibiti wa Ubora wa Madawa***

**49.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea kudhibiti ubora wa madawa yanayozalishwa nchini na kuingizwa kutoka nje. Katika kutekeleza hayo, Wizara ilisajili viuatilifu na kutoa vyeti 139 vya usajili wa viuatilifu vilivyokidhi viwango vya ubora kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Mimea ya mwaka 1997 na Kanuni za mwaka 1999. Aidha, vibali vya kuingiza viuatilifu vilitolewa kwa makampuni 320 yaliyokidhi vigezo. Vilevile, vibali 361 vya kuagiza viuatilifu vilitolewa. Wizara pia ilikagua wafanyabiashara 362 wa viuatilifu, waagizaji na wafukizaji katika maeneo ya Karatu, Monduli, Arumeru, Mbulu, Katesh, Arusha Manispaa, Arusha, Moshi Manispaa, Himo, Sanya Juu, Hai, Babati na Mbinga. Maeneo mengine ni Songea, Njombe, Makambako, Iringa Manispaa, Kilolo, Mbeya, Tukuyu, Tunduma, Ilala, Mwanza, Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Nzega, Sikonge na Igunga. Aidha, wafanyabiashara waliobainika kuuza pembejeo zisizo na ubora walichukuliwa hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa leseni na kufunguliwa mashtaka kulingana na

Sheria ya Taasisi ya Udhibiti. Katika mwaka 2015/2016 Wizara kupitia TPRI itaendelea kukagua na kusajili viuatilifu nchini.

### *Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Asili ya Biashara*

**50.*Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bodi za Mazao imeendelea kusimamia uzalishaji wa mazao makuu ya asili ya biashara katika mwaka 2014/2015. Uzalishaji wa mazao hayo umeongezeka na kupungua kwa viwango tofauti. Mazao ya Chai, Pareto, Tumbaku, Korosho, Mkonge na Sukari yameongezeka, ambapo mazao ya Kahawa na Pamba yamepungua. Sababu za ongezeko katika uzalishaji wa mazao hayo ni pamoja na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati; hali nzuri ya hewa katika maeneo ya uzalishaji; na bei nzuri anayolipwa mkulima. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao makuu ya asili ya biashara unaoneshwa katika **Jedwali Na 3.**

**Jedwali Na 3: Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Asili ya Biashara 2013/2014 hadi 2014/2015 na Matarajio 2015/2016 (Tani)**

| Zao | Uzalishaji 2013/2014 | Uzalishaji 2014/2015 | Matarajio 2015/2016 |
|---|---|---|---|
| Pamba | 245,831 | 203,313 | 200,000 |
| Kahawa | 48,982 | 40,759.2 | 62,000 |
| Chai | 33,500 | 35,500* | 36,000 |
| Pareto | 7,000 | 7,600 | 8,000 |
| Tumbaku | 100,000 | 105,881 | 104,600 |
| Korosho | 130,124 | 200,000 | 250,000 |
| Mkonge | 37,291 | 40,000* | 45,000 |
| Sukari | 294,300 | 304,007 | 328,416 |
| **Jumla** | **897,028** | **937,060.2** | **1,034,016** |

*Chanzo**:** Bodi za Mazao*
*Matarajio hadi Juni 2015

### *Pareto*

**51.*Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa zao la pareto umeongezeka kutoka tani 7,000 kwa mwaka 2013/2014 hadi tani 7,600 mwaka 2014/2015. Ongezeko hilo limetokana na hali nzuri ya mvua na uhamasishaji mkubwa uliofanywa na Bodi na wadau wake katika mikoa inayozalisha pareto. Aidha, soko la uhakika na la ushindani limesababisha ongezeko la uzalishaji wa pareto. Bodi inaendelea kuhamasisha wadau kuhusu uendelezaji wa zao la pareto. Katika mwaka 2015/2016 uzalishaji wa zao la pareto unatarajiwa kufikia tani 8,000.

### *Sukari*

**52.*Mheshimiwa Spika,*** mahitaji ya sukari nchini ni wastani wa tani 420,000 kwa matumizi ya nyumbani na tani 170,000 kwa matumizi ya viwandani. Uzalishaji wa sukari nchini kwa mwaka ni wastani wa tani 300,000 ambazo zote

ni sukari kwa matumizi ya nyumbani. Kutokana na hali hiyo, nchi yetu kwa kawaida hulazimika kuagiza tani 290,000 za sukari ili kufidia pengo la uzalishaji ambapo kati ya hizo, tani 120,000 ni kwa matumizi ya nyumbani na tani 170,000 ni kwa matumizi ya viwandani.

**53.*Mheshimiwa Spika,*** malengo ya uzalishaji msimu wa 2014/2015 yalikuwa ni kuzalisha tani 300,858. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015 ambapo viwanda vyote vilikuwa vimefunga msimu wa uzalishaji, jumla ya tani 304,007 zilikuwa zimezalishwa. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 101 ya malengo ya uzalishaji. Uzalishaji kwa msimu wa 2014/2015 umeongezeka kwa asilimia 3.3 ukilinganisha na tani 294,419 zilizozalishwa katika msimu wa 2013/2014 kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 1.**

**54.*Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 5 Mei 2015, jumla ya tani 24,900 za sukari zilikuwa katika maghala ya kampuni za sukari na tani 9,352 zilikuwa katika maghala ya wasambazaji wakubwa. Aidha, kwa kuwa sukari kwenye mzunguko wa soko ni wastani wa asilimia 10 ya akiba yote, hivyo jumla ya sukari iliyopo nchini ni takriban tani 37,677. Kiasi hicho cha sukari kinatosheleza mahitaji ya sukari nchini kwa kipindi cha mwezi mmoja.

**55.*Mheshimiwa Spika,*** kutokana na upungufu wa sukari uliopo nchini, Serikali imeidhinisha uagizaji wa tani 100,000 za sukari ili kuziba pengo la mahitaji kwa msimu wa 2014/2015. Kati ya kiasi hicho tani 88,940.25 zitaagizwa kutoka nje na tani 11,059.75 ambazo ni *Transit Sugar* zitatumika nchini kuziba pengo la sukari baada ya kutozwa ushuru stahiki. Katika kutekeleza jukumu hilo, Bodi ya Sukari imetoa leseni kwa makampuni 25 kuingiza sukari nchini kati ya mwezi Machi na Mei 2015. Sukari hiyo inayoagizwa kutoka nje inalipiwa kodi ya ongezeko la thamani ya asilimia 18 na ushuru wa forodha wa asilimia 50. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015 tani 23,775 zilikuwa zimeingizwa na tani 51,799 zilikuwa zimeagizwa. Aidha, tani 182,765 za sukari ya viwandani ziliidhinishwa kuingizwa nchini. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015 tani 97,880 zimeingizwa nchini, sawa na asilimia 53.56 ya kiasi kilichoidhinishwa.

**56.*Mheshimiwa Spika,*** changamoto kubwa iliyoikabili tasnia ya sukari nchini ni uingizwaji wa sukari kwa njia zisizo rasmi hali inayoathiri wazalishaji wa ndani kibiashara na uingizwaji wa sukari ya viwandani kwa matumizi ya kawaida. Kwa kutambua hilo Serikali inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti uingizaji wa sukari toka nje ya nchi kwa njia zisizo rasmi pamoja na kudhibiti sukari inayopitia nchini kwenda nchi jirani ambapo Serikali imeunda kikosi kazi kinachoratibiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Vyombo vya Usalama ili kuifuatilia hadi inapovuka mipaka ya Tanzania. Aidha, ukaguzi wa mara kwa mara unafanyika ili kubaini matumizi halisi ya sukari ya viwandani ili kuruhusu kiwango halisi kinachohitajika. Pia Serikali imeunda Kikosi Kazi kinachoratibiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kujumuisha Mamlaka

nyingine ili kudhibiti sukari inayoingia kwa njia za bandari zisizo rasmi kwa kufanya ukaguzi kwa kutumia boti za doria katika kupambana na bidhaa za magendo kupitia bandari bubu.

**57.*Mheshimiwa Spika,*** kwa muda mrefu kumekuwa na mgogoro kati ya kiwanda cha Sukari Mtibwa na wakulima wa miwa wa nje (*Outgrowers*) kutokana na Kiwanda au mwekezaji kutotoa malipo stahili kwa wakati kwa wakulima, bei ndogo ya miwa, kutoridhika kwa wakulima na upimaji wa kiasi cha sukari katika miwa (*rendement*) na uvamizi wa mifugo katika mashamba ya miwa. Bodi ya Sukari imekuwa ikiratibu mikutano ya pamoja kati ya Kampuni ya Miwa Mtibwa na wawakilishi wa wakulima juu ya utekelezaji wa makubaliano baina yao juu ya bei ya miwa na taratibu za kuuziana miwa kwa mujibu wa mikataba yao.

**58.*Mheshimiwa Spika,*** katika Wilaya za Kilombero na Kilosa kumekuwa na migogoro inayotokana na uwezo mdogo wa viwanda vya kusindika miwa. Hali hiyo imesababisha matatizo katika vyama vya wakulima wakati wa uvunaji; pia wakati mwingine kumekuwa na migogoro ya kimaslahi inayowahusu watendaji katika vyama hivyo. Ili kutatua migogoro hiyo, Bodi ya Sukari kwa kushirikiana na Mamlaka za Mkoa na Wilaya inaratibu utatuzi wa changamoto zilizojitokeza ambapo Mkuu wa Mkoa wa Morogoro ameunda kikosi kazi cha kushughulikia matatizo hayo. Kikosi Kazi hicho kimeanza kazi yake tarehe 22 Aprili 2015 na tayari hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kusimamisha baadhi ya viongozi wa vyama hivyo na kutoa maagizo kuhusu marekebisho ya Katiba zao ili vyama hivyo viweze kuendeshwa kwa ufanisi.

**59.** Aidha, ili kuondokana na tatizo la miwa kukosa viwanda vya usindikaji, Bodi ya Sukari imekamilisha upembuzi yakinifu wa kuanzisha viwanda vya sukari vya kati na vidogo vya kusindika sukari. Maeneo yanayopendekezwa kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda vipya vya kati na vidogo ni Mfilisi na Muhenda (Kilosa), Kiberege (Kilombero) pamoja na Kanga na Kwadoli (Mvomero).

**60.*Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa 2015/2016 kiasi cha tani 328,416 za sukari zinatarajiwa kuzalishwa nchini. Mchanganuo wa uzalishaji kwa kila kiwanda ni Kilombero tani 132,720; TPC Ltd tani 103,196; Mtibwa tani 35,000; na Kagera tani 57,500. Uzalishaji unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 304,007 za sukari zilizozalishwa msimu huu kutokana na matumizi ya mbegu mpya na bora za miwa, udhibiti wa wadudu na magonjwa ya miwa, ongezeko la kilimo cha umwagiliaji na ukarabati wa viwanda vya sukari.

***Chai***

**61.*Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa zao la chai kavu katika kipindi cha mwezi Julai 2014 hadi Juni 2015 unategemewa kufikia tani 35,500 ikilinganishwa na tani 33,500 zilizozalishwa katika msimu wa 2013/2014. Hili ni ongezeko la tani

2,000 sawa na asilimia 6. Ongezeko hili limetokana na hali nzuri ya hewa hususan mvua katika maeneo yanayolima chai pamoja na uzingatiaji wa kanuni za kilimo bora cha zao la chai. Matarajio ya uzalishaji wa chai kavu katika msimu wa 2015/2016 ni kufikia tani 36,000.

**62.** Pamoja na ongezeko hilo la uzalishaji wa Chai kavu, bado kuna fursa ya ongezeko hilo kuwa kubwa kama mgogoro uliopo kati ya wakulima na mwekezaji wa Kiwanda cha Mponde chenye uwezo wa kuchakata tani 60 za majani mabichi kwa siku ukiondolewa. Serikali imeandaa utaratibu wa kukifungua na kukiendesha kiwanda cha Mponde kwa muda wakati mgogoro kati ya wakulima na mwekezaji unatafutiwa ufumbuzi.

**63.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (TRIT) imezalisha na kusambaza miche 1,650,000 kwa wakulima wadogo. TRIT pia imeanzisha mashamba ya vyanzo vya vikonyo kwa ajili ya kuzalisha miche bora katika Wilaya za Njombe (5); Ludewa (2); Rungwe (4); Mufindi (4); Usambara, Muheza, Korogwe na Bumbuli (3). Vilevile TRIT imekamilisha ujenzi wa sehemu yenye uwezo wa kuzalisha miche bora ya chai 1,000,000 katika kituo cha Utafiti wa Chai Ngwazi na ghala la kuhifadhia tani 300 za mbolea katika kijiji cha Mkonge. Aidha, TRIT imejenga miundombinu minne (4) ya umwagiliaji kwa njia ya matone kwa wakulima wadogo katika Wilaya za Muheza, Rungwe, Mufindi na Njombe. Katika mwaka 2015/2016 Wizara kwa kushirikiana na TRIT itazalisha na kusambaza miche bora ya chai 2,700,000 na kujenga kituo cha kuzalisha miche katika Kituo cha Utafiti wa Chai cha Marikitanda.

**64. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA), imezalisha miche 960,000 katika Wilaya za Tarime na Njombe. Aidha, hekta 250 za chai zimepandwa katika Wilaya ya Njombe kwa kuhusisha wakulima 266. Vilevile TSHTDA imetoa mafunzo na vitendea kazi kwa maafisa ugani 15 na kukamilisha utafiti wa uwezekano wa wakulima kuwa na viwanda vidogo vya chai. Katika mwaka 2015/2016 TSHTDA itapanda hekta 100 za chai katika Wilaya za Tarime, Njombe na Kilolo. Vilevile itazalisha miche 2,500,000 kwa ajili ya kupanda katika hekta 170 za mashamba mapya na kujaza nafasi katika mashamba na kuajiri maafisa ugani 20.

***Kahawa***

**65.*Mheshimiwa Spika,*** hali ya uzalishaji wa kahawa imepungua kutoka tani 48,982 mwaka 2013/2014 hadi kufikia tani 40,759.2 kwa mwaka 2014/2015. Sababu za kushuka kwa uzalishaji wa zao la kahawa ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha mtawanyiko mbaya wa mvua na kuwepo kwa vipindi virefu vya ukame katika maeneo muhimu ya uzalishaji ya Mbozi,

Karagwe na Kyerwa; matumizi duni ya mbolea; mahitaji makubwa ya miche bora; na wakulima kutozingatia kanuni za kilimo bora.

**66.*Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uzalishaji wa kahawa nchini, Bodi ya Kahawa Tanzania kwa kushirikiana na wadau itaimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Kahawa utakaowezesha uandaaji wa mfumo rasmi wa kuwapatia pembejeo wakulima wadogo kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji wa kahawa yenye ubora. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na wadau inatengeneza mwongozo wa Taifa wa kutoa elimu kwa wakulima kuhusu utayarishaji wa kahawa yenye ubora kupitia viwanda vya kubangulia kahawa mbichi. Vilevile, Bodi itaendelea kutoa bei elekezi kwa wakulima kwa kutumia ujumbe mfupi wa "kahawa bei" kwa madhumuni ya kuhamasisha uzalishaji. Uzalishaji unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia tani 62,000 kwa mwaka 2015/2016.

**67.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na TaCRI katika mwaka 2014/2015 imezalisha na kusambaza miche bora ya kahawa ya vikonyo 5,200,000 ya aina ya Arabika na 1,200,000 aina ya Robusta. Pia Mbegu chotara za aina fupi ya Arabika kilo 200 zenye uwezo wa kutoa miche 400,000 zimezalishwa na kusambazwa. TaCRI pia imeendelea na utafiti wa aina 10 za kahawa ya Arabika katika Wilaya za Rombo, Tarime, Kasulu na Mbozi ambapo kati ya hizo aina tatu zimeonesha uwezo mkubwa wa kustahimili ukame.

**68.** Vilevile TaCRI imetathmini rutuba ya udongo katika mikoa 16 (Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya, Rukwa, Katavi, Kigoma, Kagera, Mara, Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Geita, Mwanza, na Morogoro) ili kutoa ushauri wa kuongeza rutuba ya udongo kwa kilimo chenye tija. Aidha, TaCRI imetoa mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha kahawa kwa wakulima wawezeshaji 6,122 na maafisa ugani 122. Katika mwaka 2015/2016 Wizara kwa kushirikiana na TaCRI itaendelea na utafiti wa kutathmini mbegu tatu za Arabika na kuzalisha na kusambaza miche bora milioni 10 ya kahawa aina ya Arabica na Robusta kwa njia ya chupa.

***Korosho***

**69.*Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa 2014/2015 makisio ya uzalishaji wa korosho yalikuwa tani 177,687.050 na uzalishaji halisi ulifikia tani 200,000. Uzalishaji huo ni ongezeko la tani 69,876.222 sawa na asilimia 54 ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 130,123.778 katika mwaka 2013/2014. Sababu ya ongezeko hilo ni usimamizi makini wa tasnia, upatikanaji wa pembejeo za korosho kwa wakati, hali nzuri ya hewa, ushiriki na uwajibikaji wa wadau wote katika sekta ndogo ya korosho, bei nzuri anayolipwa mkulima kutokana na kuimarika kwa soko kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala. Matarajio ya uzalishaji katika mwaka 2015/2016 ni tani 250,000.

***Mkonge***

**70.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 uzalishaji wa mkonge ulikuwa tani 31,762 mwezi Machi 2015 na unatarajiwa kuongezeka kufikia tani 40,000 ifikapo mwezi Juni 2015 ikilinganishwa na tani 37,291 zilizozalishwa mwaka 2013/2014 sawa na ongezeko la asilimia 7.26. Ongezeko hilo limetokana na hali nzuri ya hewa na mahitaji ya mkonge na bidhaa zake kwenye soko la dunia hususan kwenye nchi za China, Saudi Arabia, Uingereza, India, Hispania, Ujerumani, Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Israel, Japan na Nigeria limesababisha kupanda kwa bei ya Mkonge kutoka wastani wa Dola za Marekani 1,500 kwa tani kwa mwaka 2013/2014 hadi Dola 1,800 kwa tani kwa mwaka 2014/2015 kwa mkonge wa daraja la juu. Matarajio ya uzalishaji wa mkonge katika msimu wa 2015/2016 ni kufikia tani 45,000.

***Tumbaku***

**71.*Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa Tumbaku katika mwaka 2014/2015 ulifikia tani 105,881 ikilinganishwa na tani 100,000 zilizozalishwa katika mwaka 2013/2014. Sababu ya ongezeko hilo ni pamoja na matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo na hali nzuri ya mtawanyiko wa mvua katika maeneo yanayozalisha zao hilo. Katika mwaka 2015/2016 uzalishaji wa Tumbaku unatarajiwa kufikia tani 104,600. Sababu ya kushuka kwa matarajio ya uzalishaji ukilinganisha na mwaka uliotangulia ni mtawanyiko mbaya wa mvua katika mwaka 2014/2015 katika maeneo yanayozalisha tumbaku.

**72.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara kupitia TOSCI kwa kushirikiana na TORITA imekamilisha tathmini za mbegu za aina tatu za tumbaku (DDV10, DDV42 na DDV43) ambazo zinatoa mavuno ya wastani wa kilo 2,050 kwa hekta ikilinganishwa na mbegu ya K326 inayotumika sasa. Mbegu hizi zinahimili ukame, minyoo, ufundo na kukomaa kwa utaratibu na hivyo kumpa fursa mkulima kukausha tumbaku nyingi pasipo kupoteza ubora. Katika mwaka 2015/2016 TORITA itafanya utafiti wa mabani yanayotumia kuni kidogo ya kukaushia tumbaku na kubaini nishati mbadala ya kukaushia tumbaku. Aidha, TORITA itafanya majaribio ya mbegu za KRK26, CC26, CC27, CC35, DDV10, DDV42 na DDV43 kwa kushirikiana na wakulima wa kanda za Urambo, Kahama na Chunya ili kuwapa fursa wakulima kubaini mbegu zinazofanya vizuri katika maeneo husika.

***Pamba***

**73.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 ununuzi wa pamba mbegu ulifikia tani 203,313 sawa na marobota 374,564 ikilinganishwa na tani 245,831 sawa na marobota 456,976 yaliyozalishwa msimu wa 2013/2014 ikiwa ni upungufu wa asilimia 21. Sababu zilizochangia ni kuendelea kushuka kwa bei ya pamba katika soko la kimataifa na hivyo kuathiri bei kwa mkulima; mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri kilimo cha pamba kinachotegemea mvua kwa asilimia 100; uwezo mdogo wa wakulima kujinunulia pembejeo; na wakulima

kutokuzingatia kanuni za kilimo bora cha pamba. Uzalishaji wa pamba unatarajiwa kufikia tani 200,000 katika mwaka 2015/2016 kutokana na mtawanyiko mbaya wa mvua.

***Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko***

**74.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imetathmini mali na kukagua kinu cha kusaga nafaka cha Iringa na kukifanyia matengenezo ikiwa ni pamoja na kukarabati mfumo wa maji na umeme katika kinu na vihenge; kununua *power factor* ili kuthibiti mfumo wa matumizi ya umeme katika kinu na vihenge; na kulipa malimbikizo ya ankara ya umeme yaliyokuwepo kabla ya Bodi kukabidhiwa kinu hicho. Bodi pia imekausha tani 765 za shayiri ya Kampuni ya Bia Tanzania (TBL). Bodi hiyo itaanza kufanya kazi zake za msingi katika mwaka 2015/2016 na kwa kuanzia itanunua tani 50,000 za nafaka, kati ya hizo tani 30,000 zimekasimiwa katika bajeti hii na tani 20,000 zitanunuliwa kutokana na mikopo itakayotolewa na Taasisi za Fedha. Aidha, Bodi itasagisha tani 14,400 za mahindi katika kinu cha Iringa na kukausha tani 1,200 za shayiri ya TBL.

***Uzalishaji wa Mazao ya Bustani***

**75.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani katika mwaka 2014/2015 ikilinganishwa na mwaka 2013/2014. Mafanikio ya ongezeko la uzalishaji yametokana na ushirikiano wa Serikali na Sekta Binafsi katika kuendeleza Tasnia ya mazao hayo ikiwa ni pamoja na kuharakisha upatikanaji wa viuatilifu vya kuzuia uharibifu baada ya kuvunwa kulikookoa zaidi ya Dola za Kimarekani 330,000. Aidha, Wizara iliruhusu kutumika kwa Mwongozo wa Ukaguzi wa Mazao ya Bustani ulioharakisha ukaguzi wa mashamba. Vilevile juhudi za makusudi za kuharakisha usajili wa makampuni yanayojihusisha na Tasnia ya Bustani kwa madhumuni ya kupewa leseni ya EPZA zimefanyika.

**76.** Wizara kwa kushirikiana na *Tanzania Horticultural Association - TAHA* imejenga vituo vya kuratibu na kuhudumia wazalishaji na kuhifadhi mazao ya bustani katika mikoa ya Njombe (Nundu), Morogoro (Mlali) na Pwani (Kiwangwa). Vilevile Wizara kwa ushirikiano na Mradi wa Bustani wa *Aga Khan Foundation* katika mikoa ya Lindi na Mtwara imeongeza uzalishaji wa mazao ya bustani. Muhtasari wa hali ya uzalishaji wa mazao hayo ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani)**

| Zao | Uzalishaji 2013/2014 | Uzalishaji 2014/2015 | Matarajio 2015/2016 |
|---|---|---|---|
| Matunda | 4,416,690 | 4,574,240 | 4,737,100 |
| Mboga | 1,005,305 | 1,041,375 | 1,041,375 |
| Maua | 10,790 | 11,140 | 11,380 |
| Viungo | 8,377 | 8,609 | 8,629 |
| **Jumla** | **5,441,162** | **5,635,364** | **5,798,484** |

*Chanzo**:** Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika*

**77.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na TAHA imeanzisha Vituo vya Mafunzo kwa vitendo katika Vyuo vya Kilimo Tengeru, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Chuo cha Kilimo Kizimbani – Zanzibar ambapo mafunzo ya mbinu bora na teknolojia za kilimo kwa wakulima 1,000 na wanafunzi 500 yalitolewa. Vilevile wasindikaji zaidi ya 256 wamefundishwa mbinu bora za usindikaji na uhifadhi wa mazao ya bustani kwa kuzingatia ubora na viwango. Wasindikaji hao wameunganishwa na taasisi mbalimbali kama TFDA, TBS na BRELA kwa ajili ya uthibitisho wa viwango na ubora wa bidhaa zao pamoja na usajili wa biashara zao. Aidha, uanzishwaji wa mafunzo kwa vitendo kuhusu uzalishaji wa mazao ya bustani katika Chuo cha Kilimo Uyole mkoani Mbeya upo katika hatua za mwisho.

**78.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na TAHA itaendelea kusimamia uendeshwaji wa majengo ya kuhifadhia mazao ya bustani; kuunganisha wakulima na taasisi za fedha ili kupata mikopo yenye gharama nafuu; kuunganisha wakulima 1,015 na masoko na kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mazao ya bustani. Aidha, TAHA itatoa mafunzo kwa wazalishaji wa mazao ya bustani 10,000 na maafisa ugani 65 pamoja na kusambaza taarifa za masoko na dondoo muhimu za mazao ya bustani 3,500. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na TAHA inaendelea kujenga vituo vya kukusanyia mazao ya mboga na matunda katika mikoa ya Njombe na Iringa ili kupunguza upotevu wa mazao hayo kabla ya kufika sokoni.

***Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta***

**79. *Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta za alizeti, ufuta, karanga na mawese umeongezeka kutokana na kuimarika kwa ushiriki wa Sekta Binafsi katika sekta ndogo ya mazao hayo ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 5,545,627 mwaka 2013/2014 hadi tani 5,930,497 mwaka 2014/2015. Uzalishaji wa alizeti, ufuta na karanga ulifanyika katika mikoa ya Dodoma, Manyara, Singida, Mbeya, Katavi, Iringa, Njombe, Rukwa, Kigoma, Lindi na Mtwara; na mawese katika mkoa wa Kigoma na kuifanya sekta hiyo kuendelea kukua. Uzalishaji wa mazao hayo umeoneshwa katika **Jedwali Na. 5.** Katika mwaka 2015/2016 uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta unatarajiwa kufikia tani 6,295,112.

**Jedwali Na. 5: Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta (Tani)**

| Na. | Zao | Uzalishaji 2013/2014 | Uzalishaji 2014/2015 | Matarajio 2015/2016 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Alizeti | 2,755,000 | 2,878,500 | 2,995,500 |
| 2 | Karanga | 1,635,735 | 1,835,933 | 2,025,595 |
| 3 | Ufuta | 1,113,892 | 1,174,589 | 1,232,092 |
| 4 | Mawese | 41,000 | 41,475 | 41,925 |
| | **Jumla** | **5,545,627** | **5,930,497** | **6,295,112** |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika*

***Mpango wa Kuendeleza Kilimo Kusini mwa Tanzania (Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT)***

**80.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Mpango wa Kuendeleza Kilimo Kusini mwa Tanzania unaohusisha ubia kati ya Serikali, Sekta binafsi na wadau wa maendeleo uliendelea kutekelezwa ambapo taasisi zinazoshiriki katika ubia huo zimefikia 71 na takriban Dola za Kimarekani milioni 300 sawa na wastani wa Shilingi za Kitanzania bilioni 6 zimewekezwa katika miradi mbalimbali ya kilimo. Miradi hiyo ni pamoja na upanuzi wa kilimo cha chai katika mikoa ya Iringa (Mufindi) na Njombe kupitia kampuni ya Unilever; uboreshaji wa kilimo cha mpunga katika bonde la Kilombero kupitia Kampuni ya Kilombero *Plantation Ltd* kwa kushirikiana na kampuni za pembejeo za *SEED-Co, Syngenta na YARA*; Uzalishaji wa Mbegu bora za mazao kupitia kampuni za *Clinton Development Foundation*, *Mtanga Foods Ltd* na *Silver Lands Ltd*.

**81. *Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa ng'ombe wa nyama na vifaranga bora vya kuku umeanza kufanyika kupitia kampuni za *Mtanga Foods Ltd* na *Silverlands Ltd.* Uzalishaji wa Chakula bora cha mifugo unaendelea kupitia kampuni ya *Morogoro Agricultural Group na Silverlands Ltd.* kwa kutumia maharage ya soya yanayonunuliwa kutoka kwa wakulima wadogo. Kupitia mpango huo barabara ya Kilombero Mtanga imefanyiwa ukarabati mkubwa na sasa inapitika muda wote kutokana na ujenzi wa madaraja na matengenezo ya maeneo korofi.

**82.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Mpango wa SAGCOT utaendelea kutekelezwa kwa kuendelea kuhimiza upanuzi na uwekezaji katika uzalishaji wa mpunga, mahindi, sukari, mbegu bora za mazao, aina bora za mifugo, pamoja na uzalishaji na usambazaji wa pembejeo bora za mazao ya kilimo.

**83.*Mheshimiwa Spika,*** ili kuchochea ukuaji wa Sekta ya kilimo kupitia uwekezaji, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, Wabia wa Maendeleo, Majukwaa mbalimbali ya Kilimo na Wakulima ilianzisha Mfuko kichocheo wa SAGCOT *(SAGCOT Catalytic Trust Fund).* Mfuko huo unalenga kutoa msaada wa kifedha kwa ajili ya kuanzisha na kuwezesha kilimo biashara kwa wakulima wadogo katika Ukanda wa Kilimo wa Kusini pamoja na kutoa misaada kwa wakulima hao katika mifumo ya kibiashara. Kwa kuanzia Mfuko umekadiria

kuwa na mtaji wa kiasi cha dola za Kimarekani kati ya milioni 50 hadi 100. Hadi sasa mfuko umepokea ahadi zenye jumla ya kiasi cha dola za Kimarekani milioni 95.8. Ahadi hizo ni kutoka kwa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) Dola milioni 12.5, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID) Dola milioni 12.0, Benki ya Dunia Dola milioni 70, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Dola milioni 0.3, na Serikali ya Tanzania kiasi cha Dola milioni 1.0.

**84.*Mheshimiwa Spika,*** Mfuko umeanza kufanya kazi rasmi baada ya kusajiliwa chini ya Sheria ya Mifuko (*Trustee Incorporation Act, Cap 318 R.E 2002*). Aidha mfuko umeboresha muundo wake wa utumishi na kuajiri watumishi katika nafasi mbalimbali. Mfuko pia umeweka mfumo wa kifedha na kiuhasibu pamoja na utaratibu wa utoaji wa ruzuku na mikopo ya fedha kwa walengwa. Miongozo na taratibu zinazoratibu uendeshaji wa mfuko na mahusiano kati ya wakulima wadogo na taasisi au kampuni zitakazopatiwa ufadhili na mfuko imeandaliwa. Vilevile Mfuko umeanza majaribio kwa kutambua miradi michache ya uwekezaji kwa lengo la kuangalia mfumo bora wa kutekeleza miradi ya namna hiyo. Aidha, utaratibu wa kupata Kamati ya Uwekezaji umeanza na zoezi litakamilika mwishoni mwa mwezi Mei 2015. Kamati hii itakuwa na jukumu la kupokea na kupitia maombi ya kupatiwa ruzuku kutoka kwa taasisi, kampuni na wadau mbalimbali katika ukanda wa SAGCOT kwa ajili ya ufadhili wa mfuko.

**85.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Mfuko unalenga kukuza mtaji wa hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 100; kutoa msaada wa kifedha kwa ajili ya kuanzisha na kuwezesha kilimo biashara kati ya wakulima wadogo na wawekezaji wakubwa wapatao 1,000 katika ukanda wa SAGCOT. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa watumishi wapya wa Mfuko kuhusu programu ya SAGCOT, taratibu na kanuni zinazosimamia uendeshaji wa mifuko hususan mifuko inayolenga uwezeshwaji kwa wakulima wadogo. Mfuko pia utapitia sera, sheria, kanuni na taratibu zilizoanzisha Mfuko na kutoa mapendekezo ya maboresho ili kukidhi haja na mahitaji ya walengwa na wadau mbalimbali wa mfuko.

***Umwagiliaji***

**86.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilipanga kuboresha skimu 78 za umwagiliaji pamoja na maghala ya kuhifadhi mpunga kupitia BRN na kuendelea kushirikiana na Halmashauri katika kusimamia ujenzi wa miradi ya umwagiliaji. Vilevile, mradi wa PHRD ulilenga katika kujenga uwezo wa wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji wa zao la mpunga.

***Miradi ya Umwagiliaji Kupitia Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa***

**87.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia BRN imeendelea kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 19 zenye jumla ya hekta 9,531 zenye wanufaika 69,681. Skimu hizo ni Mvumi (Kilosa), Msolwa Ujamaa (Kilombero), Mkula (Kilombero), Rudewa (Kilosa), Siginali (Kilombero), Sakalilo (Sumbawanga), Ipatagwa (Mbarali), Kapyo (Mbarali), Chang'ombe, Motombaya, Kongolo Mswiswi, Gwiri, Mwendamtitu (Mbarali), Cherehani Mkoga (Iringa), Idodi (Iringa), Mapogoro (Iringa), Ugala, Karema, Mwamkulu (Mpanda). Hadi kufikia Machi 2015 ujenzi huo ulifikia asilimia 40. (**Kiambatisho Na. 2).**

**88.*Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuboresha skimu hizo ili ziweze kujiendesha kibiashara, Wizara iliingia mikataba na watoa huduma binafsi ili waweze kujenga uwezo wa wamwagiliaji kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia 2014/2015. Hadi sasa, watoa huduma binafsi wawili ambao ni *Rural Urban Development Initiatives (RUDI)* na *UNIQUE Consortium* wamepewa mkataba wa kutoa huduma katika skimu 30 za umwagiliaji katika wilaya za Kyela, Mbarali na Iringa. Aidha, maghala manane katika skimu nane za umwagiliaji za Ngana na Makwale (Kyela), Magozi na Tungamalenga (Iringa Vijijini) na Mbuyuni Kimani, Ipatagwa, Kongolo Mswiswi na Motombaya (Mbarali) yamefanyiwa usanifu na yapo katika hatua ya kuwapata wakandarasi.

**89.*Mheshimiwa Spika,*** mafunzo kwa wakulima viongozi kutoka skimu 10 za umwagiliaji kuhusu utabiri wa viwavijeshi na matumizi sahihi ya viuatilifu yamefanyika; mafunzo kwa wakulima viongozi 56 kutoka skimu tatu za umwagiliaji (WIA Mahango, Lyanyula, Igumbilo Isitu) yaliyohusu kilimo bora cha mpunga yamefanyika; mafunzo ya uendeshaji na matunzo ya skimu 12 za umwagiliaji yalitolewa kwa wakulima 60; wataalam wa skimu 12; wataalam wa umwagiliaji wa Wilaya wanne; na Maafisa Kilimo Umwagiliaji na Ushirika wanne waliotoka katika skimu za Mkula; Siginali; Mang'ula Youth; Njage na Msolwa Ujamaa; (Kilombero) Kiroka na Tulo Kongwa (Morogoro Vijijini), Mvumi na Lumuma (Kilosa) na Mkindo Kigugu na Mbogo (Mvomero). Vilevile, mafunzo yalitolewa kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya wakulima vijana 21 kutoka skimu 7 za umwagiliaji juu ya utumiaji wa pumba za mpunga katika kutengeneza mkaa.

**90.*Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kuboresha skimu 78 katika Mfumo wa BRN kwa kufanya mapitio ya usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni za kujenga skimu na maghala 58 (**Kiambatisho Na. 3**); kukarabati miundombinu ya skimu za umwagiliaji 20; ujenzi na ukarabati wa maghala 20 (**Kiambatisho Na. 4**); kupata

mtoa huduma za kitaalamu kutoka sekta binafsi kwa ajili ya skimu 48 na kuwezesha watoa huduma binafsi waliopo kwenye skimu 30.

***Miradi Mingine ya Umwagiliaji***

**91.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea na ujenzi wa skimu ya Itete yenye hekta 1,000 na wanufaika 5,000 ambapo hadi kufikia Machi 2015, ujenzi wa skimu hiyo ulikuwa umefikia asilimia 75. Ujenzi wa banio, uchimbaji na ujenzi wa mifereji mikuu yenye urefu wa kilometa 6.63 na uchimbaji wa mifereji ya kati yenye urefu wa kilometa 12.78 umefanyika. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya iliendelea na usimamizi wa ujenzi wa skimu za umwagiliaji 45 zenye hekta 11,140 na wanufaika 55,700 (**Kiambatisho Na. 5**) kupitia Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji Ngazi ya Wilaya (DIDF) ambapo hadi Machi 2015, ujenzi ulifikia asilimia 46. Ukarabati wa skimu 15 za umwagiliaji zenye eneo la hekta 4,186 unaogharamiwa kupitia Mfuko wa Pamoja wa Serikali ya Tanzania na Japan umekamilika. Aidha, Wizara iliendelea kujenga uwezo katika skimu 30 za umwagiliaji kwa kushirikisha watoa huduma binafsi katika Wilaya za Kyela, Mbarali na Iringa kutoa mafunzo mbalimbali ya kuwawezesha wakulima kuendesha kilimo cha kibiashara katika skimu hizo na kutoa mafunzo ya kilimo shadidi cha mpunga kwa wakulima wadogo wapatao 1,350 kutoka katika skimu 50.

**92.*Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mradi wa *Feed the Future* chini ya ufadhili wa USAID Serikali inakarabati Skimu ya umwagiliaji ya Dakawa yenye eneo la hekta 2,000 na kujenga hekta nyingine 500 kwa gharama ya Dola za Kimarekani 15,526,965. Vilevile Serikali inafanya upembuzi yakinifu kwa skimu za Kisegese, Udagaji, Mugugwe na Mpanga Ngalamila zenye jumla ya hekta 43,000 katika bonde la mto Kilombero.

**93.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu kwenye skimu 20 (10 za DASIP na 10 za kimkakati) na mabwawa madogo ya Lwanyo (Mbarali), Dongobesh (Mbulu) na Inala (Tabora).

***Mradi wa Policy for Human Resource Development (PHRD)***

**94.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa PHRD ambao ulilenga kuongeza tija na uzalishaji katika skimu 20 za umwagiliaji kwa kuzingatia mnyororo wa thamani **(Kiambatisho Na. 6).** Hadi Machi 2015, mafunzo kwa wakulima wadogo 1,350 kuhusu Kilimo Shadidi yametolewa. Vilevile, mafunzo yametolewa kwa wataalam wa umwagiliaji na maafisa ugani 45, viongozi wa skimu na wakulima viongozi 454 kutoka katika skimu 20 za umwagiliaji. Mafunzo hayo yalihusu usimamizi na uendeshaji wa maghala; upatikanaji wa masoko na mikopo kutoka taasisi za fedha na uendeshaji wa vikundi vya umoja wa wamwagiliaji. Aidha, Mradi huo unalenga kujenga maghala 6 katika skimu za Lekitatu, Uturo, Mombo,

Bagamoyo, Mkindo na Mkula na taratibu za kuwapata wakandarasi zinaendelea.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itajenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji na maghala katika skimu 20; kujenga na kukarabati mabwawa ya kuvuna na kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji; kuhimiza matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi na kuhamasisha matumizi ya maji chini ya ardhi; kujenga uwezo wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Taasisi zinazohusika na umwagiliaji katika ngazi za Kitaifa, Mkoa, Halmashauri na Wakulima katika usimamizi na uendeshaji endelevu wa miradi ya umwagiliaji na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika umwagiliaji.

***Zana za Kilimo***

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imehamasisha Sekta Binafsi kuingiza nchini zana bora za kilimo kwa lengo la kuongeza upatikanaji wake. Matrekta makubwa 1,212 yaliingizwa nchini mwaka 2014 ikilinganishwa na matrekta makubwa 916 yaliyoingizwa mwaka 2013. Aidha, Sekta Binafsi iliingiza matrekta madogo ya mkono 393.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia mradi wa PHRD, imenunua na kusambaza zana za kilimo zikiwemo zana za kuvuna mpunga (*Rice combine harvesters*) 64, mashine za kupura mpunga (*Threshers*) 36 na mashine za kukata mpunga (*Reapers*) 16 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kupunguza upotevu na harubu katika uvunaji wa zao la mpunga kwenye skimu 14 za umwagiliaji zilizopo katika Halmashauri 12 za Wilaya za Babati (Mawemairo), Mbarali (Ipatagwa, Uturo na Mbuyuni), Meru (Lekitatu), Kilombero (Mkula), Mwanga (Kivulini), Hai (Musa Mwinjanga), Songea (Nakahuga), Iringa Vijijni (Magozi), Kilosa (Kilangali), Mvomero (Mkindo), Korogwe (Mombo) na Bagamoyo (Bagamoyo BIDP).

**98.** Aidha, mafunzo ya matumizi bora ya mashine hizo yanaendelea kutolewa ambapo waendesha mitambo 242, maafisa zana 28, maafisa umwagiliaji 14, maafisa ugani 14, wahandisi kilimo 8 na viongozi wa skimu 28 katika Halmashauri husika watakuwa wamepatiwa mafunzo ifikapo Juni, 2015.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** zana za kilimo za kukata na kupura mpunga zimesambazwa kwa ajili ya mafunzo na uzalishaji kwenye vyuo vya kilimo na vituo vya utafiti vya Ukiriguru, Mtwara, Igurusi, Ilonga na Uyole. Chini ya utaratibu wa ASDP, Wizara imesambaza mashine sita za kupandikiza mpunga kwenye skimu za umwagiliaji za Magozi (Iringa), Mkindo (Mvomero), Mkula (Kilombero), Ipatagwa na Uturo (Mbarali) na Mvumi (Kilosa) ili kuongeza uzalishaji. Mashine hizi zina uwezo wa kupanda miche ya mpunga eka tano hadi saba kwa siku

ikilinganishwa na siku tatu kwenye eka moja za upandaji wa mkono. Skimu za umwagiliaji zilizopata mashine hizi zipo chini ya Mfumo wa BRN.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Serikali ilifanya mazungumzo na Serikali ya Poland ya kupata mkopo kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kuunganisha matrekta na zana za kilimo nchini. Hatua iliyofikiwa ni utayarishaji wa Makubaliano ya Awali unaofanywa na SUMA JKT kwa niaba ya Serikali na *Pol-Mot Holdings S.A.* inayomiliki kampuni ya *Ursus* kwa niaba ya Serikali ya Poland.

***Uendelezaji wa Kilimo Hifadhi***

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuendeleza matumizi ya teknolojia ya Kilimo Hifadhi imeunda Kikosi Kazi cha kitaifa cha Kuendeleza Kilimo Hifadhi nchini. Wajibu wa Kikosi Kazi ni kubuni mikakati na miradi ya kuendeleza Kilimo Hifadhi hapa nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mtandao wa Kilimo Hifadhi Afrika (*Africa Conservation Tillage Network - ACTN*) imekusanya takwimu za hali halisi ilivyo katika kanda za Nyanda za Juu, Kati, Kaskazini na Kusini kubaini wakulima, vikundi na taasisi zinazoendeleza teknolojia ya Kilimo Hifadhi. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na ACTN imefanya mafunzo ya matumizi ya zana za Kilimo Hifadhi na kuanzisha majaribio kwa vikundi kwenye wilaya za Iringa Vijijini, Longido, Bahi na Njombe. Aidha, Wizara imepeleka zana za kilimo hifadhi za kupandia zinazokokotwa na trekta la mkono zitakazotumika katika kutoa mafunzo katika vyuo vya kilimo na vituo vya utafiti vya Uyole, Ilonga na Igurusi.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuongeza upatikanaji na matumizi ya zana bora za kilimo nchini kwa kununua na kusimika mashine za kusindika mpunga katika skimu 14 za umwagiliaji. Pia Wizara itaandaa mapendekezo ya Sheria ya Zana za Kilimo itakayosimamia na kulinda ubora wa zana, mikataba na mazingira.

***Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo***

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) ilipanga kutumia Shilingi 6,382,800,000 ili kutoa mikopo ya zana na pembejeo za kilimo na mifugo. Hadi mwezi Aprili 2015 AGITF imepata na kutumia Shilingi 5,182,113,824.50 na kutoa mikopo ya matrekta mapya 94 na pembejeo za kilimo na mifugo kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 6.** Katika mwaka 2015/2016 Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo itaendelea kutoa mikopo ya zana na pembejeo za kilimo na mifugo.

**Jedwali Na. 6: Mikopo Iliyotolewa Katika Kipindi cha 01/07/2014 hadi 30/03/2015**

| Aina ya mkopo | Utekelezaji wake | | Thamani ya mikopo (Tshs) |
|---|---|---|---|
| | Lengo | Halisia | |
| Matrekta mapya makubwa | 84 | 94 | 4,015,386,824.50 |
| Pembejeo mchanganyiko | 50 | 21 | 949,700,000.00 |
| Matrekta ya mikono | 23 | 1 | 7,242,000.00 |
| Nyenzo za usindikaji | 8 | 2 | 57,000,000.00 |
| Nyenzo za umwagiliaji | 4 | 3 | 142,800,000.00 |
| Mashine za kuvuna | 2 | - | 0 |
| Kukarabati matrekta | - | 1 | 9,985,000.00 |
| **Jumla** | | | **5,182,113,824.50** |

*Chanzo: Mfuko wa Taifa wa Pembejeo*

***Udhibiti wa Visumbufu vya Mazao na Mimea***

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaondolea kero wakulima katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, kutoa na kuingiza mazao nje ya nchi, Wizara imeendelea kudhibiti visumbufu vya milipuko katika maeneo yaliyovamiwa na nzige, panya na kwelea kwelea na visumbufu vipya kwenye maeneo yaliyotoa taarifa. Aidha, elimu imetolewa kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu na udhibiti husishi kwa kutumia teknolojia zilizopo katika taasisi za utafiti, taasisi zisizokuwa za kiserikali na miradi mbalimbali. Vilevile Wizara imeendelea kukagua mazao yanayoingia nchini na yanayotoka nje ya nchi na kutoa elimu kwa wakaguzi. Utekelezaji wa kazi hizo ulikuwa kama ifuatavyo;

***Kudhibiti visumbufu vya Milipuko***

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara ilidhibiti makundi ya nzige katika mbuga za Katavi, Ziwa Rukwa, Malagarasi na Wembere. Wizara pia ilikabiliana na milipuko ya panya katika Wilaya za Kilosa, Ruangwa, Mvomero, Handeni, Kilwa, Iringa Vijijini, Songea na Pangani. Milipuko ya viwavijeshi imetokea na kudhibitiwa katika wilaya za Kilwa, Ruangwa na Babati. Aidha, wataalam wanaendelea kuchunguza taarifa za kutokea milipuko ya kwelea kwelea katika wilaya za Igunga, Nzega, Shinyanga Vijijini na Shinyanga Manispaa.

***Kutoa elimu ya udhibiti wa Visumbufu***

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilitoa mafunzo juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu kwa wadau 199 kutoka katika Wilaya za Mwanza, Masasi, Mtwara, Shinyanga Manispaa, Shinyanga Vijijini, Kishapu, Msalala, Ushetu, Nyamagana,

Magu, Sengerema, Misungwi, Ilemela, Ukerewe, Musoma Vijijini, Butiama, Rorya, Tarime, Bunda, Serengeti, Temeke, Kinondoni na Ilala.

***Udhibiti husishi na Zahanati za Afya ya Mimea***

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kueneza elimu ya Udhibiti Husishi nchini kwa kukusanya teknolojia za Udhibiti Husishi katika taasisi za utafiti, taasisi zisizokuwa za kiserikali na miradi mbalimbali inayojihusisha na Kilimo katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Mara, Dodoma na Morogoro. Aidha, mafunzo ya Udhibiti Husishi yalitolewa kwa wataalam wa Kilimo na wakulima 275 kwenye zao la pamba katika mikoa ya Mwanza, Simiyu na Singida.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na *Center for Agricultural and Bioscience Institute (CABI)* inatekeleza Mradi wa *Plantwise* kwa lengo la kudhibiti visumbufu vya mimea kwa kuanzisha Zahanati za Afya ya Mimea (*plant clinics*). Zahanati za Afya ya Mimea imetokana na dhana ya Zahanati za Binadamu na Wanyama, ambapo kunakuwa na Zahanati yenye vifaa vya uchunguzi na utambuzi pamoja na wataalam/Madaktari wenye ujuzi wa tiba ya mimea. Mkulima hupeleka mmea/mimea iliyougua au kuathiriwa na visumbufu katika zahanati iliyokaribu naye na kupewa ushauri. Huduma hii hutolewa bure kwa wakulima. Endapo daktari ameshindwa kutambua tatizo la mmea hupeleka katika vituo vya rufaa vya utafiti kwa hatua zaidi za utambuzi.

**109.** Wizara imetoa mafunzo kwa madaktari 86 wa mimea na zahanati 43 zimefunguliwa katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Dar es salaam, Morogoro, Dodoma, Manyara na Iringa. Vilevile mafunzo yametolewa kwa wataalam na wakulima 2,500 kuhusu namna ya kuchunguza mimea na kutambua matatizo ya visumbufu vinavyoshambulia mazao katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

***Kudhibiti visumbufu Kibiolojia***

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kudhibiti visumbufu kibiolojia kwa kuimarisha uwezo wa kituo cha Kibaha. Pia, Wizara imekamilisha ujenzi wa maabara yenye uwezo wa kuzalisha wadudu rafiki wa aina mbalimbali kulingana na aina ya visumbufu vya mimea na magugu vitakavyojitokeza. Vilevile kituo kimeendelea na utunzaji wa vizazi vya wadudu kwa ajili ya kuzalisha kwa wingi na kuwasambaza endapo milipuko ya visumbufu itajitokeza. Wadudu hao ni wa kudhibiti magugu maji wajulikanao kama mbawakavu; wadudu wa kudhibiti kidung'ata wa muhogo; na wadudu wa kudhibiti wadudu wanaoshambulia mboga.

***Udhibiti wa visumbufu vipya***

**111. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea kudhibiti visumbufu vipya ambapo gugu hatari lijulikanalo kama *Parthenium spp.* lilidhibitiwa katika mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Aidha, wakulima 590 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Lindi, Mbeya, Morogoro, Pwani, Ruvuma, Tabora na Tanga walipatiwa mafunzo ya udhibiti wa nzi waharibifu wa matunda kwa kutumia mbinu za Udhibiti Husishi wa Visumbufu vya Mimea.

**112. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwendelezo wa kudhibiti visumbufu vipya, Wizara imeingiza lita 300 za kivutia wadudu aina ya *methyl eugenol* na kuzisambaza kwa wakulima katika wilaya zinazolima matunda na mboga kwa wingi. Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) na Taasisi ya *Royal Museum for Central Africa*, Tervuren, Ubelgiji imetayarisha nakala 5,000 za kitabu cha mwongozo kwa maafisa kilimo na wakulima kinachohusu mpango wa kudhibiti nzi waharibifu wa matunda kwa Tanzania kwa madhumuni ya kupunguza tatizo hilo.

**113. *Mheshimiwa Spika,*** maeneo ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mara, Simiyu, na Mwanza yameripotiwa kutokea kwa ugonjwa mpya wa mahindi (*Maize Lethal Necrosis Disease – MLND*) ulioripotiwa kwa mara ya kwanza nchini Kenya mwaka 2011. Ugonjwa huo unasababishwa na virusi wa aina mbili ambao hushambulia kwa wakati mmoja. Wizara inaendelea kutoa elimu ya kuutambua na hatua za kuchukua punde shamba linapobainika kuathiriwa na ugonjwa huu. Aidha, uhamasishaji kwenye mikoa ishirini na mafunzo kuhusu ugonjwa yametolewa kwa maafisa kilimo 130 wa mikoa ya Kanda ya Ziwa. Wizara inaandaa mapendekezo ya sheria na kanuni za udhibiti wa ugonjwa huo. Aidha, Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) limekubali kufadhili mradi wa uelimishaji wa wakulima kuhusu ugonjwa huo katika nchi za Afrika Mashariki.

***Ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nchini***

**114. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kukagua mazao yanayoingia nchini na yanayotoka nje ya nchi pamoja na kuboresha vituo vya mipakani na kutoa elimu kwa wakaguzi. Jumla ya tani 175,289.51 za mazao mbalimbali ziliingizwa nchini na tani 714,372.40 zilisafirishwa nje ya nchi. Vyeti 5,516 vya Usafi wa Mazao na vyeti 635 vya kuingiza mazao nchini vilitolewa. Aidha, vifaa na vitabu vya hati ya usafi wa mimea vilinunuliwa na kupelekwa katika vituo vya ukaguzi vya mipakani.

**115. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara itatathmini vituo 40 vya ukaguzi mipakani ili kudhibiti ubora wa mazao yanayosafirishwa na yanayoingia nchini. Pia itadhibiti milipuko ya nzige, kweleakwelea, panya, viwavijeshi na magonjwa ya mimea. Aidha, Wizara itaandaa na kueneza

teknolojia ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao ya mahindi, mpunga, pamba, kahawa, nyanya, vitunguu na viazi katika Halmashauri 20.

***Huduma za Ugani***

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa kuboresha uenezaji wa teknolojia katika kilimo kwa kutumia mbinu shirikishi jamii katika kilimo, ikiwa ni pamoja na matumizi ya Shamba Darasa. Mashamba hayo ni njia ya kuwawezesha wakulima kujifunza kanuni za kilimo bora ikijumuisha maandalizi ya shamba, kutunza rutuba ya udongo, matumizi ya mbegu bora, viuatilifu, mbolea, zana bora na matumizi endelevu ya maji**.** Kazi zilizofanyika ni pamoja na:

***Kuanzisha na Kuwezesha Mashamba Darasa***

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 kupitia mradi wa EAAPP jumla ya mashamba darasa 166 yalianzishwa kwenye zao la mpunga kwa kushirikisha wakulima 4,500 wakiwemo wanaume 2,950 na wanawake 1,550. Aidha, vishamba vya mfano 72 vya zao la mpunga vilianzishwa na kushirikisha wakulima 72 kati ya hao, wanaume ni 40 na wanawake ni 32, na wataalam 25 kutoka vijiji 18. Vilevile vishamba vya mfano tisa vya zao la ngano vilianzishwa na kushirikisha wakulima 225 kati ya hao, wanaume ni 158 na wanawake ni 67, na wataalam tisa kutoka Halmashauri saba zinazozalisha ngano ambapo mbinu bora za uzalishaji wa mazao hayo zilionyeshwa.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mradi wa PHRD Wizara ilisaidia kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga kwa wakulima walioko kwenye Skimu 20 za umwagiliaji. Wizara pia ilitoa mafunzo katika uendeshaji wa mashamba darasa na stadi za maisha kwa wakulima 300 wa zao la mpunga wakiwemo wanaume 187 na wanawake 113 mkoani Iringa. Aidha, ziara za mafunzo na kubadilishana uzoefu katika kilimo zilifanyika katika Kanda ya Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini kwa wakulima 1,000 kati ya hao, wanaume ni 587 na wanawake ni 413 kutoka katika skimu hizo ambapo kila skimu wakulima 50 walinufaika. Mafunzo hayo yamewezesha wakulima kuzalisha zao la mpunga kutoka wastani wa tani mbili kwa hekta mwaka 2011/2012 hadi wastani wa tani saba kwa hekta mwaka 2014/2015.

***Mafunzo kwa wataalam na wakulima wawezeshaji***

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilitoa mafunzo ya kilimo bora kwa mazao ya mpunga, muhogo na ngano kwa wakulima wawezeshaji 2,075 kati ya hao, wanaume ni 1,106 na wanawake ni 969; na maafisa ugani 568 wakiwemo wanaume 430 na wanawake 138 walishiriki mafunzo ya kanuni za kilimo bora na kilimo biashara katika mazao hayo ili waweze kufundisha wakulima wengine katika maeneo yao. Mfano: Mkulima Bwana Katoto wa Wami Dakawa amefundisha kikundi cha wakulima 27 juu ya kanuni za uzalishaji wa zao la mpunga. Kijana Seva Sikabenga wa kijiji cha Ikoho mkoani Mbeya amefundisha

wakulima vijana 30 juu ya kanuni za uzalishaji wa zao la ngano. Kikundi cha Kasisa chenye wakulima 11 wamefundisha wakulima wengine 68 na Kikundi cha Nyakasungwa chenye wakulima 25 wamefundisha wakulima 120 kuhusu kilimo bora cha mpunga; na Kikundi cha Ukerewe chenye wakulima 30 wamefundisha wakulima 173 kuhusu kilimo bora cha muhogo. Ni matarajio kwamba iwapo kila mmoja wa wakulima wawezeshaji 2,075 atafundisha wakulima watano (5) tutapata wakulima 20,375 katika vijiji vya mradi watakaofahamu kanuni za kilimo bora.

***Kuimarisha vikundi vya wakulima na kuwajengea uwezo wa kuwa wajasiriamali***

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo ya kilimo biashara kwa zao la mpunga na muhogo yalitolewa kwa wakulima na vijana kwa lengo la kuwajengea uwezo ili wazalishe kwa kuzingatia mahitaji ya soko. Wakulima na vijana hao waliunganishwa na watoa huduma kama vile NMB, SIDO, RUDI na MVIWATA katika kupata leseni za biashara, mikopo, usindikaji, masoko na pia kuimarisha vikundi vya wakulima. Wakulima vijana wa mpunga 206 na Wataalam 18 kutoka vijiji 18 vya halmashauri za wilaya za Mbarali, Kyela, Sengerema, Bunda, Kilombero na Mvomero; na wakulima wa muhogo 30 na wataalam 19 kutoka Ukerewe, Bunda, Mtwara Vijijini, Tandahimba na Bagamoyo walipatiwa mafunzo.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha vikundi vya wakulima na kuwajengea uwezo wa ujasiriamali, mafunzo ya kilimo biashara na ujasiriamali yamesaidia wakulima kuhamasika kuunda vikundi na kuanza kilimo cha kibiashara. Kikundi cha Jikwamue cha Wami Dakawa wamejiunga na kujisajili kama *Community Based Organisation (CBO)* na walikopeshwa Shilingi milioni 129 na benki ya CRDB kwa ajili ya kuzalisha mpunga na kurudisha mkopo katika mwaka 2013/2014 na kukopa tena Shilingi milioni 187. Kikundi pia kimeingia mkataba na Kampuni ya Mbegu ya TANSEED International ya Morogoro wa kuzalisha tani 112 za mpunga zenye thamani ya Shilingi milioni 86.6.

***Usambazaji wa teknolojia kwa wakulima***

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza kasi ya usambazaji wa teknolojia bora za kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima, Wizara imewezesha mashirikiano na wadau wengine kutoka sekta ya umma na binafsi kama vile Wizara ya Viwanda na Biashara, Serikali za Mitaa, NMB, SIDO-MUVI, Oxfam, RUDI, MVIWATA, NURU Infocom, MIVARF na Radio za Kijamii. Zaidi ya wakulima 50,000 walipata taarifa juu ya teknolojia za uzalishaji wa mazao kupitia luninga, redio, maonesho ya sinema, machapisho, mikutano ya wadau na maonesho ya kitaifa ya kilimo. Jumla ya vipindi vya redio 102 vilirushwa hewani kupitia TBC (32), redio binafsi za FM (70) na vipindi vya luninga 16. Jumla ya watazamaji 6,565 kati ya hao, wanaume ni 3,598 na wanawake ni 2,967 walishiriki katika maonesho ya sinema katika vijiji 87 kwenye Halmashauri za Wilaya 13.

**123.** Aidha, machapisho ya vijarida vyenye mada za Kilimo Bora cha Mpunga wa Mabondeni; na Visumbufu vya Mpunga na Udhibiti wake viliandaliwa. Pia vipeperushi vyenye mada za Kilimo Bora cha Mpunga; na Kilimo Bora cha Muhogo vilichapishwa na kusambazwa kwa wakulima. Aidha Wizara iliandaa mwongozo wa utoaji huduma za ugani nchini. Vilevile Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (WARCs) 322 vimejengwa katika Halmashauri 106 kwenye mikoa 20. Kati ya hivyo vituo 224 vimekamilika na vimeanza kufanya kazi ya kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji, mashamba ya majaribio, kutoa huduma kwa mifugo na matumizi ya zana za kilimo.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ilitoa mafunzo kuhusu utoaji wa huduma za ugani kwa njia ya mtandao na simu za kiganjani kwa lengo la kuwawezesha wataalam wa ugani na wakulima kupata taarifa za kilimo na masoko. Washiriki wa mafunzo walikuwa 67, wakiwemo maafisa ugani 28 ambao kati yao 11 walitoka katika WARCs na wakulima 39 kutoka Halmashauri za Wilaya za Kilosa, Kilombero, Mvomero, Kyela, Mbarali, Sengerema, Bunda, Mkalama na Lushoto. Mafunzo haya yalihusu namna ya kutafuta taarifa kwenye mtandao, utafutaji wa masoko na utunzaji wa kumbukumbu. Mwishoni mwa mafunzo washiriki walikubaliana kuunda kundi la kupeana taarifa za kilimo na masoko kwa njia za kielektroniki.

***Maonesho ya Kilimo***

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na *Tanzania Agricultural Society* (TASO) iliratibu maonesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) yaliyofanyika kitaifa Kanda ya Kusini kwa mara ya kwanza katika uwanja wa Maonesho ya Kilimo wa Ngongo Mkoani Lindi. Kwa ngazi ya Kanda, maonesho hayo yalifanyika kwenye viwanja vya Nzuguni–Dodoma, J. K. Nyerere–Morogoro, Themi–Arusha, J. B. Mwakangale–Mbeya, Ipuli–Tabora na Nyamhongolo–Mwanza. Katika mwaka 2015/2016 Maonesho ya Kilimo Kitaifa yataendelea kufanyika katika viwanja vya Ngongo mkoani Lindi. Pia kanda mbalimbali zitaendelea kufanya maonesho hayo. Aidha, Wizara iliratibu Siku ya Chakula Duniani iliyofanyika mkoani Katavi. Katika mwaka 2015/2016 Maonesho ya Siku ya Chakula Duniani yatafanyika mkoani Simiyu.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara itavijengea uwezo vyuo vya wakulima vya Inyala (Mbeya), Ichenga (Njombe), Bihawana (Dodoma) na Mkindo (Morogoro) kwa kuvipatia vitendea kazi bora. Wizara pia itaendeleza ukarabati wa Chuo cha Wakulima Mkindo ili kukiongezea uwezo wa kutoa mafunzo kwa wakulima wengi zaidi.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuratibu maombi ya kibali cha ajira za maafisa ugani na Wataalam wa Kilimo

na Umwagiliaji ikiwa ni utekelezaji wa mkakati wa Serikali wa kuwa na Afisa Ugani mmoja katika kila kijiji ifikapo mwaka 2015. Hadi Mei 2015, idadi ya maafisa ugani katika kata na vijiji ni 10,089 ikilinganishwa na mahitaji ya maafisa ugani 15,853. Katika mwaka 2015/2016 Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI itaendelea kuratibu ajira ya watumishi 5,000 wa fani mbalimbali kulingana na upatikanaji wa kibali cha ajira.

***Utafiti***

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza aina za mbegu bora za mazao ya kilimo, Wizara katika mwaka 2014/2015 iliidhinisha aina mpya 48 za mbegu za mazao zikiwemo za mahindi (4); ngano (3); mbaazi (4); kunde (2); muhogo (4); ufuta (1); korosho (24); miwa (5); na pamba (1) zilizogunduliwa na Taasisi za Utafiti za Wizara (**Kiambatisho Na. 7**). Tanzania imekuwa nchi ya kwanza Afrika kutoa mbegu za korosho chotara (*hybrid*). Aidha, Wizara iliidhinisha aina mpya 17 za mbegu zikiwemo za mtama (2); mahindi (12); na tumbaku (3) zilizogunduliwa na sekta binafsi.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia vituo vya utafiti imezalisha jumla ya kilo 14,196 za mbegu mama ili kukidhi mahitaji ya Wakala wa Mbegu za Kilimo kwa ajili ya kuzalisha mbegu za msingi zinazotumiwa na kampuni za mbegu kuzalisha mbegu zilizoidhinishwa ili kutumiwa na wakulima. Mbegu mama zilizozalishwa ni pamoja na jamii ya nafaka kilo 1,548; jamii ya mikunde kilo 11,000; jamii ya mafuta kilo 288; na kilo 1,360 za pamba. Aidha, Wizara imeendelea kutoa na kusambaza kwa wakulima pingili za muhogo 2,691,000, marando ya viazi vitamu 2,948,800, miche 17,000 ya viazi mviringo, na miche ya migomba 10,500. Pia Wizara imezalisha na kusambaza miche ya kubebeshwa 616,500 ya korosho, miparachichi 2,500 na mapesheni 1,500.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika Mkoa wa Kagera iliendelea kutoa elimu kwa wakulima wa zao la migomba katika Kanda ya Ziwa. Hadi kufikia Aprili 2015, mimea iliyougua imeng'olewa kwa asilimia 85 hadi asilimia 98 katika maeneo yanayolima zao hilo. Aidha, utafiti unaoendelea umebaini uwepo wa mimea mitano ikiwemo Mnyaa na Mwarobaini inayotarajiwa kutumika kama madawa asilia ya udhibiti wa ugonjwa wa ubwiri unga katika zao la korosho. Pia Mbegu 4 zinazovumilia magonjwa ya muhogo ya michirizi ya kahawia na Batobato kali zimegunduliwa na kuidhinishwa na Wizara mwezi Februari mwaka huu. Utafiti kuhusu ugonjwa hatari wa mahindi (MLND) unaendelea kufanyika. Vilevile uzalishaji wa wadudu rafiki kwa ajili ya kupambana na wadudu waharibifu katika mazao ya mboga ulifanyika na wadudu hao rafiki walisambazwa katika wilaya za Arumeru, Hai na Moshi vijijini.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutumia bioteknolojia, Vituo vya Utafiti vimeweza kubaini aina mbalimbali za virusi vya magonjwa ya batobato kali na

aina tatu mpya za michirizi ya kahawia ya zao la muhogo. Kwa kutumia matokeo hayo ramani zinazoonyesha mtawanyiko wa magonjwa zimetengenezwa na kusambazwa katika Wilaya zote za mikoa ya Kanda ya Ziwa (Mara, Mwanza, Geita na Kagera). Vilevile mmea pori unaojulikana kwa jina la Mtambakuzimu unaohifadhi virusi vya ugonjwa wa batobato kali na molekuli za DNA kwenye zao la muhogo ambazo huongeza ukali wa virusi vya ugonjwa huo umegunduliwa. Utafiti wa mbinu za kuzalisha miche bora kwa njia ya chupa kwa mazao ya muhogo, mizabibu, viazi mviringo, viazi vitamu, mananasi, migomba, mikorosho, vanila, pareto, chai na matunda ya asili unaendelea na zaidi ya miche 500 ya mazao hayo imezalishwa.

***Utafiti kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo – ASDP***

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia programu ya ASDP, Wizara imeendelea kuimarisha usambazaji wa teknolojia zinazoendana na kanuni za uzalishaji wa mazao kwa walengwa ambapo majarida ya kisayansi 143 yametolewa na kusambazwa katika Wilaya mbalimbali. Pia, majarida mawili ya habari za mafanikio ya teknolojia za muhogo na mpunga ambazo wakulima walizipokea na kuzikubali yameandaliwa. Aidha, jumla ya miche bora ya kahawa 1,014,671 ilizalishwa na kusambazwa katika Wilaya za Moshi, Mbinga, Bukoba, Mbozi na Tarime.

***Programu ya Kilimo ya Kuendeleza Tija na Uzalishaji Mashariki mwa Afrika (Eastern Africa Agricultural Productivity Programme – EAAPP)***

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mradi wa EAAPP, Wizara inaendelea kukiboresha kituo cha KATRIN wilayani Kilombero, kuwa Kituo Mahiri cha Mpunga Mashariki mwa Afrika. Ukarabati wa miundombinu umefikia asilimia 74. Aidha, ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji wa mashamba ya utafiti umekamilika kwa asilimia 97. Pia ukarabati wa miundombinu ya umeme katika kituo cha utafiti cha Dakawa umefikia asilimia 50 ikiwa ni pamoja na kuezeka upya kwa ofisi ya utawala.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuboresha rutuba ya udongo, utafiti ulifanyika kwenye skimu ya umwagiliaji ya Mkula (Kilombero) ambapo sampuli za udongo zilikusanywa, kufanyiwa uchambuzi na kutolewa ushauri juu ya matumizi bora ya mbolea pamoja na kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa mradi wa PHRD, Wizara kupitia Vituo vya Utafiti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mwongozo wa mafunzo ya kilimo shadidi cha mpunga na kusambazwa kwenye Halmashauri zinazotekeleza mradi. Aidha, taarifa za mizania kwa kilimo shadidi cha mpunga zimeonesha kuwa faida inayopatikana ni Shilingi 3,667,000 ikilinganishwa na Shilingi 2,664,125 kwa hekta katika kilimo cha umwagiliaji wa

kawaida kwa bei za mwaka 2014/2015 katika skimu za Mkula Mkoa wa Morogoro na Mwamapuli mkoa wa Tabora.

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea na utafiti wa kugundua aina tano (5) za mbegu bora; njia za kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao na kuzisambaza kwa wadau. Aidha, Wizara itazalisha tani 10 za mbegu mama kwa mazao ya nafaka, mikunde, mboga na mbegu za mafuta na pingili milioni mbili za mazao jamii ya mizizi. Wizara pia itatathmini na kusambaza mbegu na miche ya mazao ya mboga na matunda yenye thamani kubwa zikiwemo nyanya, maembe, kakao, matofaa, na maparachichi katika kanda za ikolojia inayofaa kwa kilimo cha mazao hayo. Vilevile Wizara itaendelea kurekebisha mapendekezo ya matumizi bora ya mbolea kwa mazao ya mpunga na mahindi na kurekebisha ramani za udongo kwa matumizi ya wakulima na wawekezaji.

**137.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itarekebisha ramani zilizo kwenye Mfumo wa Habari za Kijiografia (GIS) kwa Wilaya tano katika kanda za ikolojia za kilimo saba zinazolenga maeneo ya uwekezaji kwenye kilimo. Wizara itaendelea kutoa ruzuku kwa taasisi nane zinazoshughulika na utafiti na kulipia michango ya uanachama katika taasisi tatu za kimataifa zinazoshughulika na utafiti wa kilimo. Wizara pia itaendelea kukiwezesha Kituo cha Taifa cha Utunzaji Nasaba za Mimea kilichopo Arusha ili kiweze kutoa huduma bora. Aidha, Wizara itaandaa mapendekezo ya Sheria ya Nasaba za Mimea; kuwezesha maabara za Bioteknolojia za Mikocheni, Ukiriguru, Uyole na Tengeru ili ziweze kufanya kazi kwa uwezo wake; na kuunda Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania.

***Hakimiliki za Mbegu***

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa mwaka 2014/2015 imeandaa rasimu ya awali ya kanuni ya Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea. Vilevile iliandaa miongozo ya uendeshaji wa majaribio ya usajili wa hakimiliki za wagunduzi na kupokea na kusajili aina mpya za mbegu za mimea 10. Wizara ilikamilisha mchakato wa Tanzania kujiunga na Shirika la Kimataifa la Hakimiliki kwa Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu Duniani – UPOV na kabla ya mwisho wa mwaka 2015 Tanzania itawasilisha hati ya kujiunga na UPOV.

**139.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wagunduzi wa mbegu mpya na wataalam wa teknolojia ya mbegu kuhusu uainishaji wa sifa za mbegu mpya kwa kuzingatia miongozo ya Shirika la UPOV na kusimamia majaribio 15 kwa ajili ya utoaji wa hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu.

***Mashamba ya kilimo cha kibiashara kwa mazao ya mpunga na miwa (BRN)***

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara ilikamilisha kufanya utambuzi wa awali katika mashamba 25 yenye jumla ya hekta 350,000 yaliyoainishwa wakati wa maabara ya kilimo katika utekelezaji wa Mfumo wa BRN kwa ajili ya uwekezaji. Mashamba 16 yalipangwa kwa ajili ya kilimo cha zao la miwa na mashamba 9 kwa kilimo cha zao la mpunga **(Kiambatisho Na. 8).** Utambuzi huo ulitoa takwimu sahihi ya uhalisia wa mashamba hayo.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2015 mashamba makubwa ya Kitengule, Lukulilo, Mkulazi na Bagamoyo yenye jumla ya hekta 114,518 yamehakikiwa na kupatiwa hati miliki ambapo mashamba ya Bagamoyo, Lukulilo na Kitengule yamepata wawekezaji. Aidha, hekta 43,200 za mashamba ya wakulima wadogo zimehakikiwa katika maeneo hayo na jumla ya Hati Miliki za Kimila 1,513 zimeandaliwa kwa wakulima wanaozunguka shamba la Lukulilo na Ngalimila.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara itahamasisha uwekezaji katika kilimo cha kibiashara katika mashamba manane ambayo ni Mvuha na Kisaki (Morogoro Vijijini), Tawi, Muhoro na Mkongo (Rufiji), Mahurunga (Mtwara Vijijini), Kasulu (Kasulu) na Kumsenga (Kibondo). Aidha, Wizara itashirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, TAMISEMI pamoja na mikoa ya Lindi, Mtwara, Rukwa, Katavi, na Tabora kuanzisha mashamba makubwa matano ya uwekezaji kwenye mikoa hiyo. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi itapima na kuwezesha upatikanaji wa Hati Miliki katika mashamba manane ya uwekezaji.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itakamilisha mapendekezo ya Sheria na Mwongozo wa Kulinda Rasilimali za Kilimo. Vilevile Wizara itawezesha upimaji na uchoraji wa ramani wa mashamba 12 ya uwekezaji. Aidha, Wizara itaendelea kuwezesha upatikanaji wa hati za haki miliki za kimila kwa wakulima wanaozunguka mashamba 15 ya uwekezaji pamoja na kuanzisha mfumo wa kuweka kumbukumbu za umiliki wa ardhi ya kilimo vijijini katika vijiji vinavyozunguka mashamba hayo ya uwekezaji ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji.

**144.** Katika mwaka 2015/2016 Wizara kupitia RUBADA itashirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na halmashauri kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo na kutenga hekta 10,000 kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, Hatimiliki za Kimila 600 kwa wakulima wadogo katika kongani ya Ludewa na Rufiji chini zitaandaliwa.

***Ajira kwa vijana***

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, imetambua makundi 828 ya vijana waliojiajiri katika kilimo kwa lengo la kuwahamasisha na kuwapa ushauri wa kilimo cha kibiashara. Kati ya makundi hayo, 276 yamesajiliwa kisheria na 552 hayajasajiliwa. Vilevile Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali katika jitihada za kuendeleza vijana kujiajiri katika kilimo cha kibiashara.

### 4.2.2 Kuongeza Upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo yasiyosimamiwa na Bodi za Mazao, juhudi za Wizara za kisekta kushirikisha Sekta Binafsi katika kilimo cha mazao ya bustani zimeanza kuzaa matunda ambapo kumekuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji wa mazao na mauzo nje ya nchi na hivyo kuongeza mapato ya fedha za kigeni. Mauzo ya mazao hayo yaliongezeka kutoka Shilingi 373,929,852,996.00 mwaka 2013/2014 hadi Shilingi 471,421,164,569.05 mwaka 2014/2015 na hivyo kuchangia katika kuongeza Pato la Taifa. Mauzo ya mazao ya bustani nje ya nchi ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 7.**

***Jedwali Na. 7:*** **Mauzo ya Mazao ya Bustani Nje ya Nchi(Sh)**

| | Julai 2013 – Juni 2014 | | Julai 2014 – Aprili 2015 | |
|---|---|---|---|---|
| **Zao** | **Kiasi (Kg)** | **Thamani (Sh)** | **Kiasi (Kg)** | **Thamani (Sh)** |
| Maua | 3,069,311 | 22,276,801,761 | 2,234,155 | 14,482,268,152 |
| Mboga | 303,148,044 | 210,380,044,631 | 159,687,508 | 411,705,281,404 |
| Matunda | 29,695,459 | 16,759,997,115 | 11,268,587 | 14,070,957,016 |
| Viungo | 6,450,101 | 98,725,994,021 | 1,368,398 | 18,503,369,301 |
| Mbegu | 1,480,415 | 25,787,015,468 | 1,880,902 | 12,659,288,696 |
| **Jumla** | **343,843,330** | **373,929,852,996** | **176,439,551** | **471,421,164,569** |

*Chanzo: TRA*

**147.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na TAHA inatoa taarifa za masoko kwa wakulima wa mazao ya bustani na kuwaunganisha na masoko. Katika mwaka 2014/2015 wakulima zaidi ya 1,000 wameunganishwa na masoko mbalimbali ndani na nje ya nchi na kupelekea ongezeko la faida kwa zaidi ya asilimia 31. TAHA imeendelea kuwasambazia wakulima wa mazao ya bustani taarifa sahihi za masoko kwa kutumia ujumbe mfupi wa maneno kwa njia ya simu za mkononi. Jumla ya wakulima 13,550 walipokea taarifa za masoko kupitia mfumo huo.

**148.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwezesha mazao ya bustani kufika sokoni kwa wakati na yakiwa katika ubora unaotakiwa, TAHA kwa kushirikiana na Serikali na wadau wengine imefanikiwa kupunguza changamoto za usafirishaji wa mazao ya bustani kwenda nje nchi. Mafanikio hayo yametokana na

kuboreshwa kwa mfumo wa utoaji vibali vya kuuza mazao nje katika mipaka ya nchi ikiwemo Namanga na KIA hivyo kuweza kupunguza muda uliokuwa ukitumika kupitisha mizigo kutoka saa 10 hadi saa mbili.

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhamasisha na kutangaza tasnia ya mazao ya bustani ndani na nje ya nchi, Wizara kwa kushirikiana na TAHA imeshiriki kwenye maonesho ya biashara ya ndani na nje ya nchi, ikiwemo maonesho ya Nanenane. Kupitia vipindi mbalimbali vya redio na luninga pamoja na mitandao ya kijamii ambavyo vimekua kivutio kikubwa sana hasa kwa vijana imewahamasisha kujiunga na kilimo cha bustani. Aidha, wanafunzi wa vyuo vikuu vya SUA na Chuo cha Uhasibu Arusha wamewezeshwa kuona fursa zilizopo katika tasnia hiyo.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** mazao makuu ya asili ya biashara yaliyozalishwa katika mwaka 2014/2015 yaliuzwa katika masoko ya nchi mbalimbali na kuliingizia Taifa Shilingi trilioni 1.39 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 1.26 zilizopatikana kutokana na mauzo ya mazao hayo katika mwaka 2013/2014. Aidha, uuzaji nje kwa baadhi ya mazao hayo bado unaendelea. Muhtasari wa mauzo ya mazao hayo na viwango vya fedha zilizopatikana vimeoneshwa katika **Jedwali Na. 8.**

**Jedwali Na. 8: Mauzo ya Mazao Makuu ya Asili ya Biashara Nje ya Nchi (2013/2014 – 2014/2015)**

| Zao | 2013-2014 | | 2014-2015** | |
|---|---|---|---|---|
| | Kiasi (Tani 000) | Thamani (Sh. M.) | Kiasi (Tani 000) | Thamani (Sh. M.) |
| Kahawa | 49.66 | 204,280.95 | 38.30 | 211,971.43 |
| Pamba | 75.82 | 147,870.95 | 45.63 | 84,836.76 |
| Mkonge | 14.21 | 31,631.50 | 8.57 | 22,652.95 |
| Chai | 28.00 | 75,676.25 | 21.09 | 56,730.70 |
| Tumbaku | 74.18 | 575,052.26 | 69.47 | 579,564.20 |
| Korosho | 124.93 | 214,360.23 | 174.06 | 432,137.91 |
| Pareto* | 1.32 | 15,403.55 | 0.91 | 5,157.92 |
| **Jumla** | **368.12** | **1,264,275.69** | **358.04** | **1,393,051.88** |

*Chanzo: Benki Kuu * Chanzo: TRA ** Hadi Machi 2015*

### Masoko kupitia Mfumo wa BRN

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwasaidia wakulima kuongeza upatikanaji wa masoko ya mazao yao. Katika Mfumo wa BRN, Wizara inajenga maghala mawili kati ya manne na kukarabati 36 kati ya 48 yaliyolengwa kupitia Mfumo wa Hifadhi na Uuzaji wa Mazao kwa Pamoja (*Collective Warehouse Based Marketing* - COWABAMA) **Kiambatisho Na. 9.**

Ujenzi na ukarabati wa maghala hayo utasaidia wakulima kuhifadhi mazao yao kwa pamoja wakisubiri kupata bei nzuri.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufikia mwezi Aprili 2015 mikataba ya ujenzi wa maghala mawili kati ya manne na ukarabati wa maghala 36 kati ya 48 imesainiwa na utaratibu wa kuhamisha fedha kwenda Halmashauri husika unaendelea. Katika kuongeza ufanisi wa usimamizi wa maghala, vikundi 27 vya wakulima (FBOs) vyenye wanachama 3,004 kutoka katika maghala yaliyopo katika Halmashuri za Wilaya za Momba (1) na Mbozi (26) vimesajiliwa na vinafanyakazi. Aidha, viongozi 136 wa vikundi hivyo wamepatiwa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa maghala. Vilevile Wataalam wa kilimo 68, wasimamizi na waendesha maghala 121 na wanachama 2,188 wamejengewa uwezo kuhusu teknolojia bora za hifadhi ya mazao ghalani, usimamizi na uendeshaji wa maghala na udhibiti wa ubora na usalama wa mazao hususan mahindi.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa mavuno wa mwaka 2014/2015 vikundi 20 vya wakulima kutoka katika maghala 20 vilihifadhi jumla ya tani 4,769.2 za mahindi**.** Kati ya hizo tani 2,425.88 kutoka katika maghala hayo ziliuzwa kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na mahindi mengine yameendelea kuuzwa kwa wanunuzi wengine.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itakarabati na kujenga maghala 80 kwa ajili ya hifadhi ya mahindi katika wilaya 12 zilizopo chini ya mpango wa COWABAMA. Kati ya maghala hayo, 57 yatajengwa, kukarabatiwa na kununuliwa vifaa kwa kutumia fedha za nyongeza zilizotengwa kumalizia miradi ya ASDP 1. Aidha, Wizara itaendeleza usanifu wa mfumo wa kukusanya na kusambaza taarifa za kilimo kwenye maghala 30 yaliyopo katika Halmashauri za Momba na Mbozi. Vilevile uanzishwaji wa muundo wa kisheria kuhusu mfumo unaotabirika wa uagizaji na uuzaji wa mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi utaendelea.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** juhudi hizi za kukarabati na kujenga maghala zinalenga kurahisisha upatikanaji wa mazao kwa wingi katika sehemu moja na hivyo kuwa kivutio kwa wafanyabiashara kununua mazao kutokana na kutumia muda mchache na gharama ndogo. Aidha, maghala yanarahisisha kudhibiti ubora wa mazao na kuunganisha katika mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani na hatimaye kuunganishwa katika mfumo wa Masoko ya Bidhaa (*Commodity Exchange*).

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara kupitia NFRA itanunua tani 250,000 za mahindi katika Kanda za Arusha, Dodoma, Kipawa, Makambako, Shinyanga, Songea na Sumbawanga. Kati ya hizo tani 50,000 zitanunuliwa kwa fedha iliyotengwa na Serikali na tani 200,000 zitanunuliwa kutokana na mikopo kutoka Taasisi za Fedha. Aidha, Wizara itakamilisha ujenzi

wa maghala mawili yaliyopo katika Halmashauri za Wilaya za Songea na Mbozi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 na tani 5,000 za nafaka mtawalia. Aidha Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, itahakikisha mazao ya wakulima yananunuliwa.

***Bodi za mazao kutafuta masoko***

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani kwa wadau wa mikoa ya Ruvuma na Pwani ili kupunguza wimbi la wanunuzi wanaotoa bei ndogo na kuwawezesha wakulima kupata bei nzuri na soko la uhakika.

**158.** Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania imeendelea kuitangaza kahawa katika masoko mapya yanayochipua kama Korea, China, Urusi na Arabuni yatakayowezesha kuimarika kwa bei ya kahawa nje ya nchi na kuwa na masoko ya uhakika. Aidha, watumishi wa Bodi ya Kahawa walihudhuria maonesho ya biashara ya kahawa katika nchi wanywaji kwa madhumuni ya uhamasishaji zaidi ili kuongeza mahitaji ya kahawa ya Tanzania nje ya nchi.

### 4.2.3 Kuimarisha Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua juhudi za sekta binafsi katika kuongeza thamani kwa mazao kabla ya kuyauza. Katika miaka ya karibuni uongezaji wa thamani kwa mazao umeendelea kukua, mathalani kwa mazao ya kahawa, chai, korosho, mkonge, mazao ya mafuta, pareto, sukari, nafaka, mboga na matunda. Wizara inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika kuongeza thamani ya mazao. Wizara pia kupitia maonesho ya Nanenane na Siku ya Chakula Duniani ilieneza teknolojia za utayarishaji, uhifadhi na usindikaji wa mazao ya chakula. Teknolojia hizo zililenga katika kuchambua, kupanga madaraja na kuzipa chapa bidhaa za nafaka na mikunde; usindikaji wa muhogo kupata unga bora na wanga; ukaushaji, ufungashaji, kuweka lebo na chapa katika mazao ya mboga na matunda, mazao ya viungo na mbegu za mafuta.

### 4.2.4 Kuwezesha na Kuimarisha Ushirika na Asasi za Wananchi katika Kilimo na Sekta nyingine za Kiuchumi

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya imetoa elimu ya ushirika kwa wakulima 670 kuhusu umuhimu wa ushirika na upatikanaji wa mikopo ya kilimo kupitia Vyama vyao. vyama vya ushirika 4,129 kati ya 7,888 vilifanya uchaguzi na viongozi 28,907 waliochaguliwa walipatiwa mafunzo ya uongozi, usimamizi na udhibiti wa mali za Vyama vyao. Aidha, Wizara kupitia COASCO imekagua vyama vya ushirika 1,847 vikiwemo Vyama vya Mazao – AMCOS 521, SACCOS 1,093 na aina nyinginezo 33 kati ya Vyama 4,000 na uchunguzi maalum umefanyika katika Vyama 29 na kubaini kasoro mbalimbali za uendeshaji na usimamizi na hatua stahiki zimechukuliwa.

Aidha, Wizara imetatua migogoro mikubwa minne ya kisheria ya Vyama vya UWAKO, Bugogwa (Mwanza), WADOKI na KNCU.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2015/2016 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Viwanda na Biashara itaendelea pia kuimarisha miundombinu ya masoko, upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu, uhifadhi wa mazao ya wakulima na uongezaji wa thamani ya mazao. Aidha, Wizara kama mdau mkuu wa Kamati ya Kitaifa ya Uratibu wa Mpango wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Kifedha itaendelea kuratibu Ushirika wa Akiba na Mikopo. Vilevile, Wizara itaimarisha utoaji wa elimu ya ushirika na biashara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ili wananchi waweze kuuelewa zaidi ushirika na kuutumia.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itakamilisha uwekaji wa mifumo ya usimamizi kutoka ngazi mbalimbali kwa kupeleka watendaji watakaotekeleza majukumu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Wizara za Kisekta itaajiri Maafisa Ushirika kwa ajili ya kuhamasisha uanzishaji na matumizi ya huduma za vyama vya ushirika**.** Vilevile Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuimarishwa ili iweze kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kutatua migogoro ya Vyama na kuimarisha usimamizi wake.

### 4.2.5 Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji, Uhifadhi, Uchambuzi na Usambazaji wa Takwimu

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Wizara zingine za Sekta pamoja na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imechukua hatua mbalimbali za kuboresha takwimu za kilimo nchini katika mwaka wa 2014/2015 kwa kutekeleza yafuatayo:

***Kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Takwimu (ARDS)***

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa takwimu za kilimo umeboreshwa kwa ufadhili wa 'JICA' ambapo fomu maalumu za ukusanyaji na utoaji wa taarifa za mwezi, robo mwaka na za mwaka zimeandaliwa. Uboreshaji huu umefanyika hasa katika ngazi ya wilaya ambapo kanzidata ambayo ni ''*web based*'' ijulikanayo kama ''*Local Government Monitoring Database 2*'' (LGMD2) hutumika katika kuingiza na kupeleka takwimu katika ngazi ya taifa kwa kutumia mtandao na wadau mbalimbali huweza kuziona na kuzitumia. Uboreshaji uliofanyika ni wa kutumia mtandao ambapo mtendaji katika ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa anafanya kazi katika kompyuta yoyote kama kuna mtandao tofauti na hali ilivyokuwa kabla ya uboreshaji.

**165.** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani imetoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 110 wa mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe, Iringa, Mbeya, Katavi, Ruvuma, Rukwa, Tabora na Kigoma ya kuwajengea uwezo wa kutumia Mfumo wa Uchambuzi wa Takwimu za Ushirika. Mfumo huu kwa sasa umeboreshwa zaidi ambapo Afisa Ushirika anaweza kuutumia kupitia mtandao.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za hali ya chakula kupitia mfumo wa uratibu wa chakula na tahadhari ya njaa. Ili kuimarisha mfumo huo, Wizara inashirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Halmashauri husika ili kupata takwimu na taarifa sahihi za hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula.

**167.** Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na taasisi za kikanda na kimataifa zikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC, USAID, WFP na FAO katika kuandaa na kusambaza taarifa za hali ya chakula. Taarifa hizi husambazwa kwa wadau kwa machapisho mbalimbali. Kupitia mashirikiano ya kimataifa, jumla ya wataalam sita wa Wizara wamepatiwa mafunzo juu ya uchambuzi wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula na hali ya chakula.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika kukusanya takwimu za wakulima wadogo wa Nyanda za Juu Kusini ili kuboresha viashiria vya umaskini. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Takwimu za kilimo kupitia ufadhili wa 'JICA'. Wizara itaendelea kukusanya taarifa za uzalishaji wa mazao, hali ya chakula na mvua katika vituo 600 vya hali ya hewa.

### 4.2.6 Kusimamia Sera na Sheria Katika Sekta ya Kilimo

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu maudhui ya Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 kupitia mikutano ya kitaalam na maonesho mbalimbali ikiwemo Sikukuu ya wakulima ya Nanenane. Aidha, Sera hii imewekwa kwenye tovuti ya Wizara ili kuwezesha wadau wengi zaidi kuifahamu.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kutekeleza sera hiyo, imeandaa Mkakati wa Kuendeleza Kilimo (ASDS) na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) awamu ya pili. Programu hiyo inalenga kubadilisha kilimo kuwa cha kisasa na cha kibiashara kwa lengo la kuongeza tija, uzalishaji, mapato na kupunguza umaskini. Utekelezaji wa ASDP II utafanywa kwa utaratibu wa Mfumo wa BRN ili kuiwezesha Serikali kufikia malengo yaliyowekwa kwa haraka zaidi.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uwezo wa wataalam wa kuchambua, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Kilimo, Wizara

inashirikiana na Washirika mbalimbali wa maendeleo kutoa mafunzo na vitendea kazi. Baadhi ya washirika wa maendeleo wanaoshiriki ni *Michigan State University, Regional Strategic Analysis and Knowledge Support (ReSAKSS), International Livestock Research Institute (ILRI)* na *Alliance for a Green Revolution in Africa (AGRA).*

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliwasilisha Bungeni muswada wa marekebisho madogo katika Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003 na Sheria ya Mbolea ya mwaka 2009 kwa lengo la kuboresha mfumo wa usimamizi na kuongeza adhabu zinazohusu makosa yatokanayo na ukiukwaji wa Sheria. Marekebisho hayo yatawezesha wakulima kufidiwa kutokana na hasara itakayosababishwa na kuuziwa mbegu au mbolea zisizo na viwango. Wizara pia ilikamilisha mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania na marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Bonde la Mto Rufiji ya mwaka 1975 yanayolenga kuboresha majukumu ya Mamlaka hiyo kwa kuipa uwezo wa kisheria wa kutekeleza Mipango na miradi mbalimbali ya kuendeleza kilimo katika bonde la mto Rufiji.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweka mfumo bora wa udhibiti wa ubora wa pembejeo za kilimo zikiwemo mbegu na viuatilifu, katika mwaka 2015/2016, Wizara itakamilisha na kuwasilisha Bungeni Muswada wa marekebisho makubwa ya Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Mimea ya mwaka 1997 na Muswada wa marekebisho ya Sheria ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki ya mwaka 1979. Aidha, Wizara itazifanyia marekebisho Kanuni za Sheria hizo ili ziwezeshe utekelezaji mzuri wa Sheria na kuwahakikishia wakulima pembejeo zenye ubora. Pia, Wizara imepanga kuwasilisha Bungeni muswada wa marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Pembejeo ya mwaka 1994 ili kuboresha mfumo wa utoaji wa mikopo ya pembejeo na huduma nyingine za kuendeleza kilimo.

### 4.2.7 Kuboresha uwezo wa Wizara kutoa Huduma

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea kuboresha utendaji kazi kwa watumishi wake kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao. Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi 255 ndani na nje ya nchi. Watumishi 153 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 102 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Mafunzo hayo yalitolewa katika fani za kilimo, utafiti kilimo, kilimo cha mboga na matunda, ufundi sanifu wa maabara, usimamizi wa fedha, usimamizi wa rasilimali watu, uongozi, huduma kwa mteja, utunzaji wa kumbukumbu, jinsia, uchumi, takwimu, sheria na ufundi sanifu. Aidha, watumishi 386 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuwapatia mafunzo watumishi wake, kutoa stahili mbalimbali za watumishi na kuwapandisha vyeo watumishi 804 wa kada mbalimbali kulingana na taratibu na kanuni za utumishi wa umma.

***Mafunzo katika Vyuo vya Kilimo***

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ililenga kufundisha wanafunzi wa Astashahada na Stashahada 2,500 ambapo waliodahiliwa walikua wanafunzi 2,748 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 248 sawa na asilimia 9.9 katika mwaka 2014/2015. Kati ya hao Astashahada ni 2,071 na Stashahada ni 677. Kozi wanazosomea ni Astashahada na Stashahada ya kilimo mseto; Stashahada za umwagiliaji, matumizi bora ya ardhi, uzalishaji wa chakula na lishe, matumizi ya zana za kilimo na uzalishaji wa mboga, maua na matunda. Jumla ya wanafunzi 2,025 wa mwaka wa pili walifanya mafunzo kwa vitendo kwa muda wa wiki nne katika vijiji, Halmashauri za wilaya na Taasisi za Utafiti na watahitimu mwezi Juni 2015.

**176.** Aidha, Wizara imepitisha Mtaala wa Stashahada ya uzalishaji wa mazao, kutoa mafunzo elekezi ya mbinu za kufundishia kwa wakufunzi 20 wa Wizara na wawili kutoka vyuo binafsi. Wizara kupitia mradi wa PHRD imetoa mafunzo kwa wakufunzi 40 na wakulima 689 wa skimu za umwagiliaji kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa zao la mpunga, masoko na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji. Vilevile Wizara imetoa mafunzo kwa wakulima 2,763 kutoka katika skimu 27 za umwagiliaji na maeneo 10 yanayolima mpunga kwa kutegemea mvua kwa ushirikiano na JICA kupitia mradi wa TANRICE 2. Wakulima 25 wa Igurusi mkoani Mbeya walilipwa fidia ya eka 38 walizotoa kwa ajili ya kujenga miundombinu ya shamba la mafunzo ya umwagiliaji ya Chuo cha Kilimo Igurusi. Aidha, Wizara imeendelea na ukarabati wa majengo katika Chuo cha Kilimo Mubondo mkoani Kigoma.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanachuo 2,500. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mradi wa TANRICE 2 itatoa mafunzo kwa wakulima wadogo katika skimu za umwagiliaji 12. Vilevile Wizara itaendelea kukarabati jengo la utawala na bweni la vyuo vya kilimo vya Mubondo na Ilonga na ujenzi wa bweni katika Chuo cha KATC – Moshi.

### 4.2.8 Kuzingatia Masuala Mtambuka katika Kilimo

***Mazingira***

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2014/2015, imeendelea kuratibu, kudhibiti, kutathmini na kuhamasisha kazi za hifadhi ya mazingira katika maendeleo ya kilimo na kutekeleza malengo ya BRN. Wizara kwa kushirikiana na wadau imekamilisha kuandaa Mpango wa Taifa wa miaka mitano wa kilimo wa kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi ambapo nakala 120 za mpango huo zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau na zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara

(*www.kilimo.go.tz*). Katika mwaka 2015/2016 Wizara itashirikiana na wadau kukamilisha uandaaji wa Programu ya utekelezaji wake.

***VVU na UKIMWI***

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI mahali pa kazi, Wizara imeendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya ili kutambua hali zao. Aidha, Wizara inaendelea kuwahudumia watumishi waliojitokeza kulingana na miongozo ya Serikali.

## 5.0 SHUKRANI

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam na Poland. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, ILO, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, AfricaRice, ILRI, CABI, FARA, *Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust*, *Rockfeller Foundation, Aga Khan Foundation, ReSAKSS, Michigan State University* na *Unilever*. Ushirikiano na misaada ya nchi na mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki; Katibu Mkuu Bibi Sophia Elias Kaduma; Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Raphael Daluti; Wakurugenzi wa Idara; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote wa Wizara; na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2015/2016. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii.

## 6.0 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2015/2016

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kupitia **Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05** inaomba jumla ya Shilingi **353,150,873,000** kama ifuatavyo:

***FUNGU 43***

**183. *Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **290,744,623,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **249,751,550,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **40,993,073,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

***FUNGU 24***

**184. *Mheshimiwa Spika,*** kiasi cha Shilingi **7,627,990,000** kinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

***FUNGU 05***

**185. *Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **54,778,260,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **383,686,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **54,394,574,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**186. *Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. SAID J. NKUMBA (K. n. y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kusoma taarifa yangu naomba nitumie fursa hii…

**MWENYEKITI:** Una Dakika 20.

**MHE. SAID J. NKUMBA (K. n. y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Sikonge kwa ushirikiano walionipa katika kipindi cha kuwatumikia kama Mbunge wao.

Nimshukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati, Mheshimiwa Profesa Msolla, Mbunge wa Kilolo, kwa kunishirikisha kwenye uongozi wa Kamati kama Makamu wake na amekuwa mwalimu wangu kutokana na uzoefu wa uongozi alionao.

Mhesimiwa Mwenyekiti, aidha, niwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa kama Makamu Mwenyekiti na kuifanya kazi yangu kuwa rahisi. Mwisho niwashukuru viongozi wote wa Chama chama Mapinduzi wa ngazi zote walionisaidia kutekeleza majuku haya ya kuwawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa wenyekiti, Kamati hii ilijadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na changamoto za utekelezaji. Aidha, Kamati ilipokea maelezo kuhusu malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali katika maeneo mbalimbali.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni ya Kamati. Kwa ujumla Kamati imeridhika na utendaji wa Wizara isipokuwa katika maeneo machache ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na ucheleweshaji na ukosefu wa fedha. Maeneo ambayo yaliathirika ni pamoja na kutofikia lengo la ukuaji wa kilimo kwa asilimia sita kwa mwaka na mfuko wa pembejeo kuendelea kupewa fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ilikumbana na changamoto zifuatazo:-

(i) Ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha uliochangia kutofikiwa kwa malengo katika kipindi husika.

Sehemu kubwa ya fedha ambazo zimetolewa na Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni zile za maeneo yanayolindwa kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa chakula cha hifadhi ya Taifa, ruzuku ya pembejeo za kilimo na michango ya taasisi za kikanda na za kimataifa zilizo chini ya Wizara. Hali hii

imesababishia Wizara kushindwa kutekeleza kwa ukamilifu malengo iliyojiwekea katika mpango na bajeti kwa mwaka 2014/2015.

(ii) Uchache wa Maafisa Kilimo na Ugani, Maafisa Ushirika, Watafiti wa Kilimo, Wahandisi na Wakaguzi wa Mazao ikilinganishwa na mahitaji halisi ya maafisa hawa katika ngazi ya Halmashauri;

(iii) Mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame, mtawanyiko mbaya wa mvua na mafuriko hivyo kuathiri upatikanaji wa chakula nchini; na

(iv) Ukosefu wa miundombinu ya barabara za kufikia maeneo ya uzalishaji, maghala na umeme kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo katika maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa changamoto nyingi zinazoikabili Wizara hii zinasababishwa na ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2014/2015, Bunge liliidhinishia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika jumla ya Sh.87,922,790,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 22 Aprili, 2015, Sh.40,982,880,943 tu sawa na asilimia 46.6 ya fedha zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge zilikuwa zimetolewa.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, hadi mwezi Aprili, 2015, jumla ya Sh.205,008,914,502 zilikuwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo, Sh.157,141,405,200 sawa na asilimia 76 zilitolewa kwa ajili ya maeneo yanayolindwa *(ring fenced)*. Hii inamaanisha kuwa ni asilimia 24 tu ya bajeti ya matumizi ya kawaida ilitolewa kwa ajili ya majukumu mengine muhimu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa kwa Serikali kutokutoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge. Ni rai ya Kamati kuwa, Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kutoa fedha zote kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Hii itafanikisha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu yake, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika chini ya Fungu 43 inaomba jumla ya Sh.290,744,623,000. Kati ya fedha hizo, Sh.249,751,550,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.40,993,073,000 ni kwa miradi ya maendeleo. Fungu 24 - Ushirika, inaombewa jumla ya Sh.7,627,990,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Fungu 05, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, inaomba Sh.54,778,260,000, kati ya fedha hizo

Sh.383,686,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.54,394,574,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazoombwa na Wizara zinakusudia kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kuwezesha uwekezaji katika kilimo cha biashara katika mashamba makubwa manane (8) ya mpunga na miwa;

(b) Kukarabati miundombinu ya skimu 20 za umwagiliaji;

(c) Kuimarisha utafiti wa mazao yenye thamani kubwa na utafiti wa magonjwa yanayoleta athari kubwa kwa mazao;

(d) Kuanzisha mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo ikiwa ni pamoja na kuanzisha benki ya takwimu kwa ajili ya mpango huo;

(e) Kutoa ruzuku kwa wakulima ili kuwawezesha wakulima kupata pembejeo za kilimo kwa bei nafuu;

(f) Kuongeza matumizi ya zana bora za kilimo;

(g) Kuimarisha uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* katika kutunza chakula cha akiba; na

(h) Kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo kame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa bajeti 2015/2016. Sekta ya kilimo imeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa ikifuatiwa na sekta nyingine. Kwa mwaka 2014, sekta hii ilichangia asilimia 31.7 ya pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 31.1 mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani asilimia 75 ya Watanzania wanashiriki katika shughuli za kilimo lakini Watanzania wengi bado wanaishi katika umaskini uliokithiri. Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao katika maeneo mbalimbali katika bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016 ili kuwezesha sekta hii kuwa yenye tija kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha umeendelea kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya Sh.383,187,544,389 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara hii inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.353,150,873,000. Bajeti hii inayoombwa imepungua kwa Sh.30,036,671,389 sawa na asilimia 7.8, ikilinganishwa na bajeti ya 2014/2015 licha ya kwamba kilimo kinatajwa kuwa ndiyo uti wa mgongo wa Taifa na kuchangia sehemu kubwa ya pato ghafi la Taifa.

Mhesimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa kuona kwamba Serikali imeshindwa kutekeleza mipango yake mizuri ya kuwakwamua wananchi kutoka katika kiwango kikubwa cha umaskini na kukuza pato la Taifa kupitia kilimo.

Kamati inashauri kuwa, kwa kuwa bajeti hii imepungua, Wizara ya Fedha ihakikishe kuwa bajeti inayoombwa na Wizara inatolewa yote na kwa wakati, ili kufanikisha malengo mazuri yaliyowekwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo. Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo umeendelea kuwanufaisha wakulima kupitia mikopo ya kununua zana za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mfuko huu ulitengewa jumla ya Sh.6,382,800,000. Hadi kufikia mwezi Aprili, Mfuko huu ulikuwa umepata Sh.5,182,113,824.50 sawa na asilimia 81 ya fedha zote. Hata hivyo, kwa kuwa si wakulima wote wenye uelewa kuhusu uwepo wa mfuko huu, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wakulima, hususan wale waishio vijijini, ili wafaidike na mfuko huu.

Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya mfuko huu na ikibidi kuuongezea fedha ili kufanikisha malengo yake. Kwa mfano, kwa mwaka 2014/2015, Mfuko ulipanga kutoa mikopo mbalimbali ikiwemo matrekta ya mikono 23 na mikopo ya pembejeo mchanganyiko 50. Hata hivyo, mfuko uliweza kukopesha trekta la mkono moja tu na mikopo ya pembejeo mchanganyiko 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa pembejeo za kilimo. Upatikanaji wa pembejeo za kilimo, hususan mbegu bora za mazao unaendelea kuwa tatizo nchini. Hali hii inachangiwa na mbegu zinazozalishwa nchini kutozwa kodi na hivyo kuwa na gharama kubwa ambazo wananchi walio wengi hawazimudu.

Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, Halmashauri hazitozi kodi kwenye mbegu zinazosafirishwa kutoka eneo moja kwenda lingine kulingana na Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003. Aidha, mbegu inayozalishwa nchini ipewe ruzuku zaidi ili kumwezesha mkulima kumudu bei ya mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na gharama kubwa kwenye mbegu za mazao mbalimbali, Kamati haifurahishwi na utaratibu wa Serikali wa kuagiza mbegu za mazao kutoka nje ya nchi ilhali uwezo wa kuzalisha mbegu zetu wenyewe upo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. SAID J. NKUMBA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mfano, kwa mwaka 2014/2015, Serikali iliagiza jumla ya tani 15,004.2 za mbegu. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi katika uzalishaji wa mbegu ndani ya nchi ambazo pamoja na mambo mengine zitahimili mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji nchini. Tanzania ina eneo kubwa la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, mpaka sasa, eneo linalolimwa kwa umwagiliaji ni takribani hekta 470,000 tu na kwamba Serikali imejiwekea lengo la kufikia hekta milioni moja kwa kipindi cha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sudani ni moja ya nchi zilizofanikiwa katika kilimo cha umwagiliaji. Jumla ya hekta takribani milioni mbili zinatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa kutegemea maji ya Mto Nile. Mazao yatokanayo na kilimo hicho hususan pamba, sukari, mtama, karanga, mbogamboga na matunda, yanakadiriwa kuchangia asilimia 64 ya Pato Ghafi la Taifa *(GDP)* la nchi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kuwa kwa kuwekeza katika Kilimo cha Umwagiliaji, Serikali itakuwa na nafasi kubwa ya kufanikiwa katika kuendeleza mazao ya biashara, ambayo ndiyo yanayoongoza kwa kukuza Pato la Taifa. Kamati inaishauri Serikali itekeleze malengo yake ya kuboresha na kujenga skimu za umwagiliaji zilizopo na kujenga mpya katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweka ukarabati wa miundombinu ya vituo vya utafiti na vyuo vya mafunzo ya kilimo kuwa moja ya vipaumbele vya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016. Pamoja na kukarabati miundombinu hii, Kamati inaishauri Serikali kwenda mbele zaidi kwa kuweka vipaumbele katika bajeti kwa ajili ya tafiti za magonjwa ya mazao kama vile mahindi, miembe, migomba, minazi na vitunguu. Tafiti hizi zinaweza kufanyika kwa kushirikiana na vyuo au nchi zenye wataalamu katika tafiti za magonjwa ya mazao kama vile Chuo Kikuu cha Wageningen nchini Uholanzi na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imepanga kutekeleza vipaumbele 15 vya Sekta ya Kilimo. Hata hivyo, katika vipengele vyote 15, mikakati thabiti ya kukuza mazao ya biashara kama vile chai, kahawa, pamba na mkonge, haijajitokeza katika vipaumbele hivyo. Aidha, mazao ya *horticulture* kama vile maua, mbogamboga na matunda, ambayo yangeweza kukuza ajira kwa vijana na pia kukuza Pato la Taifa, hayajatajwa katika vipaumbele hivyo. Kamati inaishauri Wizara kuweka mikakati madhubuti na kuelekeza bajeti ya kutosha katika mazao ya biashara na *horticulture*, ili kukuza pato la mkulima na Taifa kwa ujumla na hivyo kuondoa umaskini uliokithiri miongoni mwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto inayozikabili utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ni ukosefu wa fedha ambao umepelekea Miradi kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi 2015, Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Miradi hiyo. Moja ya Miradi iliyotembelewa ni Mradi wa Ujenzi wa Bwawa na miundombinu ya Skimu ya Umwagiliaji ya Inala iliyoko Mkoani Tabora. Ujenzi wa Bwawa la Inala kwa ajili ya umwagiliaji ulianza tarehe 9 Aprili 2011 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 29 Novemba 2011. Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 1,059,342,651.80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kusikitisha, mpaka Kamati inafanya ziara hiyo ya ukaguzi, Mradi huu ulikuwa haujakamilika. Kamati ilibaini kuwa, kutokamilika kwa Mradi huu kulichangiwa na mambo mbalimbali ikiwemo kutopatikana fedha kwa wakati na mkandarasi kutekeleza ujenzi wa Mradi chini ya kiwango. Kamati inaishauri Serikali kuwa, ni vyema ikaweka kipaumbele katika kuelekeza bajeti katika Miradi iliyoanza kutekelezwa na kuikamilisha kwanza kabla ya kuanza Miradi mipya. Aidha, Serikali ihakikishe inawapata Wakandarasi wenye uwezo na uzoefu wa kukamilisha Miradi yenye ubora na kwa wakati. Hali hii itawezesha Wizara kuwa na Miradi yenye tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, uzalishaji wa mazao ya biashara hususan pamba, kahawa na mkonge, umepungua kwa kiasi kikubwa. Hali hiyo imechangiwa na uwezo mdogo wa wakulima kugharamia pembejeo, wakulima kutokuwa na elimu ya matumizi bora ya mbolea na mfumo wa kodi usiotoa nafuu kwa mzalishaji.

Kwa kuwa ni dhahiri kuwa Taifa linakosa mapato mengi kutokana na uzalishaji mdogo wa mazao, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mikakati madhubuti itakayosaidia ongezeko la uzalishaji wa mazao hayo. Hii ni pamoja na kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora ya mbolea, kuongeza

ruzuku za pembejeo na kurekebisha mfumo wa kodi ambao utatoa nafuu kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchache wa Maafisa Kilimo na Ugani, Maafisa Ushirika, Mafundi Mchundo, Wahandisi na Wakaguzi wa Mazao umeendelea kuwa changamoto katika Halmashauri zetu. Kwa mfano, hadi 2015 idadi ya Maafisa Ugani ilikuwa 9,558 kati ya mahitaji halisi ya wagani 15,802.

Kwa kuwa maeneo mengi yanayotumika katika kilimo yako vijijini, Kamati inaishauri Serikali kutoa kibali cha kuajiri Maafisa Ugani wengi zaidi katika ngazi hizo. Aidha, ikiwezekana Maafisa Kilimo wote katika ngazi ya Halmashauri waajiriwe moja kwa moja mara wanapohitimu masomo yao.

Kamati inaishauri Serikali kuwa na mikakati ya kuwa na masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi kuongeza thamani ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati. Aidha, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Masato Wasira na Naibu Waziri Mheshimiwa Godfrey Zambi, kwa ushirikiano wao mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. Aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu - Ndugu Sophia Kaduma na Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Yamungu Kayandabila, pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, ninawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge - Ndugu Charles Mloka na Katibu wa Kamati hii Ndugu Grace Bidya akisaidiwa na Ndugu Sophia Vumbi, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa mwaka 2015/2016 kama ifuatavyo:-

Fungu 43 shilingi 290,744,623,000, Fungu 24 shilingi 7,627,990,000 na Fungu 05 shilingi 54,778,260,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii ilijadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na changamoto za utekelezaji. Aidha, Kamati ilipokea maelezo kuhusu malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali katika maeneo mbali mbali.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni ya Kamati. Kwa ujumla Kamati imeridhika na utendaji wa Wizara isipokuwa katika maeneo machache ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na ucheleweshaji na ukosefu wa fedha. Maeneo ambayo yaliathirika ni pamoja na kutofikia lengo la ukuaji wa kilimo kwa asilimia sita (6%) kwa mwaka na mfuko wa pembejeo kuendelea kupewa fedha kidogo.

## 3.0 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ilikumbana na changamoto zifuatazo:-

a) Ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha uliochangia kutofikiwa kwa malengo katika kipindi husika;

b) Sehemu kubwa ya fedha ambazo zimetolewa na Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni zile za maeneo yanayolindwa (kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa chakula cha hifadhi ya Taifa, ruzuku ya pembejeo za kilimo na michango ya Taasisi za kikanda na za kimataifa zilizo chini ya Wizara. Hali hii imeisababishia Wizara kushindwa kutekeleza kwa ukamilifu malengo iliyojiwekea katika mpango na bajeti kwa mwaka 2014/2015;

c) Uchache wa maafisa Kilimo na Ugani, Maafisa Ushirika, watafiti wa kilimo, wahandisi na wakaguzi wa mazao ikilinganishwa na mahitaji halisi ya maafisa hawa katika ngazi ya Halmashauri;

d) Mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame, mtawanyiko mbaya wa mvua na mafuriko hivyo kuathiri upatikanaji wa chakula nchini; na

e) Ukosefu wa miundombinu ya barabara za kufikia maeneo ya uzalishaji, maghala na umeme kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo katika maeneo ya uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa changamoto nyingi zinazoikabili Wizara hii zinasababishwa na ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Bunge liliidhinishia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika jumla ya shilingi **87,922,790,000/=** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo**.** Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 22 Aprili, 2015 shilingi **40,982,880,943/=** tu sawa na asilimia **46.6** ya fedha zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge zilikuwa zimetolewa.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya shilingi **205,008,914,502/=** zilikuwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo, shilingi **157,141,405,200/=** sawa na asilimia **76** zilitolewa kwa ajili ya maeneo yanayolindwa (ring fenced). Hii inamaanisha kuwa ni asilimia **24** tu ya bajeti ya matumizi ya kawaida ilitolewa kwa ajili ya majukumu mengine muhimu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasikitishwa kwa Serikali kutokutoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge. Ni rai ya Kamati kuwa, Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kutoa fedha zote kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Hii itafanikisha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

## 4.0 MAOMBI YA FEDHA NA MALENGO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika chini ya Fungu 43 inaomba jumla ya **shilingi 290,744,623,000/=.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 249,751,550,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 40,993,073,000/=** ni kwa miradi ya maendeleo. **Fungu 24,** Ushirika, inaombewa jumla ya **shilingi 7,627,990,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida; na **Fungu 05,** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, inaomba **shilingi 54,778,260,000/=,**kati ya fedha hizo **shilingi 383,686,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 54,394,574,000/=** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha zinazoombwa na Wizara zinakusudia kutekeleza kazi mbali mbali ikiwa ni pamoja na:-

a) Kuwezesha uwekezaji katika kilimo cha biashara katika mashamba makubwa manane (8) ya mpunga na miwa;

b) Kukarabati miundombinu ya skimu **20** za umwagiliaji;

c) Kuimarisha utafiti wa mazao yenye thamani kubwa na utafiti wa magonjwa yanayoleta athari kubwa kwa mazao;

d) Kuanzisha mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo ikiwa ni pamoja na kuanzisha benki ya takwimu kwa ajili ya mpango huo;

e) Kutoa ruzuku kwa wakulima ili kuwawezesha wakulima kupata pembejeo za kilimo kwa bei nafuu;

f) Kuongeza matumizi ya zana bora za kilimo;

g) Kuimarisha uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) katika kutunza chakula cha akiba; na

h) Kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo kame.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA WIZARA KWA MWAKA WA BAJETI 2015/2016

**5.1** **Mheshimiwa Spika**, Sekta ya kilimo imeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa ikifuatiwa na sekta nyingine. Kwa mwaka 2014, sekta hii ilichangia asilimia 31.7 ya pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 31.1 mwaka 2013.

5.2 **Mheshimiwa Spika,** takribani asilimia 75 ya Watanzania wanashiriki katika shughuli za kilimo, lakini Watanzania wengi bado wanaishi katika umaskini uliokithiri. Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao katika maeneo mbali mbali katika bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2015/2016, ili kuwezesha sekta hii kuwa yenye tija kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

### 5.2.1 Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** Ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha umeendelea kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi **383,187,544,389/=** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Hata hivyo, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara hii inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **353,150,873,000/=.** Bajeti hii inayoombwa imepungua kwa shilingi **30,036,671,389/=** sawa na asilimia **7.8,** ikilinganishwa na bajeti ya 2014/2015, licha ya kwamba kilimo kinatajwa kuwa ndio uti wa mgongo wa Taifa na kuchangia sehemu kubwa ya pato ghafi la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasikitishwa kuona kwamba, Serikali imeshindwa kutekeleza mipango yake mizuri ya kuwakwamua wananchi kutoka katika kiwango kikubwa cha umaskini na kukuza pato la Taifa kupitia kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa**,** kwa kuwa bajeti hii imepungua, Wizara ya Fedha ihakikishe kuwa bajeti inayoombwa na Wizara inatolewa yote na kwa wakati, ili kufanikisha malengo mazuri yaliyowekwa na Wizara.

### 5.2.2 Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo umeendelea kuwanufaisha wakulima kupitia mikopo ya kununua zana za kilimo. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mfuko huu ulitengewa jumla ya shilingi **6,382,800,000/=.** Hadi kufikia mwezi Aprili, Mfuko huu ulikuwa umepata shilingi **5,182,113,824.50/=** sawa na asilimia **81** ya fedha zote. Hata hivyo, kwa kuwa si wakulima wote wenye uelewa kuhusu uwepo wa mfuko huu, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wakulima, hususan wale waishio vijijini, ili wafaidike na mfuko huu.

Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya mfuko huu na ikibidi kuuongezea fedha ili kufanikisha malengo yake. Kwa mfano,kwa mwaka 2014/2015 Mfuko ulipanga kutoa mikopo mbalimbali ikiwemo matrekta ya mikono 23 na mikopo ya pembejeo mchanganyiko 50. Hata hivyo, mfuko uliweza kukopesha trekta la mkono moja (1) tu na mikopo ya pembejeo mchanganyiko 21.

### 5.2.3 Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa pembejeo za kilimo, hususan mbegu bora za mazao unaendelea kuwa tatizo nchini. Hali hii inachangiwa na mbegu zinazozalishwa nchini kutozwa kodi na hivyo kuwa na gharama kubwa ambazo wananchi walio wengi hawazimudu. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, Halmashauri hazitozi kodi kwenye mbegu zinazosafirishwa kutoka eneo moja kwenda jingine kulingana na Sheria ya Mbegu ya Mwaka 2003. Aidha, mbegu inayozalishwa nchini ipewe ruzuku zaidi ili kumwezesha mkulima kumudu bei ya mbegu**.**

**Mheshimiwa Spika,** mbali na gharama kubwa kwenye mbegu za mazao mbalimbali, Kamati haifurahishwi na utaratibu wa Serikali wa kuagiza mbegu za mazao kutoka nje ya nchi ilhali uwezo wa kuzalisha mbegu zetu wenyewe upo. Kwa mfano, kwa Mwaka 2014/2015, Serikali iliagiza jumla ya tani 15,004.20 za mbegu. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi katika uzalishaji wa mbegu ndani ya nchi ambazo pamoja na mambo mengine zitahimili mazingira yetu.

### 5.2.4 Kilimo cha umwagiliaji nchini

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ina eneo kubwa la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, mpaka sasa, eneo linalolimwa kwa umwagiliaji ni takribani hekta 470,000 tu na kwamba Serikali imejiwekea lengo la kufikia hekta milioni 1kwa kipindi cha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, nchi ya Sudan, ni moja ya nchi zilizofanikiwa katika kilimo cha umwagiliaji. Jumla ya hekta takribani milioni mbili (2) zinatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa kutegemea maji ya Mto Nile. Mazao yatokanayo na kilimo hicho (hususan pamba, sukari, mtama, karanga , mbogamboga na matunda) yanakadiriwa kuchangia asilimia 64 ya pato ghafi la taifa (GDP) la nchi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina amini kuwa kwa kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji, Serikali itakuwa na nafasi kubwa ya kufanikiwa katika kuendeleza mazao ya biashara ambayo ndio yanaongoza kwa kukuza pato la Taifa. Kamati inaishauri Serikali itekeleze malengo yake ya kuboresha na kujenga skimu za umwagiliaji zilizopo na kujenga mpya katika mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

### 5.2.5 Kuboresha Miundombinu ya Vituo vya Utafiti na Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweka ukarabati wa miundombinu ya vituo vya utafiti na vyuo vya mafunzo ya kilimo kuwa moja ya vipaumbele vya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kukarabati miundombinu hii, Kamati inaishauri Serikali kwenda mbele zaidi kwa kuweka vipaumbele katika bajeti kwa ajili ya tafiti za magonjwa ya mazao kama vile mahindi, miembe, migomba, minazi na vitunguu. Tafiti hizi zinaweza kufanyika kwa kushirikiana na vyuo/nchi zenye wataalamu katika tafiti za magonjwa ya mazao kama vile chuo kikuu cha Wageningen nchini Uholanzi na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

## 5.3 MAONI YA JUMLA

**5.3.1 Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2015/ 2016, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imepanga kutekeleza vipaumbele 15 vya sekta ya Kilimo. Hata hivyo, katika vipengele vyote 15, mikakati thabiti ya kukuza mazao ya biashara kama vile chai, kahawa, pamba na mkonge hayajajitokeza katika vipaumbele hivyo. Aidha, mazao ya *horticulture* kama vile maua, mbogamboga na matunda, ambayo yangeweza kukuza ajira kwa vijana na pia kukuza pato la Taifa, hayajatajwa katika vipaumbele hivyo.

Kamati inaishauri Wizara kuweka mikakati madhubuti na kuelekeza bajeti ya kutosha katika mazao ya biashara na *horticulture*, ili kukuza pato la mkulima na Taifa kwa ujumla na hivyo kuondoa umaskini uliokithiri miongoni mwa jamii.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto inayokabili utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya sekta ya kilimo ni ukosefu wa fedha ambao umepelekea miradi kutokamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Machi 2015, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa miradi

hiyo. Moja ya miradi iliyotembelewa ni mradi wa Ujenzi wa Bwawa na miundombinu ya skimu ya umwagiliaji ya Inala mkoani Tabora.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa bwawa la Inala kwa ajili ya umwagiliaji ulianza tarehe 09/04/2011 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 29/11/2011. Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi **1,059,342,651.80/=.**

**Mheshimiwa Spika,** katika hali ya kusikitisha, mpaka Kamati inafanya ziara hiyo ya ukaguzi, mradi huu ulikuwa haujakamilika. Kamati ilibaini kuwa kutokamilika kwa mradi huu kulichangiwa na mambo mbali mbali ikiwemo kutopatikana fedha kwa wakati na mkandarasi kutekeleza ujenzi wa mradi chini ya kiwango. Kamati inashauri Serikali kuwa, ni vema ikaweka kipaumbele katika kuelekeza bajeti katika miradi iliyoanza kutekelezwa na kuikamilisha kwanza kabla ya kuanza miradi mipya. Aidha, Serikali ihakikishe inawapata wakandarasi wenye uwezo na uzoefu kwa kukamilisha miradi yenye ubora na kwa wakati. Hali hii itawezesha Wizara kuwa na miradi yenye tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

**5.3.3 Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2014/2015, uzalishaji wa mazao ya biashara hususan pamba, kahawa na mkonge umepungua kwa kiasi kikubwa. Hali hiyo imechangiwa na uwezo mdogo wa wakulima kugharamia pembejeo, wakulima kutokuwa na elimu ya matumizi bora ya mbolea na mfumo wa kodi usiotoa nafuu kwa mzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa ni dhahiri kuwa Taifa linakosa mapato mengi kutokana na uzalishaji mdogo wa mazao hayo, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mikakati madhubuti itakayosaidia ongezeko la uzalishaji wa mazao hayo. Hii ni pamoja na kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora ya mbolea, kuongeza ruzuku za pembejeo na kurekebisha mfumo wa kodi ambao utatoa nafuu kwa mkulima**.**

**5.3.5 Mheshimiwa Spika**, uchache wa maafisa Kilimo na Ugani, maafisa ushirika, mafundi mchundo, wahandisi na wakaguzi wa mazao umeendela kuwa changamoto katika Halmashauri zetu. Kwa mfano, hadi Aprili, 2015 idadi ya maafisa ugani ilikuwa 9,558 kati ya mahitaji halisi ya wagani 15,802 katika kata na vijiji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa maeneo mengi yanayotumika katika kilimo yako vijijini, Kamati inaishauri Serikali kutoa kibali cha kuajiri maafisa ugani wengi zaidi katika ngazi hizo. Aidha, ikiwezekana

maafisa kilimo wote katika ngazi ya Halmashauri waajiriwe moja kwa moja mara wanapohitimu masomo yao.

**5.2.5 Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuwa na mikakati ya kuwa na masoko ya uhakika ndani nan je ya nchi kwa kuongeza thamani ya mazao.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Said J. Nkumba, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa, Mb Mjumbe
4. Mhe. Subira Mgalu, Mb ‘’
5. Mhe. Asaa Othman Hamad, Mb ‘’
6. Mhe. Abdulsalaam S. Ameir, Mb “
7. Mhe. Abdalla Haji Ali, Mb “
8. Mhe. Namelok E. M. Sokoine, Mb “
9. Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma, Mb “
10. Mhe. Sylvestry Francis Koka, Mb “
11. Mhe. Moshi S. Kakoso, Mb “
12. Mhe. Kheri Khatib Ameir, Mb “
13. Mhe. Meshack Jeremia Opulukwa, Mb “
14. Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mb “
15. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb “
16. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb ‘’
17. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb “
18. Mhe. Donald Kelvin Max, Mb “
19. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb ‘‘
20. Mhe. Haji Juma Sereweji, Mb ‘’
21. Mhe. Jitu VRAJLAL Soni, Mb ‘’
22. Mhe. Dkt Lucy Sawere Nkya, Mb ‘’

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, Mhe. Stephen Masato Wasira (Mb) na Naibu waziri Mhe. Godfrey Zambi, (Mb) kwa ushirikiano wao mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Sophia Kaduma na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Charles Mloka na Katibu wa Kamati hii Ndugu Grace Bidya akisaidiwa na Ndugu Sophia Vumbi kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati**.**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2015/2016 kama ifuatavyo : **Fungu 43** shilingi **290, 744, 623,000/=, Fungu 24** shilingi **7, 627, 990,000/= na Fungu 05** shilingi **54, 778, 260,000/=.**

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**
23 Mei, 2015

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ninamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Opulukwa! *(Makofi)*

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Taarifa hii ni ndefu, basi ningependa iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge, kama ambavyo imewasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9), Toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kususu Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe, kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuitumikia Kambi Rasmi ya Upinzania na UKAWA kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mipango mbalimbali inayoandaliwa na Serikali kuhakikisha kilimo kinakuwa cha kisasa na hivyo kuzalisha chakula cha kutosha na pia mazao mengi ya biashara na hivyo, kuongeza kipato kwa mwananchi mmoja mmoja, kukuza Pato la Taifa na kuongeza thamani ya mauzo yetu nchi za nje. Hata hivyo, matokeo haya hayaakisi thamani ya fedha zinazowekwa katika Sekta hiyo, kwani wakulima wameendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Afrika kupitia *NEPADs,* waliasisi Programu ya Kuendeleza Kilimo Mwaka 2003 kwa kikao kilichofanyika Maputo nchini Msumbiji kwa Viongozi wa nchi za Afrika kukubali na kuchukua dhamana ya kutoa utaalamu na msaada wa fedha kwa sekta ya kuendeleza kilimo kwa nchi zao kwa kutenga asilimia kumi ya bajeti ya nchi zao kuelekezwa kwenye Sekta ya KIlimo na Maendeleo Vijijini. Hadi sasa lengo hilo la kutenga asilimia kumi ya bajeti halijatekelezwa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi.

Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua, lini Serikali itaanza kutenga asilimia kumi ya bajeti yake kwenye Sekta ya Kilimo kama maazimio ya viongozi wa nchi yaliyofikiwa huko Maputo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro baina ya wakulima na wafugaji itaendelea kudumu kwa muda mrefu zaidi endapo haitapatiwa ufumbuzi, ikiwemo jitihada za viongozi kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji.

Hivi sasa katika maeneo yenye migogoro, uhasama baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi umefikia kiwango cha juu; ambapo imekuwa vigumu kwa jamii hizo kukaa pamoja kushirikiana katika shughuli za ujenzi wa taifa na hivyo kusababisha mapigano ya mara kwa mara na hata mauaji miongoni mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi haina nia ya dhati kumaliza migogoro hiyo, kwani kamati zote ambazo zilikwishaundwa na Serikali na pia asasi binafsi zilikwishatoa suluhisho lake, lakini imeshindwa kutekeleza mapendekezo ya kamati hizo. Hivyo basi, Serikali makini ijayo ya vyama vinavyoundwa na UKAWA inaahidi kutekeleza yale yote ambayo tayari yalikwishafanyiwa utafiti wa kina na kutoa suluhisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Pamba ni la pili kwa uingizaji wa fedha za kigeni baada ya Zao la Kahawa, likichangia asilimia 40 ya ajira nchini. Zao hili limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali pamoja na mambo mengine, zikiwemo tija ndogo, bei ndogo ya pamba yenyewe kwa kulinganisha na

gharama za uzalishaji, kilimo cha mkataba, uuzaji nje wa pamba ghafi kwa asilimia 75, ruzuku ndogo kutoka katika Bajeti ya Taifa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya zao na biashara ya pamba hapa nchini hayawezi kumalizwa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, kwani Wasimamizi Wakuu wa Sekta hii ya Pamba ndiyo wanaofanya biashara ya pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi kabla ya soko huria kulikuwa na mfumo maalumu wa uzalishaji wa mbegu, hali iliyofanya kuwepo kwa mbegu ya kutosha na bora kwa ajili ya kupanda. Baada ya mfumo wa uzalishaji wa mbegu kukoma, hali ya ubora wa mbegu za kupanda ilianza kuwa ya mashaka na hasa baada ya soko huria kuanza hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa upatikanaji wa mbegu za kupanda kwa sasa ni wa mbegu inayotokana na pamba iliyolimwa na mkulima wa kawaida katika mazingira duni ya utunzaji yasiyo na usimamizi wa kitaalamu. Katika mfumo huu limekuwa ni jukumu la Bodi ya Pamba kuhakikisha kuwa, kila kampuni ya uchambuaji iliyonunua pamba kutoka kwa wakulima mbalimbali katika msimu husika, inahifadhi sehemu ya mbegu iliyotokana na pamba hiyo, kisha kampuni hiyo kuzisambaza mbegu hizo katika Wilaya mbalimbali. Mfumo huu unajulikana kama mfumo wa mbegu mzunguko *(recycled seed system)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mfumo uliotajwa hapo juu, ulikuwepo mfumo mwingine rasmi wa kuzalisha mbegu za pamba. Fedha zote zilikuwa zinatolewa na Serikali kwa lengo la kuwasaidia wakulima kupata pembejeo. Hivi karibuni Serikali ilifanya juhudi za kuanzisha mfumo huu rasmi uliokuwa umekufa wa uzalishaji wa mbegu za kupanda, ambapo Kampuni ya Quton (T) Ltd ilipewa kazi hiyo ya kuzalisha mbegu tangu Mwaka 2009 hadi leo.

Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji yafuatayo:-

Kwa nini Quoton ambayo siyo Taasisi ya Serikali ipewe jukumu kubwa kama hilo wakati hawawezi kukaguliwa na Serikali? *(Makofi)*

Kwa nini kazi ya kuelimisha wakulima ifanywe na Quoton badala *Tanzania Cotton Board*?

Kwa nini Serikali isianzishe mfuko kwa ajili ya kuzalisha mbegu kwa taasisi zote kama TOSC, Ukiriguru na TCB kwenye bajeti yake ya Wizara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuanzishwa kwa kilimo cha mkataba nchini ni kuweza kumsaidia mkulima wa pamba kupata fedha nyingi kwa kuzalisha kwa tija wakati akitumia pembejeo anazokopeshwa na huduma za

ugani, kumhakikishia mnunuzi mchambuaji upatikanaji wa pamba nyingi na ubora wa kuongeza soko la pamba ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume na matarajio ya wengi, kilimo hiki kimeendelea kulalamikiwa na wakulima katika maeneo mbalimbali nchini yanayolima pamba ukiwemo Mkoa wa Simiyu ambao unaongoza kwa kulima Zao hilo la Pamba, kutokana na mikataba wanayoingia na makapuni kutoweka wazi kiasi cha fedha atakachokatwa mkulima wakati wa kuuza na kutojua bei ya pamba yake wakati wanapoingia mkataba, kitendo ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani inakipinga kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inatajwa katika Bara la Afrika kuwa katika nafasi ya pili kwa uzalishaji wa Zao la Korosho ikifuatiwa na Nigeria; lakini kilimo cha korosho kimekuwa kikikabiliwa na matatizo mengi ambayo mpaka sasa hayajapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaeleza kuwa mahitaji ya korosho Duniani yanakuwa kwa asilimia kila mwaka, ikiwa ni ishara kwamba, Tanzania inapaswa kuimarisha uwekezaji wa zao hilo. Hivi sasa Tanzania inakadiriwa kubangua asilimia mbili tu ya korosho zote nchini na kiasi kinachobaki kinauzwa nje kama mali ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na *The Agricultural Non State Actors Forum (ANSAF)* mwaka 2008, kuuza korosho nje ya nchi bila kubanguliwa kuna hasara zake, kwani wakulima wamekuwa wakipata kipato kidogo huku Serikali ikikadiriwa kupoteza Dola za Marekani milioni 110 kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo miaka ya 70 wakati wa utawala wa Mwalimu Nyerere, Mikoa ya Kusini ilijenga viwanda 12 vya kubangua korosho ili kuongeza ubora wa mazao hayo, lakini viwanda hivyo vimefungwa na vimekuwa vikitumika kama maghala. Aidha, inasemekana viwanda vingi vimeuzwa kwa watu binafsi kama ilivyokuwa kwa viwanda vya Lindi, Mtama pamoja na Nachingwea.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza Watanzania kwa nini iliuza viwanda hivyo ilhali vilikuwa ni muhimu sana katika uongezaji wa thamani ya Zao la Korosho? Pia Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuvirudisha viwanda vyote ilivyoviuza kinyemela kwa wadau binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebainika kuna wizi mkubwa wa *export levy* ambapo korosho zilizouzwa nje mwaka 2012 ni tani 140,000. Cha kushangaza ni tani 80,000 tu ndizo zilizolipiwa ushuru wa forodha katika Bandari ya Mtwara na

tani 60,000 zilizobaki fedha hazikulipiwa ushuru kabisa. Jambo hili limezisababishia Halmashauri zinazolima korosho kukosa mapato.

Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji; kwa nini korosho isafirishwe kupitia Bandari ya Dar es Salaam badala ya Bandari ya Mtwara ambako ndipo kituo kikubwa cha usafirishaji wa korosho kwenda nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa Zao la Kahawa umekuwa ni wastani wa tani 40,000 kwa mwaka. Zaidi ya asilimia 90 ya kahawa yote inayozalishwa hapa nchini inazalishwa na wakulima wadogo wadogo. Sekta ndogo ya Kahawa inatoa kipato cha moja kwa moja kwa zaidi ya familia 80,000 na kutegemewa na zaidi ya Watanzania milioni 2.5 kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Kaskazini ambayo ndiyo mkulima mkubwa wa kahawa nchini, wameamza kung'oa miche ya kahawa na badala yake kuanza kupanda mbogamboga na matunda kwa sababu ya gharama ya pembejeo kuwa kubwa sana. Miti mingi ya kahawa imezeeka na inatakiwa ibadilishwe na miche mipya iliyo bora zaidi. Kasi ya ubadilishaji wa miche hii ya zamani na kupanda mipya ni dogo sana.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iviwezeshe vituo vya utafiti kama *TACRI* kilichopo Lyamungo ili kuongeza kasi ya kubadilisha miche hii iliyozeeka kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hujuma zinazofanywa na Makampuni makubwa katika Minada; katika mnada wa kahawa kuna kitu kinachoitwa *buy back-system*. Mfumo huu umebuniwa na makampuni makubwa ambayo yanasajili makampuni madogo madogo ambayo yananunua kahawa ya wakulima moja kwa moja na kuipeleka katika Mnada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hujuma hii inayasaidia makampuni hayo kununua kwa bei ndogo ya mnada na wanapata bei kubwa wanapouza nje *(export price)*. Hujuma hizi Serikali ya Chama cha Mapinduzi na vyombo vyake husika inazifahamu lakini haichukui hatua za kulinusuru zao hili ili wakulima waweze kupata bei inayoendana na gharama za uzalishaji, badala yake inakaa kimya. Hii ina maana kuwa wahusika nao wananufaika binafsi na mfumo huu wa *buy-back*.

Kambi Rasmi inasema, kwa kuwa ukweli wa hujuma hizi na suluhisho upo kwenye makabrasha, basi suluhisho ni rahisi sana pale UKAWA itakapopata ridhaa ya Wananchi kuendesha Serikali itakayokuwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tasnia ya sukari ni muhimu katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi. Wastani wa nguvu kazi ya watu 2 - 3 katika familia kwenye maeneo ambayo yanalima miwa, tasnia hii inatoa ajira ambazo siyo za moja kwa moja *(secondary employment)*. Aidha, tasnia hii inawaingizia wakulima kiasi cha takribani Dola za Kimarekani milioni 2.7 kwa mwaka. Pia shughuli zingine zinazohusiana na tasnia hii ya sukari, zinaliingizia Taifa mapato ya takribani shilingi bilioni 12.7 ambayo ni *total tax revenue* kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku chache zilizopita wamiliki wa viwanda vya sukari nchini walisema viwanda vyao viko hatarini kufa kutokana na Serikali kuendelea kuagiza sukari kutoka nje ya nchi na kupelekea sukari ya ndani kukosa soko na kuvifanya viwanda hivyo kupunguza wafanyakazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya wamiliki wa viwanda vya sukari yanayotolewa ni kutokana na soko la ndani kutekwa na sukari inayoingizwa kutoka nje ya nchi na wafanyabiashara wakubwa. Hata Serikali yenyewe ilishakiri kwamba, sukari nyingi inayopitia Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi jirani *(transit)*, imekuwa ikishushwa na kutumika hapa nchini kiasi cha viwanda vya ndani kushindwa kushindana na sukari hizo kwenye soko la ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa Viongozi wa Kisiasa kwenye Uongozi wa Ushirika kulileta manung'uniko mengi kwa Wanaushirika wa Tumbaku Mkoani Tabora. Kwa mfano, Viongozi wa CCM wa Mkoa na Madiwani wa CCM walikuwa ndiyo Viongozi wa Ushirika wakiacha wakulima wakiibiwa na kudhulumiwa fedha zao.

Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika iliyopitishwa katika Bunge lako Tukufu mwaka 2014, imewaweka nje lakini mpaka sasa hatua za kuwafikisha mahakamani Viongozi wa Ushirika walioshiriki ubadhirifu huo bado zinasuasua. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwafikisha mahakamani mara moja wale wote walioshiriki katika ubadhirifu wa mali za washirika na itoe taarifa kwa umma kuhusu utekelezaji wa hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inaweza kuongeza uzalishaji wa Zao la Chai na kuliingizia Taifa fedha za kigeni kama nchi nyingine za Kiafrika, iwapo Serikali itaweka mazingira mazuri kwa kutumia fursa zilizopo. Uzalishaji wa Zao la Chai Duniani umeongezeka katika kipindi cha miaka mitano kutoka tani milioni 4.6 mwaka 2009 hadi tani 4.91 mwaka 2013, wakati kwa Tanzania imechangia kidogo huku kukiwa na fursa nyingi zinazopotea.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mazao Mchanganyiko na Wakala wa Chakula, yaani *NFRA* ni vyombo muhimu sana kwa ustawi wa Jamii ya Watanzania na hasa jamii maskini ili kuhakikisha usalama wa chakula. Hata

hivyo, kwa sehemu kubwa kuna manung'uniko ya kiutendaji kwenye Bodi ya Mazao Mchanganyiko na uwepo wa wafanyabiashara wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko unaweza kudidimiza jitihada za vijana kujikwamua na umaskini kutokana na kununua, kutunza, kuchakata na kuuza bidhaa, baada ya kuziongezea thamani. Kwa kuwa nchi hii inalenga kutengeneza ajira, kuna haja ya kuhakikisha shughuli za Bodi ya Mazao Mchanganyiko inaunganisha vijana na fursa badala ya kuwaondoa vijana kwenye ajira zao.

Mheshimiwa Spika, ni bora Serikali ikaweka wazi kuwa siku hizi imeanza kufanya biashara na kushindana na wananchi wake. Vinginevyo, Wizara za Kilimo, Viwanda na Kitengo cha Uwezeshaji, ziweke mikakati ya kuibua makampuni ya kizalendo ili yaweze kuchangia kuleta ajira na kuboresha Uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sukari na mchele ni miongoni mwa bidhaa zinazotengeneza sehemu kubwa ya kapu la mlaji *(consumer's basket)* kwa Watanzania. Hata hivyo, siku za karibuni uingizaji wa bidhaa hizi unatekelezwa kwa mfumo ambao unadidimiza jitihada za wakulima maskini wa Kitanzania na hivyo kuwanyang'anya kipato chao. Mfano, Wakulima wa Miwa kule Kilombero wamefikia kushindwa kumwuzia mwekezaji miwa, kwa kuwa mwekezaji ameshindwa kuuza sukari iliyoko kiwandani kutokana na uingizwaji wa sukari yenye ruzuku kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, suala la mchele pia halina tofauti na sukari, kwa kuwa mwaka 2014/15 wakulima wengi wameshindwa kuuza mchele kwa bei ya faida kutokana na uingizwaji wa mchele kwa njia za panya na ukwepaji wa ushuru. Wakulima walishindwa kuuza mchele kwa mwaka 2014/15 wakajikuta wakiuza gunia moja kwa shilingi 30,000 badala ya shilingi 90,000. Kwa kuwa wengi wa wakulima hawa wamelima kwa mkopo, inakuwa ngumu kuweza kurudisha gharama za uzalishaji na hivyo wametumbukizwa kwenye lindi la madeni pamoja na umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mazao ya chakula na hapa nitapenda kuongelea Zao la Muhogo. Kilimo cha Muhogo kwa chakula na biashara. Nchini Tanzania, muhogo unatajwa kuwa zao la pili kwa kuchangia Pato la Taifa kwa asilimia 19 baada ya mahindi. Pamoja na hayo zao, hili lina faida nyingi kijamii na hata kiuchumi na kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, muhogo ni zao ambalo linaweza kuzalisha bidhaa zaidi ya 300, zikiwemo zile za chakula na ambazo si za chakula. Majani yake hutumika kama mboga na dawa pia. Katika viwanda, mazao yanayopatikana katika mizizi yenyewe, miti na majani, huweza kuzalisha bidhaa za anuwai.

Baadhi ni vifaa vya nguo, karatasi, mafuta, kilevi, dawa za binadamu, plastiki na kadhalika. Vilevile wanga wa muhogo hutumika kutengeneza dawa za madoa, gundi katika samani, rangi za awali katika kuta za nyumba na sukari *(Sugar Syrup)*.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa wakulima walio wengi wanajipatia kipato kizuri kutokana na umaarufu na umuhimu wa Zao la Muhogo Duniani kote, ambapo wafanyabiashara kutoka Bara la Asia kama vile China, wana mahitaji makubwa ya Zao la Muhogo kwa ajili ya viwanda nchini mwao. Kambi Rasmi inaitaka Serikali kutilia mkazo zao hili kwa faida ya wakulima na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, *GMO* ni kifupi cha maneno ya Kiingereza yaani *Genetically Modified Organisms.* Viumbe hivi ni zao la teknolojia mpya ya kibaliojia ijulikanayo kama *Biotechnology.* Wanasayansi mbalimbali katika Ukanda wa Afrika Mashariki wamekuwa wakitafiti juu ya uwezekano wa kutumia teknolojia ya Uhandisi wa Jeni *(GMO)* katika kilimo. Hatua hii inatokana na teknolojia hiyo kuwa na upinzani kwa kile kinachoelezwa kuwa ikitumika inaweza kusababisha athari za kiafya na za kimazingira.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, watafiti mbalimbali Duniani wamekuwa wakiitetea teknolojia hiyo kuwa ni salama na tayari baadhi ya nchi kama vile Marekani, India na China zimeshaanza kutumia teknolojia hiyo katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, nchi mbalimbali zimekuwa zikitamani kuona wananchi wake ….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. MESHACK J. OPULUWA - MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA MHESHIMIWA MESHACK JEREMIAH OPULUKWA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(*Inatolewa Chini ya Kanuni ya 99(9) toleo la mwaka 2013*

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzanikususu Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani nyingi kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freema Mbowe, kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuitumikia Kambi Rasmi ya Upinzania na UKAWA kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa salaam za pole kwa Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu kwa kusimamishwa kazi siku ya jumamosi ya tarehe 18.05.2015 kwenye kikao walichokaa na Mbunge wao ili kumwelezea kero zao kwa lengo la kuziwakilisha Bungeni. Hakika haki ya walimu hawa haitapotea kamwe ila yaweza kucheleweshwa tu.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha kabisa na kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Meatu kwa ushirikiano mkubwa na imani waliyonayo kwangu kama mwakilishi wao. Niliwaahidi kuwatumikia kwa moyo wangu wote na naendelea kuwaahidi kuwa imani yao kwangu haitopotea bure na Mungu aendeele kuwabariki.

**Mheshimiwa Spika**, Kumekuwa na mipango mbalimbali inayoandaliwa na Serikali kuhakikisha kwamba Kilimo kinakuwa cha kisasa na hivyo kuzalisha chakula cha kutosha na pia mazao mengi ya biashara hivyo kuongeza kipato kwa mwananchi mmoja mmoja, kukuza pato la Taifa na kuongeza thamani ya mauzo yetu nchi za nje.Lakini matokeo yake hayaakisi thamani ya fedha zinazowekwa katika sekta hiyo, kwani wakulima wameendelea kuwa masikini.

**Mheshimiwa Spika**, Umoja wa Afrika kupitia NEPAD's waliasisi program ya kuendeleza Kilimo mwaka 2003 (CAADP) kwa kikao kilichofanyika Maputo nchini Msumbiji kwa Viongozi wa nchi za Afrika kukubalina kuchukua dhamana ya kutoa utaalamu na msaada wa fedha kwa sekta ya kuendeleza kilimo kwa nchi zao kwa kutenga asilimia 10 ya bajeti ya nchi zao kuelekezwa kwenye sekta ya kilimo na maendeleo vijijini. Hadi sasa lengo hilo la kutenga 10% ya bajeti halijatekelewa na serikali hii.**Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua, lini**

**serikali itaanza kutenga 10% ya bajeti yake kwenye sekta ya kilimokama ambavyo maazimio ya viongozi wa nchi yaliyofikiwa huko Maputo yanavyotaka?**

**Mheshimiwa Spika,**Wadau mbalimbali wa kilimo wamekuwa tukiishauri Serikali kuyapatia ufumbuzi matatizo ambayo tayari watafiti walishayatolea suluhu ya nini kifanyike lakini kutokana na udhaifu wa kiutendaji wa Serikali ya CCM imeshindwa. Hivyo basi sasa ni muda mwafaka kwa vyama vinavyounda UKAWA kuongoza Serikali ili kuyaweka kwa vitendo yale yote ambayo tumekuwa tukishauri kuyatekeleza.

**Mheshimiwa Spika,**Hakuna suluhisho ambalo halijulikani kwa Serikali,tatizo kubwa ni kwamba watendaji waandamizi wa Serikali wanafaidika binafsi kutokana na matatizo hayo, hivyo basi **Kambi Rasmi inawataka wananchi watuunge mkono ili kuondokana na madhira hayo ya miaka mingi yaliyosababishwa na utendaji usiojali wa Serikali ya CCM.**

## 2. MIGOGORO KATI YA WAKULIMA, WAFUGAJI NA WAWEKEZAJI

**Mheshimiwa Spika,** Migogoro baina ya wakulima na wafugaji itaendelea kudumu kwa muda mrefu zaidi endapo haitapatiwa ufumbuzi, ikiwemo jitihada za viongozi kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji. Hali ya sasa ya migogoro hiyo ni mbaya zaidi na inatishia kutoweka kwa amani, umoja na utangamano wa wananchi katika maeneo yenye migogoro na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Hivi sasa katika maeneo yenye migogoro, uhasama baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi umefikia kiwango cha juu; ambapo imekuwa vigumu kwa jamii hizo kukaa pamoja katika mikutano, kushirikiana katika shughuli za ujenzi wa taifa au za kijamii, kutumika kwa lugha za kibaguzi na ukabila na hivyo kusababisha mapigano ya mara kwa mara na hata mauaji miongoni mwao kama ilivyo sasa katika mikoa ya Morogoro, Manyara, Arusha Shinyanga, Simiyu na maneo mengi nchini.
**Mheshimiwa Spika,** Matatizo ya migogoro ya ardhi baina ya wakulima/wafugaji na wawekezaji hayawezi kupatiwa ufumbuzi kwani inaonekana watendaji waandamizi wa Serikali ni sehemu ya matatizo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa Serikali hii ya CCM haina nia ya dhati kumaliza migogoro hiyo, kwani kamati zote ambazo zilikwishaundwa na Serikali na pia asasi binafsi zilikwishatoa suluhisho lake, lakini imeshindwa kutekeleza mapendekezo ya kamati hizo. Hivyo basi, Serikali makini ijayo ya vyama vinavyounda UKAWA inaahidi kutekeleza yale yote ambayo tayari yalikwishafanyiwa utafiti wa kina na kutoa suluhisho.

## 3. MAZAOYA BIASHARA

### A i): Pamba

**Mheshimiwa Spika**, Zao la pamba ni la pili kwa uingizaji wa fedha za kigeni baada ya zao la kahawa, likichangia asilimia 40 ya ajira nchini, limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali pamoja na mambo mengine zikiwemo tija ndogo, bei ndogo ya pamba yenyewe kwa kulinganisha na gharama za uzalishaji, kilimo cha mkataba, uchafuzi wa pamba, uuzaji nje wa pamba ghafi kwa asilimia 75, zana na pembejeo duni, utegemezi wa mvua, mabadiliko ya tabia nchi, udanganyifu katika mizani na kutokuwa na taarifa zinazohusu mabadiliko ya bei. Ushuru mkubwa unaoongeza mzigo kwa mkulima; Uwezo hafifu wa viwanda vya kuchambua pamba; Ruzuku ndogo kutoka katika bajeti ya Taifa; Ushindani usiozingatia Kanuni; Kulegea kwa Miongozo na Kanuni za zao la pamba n.k.

**Mheshimiwa Spika,** Suluhisho la matatizo haya yote yamefanyiwa utafiti,na Serikali ya CCM inaelewa lakini inashindwa kusimamia utekelezaji wake.Matatizo ya zaona biashara ya Pamba hapa nchinihayawezi kumalizwa na Serikali hii ya CCM kwaniWasimamizi wakuu wa Sekta hii ya Pamba ndio wanaofanya biashara ya Pamba. Hivyo sio rahisi kwa watu hao kutoa suluhisho la kudumu.

### ii) Pembejeo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa miaka mingi kabla ya soko huria kulikuwa na mfumo maalumu wa uzalishaji wa mbegu hali iliyofanya kuwepo na mbegu ya kutosha na bora kwa ajili ya kupanda. Baada ya mfumo wa uzalishaji wa mbegu kukoma, hali ya ubora wa mbegu za kupanda ilianza kuwa ya mashaka na hasa baada ya soko huria kuanza hadi sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa upatikanaji wa mbegu za kupanda kwa sasa ni wa mbegu inayotokana na pamba iliyolimwa na mkulima wa kawaida katika mazingira duni ya utunzaji yasio na usimamizi wa kitaalamu. Katika mfumo huu limekuwa ni jukumu la Bodi ya pamba kuhakikisha kuwa kila kampuni ya uchambuaji iliyo nunua pamba kutoka kwa wakulima mbalimbali katika msimu husika inahifadhi sehemu ya mbeguiliyotokana na pamba hiyo, kisha kampuni hiyo kuzisambaza mbegu hizo katika Wilaya mbalimbali hadi vijiji kwa maelekezo ya Bodi ya pamba kwa kushirikiana na kamati za mazao za Wilaya husika. Mfumo huu unajulikana kama mfumo wa mbegu mzunguko (recycled seed system).

**Mheshimiwa Spika,**Ikiacha mfumo nilioutaja hapo juu, ulikuwepo mfumo mwingine (rasmi)wa kuzalisha mbegu za pamba. Fedha zote zilikuwa zinatolewa

na serikali kwa lengo la kuwasaidia wakulima kupata pembejeo. Hivi karibuni Serikali ilifanya juhudi za kuanzisha mfumo rasmi wa uzalishaji wa mbegu za kupanda ambapo kampuni ya Quton (T) LTD ilipewa kazi hiyo ya kuzalisha mbegu tangu Mwaka 2009 hadi leo.

**Kambi rasmi ya upinzani inahoji yafuatayo;**

- **kwa nini Quoton ambayo siyo taasis ya Serikali ipewe jukumu kubwa kama hilo wakati hawawezi kukaguliwa na Serikali**?
- **Kwa nini kazi ya kuelimisha wakulima ifanywe na quoton badala TCB**?
- **Kwa nini serikali isianzishe mfuko kwa ajili ya kuzalisha mbegu kwa taasis zote TOSC, UKIRIGURU, TCB, kwenye bajeti ya wizara?**

**iii) Kilimo cha Mkataba**

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la kuanzishwa kilimo cha mkataba nchini ni kuweza kumsaidia mkulima wa pamba kupata pesa nyingi kwa kuzalisha kwa tija wakati akitumia pembejeo anazokopeshwa na huduma za ugani, kumhakikishia mnunuzi, mchambuaji upatikanaji wa pamba nyingi na ubora na kuongeza soko la pamba ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kinyume na matarajio ya wengi, kilimo hiki kimeendelea kulalamikiwa na wakulima katika maeneo mbalimbali yanayolima pamba ukiwemo mkoa wa Simiyu ambao unaongoza kwa kulima zao hilo,kutokana na mikataba wanayoingia na makapuni kutoweka wazi kiasi cha fedha atakachokatwa mkulima wakati wa kuuza, ili kulipa mkopo wa pembejeo za mbegu,viuadudu na huduma za ugani alizokopeshwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kilimo cha mkataba siyo kibaya ni mikataba mibovu ambayoinamgandamiza na kumnyonya mkulima na kumpendelea mchambuaji wa pamba. Mkulima hajui bei ya pamba yake wakati wanapoingia mkataba kitendo ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani inapingwa kwa nguvu zote.

**B) Korosho**

**Mheshimiwa Spika,**Tanzania inatajwa katika Bara la Afrika kuwa katika nafasi ya pili kwa uzalishaji wa zao hilo, ikifuatiwa na Nigeria. Lakini kilimo cha korosho kimekuwa kikikabiliwa na matatizo mengi ambayo mpaka sasa hayajatatuliwa. Wakulima wa zao la korosho nchini wako hatarini kupoteza soko duniani kufuatia udanganyifu unaodaiwa kufanyika katika maghala ya kuhifadhi zao hilo wakati zikisubiri kusafirishwa kwenda nje.

**Mheshimiwa Spika,**Takwimu zinaeleza kuwa mahitaji ya korosho duniani yanakuwa kwa 8% kila mwaka, ikiwa ni ishara kwamba Tanzania inapaswa

kuimarisha uwekezaji wa zao hilo.Hivi sasa Tanzania inakadiriwa kubangua 2%i tu ya korosho yote nchini na kiasi kinachobaki kinauzwa nje kama mali ghafi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na the Agricultural Non State Actors Forum (ANSAF) mwaka 2008, kuuza korosho nje ya nchi bila kubanguliwa kuna hasara zake kwani wakulima wamekuwa wakipata kipato kidogo huku serikali ikikadiriwa kupoteza dola 110 milioni, kila mwaka. Utafiti huo ulipewa kichwa cha habari. "Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara ya Korosho Tanzania". "Vikwazo vya kujenga viwanda vya kubangua korosho nchini, vimesababishwa na udhaifu wa sera, ukosefu wa fedha na kutokuwapo kwa uzoefu katika soko la kimataifa," sehemu ya utafiti, inaeleza.

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo miaka ya 70 wakati wa utawala wa Mwalimu Nyerere, mikoa ya kusini ilijenga viwanda 12 vya kubangua korosho(processing industries)  ili kuongeza ubora wa mazao hayo lakini viwanda hivyo vimefungwa na vimekuwa vikitumika kama maghala (godows) tu. Aidha inasemekana viwanda vingine vimeuzwa kwa watu binafsi wakiwemo waliokuwa viongozi waandamizi wa Serilakali ya na CCM na wale CCM kwa kiwanda cha Lindi, Mtama na Nachingwea. **Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza watanzania kwanini iliuza viwanda hivyo ili hali vilikuwa ni muhimu sana katika uongezaji wa thamani ya zao la korosho ili kuwaongezea kipato wakulima?**

**Pia Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuviruddisha viwanda vyote ilivyoviuza kinyamela kwa watu binafsi kwa faida wa wakulima ya Korosho nchini.**

**Mheshimiwa Spika**, imebainika kuwa wizi mkubwa wa export levy ambapo korosho zilizouzwa nje mwaka 2012 ni tani 140,000. Cha kushangaza ni tani 80,000 tu ndizo zilizolipiwa ushuru wa forodha katika bandari ya Mtwara, na tani 60,000 zilizobaki fedha hazikulipiwa ushuru.Jambo hili limezisababishia halmashauri zinazolima korosho kukosa mapato. **Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, kwa nini korosho isafirishwe kupitia bandari ya Dar es Salaam badala ya bandari ya Mtwara ambako ndipo kituo kikubwa cha usafirishaji wa korosho kwenda nje?**

**Mheshimiwa Spika**, Zao hili linakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na ukosefu wa viwanda vya kubangulia korosho na kusababisha wakulima kuuza korosho ambazo hazijabaguliwa.Changamoto nyingine katika zao la korosho ni mfumo wa stakabadhi ghalani. Mfumo huu umewaathiri wakulima kwa kiasi kikubwa kwani umeshindwa kukidhi mahitaji ya soko huria na wakulima kushindwa kunufaika na soko.

**Mheshimiwa Spika**, Utafiti huo wa ANSAF unaonesha kuwa bei anayopewa mkulima ni asilimia 46% tu kati ya 100. Makato yanayokula kwa Mkulima yako kama ifuatavyo;

1. Gharama za soko yaani vyama vya msingi na ghala ni shilingi 286/kg sawa na asilimia 34%

2. Kodi anayotozwa mkulima ni 4%

3. Mchakato wa gharama za kusafirisha nje 6%

**Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji kamakwa makato haya ni kweli Mkulima anaweza kujikomboa kutokana na zao la Korosho?**
**Mheshimiwa Spika**, Hali halisi ilivyo katika matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni tofauti kabisa na sheria inavyotaka. Kwani wananchi wanalazimishwa kuuza mazao yao kwenye vyama vya msingi badala ya wakulima kwenda moja kwa moja kwenye Ghala. Na katika kuuza kwenye vyama vya msingi wanatozwa ushuru na wakipeleka kwenye ghala wanalipishwa ushuru. Aidha bei inayotolewa na vyama ni ndogo sana ambayo sio shindani. Hii inapelekea kukosa maana kwa uanzishwaji wa mfumo huu. **Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, kwa kuwa sheria iko wazi na Serikali ya CCM imeshindwa kuisimamia ni muda mwafaka kukaa pembeni na Serikali ijayo ya UKAWA ikaitekeleza sheria hiyo kwa maendeleo ya wakulima na kilimo husika.**

**C) Kahawa**
**Mheshimiwa Spika,** Kahawa ni zao la pili kwa mauzo ya nje nyuma ya Tumbaku kwa mazao ya kilimo na linachangia asilimia 4% ya jumla ya mauzo ya nje kwa kipindi cha mwaka 2004-2011. Uzalishaji wa zao la kahawa umekuwa ni wastani wa tani 40,000 kwa mwaka na takriban asilimia 100 ya uzalisahaji huo ni kwa mauzo ya nje. Mnada wa Kahawa yote inayozalishwa hapa nchini huuzwa kwa mnada Mjini Moshi.

**Mheshimiwa Spika**, zaidi ya asilimia 90% ya kahawa yote inayozalishwa hapa nchini inazalishwa na wakulima wadogo. Sekta ndogo ya Kahawa inatoa kipato cha moja kwa moja kwa zaidi ya familia 80,000 na kutegemewa na zaidi ya watanzania 2.5 million kuendesha maisha yao (URT-Coffee Board and TACRI, 2010).

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania imegawanyika katika maeneo makuu matatu ya kanda za uzalishaji wa Kahawa, ambazo ni; 1. Nyanda za Kaskazi yenye mikoa ya Kilimajaro na Arusha: 2. Nyanda za Kusini yenye mikoa ya Mbeya, Ruvuma na Wilaya ya Ludewa; 3. Ukanda wa Ziwa Viktoria wenye Mkoa wa Kagera na Mara hasa wilaya ya Tarime. Pia kuna maeneo mengine yenye fursa kubwa

kwa uzalishaji wa Kahawa ambayo ni: Tanga, Iringa, Manyara, Morogoro, Kigoma, Mwanza, Rukwa na Mara.

**Mheshimiwa Spika**, Mikoa ya Kaskazini ambayo ndiyo mkulima mkubwa wa Kahawa nchini wameamza kung'oa miche ya kahawa na badala yake kuanza kupanda mbogamboga na matunda kwa sababu ya gharama ya pembejeo kuwa kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Miti mingi ya Kahawa imezeeka na inatakiwa ibadilishwe na miche mipya iliyo bora zaidi. Kasi ya ubadilishaji wa miche hii ya zamani na kupanda mipya ni dogo sana. **Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iziwezeshe kituo cha utafiti kilichopo Lyamungo (TACRI) ili wafanye kazi ya kubadilisha miche iliyozeeka kwa kasi.**

**Mheshimiwa Spika**, KNCU inalalamikiwa kwa kuuza magari, mashamba na nyumba za ushirika bila kufuata utaratibu. Kambi **Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuingilia kati swala hili haraka iwezekanavyo ili kulinusuru zao hili la kahawa na sharia ichukue mkondo wake kwa wale wote ambao wametumia madaraka yao vibaya na kufuja mali za Ushirika.**

**4. HUJUMA ZINAYOFANYWA NA MAKAMPUNI MAKUBWA KATIKA MNADA**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mnada wa kahawa kuna kitu kinachoitwa "buy back-system" mfumo huu umebuniwa na makampuni makubwa ambayo yanasajili vikampuni vidogo vinavyonunua kahawa ya wakulima moja kwa moja na kuipeleka katika mnada wa kahawa na kwakuwa kampuni hizo ni mali ya Kampuni moja kubwa. Jambo hilo hushusha kwa makusudi bei ya mnada na hivyo Kampuni Mama ununua kahawa hiyo kwa bei ambayo vyama vya ushirika hushindwa kuinunua.

**Mheshimiwa Spika**, Hujuma hii inayasaidia makampuni hayo kununua kwa bei ndogo ya mnada na wanapata bei kubwa wanapouza nje (Export price).Hapa wao wanavizuia vyama vya ushirika kupata bei nzuri kwenye mnada (premium prices at auction).

**Mheshimiwa Spika**, Hujuma hizi Serikali ya CCM na vyombo vyake husika inazifahamu lakini haichukui hatua za kulinusuru zao hili ili wakulima waweze kupata bei inayoendana na gharama za uzalishaji, badala yake inakaa kimya maana yeke ni kuwa wahusika nao wananufaika binafsi mfumo huo wa "buy-back". **Kambi Rasmi inasema kwakuwa ukweli wa hujuma hizi na suluhisho upo kwenye makabrasha basi suluhisho ni rahisi pale UKAWA utakapopata ridhaa ya wananchi kuendesha Serikali.**

**5. MATUMIZI YA KAHAWA KWA SOKO LA NDANI**
Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu za FAO inaonesha kuwa ni asilimia 4.2% ya Kahawa yote inayozalishwa nchini ndiyo inayotumika katika soko la Ndani. Aidha tawkimu zinaendelea kusema kuwa tangu mwaka 2003 kiasi cha kahawa inayotumika nchini inaendelea, Jambo hili linatokana na kupungua kwa utamaduni wa unywaji wa kahawa kwenye jamii zetu. Hivyo basin i jukumu la watanzania wote hasa vyombo vyenye thamana ya kuendeleza zao hili kuhamasisha watanzania kunywa kahawa suala hili litaongeza uwezo kwa wazalishaji wa ndani na si kutegemea soko la nje ambalo tayari limekwishahujumiwa.

**D) Miwa/ Sukari**
**Mheshimiwa Spika**, Tasnia ya sukari ni muhimu katika Nyanja zote za kijamii na kiuchumi, sekta inazalisha ajiraza moja kwa moja kwa watu takriban 14,000 na inategemewa na familia zipatazo 30,000. Wastani wa nguvu kazi ya watu 2-3 katika familia kwenye maeneo ambayo yanalima Miwa, tasnia hii inatoa ajira ambazo sio za moja kwa moja (secondary employment) zaidi ya ya watu 80 000. Aidha, tasnia hii inawaingizia wakulima kiasi cha shilingi bilioni 4 kila mwaka, takriban USD 2.7MILIONI, pia shughulizi zingine zinazohusiana na tasnia hii ya sukari zinaliingizia taifa mapato ya takriban shilingi 12.2 bilioni (1.7%of total tax revenue) kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Mahitaji ya sukari kwa mwaka ni tani 590, 000, viwanda vya ndani huzalisha tani 300,000, sukari inayoagizwa kwa ajili ya viwanda ni tani 170,000, hivyo mahitaji yanayobaki huagizwa nje ya nchi.Siku chache kupita baada ya Wamiliki wa Viwanda vya Sukari nchini kusema viwanda Vyao viko hatarini kufa kutokana na serikali Kuendelea kuagiza sukari ya nje ya nchini na kupelekea Sukari ya ndani kukosa soko nakuvifanya Viwanda hivyo kupunguza wafanyakazi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeshasema kwamba kamwe haitoacha kuagiza Sukari toka nje nchi kutokana na Viwanda Vilivyopo nchini kukosa uwezo wa kuzalisha Sukari za Matumizi ya Viwandani kwani Viwanda vya ndani vinauwezo wa kuzalisha sukari za majumbani peke yake. Serikali imekiri kwamba tatizo inalokumbana nalo ni Uingizaji wa Sukari Kinyemela kutoka nje ya nchini ambao ndio limekuwa kikwazo katika Viwanda hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, Malalamiko ya wamiliki wa viwanda vya sukari yanayotolewa kutokana na soko la ndani kutekwa na sukari inayoingizwa kutoka nje ya nchi na wafanyabiashara wakubwa.Hata Serikali inakiri kwamba sukari nyingi inayopitia bandari ya Dae rs Salaam kwenda nchi jirani (trasit) imekuwa ikishushwa na kutumika hapa nchini kiasi cha viwanda vya ndani kushindwa kushindana na sukari hizo kwenye soko la ndani. **Hii inadhihirisha jinsi**

**gani Serikali ya CCM ilivyochoka kiasi kushindwa kutekeleza majukumu yakeipasavyo.**

**E) Tumbaku**

Kuwepo kwa viongozi wa kisiasa kwenye uongozi wa ushirika kulileta manung'uniko mengi kwa wana ushirika wa Tumbaku. Kwa mfano, viongozi wa CCM wa Mkoa na Madiwani wa CCM walikuwa ndiyo viongozi wa ushirika wakiacha wakuklima wakiibiwa na kudhulumiwa fedha zao. Sheria mpya ya vyama vya ushirika iliyopitishwa katika Bunge lako tukufu mwaka jana imewaweka nje lakini mpaka sasa hatua za kuwafikisha mahakamani viongozi wa ushirika walioshiriki ubadhilifu bado zinasuasua**. Kambi Rasmi ya Upinzania inatitaka Serikali kuwafikisha mahamani mara moja wale wote walioshiriki katika ubadhilifu wa mali za wanaushirika na itoe taarifa kwa umma kuhusu utekelezaji wa hatua hiyo.**

**F) Chai**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania inaweza kuongeza uzalishaji wa zao la chai na kuliingizia Taifa fedha za kigeni kama nchi nyingine za Kiafrika, iwapo Serikali itaweka mazingira mazuri kwa kutumia fursa zilizopo. Uzalishaji wa zao la chai duniani umeongezeka katika kipindi cha miaka mitano kutoka tani milioni 4.6 mwaka 2009 hadi tani 4.91 mwaka 2013 wakati kwa Tanzania imechangia kidogo, huku kukiwa na fursa nyingi zinazopotea.

**6. BODI YA MAZAO MCHANGANYIKO (COPB) + WAKALA WA CHAKULA (NFRA)**

**Mheshimiwa Spika,**Vyombo hivi ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii ya watanzania, na hasa jamii masikini ili kuhakikisha usalama wa chakula. Hata hivyo, kwa sehemu kubwa, kuna muingiliano wa kiutendaji, na hasa Cereals and Other Produce Board (CoPB) na uwepo wa wafanyabiashara wadogo na wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Uwepo wa CoPB unaweza kudidimiza jitihada za vijana kujikwamua na umasikini kutokana na kununua, kutunza, kuchakata na kuuza bidhaa baada ya kuziongezea thamani. Kwa kuwa nchi hii inalenga kutengeneza ajira sawa ilivyo kwenye FYDP, MKUKUTA na TDV2025, kuna haja ya kuhakikisha shughuliza za Bodi ya mazao mchanganyiko inaunganisha vijana na fursa badala ya kuwaondoa vijana kwenye ajira.

**Mheshimiwa Spika,** Pia ni bora serikali ikaweka wazi kuwa siku hizi imengia kufanya biashara na kushindana na wananchi wakekwenye ufanyaji wa biashara. Vinginevyo wizara za kilimo, viwanda na kitengo cha uwezeshaji (commission of planning and empowerment) ziweke mikakati ya kuibua makampuni ya kizalendo (madogo na ya kati) ili yaweze kuchangia kuleta ajira na kuboresha uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inajiuliza kama Serikali inafanya biashara ya mazao hasa ya nafaka ni sababu zipi iliviuza viwanda vyake vyote vilivyokuwa vinaongeza thamani ya mazao? Hii ni sababu ya kwamba Serikali ya CCM imechoka kufikiri na inasahau upesi maamuzi yake, hivyo basi tunawataka watanzania waiweke pembeni na Serikali mpya ijayo ya Upinzani ifanye kazi.

**7. UINGIZWAJI WA MCHELE NA SUKARI**

**Mheshimiwa Spika,** Bidhaa za Sukari na Mchele ni miongoni mwa bidhaa zinazotengeneza sehemu kubwa ya kapu la mlaji (consumer's basket) wa kitanzania. Hata hivyo siku za karibuni uingizaji wa bidhaa hizi umetekelezwa kwa mfumo ambao unadidimiza jitihada za wakulima masikini wa kitanzania na hivyo kuwanyang'anya kipato chao. Mfano, wakulima wa miwa kule Kilombero wamefikia kushindwa kumwuzia mwekezaji miwa kwa kuwa mwekezaji ameshindwa kuuza sukari iliyoko kiwandani kutokana na uingijzaji wa sukari yenye ruzuku ya hali ya juu kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,**Suala la mchele pia, halina tofauti na sukari, kwa kuwa, mwaka 2014/15 wakulima wengi wameshindwa kuuza mchele kwa bei ya faida (baada ya kutoa gharama za uzalishaji) kutokana na uingizwaji wa mchele kwa njia za panya na ukwepaji wa soko. Wakulima walishindwa kuuza mchele kwa mwaka 2014/15 wakajikuta wanauza gunia kwa Tzs 30,000 badala ya Tzs 90,000 kwa miezi ambayo bei huwa ni ya kawaida. Kwa kuwa wengi wawakulima hawa wamelima kwa mkopo (trekta ama madawa), inakuwa ngumu kuweza kurudisha gharama za uzalishaji, na hivyo wametumbukizwa kwenye lindi la madeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, kama soko la mazao ya wakulima linahujumiwa na Serikali hii ya CCM ikielewa fika bila ya kuchukua hatua, ni kwa vipi jitihada za wakulima kukopa mitaji zitaweza kuinua wakulima hao na sekta nzima ya Kilimo? Kambi Rasmi ya Upinzani inasema sasa ni muda mwafaka Serikali chovu ya CCM ikakaa pembeni na kuona jinsi gani kilimo kitakavyoweza kulikomboa taifa letu.

**8. MAZAO YA CHAKULA**

**i) Kilimo cha muhogokwa chakula na biashara**

**Mheshimiwa Spika**, Nchini Tanzania, muhogo unatajwa kuwa zao la pili kwa kuchangia pato la taifa kwa asilimia 19 baada ya mahindi. Pamoja na hayo. Zao hili lina faida nyingi kijamii na hata kiuchumi na kwa maendeleo ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Ni zao ambalo linaweza kuzalisha bidhaa zaidi ya 300, zikiwemo zile za chakula na ambazo si za chakula viwandani. Majani yake hutumika kama mboga na dawa pia. Katika viwanda, mazao yanayopatika katika mzizi wenyewe, miti namajani huweza kuzalisha bidhaa anuwai. Baadhi ni

vifaa vya nguo, karatasi, mafuta, kilevi, dawa za binadamu, na plastiki. Vilevile wanga wa muhogo hutumika kutengeneza dawa za madoa, gundi katika samani, rangi za awali katika kuta za nyumba na sukari (Sugar syrup).

**Mheshimiwa Spika,** Hivi sasa zao la muhogo limezidi kupata umaarufu zaidi, ambapo kadri siku zinavyokwenda linabadilika na kuwa zao la kibiashara. Katika nchi nyingi za Afrika kama vile Afrika ya kusini, Nigeria, Ghana na kwingineko, kuna viwanda vikubwa kwa ajili ya kusindika mihogo na kupata bidhaa mbalimbali. Mojawapo ya bidhaa kubwa zinazotengenezwa katika viwanda hivyo ni pamoja na wanga, madawa, kiungo cha kuongeza ladha kwenye vyakula, pamoja na *glucose* inayotokana na muhogo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hivi sasa wakulima walio wengi wanajipatia kipato kizuri kutona na umaarufu na umuhimu wa zao la muhogo duniani kote, ambapo wafanyabiashara kutoka bara la Asia kama vile uchina, wana mahitaji makubwa ya zao la muhogo kwa ajili ya viwanda nchini mwao. Kwa mantiki hiyo unaweza kuona ni kwa namna gani zao hili lilivyo na umuhimu mkubwa tofauti na linavyochukuliwa na jamii nyingi za wakulima barani Afrika kuwa ni zao la kimaskini. **Kambi Rasmi ya Upinzania inasema Serikali ijayo ya Upinzani itatilia mkazo zao hili kwa faida ya wakulima na Taifa kwa ujumla.Kwani Serikali iliyoshindwa kuona fursa ya CCM itakuwa kando.**

**ii) Teknolojia ya GMO katika Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** GMO ni kifupi cha maneno ya kiingeraza yani Genetically Modified Organisms. Viumbe hivi nizao la teknolojia mpya ya kibaliojia ijulikanayo kama Biotechnology.Wanasayansi mbalimbali katika ukanda wa Afrika Mashariki wamekuwa wakitafiti juu ya uwezekano wa kutumia teknolojia ya Uhandisi Jeni (GMO) katika kilimo.Hatua hii inatokana na teknolojia hiyo kuwa na upinzani kwa kile kinachoelezwa kuwa ikitumika inaweza kusababisha athari za kiafya na kimazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, watafiti mbalimbali duniani wamekuwa wakiitetea teknolojia hiyo kuwa ni salama na tayari baadhi ya nchi kama vile Marekani, India na China zimeshaanza kutumia teknolojia hiyo katika kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Ni ukweli usiopingika kwamba teknolojia ya GMOinaweza kumsaidia mkulima kuvuna mazao mengi katika eneo dogo, kutotumia au kutumia kidogo dawa za kuulia wadudu na mazao kumea vyema kwenye maeneo yenye mvua kidogo.Nchi mbalimbali zimekuwa zikitamani kuona wananchi wake wanazalisha chakula cha kutosha na pengine kuwa na ziada kwa ajili ya kuuza, lakini zimekuwa na hofu ya kujiingiza kichwa kichwa kwa kuwa ni teknolojia mpya.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano mzuri ni Rais Jakaya Kikwete alipotembelea Taasisi ya Tafiti za Kilimo ya Mikocheni (MARI), Machi mwaka 2013 na kuhimiza wanasayansi kuharakisha utafiti wa teknolojia ya GMO, ili Watanzania waanze kuifaidi.**Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua lini tafiti hizi zitakamilika nanini kauli Serikali kuhusu GMO.**

**9. MAPITIO YA BAJETI KWA MWAKA 2015/16**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara katika mwaka wa fedha 2015/2016 katika vifungu vyote vitatu (43, 24 na 05) inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **353,150,873,000** ambapo shilingi **95,387,647,000** ni kwa ajili ya maendeleo sawa na **27%**. Fedha nyingine yote inayobaki ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kitendo ambachoi kinaonyesha dhahiri kwamba serikali haina utashi wa kuendeleza kilimo nchini pamoja na kwamba zaidi ya **80%** ya watanzania wanategemea kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa serikali imeshindwa kabisa kusimamia kilimo nchini na kuwaacha watanzania wakihangaika ovyo.**Kambi Rasmi ya Upinzani inawaomba wanachi kuunga mkono juhudi zinazofanya wa vyama vinavyounda UKAWA ili kukiweka chama cha mapinduzi pembeni kwa ajili ya mstakabali wa nchi.**

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani – Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika**
**23.05.2015**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wageni walioko Bungeni asubuhi hii ni wafuatao:-

Wageni wa Mheshimiwa Steven Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika ambao ni Bi. Sophia Kaduma - Katibu Mkuu, Injinia Raphael Daluti – Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Yamungu Kayadambila - Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Wasanga Shayo - Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu, Dkt. Fidelis Miaka - Mkurugenzi wa Maendeleo ya Utafiti.

**WABUNGE FULANI:** Hawapo!

**MWENYEKITI:** Wapo kwenye chumba chao maalum.

Ndugu Fidelis Miaka - Mkurugenzi wa Maendeleo ya Utafiti, Ndugu Twahili Nzalawehe - Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao, Bi. Anne Asenga -

Mkurugenzi wa Mafunzo, Injinia Seif Lusemwa - Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji, Dkt. Audax Rutabanzibwa - Mkurugenzi wa Tume ya Ushirika, Dkt. Charles Walwa - Mkurugenzi Mtendaji *NFRA*, Ndugu Hatman - Mkaguzi wa Nje, Injinia Marko Lyimo - Mkurugenzi wa Zana za Kilimo, Ndugu Simkanga - Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Bi. Asia Mohamed - Mkaguzi wa Ndani, Wakuu wa Idara Bodi za Mazao na Taasisi zilizo chini ya Wizara na Maafisa 100 kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Wageni wa Mheshimiwa Freeman Mbowe - Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ambapo ni Ndugu Evans Saul kutoka Marian Secondary School, Ndugu Ramadhani Khalifa kutoka DCT Secondary School, Ndugu Asha Jafari kutoka DCT Secondary School, Ndugu Frank Joshua kutoka Azania Secondary School na Ndugu Abubakary Mohamed kutoka Kiwanja cha Ndege Secondary School.

Wageni wa Mheshimiwa Chacha Mariba Nyangwine ambao ni Samuel Mkurya Mangalaya - Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Wilaya ya Tarime, Marwa Mkare Manenga - Msaidizi wa Mbunge Tarafa ya Ingwe Tarime, Ndugu Ngocho Seronga - Mkazi wa Tarime.

Mgeni wa Mheshimiwa Gosebert Blandes ni Ndugu Mutalemwa Stanley Kahoza, ambaye ni mdogo wake.

Wageni walioko Bungeni kwa mafuzo ni wanafunzi 10 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara CBE Dodoma; karibuni sana Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kuchangia na leo kama kawaida kwa mujibu wa Kanuni kama iliovyotenguliwa ni dakika saba tu, tunaanza na Mheshimiwa Sakaya, ajiandae Mheshimiwa Mwatuka!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia Hotuba iliyoko mbele yetu. Kwa sababu ya muda, nitakwenda moja kwa moja kwenye mchango wangu.

Ninaomba nizungumzie suala la upatikanaji wa pembejeo. Serikali imeingiza utaratibu mpya mwaka jana wa upatikanaji wa pembejeo ambao ulikuwa haujafanyiwa uchambuzi wa kutosha, matokeo yake mpaka leo wananchi hawakuweza kupata pembejeo.

Tulikuwa na utaratibu wa zamani ingawa ulikuwa na upungufu wake lakini ulioingia, wananchi wameunda vikundi, wametoa fedha zao shilingi 20,000 mwaka mzima Serikali haikuweza kutoa fedha Benki ili wananchi wale wapatiwe mikopo. Kwa hiyo, badala ya kuendelea kusaidia kilimo kishamiri,

tumeendelea kuonyesha kwamba, wananchi wanakosa pembejeo, matokeo yake kilimo kinaendelea kudumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kwenye suala la tumbaku na hili ni muhimu. Ni ukweli ulio wazi kuwa, Serikali inajua namna gani ambavyo tumbaku inachangia kwenye Pato la Taifa. Kwa miaka kumi ambayo nimekaa ndani ya Bunge hili, tumeendelea kuzungumzia matatizo makubwa yanayotokana na Zao la Tumbaku; wakulima kuendelea kuwa masikini, kutokuwepo masoko yenye tija, kuendelea kuwepo kwa ulanguzi wa hali ya juu, kuendelea kutumika kwa dola tangu Mheshimiwa Waziri Wasira akiwa kwenye Wizara hii miaka iliyopita, sasa hivi ni mara ya pili ameingia pale. Alisema atashughulikia kuhakikisha Zao la Tumbaku linakuwa na tija kwa wakulima.

Leo amerudi hapa, tunataka leo atupe majibu ni kwa nini mpaka sasa hivi tumbaku inanunuliwa kwa dola?

Kwa nini mpaka sasa hivi bei ya tumbaku inapangwa na makampuni na siyo wakulima kama mazao mengine?

Kwa nini mpaka sasa hivi kuna urasimu kwenye haya makampuni?

Kama kweli Serikali haina mikono yake ni kwa nini makampuni haya yameendelea kulelewa wakati yanaumiza wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa miaka minne mfululizo, tumbaku imekuwa ikinunuliwa kwa dola 2.13. Mwaka huu kwa kusikitisha sana, kwa taarifa ambazo ni za uhakika, makampuni yameamua yatanunua tumbaku kilo moja kwa dola mbili na senti sita.

Kuzalisha tumbaku kilo moja ni dola 1.8, mkulima pamoja na shida zote aje kuuza kwa dola 2.6. Kweli hawa wakulima dola 2.06 wanaweza kunyanyuka mahali hapa? Ninaomba Serikali iingilie kati, ninasikia Kikao cha Bodi kimekaa, wakulima wamekubali wamesaini mikataba. Wamedanganywa na Serikali kwenye masuala ya msingi kama haya. Wapeleke watu waende ku-*bargain* na haya makampuni, ni watu wakubwa, haya makampuni yako kwa ajili ya biashara yanawanyonya wakulima. Leo mkulima wa kawaida anaenda ku-*bargain* bei wapi na wapi! *(Makofi)*

Tumbaku mwaka huu haitauzwa kama bei haipandi. Tunajua makampuni yanauza tumbaku kwa dola 4 mpaka 4.8, wananunua kwa dola 2.06; huu ni wizi. Huu ni wizi uliopitiliza, mkulima hawezi kutoka hapa, inasikitisha sana. Matatizo ni mengi, miaka yote Serikali gani kwa muda wa miaka 10 mmeshindwa kuzingatia maoni yetu na mapendekezo yetu? *(Makofi)*

Nenda Mkoa wa Tabora ukaangalie nyumba ambazo wanakaa Wakulima wa Tumbaku, mtu analima miaka kumi hata kuezeka nyumba kwa bati anashindwa. Hatuwezi kwenda kwa mpango huu, inasikitisha sana. *(Makofi)*

Niende kwenye Ushirika. Sheria mpya ya Ushirika iliamua kabisa kuwa, Wanasiasa wote wakae pembeni na kweli Sheria imeshaanza kutekelezwa, Wanasiasa wanatakiwa wakae pembeni. Waziri aliyepita aliweza kupeleka timu maalumu kufanya uchunguzi Mkoa wa Tabora, Vyama vyote vya Ushirika vikafanyiwa uchunguzi na taarifa iko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo hakuna hatua iliyochukuliwa na ikiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora, ndiyo aliyekiua Chama Kikubwa cha Ushirika Mkoa wa Tabora. Mpaka leo hatua hazichukuliwi wakati ambapo shida bado ipo. Vyama Vya Ushirika vinatakiwa kushamiri viwe vyenyewe viweze kufanya kazi vizuri. Wakulima walibambikwa madeni ambayo yalisababishwa na tatizo hilo hilo, wakulima wameendelea kuwa maskini mpaka leo, tumbaku imeendelea kuwa shida kwa sababu Vyama vya Ushirika viliingiliwa na Wanasiasa. Kwa nini taarifa iko wazi toka mwaka jana mpaka leo hatua hazichukuliwi?

Tunaitaka Serikali ilete majibu Bungeni ni nini hatima ya wizi uliofanyika kwenye Chama Kikuu cha Ushirika Mkoani Tabora mpaka leo majibu hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la sukari; ni kweli Serikali ilitoa vibali wakati fulani kwa ajili ya sukari kuingizwa baada ya kuona sukari ilikuwa kidogo. Mpaka sasa sukari tunayo ya kutosha ndani ya nchi yetu; kwa nini bado Serikali inaendelea kutoa vibali vya kuingiza sukari ndani ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaua viwanda vyetu ndani ya nchi. Wafanyakazi wanaachishwa kwenye viwanda, leo wengi wameondolewa kwenye viwanda kwa sababu sukari inaingizwa ndani ya nchi, wanakosa mahali pa kuuza sukari yao. Ninaiomba Serikali, leo Mheshimiwa Wasira uje na majibu hapa; kwa nini unaendelea kutoa vibali sukari kuingizwa nchini wakati tuna viwanda vingi na sukari ipo ya kutosha ndani ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kwenye masoko; tumekuwa tunakosa masoko mengi ya mazao yetu kwa sababu ya utaratibu mbovu ambao upo ndani ya Serikali. Kuna Kitengo cha Masoko ambacho kinatakiwa kitafute masoko kwa ajili ya mazao mbalimbali. Kitengo kile kiko ndani ya Wizara ya Viwanda na Biashara na tunajua nchi hii tunasema ni nchi ya kilimo,

kilimo ni uti wa mgongo. Kama tunazalisha mazao ambayo hatuwezi kutafuta masoko ya uhakika, tunawaumiza wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa kile Kitengo cha Kutafuta Masoko ambacho kipo ndani ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kije Wizara ya Kilimo ili waweze kutafuta masoko ya uhakika kwa ajili ya mazao ya wakulima wetu. Wakulima wetu wameendelea kulima, tumeona mwaka jana, tumelima mahindi hapa mengine mpaka leo yanaoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, nimetembea Mkoa wa Ruvuma, nimekwenda Lindi, nimekwenda Mtwara, wakulima wamelima mahindi, wamepeleka kwenye maghala, yameharibikia kwenye Maghala ya Serikali, wanarudishiwa mazao yao yakiwa yameoza; huu ni wizi kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuchukua mazoa ya wakulima, unayakusanya kwenye maghala, mnashindwa kuwalipa, badala ya kuwapa hela mnarudisha mahindi! Serikali ninaomba muache tabia hii mbaya na ninawaomba wakulima wote ambao wamefanyiwa uonevu mhakikisha mnawalipa fedha zao na siyo kuwarudishia mahindi ambayo yameoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri kasema katika Hotuba yake, mwaka jana tulikuwa na chakula kingi sana, karibu asilimia 130. Nimuulize swali; kama tulikuwa tuna chakula kingi ni kwa nini shule za sekondari zilifungwa kwa sababu ya kukosa chakula? *(Makofi)*

Serikali kwa nini shule zilifungwa watoto wetu wakarudishwa nyumbani, wakokasa elimu, wakakosa mitaala, kwa sababu Serikali mmeshindwa kulipa fedha za wazabuni, mmeshindwa kutoa chakula mashuleni, watoto wanaendelea kutaabika! Kama kuna chakula cha kutosha kipelekwe pia mashuleni watoto wetu waweze kusoma vizuri na waweze kunufaika na elimu yao.

Nizungumzie kidogo magonjwa. Tumekuwa na shida kubwa sana ya magonjwa ya mazao hapa nchini na kwa bahati mbaya, Hotuba yote ya Mheshimiwa Waziri, hakuna sehemu alipozungumzia namna gani ambapo ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwatuka, ajiandae Mheshimiwa Vita Kawawa!

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu aliye Mwingi wa Rehema, ambaye amenifikisha siku hii ya leo. Kabla

sijaenda kwenye mchango wangu, nitoe ombi kwako, utaratibu unaotumika wakati wa kuchangia huu ule wa Taarifa, Mwongozo, unaharibu utaratibu. Kwa hiyo, ninaomba yawepo mabadiliko.

Sasa niende kwenye ajenda iliyoko mbele yetu. Inafahamika kabisa kuwa, kilimo ni uti wa mgongo. Kila mahali watu wanajua kuwa hawawezi kuishi vizuri bila chakula na kama ilivyo kawaida, ili chakula kipatikane ni lazima pawe na wakulima. Nikuchukulia upande wa kule Kusini hasa Masasi, bado wakulima tumebaki na kilimo kile cha 1947 cha jembe la mkono. Ukweli ni kwamba, hakuna mtu anayeweza kulima hekari kumi, ishirini, kwa kutegemea jembe la mkono peke yake; hii siyo rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikia wenzetu kila wakati wamepelekewa matrekta ya mkopo. Kilimo Kwanza kile kilifahamika kuwa kilikuwa kinagawa matrekta. Sasa Kusini nikichukua hiyo Masasi, bado sijapata kitu hicho na sijasikia matrekta yameletwa pale kwa ajili ya mikopo kwa watu au kwa vikundi.

Vikundi vipo lakini vile ambavyo havina uwezo wa kupata fedha za kuweza kununua trekta. Kipindi fulani zilitolewa zile *power tiller* ambazo zilikuwa hazifai kwa kilimo, kutegemea kwamba mtu atachukua *power tiller* ataenda kulima shamba lake la hekari kumi au zaidi. Ninaiomba Serikali ione umuhimu wa kupeleka matrekta watu wakopeshwe kule. Ukitegemea vikundi kwamba watoe pesa ndiyo wapate, itakuwa siyo rahisi. Vikundi vilivyopo kule vilivyo vingi ni vile vya *VICOBA,* ambavyo wanaweka zile pesa na wanakopeshana wenyewe. Kiwango wanachoweka ni kidogo kulingana na uchumi ulivyo katika nchi yetu. Hivyo, naomba waangaliwe watu wale kule, trekta ziende kama zinavyoenda sehemu zingine. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, kilimo hicho hicho cha mkono wanajitahidi sana kulima mazao ya biashara; kwa mfano, licha ya korosho, wanalima mbaazi, choroko na ufuta. Sasa ufuta na mbaazi walau afadhali yana soko la kueleweka, lakini choroko bado sijagundua kama kuna sehemu ambayo wananunua kwenye vyama vya msingi. Hivyo, naomba uwezekano wa kuwatafutia masoko ya uhakika ili waweze kuuza. Kuna mazao mengine yanalimwa lakini hayana soko, soko lao ni hawa wanaonunua kwa bataweli. Mahindi hakuna soko kule, anayepata pesa anapata kwa watu binafsi ambao wanapita kununua labda wenye shida zao na wengine ambao wananunua kwa ajili ya biashara. *(Makofi)*

Jambo la kushangaza; Serikali haina soko kule la mahindi, hakuna, sasa wanapojitolea wafanyabiashara hawa wetu wadogo wadogo wa kangomba hawa, wakikusanya wananyang'anywa na Serikali. Mwingine juzi juzi hapa walimfuata mpaka nyumbani kwenda kuchukua nyumbani, amenunua huko kijijini amekwenda kuweka nyumbani kwake ili afanye utaratibu wa kupata

soko. Serikali ilienda huko na kumnyang'anya mmoja ambaye alieleza taarifa zake.

Sasa hilo linakuwa ni uonevu, kwa sababu soko la mahindi hakuna na wakulima nao pesa hawana, wanategemea anapopita mnunuzi wa kangomba apate senti imsaidie kwa matumizi yake nyumbani. Hivyo, ni vyema basi waruhusiwe hawa wa vikundi vidogo vidogo wanaoamua wenyewe kwamba wanakusanya mazao ili wayauze wenyewe na katika kufanya hivyo, itasaidia kwa sababu mkulima atapata pesa yake kamili; za Serikali zinakwenda. Kwa hiyo, waruhusiwe, wanapopata pesa kamili na maendeleo ndipo yanapopatikana, kwa sababu amepata pesa zake anapangia sasa nitafanya hiki na kile. Tofauti na wale wanaopita kwenye stakabadhi ghalani ambao wanapata kidogo kidogo haziwafikishi kwenye malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbegu; megu hizi za kisasa kule Kusini hasa Masasi, sijaona naona kwa wale wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanapata kidogo wakauza kwa yule ambaye anajua au ana uwezo. Kwa sababu bei mle madukani ni kubwa. Kilo moja ya mahindi utakuta shilingi saba ama sita ukipata kilo mbili basi ndiyo shilingi kumi na kitu. Sasa mkulima mdogo ambaye mapato yake ni ya chini, hawezi kupata mbegu zile.Kwa hiyo, Serikali iangalie, ipeleke fungu maalum apatikane wakala ambaye anaweza kuuza mbegu hizo za mahindi, mpunga na mazao mengine ambayo yanapatikana mbegu za kisasa. Kule mbegu walizonazo ni zilezile za asili. Kwa hiyo, naomba Serikali …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Namwita Mheshimiwa Vita Kawawa, ajiandae Mheshimiwa Chibulunje na Mheshimiwa Ahmed Salim!

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kunipa fursa hii niweze kuchangia katika Wizara yetu. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuandaa Hotuba na kuwasilisha vizuri. Naomba niendelee na changamoto zilizojitokeza msimu uliopita kutokana na upatikanaji wa pembejeo.

Naishukuru sana Serikali mwaka huu, katika aya ya 41 kwenye Hotuba imesema Serikali itarejesha utaratibu uleule wa vocha uliokuwa unatumika nyuma mwaka huu. Kwa sababu mwaka jana wakulima wamepata shida sana ya upatikanaji wa pembejeo. Utaratibu ule haukuwafikia wakulima wengi wa pembejeo hasa wa mahindi. Kwa hiyo, baada ya Serikali kuiona changamoto hii na mmeamua kurudisha utaratibu ule, tunaomba urudishwe utaratibu ule wa utoaji wa vocha na Serikali mmesema mtagharimia asilimia 50. Tunawapongeza sana Serikali kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna changamoto baada ya uzalishaji wa masoko ya mazao. Naomba niseme na pia nitumie fursa hii kuwatangazia wanunuzi wote wa ufuta na mbaazi; sasa hivi Namtumbo tuna ufuta mwingi na tuna mbaazi nyingi waende wakanunue, wakulima tunapata shida kwa soko. Kwa hiyo, natumia fursa hii wakulima kokote, wanunuzi wowote nchini, wakanunue ufuta Namtumbo na mbaazi zitakapokuwa tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema katika mazao mchanganyiko tumekuwa tukipata shida sana ya masoko. Kwa hiyo, tunaomba Bodi ya Mazao Mchanganyiko, ifanye kazi yake inavyotakiwa, ifike katika Halmashauri zetu, ifike kwa wakulima wetu! Ili wakulima wasibabaike katika masoko. Wakulima kama hawa wanavyosema sisi tunauza kupitia inaitwa madumla, vile visado, bila kupata haki ile ya uhalali wa kilo. Kwa hiyo, tunaomba sana Bodi ya Mazao ifike kama ilivyokuwa zamani *GAPEX*, tunaomba ifikie hivyo kwenye mazao haya mchanganyiko ya ufuta na mbaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine, nataka kuzungumzia tumbaku. Tumbaku imekuwa na changamoto; kwanza, duniani huko inapigwa vita kwenye soko lake, watu wa afya wanalipiga vita lazima kwanza tulifahamu hilo. Tumbaku hiyo hiyo mnakumbuka zamani tulikuwa tunasema matangazo yalikuwa yanatangazwa tahadhari sigara siyo nzuri kwa afya yako. Leo sigara zimetungwa sheria mpaka ndani ya Bunge hili kwamba, watu wasivute sigara hadharani, wawe wanavuta kwenye vyumba maalum, duniani huko kote. Kwa hiyo, soko lenyewe la tumbaku limekuwa linafinywa kwa masharti mbalimbali ya afya.

Kwa hiyo, lazima tuzingatie kwamba ni kweli dola ya tumbaku kwa kilo moja ilifika mpaka dola nne. Tanzania hapa tuliuza mpaka zaidi ya dola tatu kwa kilo moja, lakini ilishuka mwaka jana ikawa dola 2.13, kwa sababu ya mbano na vita inayopigwa tumbaku. Lazima hilo kwa ujumla tulifahamu, vita ipo kubwa na soko la zao lolote linaendana na hitaji. Hitaji linapobanwa, soko nalo linashuka. Kwa hiyo, kwanza lazima tulielewe hilo.

La pili, Mheshimiwa Sakaya amesema hapa kwamba, wanunuzi ndiyo wanapanga bei ile. Hapana, kunakuwa na Wakulima, Viongozi wa Serikali ambao wanatoka Wizara ya Kilimo, Bodi ya Tumbaku na Wanunuzi ndiyo wanazungumza kuhusu suala la bei. Utafiti unakuwa umeshafanyika, wanakubaliana bei ya duniani ipo bei gani na soko litakuwa mwaka huo bei gani. Kwa hiyo, kunakuwa na *negotiations* pale kujadili bei hiyo ya soko. Kuna changamoto nyingine kweli ya Ushirika na tunaomba Serikali iendelee kulisimamia. Kuna maeneo mengine viongozi hawa wamefikishwa Mahakamani. Tunaomba tusimamie wale ambao ni wabadhirifu katika eneo hili basi waweze kufikishwa kwenye Vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lingine, zao hili linazalisha, limeuza nje zaidi ya bilioni mia tano na sabini na kitu, lakini leo hii Serikali, naizungumzia Serikali kwa maana inayotoa fedha Serikali Kuu, Hazina, sizungumzii Wizara ya Kilimo wao wanategemea hela kutoka Hazina. Hazina, fedha zinazoingiza *inland revenue* zaidi ya bilioni mia sitini kwa mwaka. Zao hili pia linasimamiwa kwa uteuzi na Serikali chini ya Bodi ya Tumbaku. Bodi ya Tumbaku gharama ya kusimamia soko hili mwaka huu ni shilingi milioni mia tano kumi na saba, ni nusu ya bilioni, *half a billion*! Ninyi mnaingiza zaidi ya bilioni mia moja na sitini na nane, mnashindwa kuwapa hela hizi ili wafanye kazi hiyo? Sasa hivi soko limetangazwa toka mwezi wa tano linashindwa kufanyika kwa sababu hakuna fedha za kuendeshea soko hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima ufanyike uteuzi ili mpate mabilioni hayo ya fedha ili Makampuni yauze nje tupate zaidi ya dola mia nne na sitini. Mpaka leo hii Hazina inashindwa kutoa hela Wizara ya Kilimo ikasambaza fedha hizi kwenye Bodi ya Tumbaku na kwenye masoko ya tumbaku kazi ikafanyika.

Magari yamesimama hakuna, wateuzi wanashindwa kwenda kufanya kazi yake, kwa sababu ya *half a billion shillings only,* ambapo ninyi mnaingiza zaidi ya bilioni mia moja na sitini kwa mwaka! Sasa tutafanyaje kazi hii? Tunawaomba sana Hazina isimamie hili.

Nakupongeza Waziri umeruhusu mchakato huu kwamba, wadau wachangie ili kazi hii iweze kwenda. Serikali iko nyuma imetunga sheria ilisema itagharimia asilimia mia moja. Kwa nini sasa inashindwa kutimiza wajibu wake wa kugharimia hii mpaka sasa tunahangaika ili tupate wadau wachangie? Sisi tulishasema huko nyuma tumetoa ushauri, basi kazi hii inafanyika bure. Kazi ya uteuzi, kazi inayofanywa na wateuzi moja ni kuangalia *crop survey*. Kazi ya uteuzi wa tumbaku yote inafanyika bure. Serikali ninyi ndiyo mnatakiwa muigharimie. Tulitoa ushauri nyuma huko kwamba, jamani angalau basi … *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chibulunje, ajiandae Mheshimiwa Ahmed Salum na Mheshimiwa Machali!

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ambayo naiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja wa wadau wa karibu sana na Wizara hii kwani nilishakuwa Mtumishi wa Umma katika maisha yangu yote,

nimetumikia Wizara hii katika Sekta ya Ushirika, lakini pia niliwahi kupata hekima ya kupewa fursa ya kutumika kama Naibu Waziri katika Wizara hii. Kwa hiyo, nawapongeza sana wenzangu katika Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, wakiongozwa na Waziri Wasira pamoja na Naibu wake, pamoja na Katibu Mkuu - Bi. Sophia na Naibu Makatibu Wakuu. Nawapongeza sana na nawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Nataka nitumie fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Chilonwa, kwa heshima kubwa waliyonipa kwa kipindi cha miaka ishirini, kuanzia mwaka 1995 wamenichagua kwa vipindi vinne mfululuzo. Kwa vile nilikuwa nimeshawatangazia azma yangu ya kustaafu mwaka huu na nilishawashukuru, nataka tu nitumie nafasi hii kuwakumbusha tena kwamba, waenzi yale mafanikio tuliyoyapata katika kipindi hicho cha uongozi wangu. Nami nataka niwaambie tu kwamba, yale mafanikio wao ndiyo mashahidi, waendelee kuyaenzi na wayatumie katika kuhakikisha Chama cha Mapinduzi kinapata ushindi mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nitazungumza kwa kifupi sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri atazame suala la uhaba wa chakula uliopo katika Mkoa wangu wa Dodoma pamoja na Jimbo langu la Chilonwa kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri, ametaja hapa katika ukurasa wa kumi kwamba, Mikoa iliyokumbwa na ukame mwaka huu ni pamoja na Dodoma na Mikoa hii ya kati. Kwa hiyo, nataka nimwombe ahakikishe utaratibu wa kupeleka chakula katika maeneo haya hususan kwenye Jimbo langu la Chilonwa ufanyike haraka, kwa sababu wananchi hawakuvuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la umwagiliaji. Tumesoma humu kwenye Hotuba kwamba, ipo mipango mizuri ya umwagiliaji katika mabonde mbalimbali. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla kwamba, maadam sasa hivi ipo Tume ya Umwagiliaji, hebu ingetoa kipaumbele pia katika maeneo kame. Sambamba na hii mipango ambayo imeandaliwa kwa ajili ya mabonde mbalimbali katika nchi, lakini kipaumbele kingekuwa katika mikoa kame. Kwa sababu, kilimo katika mikoa hii kame ni cha kubahatisha sana kwa kutegemea maji ya mvua. Maji yakishakosekana, mvua ikishakosekana, ndiyo hakuna chakula. Serikali inaingia hasara kubwa sana ya kuwalisha watu chakula, lakini kama ingegharimia Mradi wa Umwagiliaji katika maeneo haya kame, kwa hakika chakula kingekuwa ni cha uhakika. Kwa hiyo, niwaombe tu kwamba, Tume ya Umwagiliaji ambayo sasa hivi imekwishaanza kazi, kipaumbele chake kingine kiwe katika maeneo kame na hususan Mkoa wetu wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nijielekeze katika eneo la Ushirika. Hali ya Ushirika katika nchi hairidhishi. Baadhi ya wasemaji waliotangulia hapa wanazungumzia ubadhirifu unaoendelea katika Vyama vya Ushirika,

wanazungumzia habari ya wizi. Mara zote nimekuwa nikisema kwamba, dawa kubwa ya kuhakikisha Vyama vyetu vya Ushirika vinasimamiwa kwa karibu, ni suala la kuimarisha Idara ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya kufuatilia kwa karibu sana ubadhirifu na wizi unaoendelea katika Vyama vya Ushirika na kuwapa Wanachama taarifa, hatimaye Wanachama wenyewe waweze kusimamia mambo yao kama inavyotakiwa yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita tulipitisha Sheria hapa ya Ushirika ya Mwaka 2013 na humo ndani ilikuwemo kuundwa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambayo ilitakiwa ijielekeze katika suala zima la kuimarisha hii kada ya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Nimeona kwenye Hotuba humu kwamba, shughuli zitaanza lakini kwa bahati mbaya imechelewa sana kuanza.

Mimi ningependa kujua ni kwa nini shughuli za Tume ya Ushirika hazijaanza mpaka sasa hivi? Zingekuwa zimeanza, kwa sababu mtandao wa Watumishi wa Ukaguzi unakwenda mpaka kule Wilayani, pengine ingeweza kusaidia sana kutatua hata hayo matatizo mengine ambayo yanatajwa hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwoma Mheshimiwa Waziri, ahakikishe anaharakisha suala hili la Tume ya Ushirika ambalo tayari lilikuwa limeshaelezwa katika sheria. Mheshimiwa Waziri hapa ameelezea habari ya utekelezaji wa Programu Kabambe ya *Modernization* ya Ushirika. Hii programu ni ya miaka kumi, toka 2005 mpaka 2015.

Mimi ningetegemea sasa hivi Wizara ingekuwa inaandaa tathmini ya kuhakikisha yale ambayo yalikuwa yameainishwa katika ile programu sasa yameleta mafanikio kwa kiasi gani. Kwa hiyo, niombe tu kwamba, maadam sasa hivi huu ndiyo mwaka wa mwisho, iandaliwe sasa tathmini ya utekelezaji wa programu hii, tuweze kuona ni nini tumefanikiwa na wapi tumekuwa na upungufu, kuhakikisha shughuli za Vyama vya Ushirika zinaendeshwa na kurudisha imani kwa Wanachama wetu na kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinasimamiwa na kuendeshwa na kuwapa matumaini wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza imegongwa na mimi kwa sababu nataka kustaafu vizuri, naomba kuunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ahmed Salum, ajiandae Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Genzabuke!

**MHE. AHMED ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, naunga mkono hoja sina tatizo, lakini kwenye vifungu kule ndiyo tutakuja kuona namna gani Wizara itanijibu vizuri kwa haya ninayotaka kuongea.

Kabla siajendelea, naomba kutoa taarifa kuwa, katika Jimbo la Solwa askari wetu hawa wa zimamoto wameenda kuwatoza watu kodi au sijui ndiyo ushuru wa zimamoto kwenye maeneo ya vijijini sana. Wamefanya hivyo Tinde, wamekamata watu, wamefanya hivyo Didia wamesumbua watu, Salawe pamoja na Samagazi.

Naomba sana Wizara ya Mambo ya Ndani isitishe zoezi hili kwani wafanyabiashara, akina mama ntilie, wanakamatwa wanatozwa shilingi elfu thelathini. Mtu ana kilo moja ya mchele anatozwa shilingi elfu thelathini au anafungwa. Sasa naomba hili zoezi lisitishwe ili sasa elimu itoke vizuri waweze kuona namna gani ya kulipa kodi yao hii vizuri.

Baada ya kusema hayo, tatizo la njaa katika Mkoa wa Shinyanga au Mikoa ambayo inakumbwa na matatizo ya njaa mara kwa mara ni kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Sisi katika Jimbo la Solwa inatukumba mara kwa mara, tukipungukiwa au mvua ikikosa kunyesha kidogo likaja jua kali, mazao yote yanakauka. Ikija mvua kali kutokana na jiografia tu ilivvyo, inasomba mazao yote yale na tatizo la njaa linaanza kuibuka. Hivi ninavyosema, tatizo la njaa limeshaanza kunyemelea Jimbo la Solwa.

Mabadiliko ya hali ya hewa yanatusumbua sasa kwa muda mrefu katika Jimbo la Solwa. Wizara ya Kilimo ninaishauri ili kuondokana na tatizo la njaa katika Jimbo hili la Solwa au Mikoa yote au Mkoa wa Shinyanga ni pamoja na kuweka fedha kwenye suala zima la *irrigation scheme*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Solwa tuna *irrigation scheme* kama nne au tano. Hii ndiyo suluhu, kwa sababu kama mvua haiji, jua ni kali, yale maji yaliyovunwa kwenye bwawa yataweza kumwagiliwa kwenye majaruba au kwenye mashamba ya mpunga na kuweza kulisha.

Kata za Bukande na Didia zinalima mpunga kwa wingi sana, zinaweza kulisha Mkoa mzima wa Shinyanga. Hivi ninavyozungumza, Kahama inalishwa na Kata moja tu ya Lebukande. Isholologo kuna *irrigation scheme*, Kata ya Usule, ilikuwa kwenye Mpango wa *DASIP*, Benki ya Afrika ilitoa fedha. Tatizo kubwa lililojitokeza hapa ni kwamba, Wizara badala ya kuihusisha Halmashauri yetu katika suala zima la Mradi huu, wakaweka mkataba moja kwa moja Wizarani, wakampa mkandarasi, akalipwa milioni 147. Imefika tu asilimia 40 mradi ule umesimama, *Bank of Africa* imevuta hela zake, kwa sababu Mkandarasi hakumaliza Mradi kwa wakati. Sasa tatizo limekuwepo, Mradi upo umesimama. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atakapokuja ku-*wind up,* anijibu tunatatua tatizo hili kwa namna gani na fedha zitapatikana kwa namna gani. Ninashauri sana endapo kama Mkandarasi mwingine atapatikana, ihusishwe Halmashauri yetu ili tuweze kusimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi mwingine upo Nsalala pamoja na Nyida. Mwaka juzi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alijibu akasema kwamba, fedha zimepatikana, sasa tunakwenda kukamilisha Mradi huu, lakini mpaka sasa hivi hatujapata. Masengwa pale kuna Mradi huu wa *Irrigation Scheme*, tatizo kubwa katika Miradi yote hii ya IsholoIo, Nsalala, Nyida na Samuye ni kutengeneza au kuchimba mabwawa ili yaweze kufanya kazi vizuri. Sasa hivi Miradi yote hii tumeweka fedha nyingi na hakuna hata Mradi mmoja unaofanya kazi vizuri kwa Wakulima. Naomba sana majibu yawe mazuri ili wakulima hawa waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Irrigation Scheme* Kanda ya Ziwa, walikuja kufanya utafiti tena, walipita katika Kijiji cha Amani Kata ya Sarawe wakasema hili eneo linafaa. Ninashauri warudi tena waende na Kata ya Bukandi waone ni namna gani ya kuweza kuibua Mradi mpya wa *Irrigation Scheme*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu za pamba sasa hivi imekuwa ni tatizo sana kwa Wakulima wa Pamba. Kiwanda cha Wachina wanaonunua mbegu za pamba kwa ajili ya kupata mafuta, wameongeza bei kutoka kati ya shilingi mia tano mpaka mia saba. Matokeo yake ni kwamba, mbegu zile badala ya kwenda kwa wakulima, zimekwenda moja kwa moja kwenye kiwanda hiki. Sasa ninaomba Wizara iwe ina mfumo mzuri, biashara kama biashara sina tatizo nalo, lakini kama kuna mbegu ambazo zitakwenda kwa ajili ya kiwanda cha mafuta ya pamba, basi ijulikane na kama kuna mbegu kwa ajili ya wakulima, uwekwe mfumo mzuri wa kutofautisha hivi vitu, *otherwise,* Wakulima wa Pamba watapata matatizo miaka nenda rudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna njia nyingine zaidi ya kuongeza viwanda viwili, vitatu. Kuna kiwanda kimoja tu cha nyuzi, mwaka juzi bei ya pamba ilikuwa shilingi 1,200, leo ni shilingi 690 mpaka shilingi 750 na kiwanda kipo! Ushauri wangu ni kwamba, Serikali izidi kutafuta wawekezaji ndani na nje ya nchi. Hakuna mwarobaini mwingine zaidi ya kuwa na viwanda vingi, ukiwa na viwada vingi unatengeneza ushindani na bei. Hivi sasa kukiwa na kiwanda kimoja tu akiminya bei basi bei inashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo inawekwa Dar es Salaam; Dar es Salaam kuna wakulima wapi? Hivi Dar es Salaam kuna wakulima? Watazame maeneo ambayo kuna wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashauri Morogoro pale au Shinyanga hasa Shinyanga. Shinyanga siyo kwa sababu ni Mkoa ninaotoka mimi, ni Mkoa ambao upo katikati kwa maana ya Kagera, Mwanza, Singida na mikoa mingine. Ikiwekwa Benki ya Kilimo Shinyanga, itaweza kuwa karibu sana na Wakulima wa Kanda hiyo yote wanaolima mazao mbalimbali. Unamtoa

mkulima kutoka Mwakitoliyo unampeleka Dar es Salaam wapi na wapi! Hapo tunatengeneza *scenario* ambayo haieleweki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri sana hii…..

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha. Sasa ninamwita Mheshimiwa Machali, ajiandae Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Genzabuke!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kuwa siungi mkono hoja ambayo imetolewa na Waziri wa Kilimo, kwa sababu mbalimbali. Kwanza, bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2015/16 inaonekana kupunguzwa. Imepungua kwa sababu mwaka wa fedha uliopita inaonekana katika vitabu nilivyokuwa navipitia vya Wizara ilikuwa shilingi 383,187,544,389, mwaka huu wanatuletea bajeti ya shilingi bilioni 353, kuna takribani bilioni 30 ambazo zimepungua kutoka kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mwaka wa jana na kila mwaka tumekuwa tukilieleza Bunge lako kwamba, Wizara ya Kilimo imekuwa inatengewa fedha kidogo. Sasa kama mwaka wa fedha ambao umepita, bajeti bado ililalamikiwa kwamba ni ndogo, *still* tunavyokwenda mbele bajeti inazidi kupunguzwa; ni wakati gani tutakuja kumsaidia huyu mkulima ambaye anakosa pembejeo, anakosa madawa kwa ajili ya ku-*support* kilimo, mkulima ambaye anahitaji pengine mikopo kupitia Vyama vya Ushirika? Tunawezaje kumsaidia mkulima huyu kama siyo kumnyonga na hatimaye watazidi kuwa maskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafahamika kwamba, zaidi ya asilimia 80 ya Wananchi wa Taifa letu ni wakulima. Sasa kwa bajeti hii ambayo inaonekana kupungua tunawasaidiaje wakulima hawa? Wizara ya Kilimo naomba wakati mnakuja ku-*wind up* mtuambie ni sababu gani ambazo zimepelekea bajeti ya kilimo mwaka huu ishuke? Huyu Mkulima mnamsaidia namna gani?

Ninaomba nipate majibu kuhusiana na suala hili. Msije na sababu kwamba ni *ceiling*. Ina maana ninyi mna wajibu kama Viongozi wa Wizara kuhakikisha mnaitetea bajeti yenu. Mkisema mmepewa ukomo wa bajeti, ufinyu wa bajeti, hatuwaelewi! Tumeshuhudia Wizara nyingine wanapambana wanaongezewa fedha. Mkitoa majibu hayo mtakuwa mmeonesha udhaifu mkubwa sana. Tunaomba mtueleze sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, aliyezungumzia kuhusu bei ya tumbaku. Ni wazi kabisa kwamba, Mkulima wa Tumbaku ananyonywa kwa kiasi kikubwa. Kama kweli Mkulima wa Tumbaku anauza kilo moja kwa dola 2.5 halafu haya makampuni yanakwenda kuuza bei ya tumbaku kwa dola 4 hadi dola 4.6, huu ni wizi wa mchana kweupe! Wizara ya Kilimo na mimi ninaleta swali kwenu mtuambie mtawasaidiaje Wakulima wa Tumbaku wapate bei nzuri, waache kunyonywa na kuonewa kama ambavyo imekuwa kwa miaka nenda rudi wanalalamika?

Kwanza, malipo yao yamekuwa yanacheleweshwa na makampuni haya, lakini *still* mnawalipa bei ndogo. Tunaomba ufafanuzi ili tujue ni sababu gani za msingi. Ninyi kama Serikali mliyopewa dhamana mnawezaje kukubali, mnaelewa bei ya soko la Dunia haya makampuni yakinunua yanakwenda kuuza kwa dola nne, lakini bado yananunua kwa bei ya chini kwa kiwango cha dola mbili. Tunaomba kauli ya Serikali ni lini mtaweza…

**MWENYEKITI:** Kengele ya kwanza tayari, hii kengele kidogo ina matatizo, kwa hiyo, ninakutahadharisha kengele ya kwanza tayari.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nitaomba kupata ufafanuzi ni lini mtawasaidia wakulima hawa?

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la sukari, naomba mtueleze pia Wizara ya Kilimo, mnakubali vipi sukari ya nje izidi ku-*flow* hapa nchini kama kweli ninyi mnafahamu suala la kuzidi kuruhusu bidhaa za nje ambazo zinapatikana hapa nchini kuzidi ku-*flow* kwa kasi kubwa ni kuua viwanda vya ndani; lakini pia mnasababisha ajira za watu ambao wanafanya kwenye viwanda vya ndani na sekta ya kilimo cha miwa wapoteze ajira zao? Tuambieni ni lini mta-*discourage* masuala haya ya kuruhusu sukari kutoka nje kuweza kuja au mtuambie mmewekwa mfukoni na baadhi ya makampuni ya nje au kuna nini nyuma yenu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwazungumzie Wakulima wa Jimboni kwangu. Wakulima wanaidai Serikali kupitia *NFRA* pamoja na maeneo mengine nchini. Mheshimiwa Waziri nilikuwa napitia hotuba yako, inaonesha bado mnadaiwa, kati ya bilioni 89 bado mnadaiwa takribani bilioni 12. Naomba kauli ya Serikali ni lini pesa hizi za wakulima ambao wamecheleweshewa malipo yao sasa watalipwa waweze kuondokana na matatizo ambayo yamewakabili kwa muda wote ambao mmechelewa kuwalipa pesa zao?

Serikali imekuwa na kaulimbiu ya kusema KILIMO KWANZA, lakini tumeshuhudia Serikali hii hii ikiwapiga na kuwaondoa wakulima ambao wanalima kwenye Mapori ya Kegera Nkanda katika Wilaya ya Kasulu! Mnasema KILIMO KWANZA kwamba, wananchi wajitokeze na walime kwa

nguvu, walime kwa kasi waweze kujiondoa na umaskini, lakini wananchi ambao wamekuwa wanalima katika eneo maarufu la Kagera Nkanda kwa miaka zaidi ya 40, tumeshuhudia wakikamatwa na kupigwa na askari, tumeshuhudia wakikamatwa na kunyang'anywa mazao yao wakisema ni Hifadhi. Sasa unajiuliza; hivi miaka zaidi ya 40 yote ambayo wamekuwa wakilima wakulima hawa kule Serikali ilikuwa wapi; mlikuwa mmeenda likizo?

Tunaomba kauli ya Serikali, ni kwa nini mnawashawishi wananchi wajiingize kwenye Sekta ya Kilimo lakini bado imekuwa ni kazi ya Serikali kutumia Vyombo vya Ulinzi na Usalama, mnatumia mgambo na Polisi kwenda kuwaondoa? Huu ni uonevu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele ya pili. Mheshimiwa Selasini, ajiandae Mheshimiwa Genzabuke!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kupewa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwasikiliza Wabunge wote wanaochangia hoja hii, hoja ya masoko ni hoja ambayo kila mmojawetu anaizungumza. Nami nitaizungumza, lakini nataka niizungumze nikihusisha na tukio ambalo lilitokea katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Mahindi limelimwa kwa ufanisi mkubwa sana hapa nchini kwa miaka kadhaa iliyopita. Wafanyabiashara wa zao hili la mahindi hasa wa Jimboni kwangu, wamekuwa wakijibidiisha sana kwenda mikoa mbalimbali hasa Ruvuma, kule Manyara, Mbeya na maeneo mengine, kununua mahindi kwa ajili ya masoko yao ambayo wamekuwa wakiyapata nchi jirani ya Kenya, Somalia mpaka hata Sudani ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara hawa wamekuwa na mvutano mkubwa sana wa muda mrefu na wa mara kwa mara kati yao na Serikali ya Mkoa pamoja na Askari Polisi wa Mkoa wa Kilimanjaro. Mwaka juzi na mwaka jana wafanyabiashara wa mahindi katika Soko la Holili na Soko la Tarakea, wamekuwa wakipewa vizuizi vingi sana katika kuvusha mahindi yao kuyapeleka kwenye masoko nje ya nchi. Ilifikia hata hatua Mkuu wa Mkoa akaamua kuanzisha soko la mahindi eneo la Himo na kuua lile soko la mahindi la Holili ambalo lilikuwa linawasaidia sana wafanyabiashara hawa na vijana katika kuwaongezea ajira na kuwapunguzia umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sakata hili baadhi ya Polisi walijitajirisha sana kwa kuwanyang'anya wafanyabiashara mahindi yao pamoja na pesa

zao. Pamoja na hayo, Mkuu wa Mkoa alituambia katika *RCC* kwamba, katika nyang'anya nyang'anya hii walikusanya shilingi bilioni mbili ambazo zingetumika kwa ajili ya kupeleka mashuleni kusaidia elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninaishangaa Serikali, wakati ina kilio kwamba wafanyabiashara watafute masoko, lakini hapo hapo Serikali za Mikoa na za Wilaya zinawakatisha tamaa wafanyabiashara wanapohangaika wenyewe kutafuta masoko yao kwa ajili ya kuuza mahindi haya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ifanye uchunguzi wa jambo hili ambalo Wananchi wa Holili na Wananchi wa Rombo hawatalisahau. Walinyanyaswa sana na Polisi, walinyang'anywa mahindi yao, walinyang'anywa fedha zao. Mimi nilishuhudia polisi wakivuka na viroba vya pesa ambavyo walikuwa wanawanyang'anya wafanyabiashara!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Himo njiapanda ya kwenda Mwika kuna eneo linaitwa Kilacha, polisi wanaweka gari lao pale utafikiria wanafanya kazi ya kuzia labda magendo ya namna gani, lakini kila wakiona *pick up* inapita na mahindi wanawanyang'anya! Sasa kama kweli hakuna masoko, kama kweli mahindi yamefurika, ni kwa nini Serikali haisimamii hili soko la mahindi ambalo wafanyabiashara ndogondogo wanalipata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia uchunguzi ufanywe kwa Soko la Mahindi la Himo, kwa sababu inasemekana huu ni mradi binafsi wa Mkuu wa Mkoa na watu wake, kwa sababu hata wanaotoza ushuru pale hawaeleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye soko la ndizi. Ukienda nchi za nje ndizi sita tu zinauzwa *pound* tano, sawa na shilingi 13,500. Katika maeneo yetu sisi wengine, zao la Kahawa ambalo ndiyo lilikuwa Zao la Biashara katika Wilaya ya Rombo linaelekea kufa na kifo chake kinasababishwa na bei ndogo ya kahawa ukilinganisha na gharama kubwa za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya madawa imekuwa kubwa sana, bei ya uzalishaji imekuwa kubwa sana, kahawa zimechoka zimezeeka, kiwango cha ubadilishaji au cha upatikanaji wa kahawa mpya kwa ajili ya kubadilisha na ya zamani kimekuwa kidogo sana; kwa hiyo, wakulima wamekata tamaa na matokeo yake sasa wameamua kujikita kwenye ZAO la Ndizi na mazao mengine ya mbogamboga kama kabeji, nyanya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeliomba Serikali iangalie namna ya kufanya utafiti na kuwasaidia hawa Wakulima kuweza kupata bei nzuri au soko zuri la ndizi ambazo sasa zimekuwa nyingi na zinaoza; na kwa sababu hiyo zinaleta

umaskini kwa sababu zao walilokuwa wanategemea la kahawa ndiyo hivyo tena na vilevile zao hili la ndizi limekuwa na ushindani mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu ushirika na hapa ninataka nizungumze juu ya *KNCU*. *KNCU* ni Chama cha Ushirika cha Wilaya za Hai, Moshi na Rombo. *KNCU* sasa hivi kinachofanywa na baadhi ya Viongozi wake ni jambo la kusikitisha sana.

Hili ninalolizungumza bahati nzuri tulishaliongea na Naibu Waziri, Mheshimiwa Zambi, ambaye alitupa maelezo na alitupa ushauri wa kutosha lakini ule ushauri hautekelezeki kwa sababu ya ubabe wa baadhi ya Viongozi wa *KNCU*. Hapa ninaiomba Serikali iingilie kati. Mali za *KNCU* zinauzwa, majumba yanauzwa, magari yameuzwa, hoteli zimeuzwa, sasa mashamba yanauzwa na baadhi ya viongozi, wakidai wanataka kulipa deni la *KNCU* ambalo haliishi. Serikali isipoingilia kati, wakulima wanapata hasara, wakulima wanakata tamaa na Ushirika huu utakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *KNCU* ni Chama ambacho kimesaidia sana Wakulima wa maeneo haya katika mambo mbalimbali. *KNCU* imesomesha Wanachama wake, *KNCU* imesaidia katika mambo mengi, lakini watu wachache wanataka kuiua kwa faida zao wenyewe. Naomba sana Wizara iliangalie hili na itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu mazao mchanganyiko hasa *horticulture*. Yapo maeneo katika nchi hii yanalima matunda mengi sana; maembe, machungwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ajabu ukienda kwa mfano pale Segera, watu kutoka Kenya wanakuja kununua machungwa pale wanayapeleka Kenya, yakifika huko wanatengeneza *concentrate* wanarudisha *concentrate* hapa nchini wanakuja kuuza kwa ajili ya viwanda vyetu. Ninaomba sana tuangalie uwezekano wa kusaidia hawa wakulima na siyo wakulima … *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Selasini kengele ya pili. Mheshimiwa Genzabuke, ajiandae Mheshimiwa Sara Msafiri, ajiandae Mheshimiwa Mheshimiwa Dkt. Nkya!

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Kwanza kabisa, kabla sijasahau naunga mkono hoja hii ili bajeti iweze kupita, pembejeo ziweze kupatikana, madawa yapatikane na Wananchi wa Kigoma na sehemu nyingine katika nchi yetu waweze kunufaika kupitia Bajeti hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hiyo.

Ninaipongeza Serikali kwa sababu kwa miaka miwili mfululizo kwa maana ya mwaka 2013/14 na mwaka 2014/15, Taifa limejitosheleza kwa chakula hadi kufikia utoshelevu kwa asilimia 125.

Naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Tumejitosheleza kwa kiasi kikubwa, mazao yalipatikana kwa wingi, lakini likajitokeza tatizo la ukosefu wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Wizara ya Viwanda na Biashara itusaidie kupitia Kitengo kile, mazao yanapokuwa mengi waweze kutusaidia kutafuta masoko, ili wananchi wetu waweze kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mwaka uliopita Wananchi wa Ruvuma, Rukwa na sehemu mbalimbali katika nchi yetu, wamelalamika kwa sababu mahindi yao yalikosa soko, mpunga ulikosa soko, sukari nayo ilikuwa tatizo.

Kwa hiyo, tunaomba Wizara ya Biashara ijitahidi kupitia Kitengo hicho. Walianza kurushiana mpira; wakulima wanasema ni Wizara ya Kilimo ndiyo inatakiwa kutafuta soko, lakini huku nako Wizara ya Biashara nayo inatakiwa itafute ni jinsi gani inaweza kupata soko.

Kwa hiyo, ninaomba Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara, wote kwa pamoja wakae mezani, waone ni jinsi gani wanaweza kutafuta ufumbuzi ili wananchi wasiendelee kuzalisha chakula na kupata shida badala ya kupata neema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa kuendelezwa ni nini? Ni kuhakikisha uzalishaji unakuwa endelevu. Hatua za kuchukua ni kutenga fedha za ziada kwa kilimo cha umwagiliaji kama tunavyofanya kwa miradi ya maji, barabara na umeme vijijini kwa maana ya *REA*. Zitengwe pesa kwa ajili ya kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji nacho kinakua kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo kilimo cha umwagiliaji kimeshamiri, kama vile Wilaya ya Kakonko, wananchi maisha yamebadilika

ghafla, wanazalisha mpunga! Mpunga umekuwa mwingi, kwa sasa hivi hawana njaa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini barabara ya Kigoma – Nyakanazi itakapokuwa imekamilika, wananchi wale wataondokana na umasikini kwa sababu wataweza kupeleka mchele kwenda kuuza sehemu mbalimbali, vilevile ni wakulima wa alizeti. Naamini wataweza kunufaika kwa sababu wanalima mpunga kutokana na kilimo cha umwagiliaji. Mwanzo kabla hawajalima kilimo hicho cha umwagiliaji, walikuwa ni masikini sana, lakini sasa wameweza kuwa na hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sehemu zile ambazo hakuna kilimo cha umwagiliaji, nashauri Serikali iweke mpango maalum chini ya *BRN* ili kujenga mabwawa katika Mikoa isiyokuwa na mito ya kudumu na mifereji ya umwagiliaji. Naomba mabwawa yajengwe. Tukifanya hivyo, ukame hautaathiri mazao na zaidi ya 25% ya mazao itakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itekeleze sasa yafuatayo ambayo nakumbuka yamekwishapitishwa na Bunge lako Tukufu. Moja, Sera ya Taifa ya Umwagiliaji, Sheria ya Umwagiliaji itumike, isikae vitabuni tu, ifanye kazi na Mfuko wa Umwagiliaji uanze kufanya kazi. Mfuko huu ukianza kufanya kazi, wananchi wale wanaoishi maeneo ambayo ni kame wataweza kunufaishwa na mfuko huu kwa sababu mabwawa yatachimbwa, maji yatahifadhiwa, watalima kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nashauri Tume ya Umwagiliaji ianze kazi mara moja! Nashauri Tume ya Umwagiliaji ianze kazi mara moja. Naomba Mheshimiwa Waziri aeleze, Ofisi za Umwagiliaji katika Mikoa na Wilaya zimeanzishwa kama zilivyopitishwa ndani ya Bunge hili? Tunataka kujua! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, naenda haraka haraka, naomba nizungumzie mambo ya ushirika. Mheshimiwa Chiza, mwezi uliopita alikuwa Kigoma, alipofanya ziara katika Mkoa wa Kigoma alikutana na Wajasiriamali wa Jukwaa la Wanawake akaongea nao, wakamwomba Mfuko wa Uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa wanawake wanaojishughulisha na kilimo, biashara ya chakula na mazao ya kilimo, Idara ya Ushirika iwasaidie wanawake wa Kigoma wapate mashine na viwanda vidogo vya kusindika mazao yao. Kwa sasa hivi tunamshukuru Mungu, kupitia Sera nzuri ya Chama chetu cha Mapinduzi, tuna umeme japokuwa haujawa wa gridi ya Taifa, lakini naamini kupitia mpango huu wa Umeme Vijijini, wananchi wataweza kuanzisha

viwanda na kunufaika kupitia viwanda hivyo ambavyo tutakuwa tumepatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali isimamie vizuri ruzuku ya pembejeo, wakulima washirikishwe kikamilifu. Uzoefu unaonesha kuwa miaka ya nyuma mbolea nyingi imeuzwa nchi za nje. Nimekuwa nikilalamika muda mrefu, mbolea ilikuwa ikipelekwa, badala ya kuwanufaisha wakulima, ilikukuwa inaenda kuwanufaisha wananchi wa nchi jirani ya Burundi. Kwa hiyo, naomba mweke mipango mizuri ili wananchi waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wamekuwa wakidanganywa wakati mbolea ilipokuwa ikiuzwa kwa njia ya ruzuku, wanapelekwa kusainishwa vocha za pembejeo. Utaratibu huu haukuwa mzuri, tunaomba uangaliwe kwa kuwa na suala la wasimamizi kudanganya wakulima na kuandika taarifa za uwongo, lilikithiri. Sasa hivi hatutaki, tunaomba mpango huu… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sara Msafiri na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, ajiandae!

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti hii. Kwanza, naipongeza Kamati kwa Taarifa yake nzuri, lakini vilevile naipongeze Wizara kwa kazi nzuri inayoifanya. Pamoja na pongezi hizo, naomba sasa nianze kuchangia kwenye suala la matrekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, suala la kilimo ni shughuli ambayo inachukua karibu takribani asilimia 75 ya Watanzania. Kwa hiyo, ni sekta kubwa sana na ambayo inategemea uchumi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza kabisa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kupitia *SUMA – JKT;* waliweza kushusha bei ya matrekta, yaliuzwa kwa bei nafuu na wananchi wamefaidika. Niseme tu kwamba kwa Mkoa wa Morogoro ambao natoka, ndiyo Mkoa unaoongoza kwa kununua matrekta mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, bado ule mfumo uliotumika wa kupeleka haya matrekta na kununuliwa na wakulima, siyo mzuri. Lazima ufanyiwe marekebisho kwa sababu walionufaika sana na ule mfumo ni wafanyabishara. Ukiangalia wakulima ambao wako kwenye vikundi vile vya kilimo, haukuwafaidisha sana kwa sababu wao wana vikundi vidogo, lakini Halmashauri zilikuwa hazitambuliwi kwenye huu mfumo wa kupeleka haya matrekta! Matokeo yake sasa wafanyabiashara ndio walifaidika na huu mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu ihakikishe kwamba Halmashauri zinashirikishwa. Kuandaliwe mfumo ambao Halmashauri itatambua hivi vikundi vya wakulima viweze kukopeshwa haya matrekta ili waweze kufaidika na mfumo huu wa moja kwa moja wa kupata matrekta kuliko wafanyabiashara wananunua halafu wanawakodisha wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile haya matrekta ya *SUMA – JKT* nadhani yanatoka India. Kwa hiyo, unakuta wakulima wenye matrekta haya wanapata shida kupata vipuri *(spare),* matokeo yake sasa unakuta matrekta yanaharibika kwa muda mrefu, msimu wa kilimo umefika, wanashindwa kufanya kazi. Kwa hiyo, naiomba sasa *SUMA – JKT* na Serikali yangu kuhakikisha kwamba wanaingiza *spare* za kutosha za haya matrekta ili wakulima waweze kutumia matrekta na waachane na jembe la mkono la moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nataka kuongelea kwenye masuala ya kilimo cha miwa. Mkoa wa Morogoro tunalima miwa na maeneo mengine yanalima miwa. Tuna Kiwanda cha Mtibwa na Kilombero kule tuna viwanda viwili, lakini bado kuna changamoto kubwa sana kwenye kilimo cha miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kila mara tumekuwa tunaongelea hizi changamoto, lakini bado, nasema Serikali yangu na ukisoma ripoti za Kamati zote mbili, inaonekana Serikali inatakiwa iongeze nguvu kuhakikisha inatatua matatizo kwa wakulima wa miwa na viwanda.

Kwa mfano, kwenye Wilaya ya Mvomero (Morogoro), kuna kiwanda cha Mtibwa; wakulima hivi ninavyoongea wanadai pesa zaidi ya Shilingi milioni 500. Vikundi vya kilimo cha miwa vinadai. Kiwanda kinashindwa kuwalipa wafanyakazi kuanzia mwezi wa Pili mpaka mwezi wa Tano, wafanyakazi wa Kiwanda cha Mtibwa wanadai mishahara yao. Hivi ninavyoongea, mwekezaji amesema atawalipa kwa awamu na madeni haya yatakwisha mwezi wa Nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaangalia kimsingi hawa wafanyakazi wanafanya kazi kwa mkopo, jambo ambalo haliwezdkani, wanashindwa kuhudumia mahitaji yao mengine! Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kulikuwa na Sheria inasema kwamba ndani ya kilometa 50 kusiwe na kiwanda kingine. Lakini unaona wakulima wa miwa mazao yao yanaoza shambani, kiwanda ni kimoja, hakina uwezo wa kuvuna miwa yote ya wakulima. Serikali ihakikishe inabadilisha hii sheria na itafute mwekezaji, iongeze ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na viwanda vingi, kukiwa na ushindani, hata haya matatizo kwamba kuna baadhi ya viwanda vinaficha sukari, ndiyo

maana sukari inakosekana, itakuwa hakuna kwa sababu viwanda vitakuwa vingi na mkulima ataamua mazao yake auze wapi; na Serikali itaweza kuwasaidia wakulima waweze kuondokana na umasikini. Wakulima wanadaiwa hela nyingi, wamekopa kwenye mabenki, kwenye *SACCOS,* wanashindwa kulipa. Wanadai kiwanda na miwa mingine inaharibika shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wakulima wameitikia mapinduzi ya kilimo, wanalima kisasa, wanalima kwa wingi, kiwanda kilichopo hakina uwezo wa kuvuna miwa yote, kwa nini sasa Serikali isiwekeze kiwanda kingine? Inalazimisha Sheria za zamani, zimepitwa na wakati, watu wana matrekta wanalima kisasa, wanatumia mbolea, miwa inaharibika; watu wanafilisiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo inawekwa Dar es Salaam; mkulima gani ataenda Dar es Salaam? Hii benki ni lazima iwe *centred* kwenye Mikoa ambayo inalima kwa sababu ni moja kwa moja ya wakulima. Ianzishe na matawi hata kwenye Kanda. Kila kitu Dar es Salaam, haiwezekani. Lazima tuwe na usawa katika mgawanyo wa rasilimali. Kama ni masuala ya kilimo, iangaliwe Mikoa ambayo inalima. Sasa hivi tuna umeme wa kutosha, hakuna tena sababu kwamba kila kitu kiwe Dar es Salaam. Waje wawekeze kwenye Mikoa ambayo shughuli hizo zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni madai ya wakulima; Serikali bado inadaiwa na wakulima. Ni muda sasa wakulima walipwe pesa zao na Serikali isikope tena wakulima, wanashindwa kusomesha watoto, wanashindwa kulipia huduma za afya, wanashindwa hata kuchangia ile michango ambayo ni moja kwa moja inaenda kuwasaidia katika huduma za kijamii. Serikali iandae utaratibu; najua imeanza kulipa wakulima, lakini inalipa kwa *speed* ndogo. *(Makofi)*

Sasa hivi wakulima wanakaribia kuvuna, mazao yatakuwa kwenye maghala. Wana deni wanaloidai Serikali, halijaisha. Sasa haya mazao watakayoyavuna wataenda kuuza wapi? Kwa hiyo, naiomba Serikali itafute masoko. Umasikini wa Watanzania siyo sawasawa na umasikini wa watu wa Sudan au Ethiopia. Watanzania wanalima na wana mazao; wana ng'ombe na wana mifugo; inakuwaje wanaendelea kuwa masikini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu amelima na ana mazao, Serikali isaidie ipate soko la uhakika. Lakini kuendelea kuwakopa wakulima ni kuwarudisha nyuma na ni kurudisha Watanzania nyuma maana wao ndiyo asilimia 80 ya Watanzania wote. Sasa kama wote wako kwenye hali duni, tutaondokanaje na umasikini? Tutaongezaje uchumi wetu tukawa kwenye uchumi wa kati? Kwa hiyo, naiomba Serikali iandae mfumo; wakulima wanalima na wanavuna kwa faida. Sasa Serikali itafute masoko kwa wakulima, iondokane

na mfumo huu wa kuwakopa wakulima ili na wao waweze kusomesha watoto, kujenga nyumba nzuri na wapate huduma za afya na za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo yalikuwa yangu. Mwisho, migogoro ya wakulima na wafugaji itafutiwe ufumbuzi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya na Mheshimiwa Bura, naona hayupo, Mheshimiwa Mtutura, jiandae.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nami nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kazi nzuri na juhudi zao za kuboresha kilimo katika nchi yetu, tukijua kwamba kilimo ndiyo ajira namba moja kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Menyekiti, naomba niseme kwamba katika Jimbo langu ajira kubwa kwa wananchi wangu kwa asilimia karibu 90 ni kilimo. Naomba nimpongeze, lakini niseme kwamba hiki kilimo bado hakijaleta tija wala kubadilisha maisha ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kuhusu mabadiliko ya tabia-nchi ambavyo yameathiri kilimo katika sehemu nyingi za nchi hii, hususan katika Jimbo langu na Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka miwili mfululizo tumeendelea kupata mafuriko katika Wilaya ya Morogoro Vijijini na matokeo yake ni kwamba hata Skimu za Umwagiaji ambazo zilikuwa zimeanza kujengwa na zilikuwa hazijamalizika, nyingine zimeendelea kuathirika. Nashukuru kwamba kwenye bajeti ya mwaka 2015/2016 nimeona Wizara imejizatiti kukarabati Skimu kama tatu

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kukarabati hizo Skimu, ili tupunguze tatizo la mafuriko, naomba watutengenezee mabwawa kwa ajili ya kuhifadhi maji tuweze kuwa na umwagiliaji endelevu, tuondoe umasikini katika eneo la Kiloka, Mbaragwe, Tulo Kongwa pamoja na Matuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Skimu ya Matuli, imejengwa muda mrefu, lakini inatumika tu wakati wa mvua. Sasa hakuna sababu ya kuwa na Skimu kama wakati wa kiangazi hatuwezi kumwagilia. Naomba Wizara iangalie hiyo Skimu ya Matuli kwa sababu tuna eneo kubwa la kilimo pale; ikiweza kufanya kazi kwa mwaka mzima, tutaongeza tija ya kilimo kwa wakulima, tutaondoa

umasikini na Halmashauri yetu itaacha kuendelea kuwa na umasikini tuliokuwanao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sasa mashamba ya *BRN*. Katika Wilaya ya Morogoro Vijijini tumekuwa na maeneo mawili ambayo yamechukuliwa mashamba. Shamba moja liko katika Kata ya Mkulazi, shamba namba 217. Kwenye hilo shamba bado kuna vijiji vimo ndani na tuliomba tuweze kupata ekari 3,000 kwa ajili ya wananchi wanaohamishwa kutoka kwenye eneo la Kidunda, kupisha bwawa la Kidunda. Mpaka sasa hivi nashindwa kuelewa kwamba kigugumizi kinatoka wapi? Kwamba hili eneo lote linakabidhiwa *TIC* bila kuangalia mahitaji ya wananchi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema hivi, kwa sababu wanakuja kulima miwa na mpunga ili matatizo yanayotokea Mtibwa yasije kutokea tena katika eneo hili, basi maeneo ya wananchi yatayarishwe, halafu atakayekuja kuwekeza kule, aingie Mkataba na wananchi kwamba atanunua miwa ya wale ambao wanalima kuzunguka kwenye eneo hilo, isije ikawa kwamba yeye atanunua kama hisani kwao. Kwa sababu, wao mchango wao ni ile ardhi. Kwa hiyo, hao waangaliwe kwa jicho la upendeleo kwa sababu Kijiji na wananchi ndio wenye ardhi, yule anakuja kuwekeza. Kwa hiyo, akiwekeza basi, iwe ni faida kwa wale wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie masoko. Masoko yamekuwa ni matatizo. Nashukuru kwamba Wizara na Serikali imeanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko, lakini hii Bodi bado haijaanza kazi. Mimi inaniumiza sana kwa sababu wananchi wangu wa Morogoro Vijijini kule wanalima sana ufuta, lakini hawa wananchi wanadhulumiwa kwa sababu anakuja mnunuzi huyu anasema niuzie kwa kisadolini; mwingine anasema niuzie kwa *plastic*! Sasa *plastic* kuna ndoo ya lita 20 na ndoo ya lita 10!

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu wanawaweka rehani kwamba, wanakaa kwa pamoja wana-*colude* wale wanunuzi! Wanasema kwamba, sisi tunaamua kwamba ni Shilingi hizi; tusinunue. Kwa hiyo, wananchi wanakaa na ufuta wao ndani, ni masikini. Kwa hiyo, inafika mahali wana-*give up* wanaamua kuuza!

Kwa hiyo, hawa wanunuzi wanawanyonya watu wetu; tunaomba Bodi ya Mazao Mchanganyiko ianze kazi mapema iwezekanavyo. Naomba kama ikiwezekana basi, Makao yake Makuu yawe Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu waliotoa wazo kwamba Benki ya Kilimo isikae Dar es Salaam iweke Makao yake Makuu katika Mkoa wa Morogoro. Pale Morogoro wanaotoka Kusini, ni karibu. Watakaotoka Kusini au Mashariki na Magharibi ni karibu; na tunalima sana katika Mkoa wa

Morogoro; katika eneo la Mahenge pamoja na Kilombero, limeingia kwenye mpango wa *SAGCOT*.

Kwa hiyo, naomba hiyo benki, pamoja na benki nyingine ambazo zitagusa wakulima na wananchi walio wengi vijijini, ziache kuwekwa Dar esSalaam kwa sababu Dar es Salaam imeshaendelea vyakutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mfumo au utaratibu wa ruzuku ya pembejeo. Kwa mwaka huu, naomba kusema kwamba wananchi wangu hawakuweza kupata faida ya hii ruzuku kwa sababu hawakujua huu utaratibu mpya. Naomba elimu itolewe, halafu na Halmashauri sasa iwajibike vya kutosha kuhakikisha kwamba kunakuwepo na vikundi madhubuti ambavyo vitawahudumia wananchi wote, siyo *section* ya wananchi tu; kwa sababu wananchi wote ni Watanzania na wana haki ya kupata ruzuku ambayo inatolewa na Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pembejeo umekuwepo kwa muda mrefu, lakini ukienda Kisaki, ukaenda Mkulazi, ukamwuliza mwananchi kwamba kuna Mfuko wa Pembejeo, atakushangaa sana kwa sababu hawajajitangaza, hawajatoa elimu na wanaofaidika ni watu wa mijini na wafanyabiashara wakubwa wakubwa. Ndiyo sababu, sehemu kama kule kwetu Tarafa ya Ngerengere, mashamba ni makubwa lakini wananchi wanategemea kilimo cha kutumia ng'ombe ambao nashukuru Wasukuma wameleta ng'ombe wachache, lakini wasilete wengi kwa sababu wataharibu badala ya kujenga na migogoro itaendelea; naomba Mfuko wa Pembejeo uangalie namna ambavyo utakwenda kwa walengwa ambao ni wakulima masikini wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni usindikaji wa mazao. tuna matunda mengi sana Morongoro.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ni kengele ya pili hiyo. Mheshimiwa Bura hayupo; namwita Mheshimiwa Mtutura na Mheshimiwa Juma Nkumba jiandae.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Naanza moja kwa moja juu ya zao letu kuu la uchumi katika Jimbo lile la Tunduru Kusini, Tunduru Kaskazini na Mikoa ile ya Kusini yote kwa ujumla zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yoyote duniani, wanapotunga sheria dhamira ni kutatua kero inayowazunguka katika eneo husika, lakini pale inapoonekana sheria ile iliyotungwa haitatui kero iliyokusudiwa, basi sheria hiyo mara zote inakosa uhalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kuzungumzia suala hilo hasa suala la Sheria ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Watumishi wengi wa Serikali na hata vyombo vile vinavyosaidia katika ununuzi wa zao la korosho, wamekuwa wakiunga mkono sana sheria hii bila kufanya tathmini ya kutosha kwa wakulima wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa kwamba hii Sheria ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani imefanya vizuri sana hasa kwa eneo la Tandahimba, kidogo na Newala. Lakini maeneo mengi, chukua Pwani, nenda Nachingwea (Lindi), Masasi (Tunduru) bado sheria hii ni kero. Hata huko Newala na Tandahimba kuna baadhi ya wakulima nao bado wanailalamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sheria hii inaweza ikaleta unafuu kwa watu wachache na walio wengi bado wanailalamikia, sheria hii inakosa uhalali mbele ya jamii. Sheria yenyewe ukiangalia vifungu vyake vimekaa vizuri, lakini kuna mianya ambayo imejitokeza pale kwa watu ambao hawana nia njema kwa wakulima wetu wa korosho kuitumia vibaya. Matokeo yake sasa mkulima ambaye ndiye anayetakiwa kuneemeka na mazao yake ya korosho, ndio anakuwa mhanga wa kwanza kuadhibiwa na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo ni nyingi; mkutano uliopita niliwahi kutaja baadhi ya tozo, vyama vya msingi vinakwenda kukopa fedha katika mabenki, riba hii inalipwa na mkulima ambaye hakushiriki hata mara moja katika kuhakikisha kwamba fedha zile zinapatikana kule benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini riba hii ilipwe na mtu ambaye hakushiriki katika majadiliano ya kukopa hizi fedha? Kwanini mkulima abebeshwe mzigo wa gharama mbalimbali zinazotokana na sheria hii? Lakini kikubwa zaidi, Sheria ile ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani ambayo nasema kwamba kimuundo ni nzuri lakini utekelezaji wake bado ni matatizo, Kwanini isiandaliwe mazingira ambayo mkulima atalipwa fedha zake mara moja, badala ya kulipwa robo robo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaumiza sana! Mkulima amejinyima mwaka mzima ili aweza kunufaika kutokana na zao lake la korosho; lakini cha ajabu, anapovuna, akipeleka kuuza korosho zake, leo atalipwa nusu, kesho atalipwa robo, keshokutwa analipwa robo. Maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa wiki uliyopita, niliwahi kuzungumzia hapa kwamba hivi ni mfanyakazi gani ambaye atakuwa tayari kulipwa mshahara wake baada ya mwisho wa mwezi robo robo? Kama hakutafumka maandamano hapa au mgomo wa nchi nzima! Sasa kwanini mkulima huyu mnyonge aendelee kunyanyaswa kiasi hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msimu huu unaokuja, Serikali iandae mazingira ambayo mkulima atalipwa fedha zake za korosho mara moja fedha zote. Yaandaliwe mazingira ambayo mkulima hatahusika kwa namna yoyote juu ya hiyo mikopo ambayo wanakopa huko, kwa sababu tunambebesha mzigo ambao yeye hakuhusika kwa namna yeyote katika kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inasema wazi kwamba korosho zikusanywe, ziwekwe kwenye ghala, ziuzwe ndipo mkulima alipwe fedha zake. Haya mambo ya kwenda kukopa huko mmeyatoa wapi? Haya mambo ya kumlipa mkulima nusu nusu mmeyatoa wapi, wakati sheria haijazungumza chochote juu ya suala hilo?

Kwa hiyo, tunaomba Serikali itenge fedha za kutosha, ikatoe elimu kwa wananchi, ikatoe elimu kwa wakulima kwamba korosho zao zikusanywe ziwekwe kwenye ghala, ziuzwe ndipo walipwe fedha zao zote kwa mara moja. Kwa sababu huwezi kukaa na fedha za mtu ilhali mtu mwenyewe ana matatizo.

Kipindi hiki cha mavuno ya korosho ndicho kipindi cha wananchi cha kutatua matatizo yao, ndicho kipindi ambacho wanatakiwa wapeleke watoto sekondari, ndicho kipindi ambacho yeye anatakiwa aandae pembejeo za mazao za chakula.

Sasa fedha zake mnakaa nazo, atatumia fedha zipi kumwandaa mtoto kwenda shule? Atatumia fedha zipi kuandaa pembejeo za mazao ya kilimo ilhali fedha zimekamatiwa kwenye Vyama vya Ushirika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa, kwa sababu uchaguzi umepita mwaka jana, Vyama vingi vya Msingi vina uongozi mpya; nawaomba wakulima wajenge imani kwa uongozi huo mpya uliopo sasa hivi, wakishawishiwa kwamba korosho zao wazikusanye ziwekwe kwenye ghala, wakubali wakiwa na imani kabisa sasa hivi uongozi katika Vyama vyetu vya Msingi ni mpya. Tunaamini kabisa wao watakuwa waaminifu jinsi tulivyowaamini katika uchaguzi ule uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii vilevile kumpongeza sana Mwenyekiti wetu mpya wa Chama cha Ushirika (TAMCU), Ndugu Kambutu, wananchi wa Tunduru wamekuwa na imani naye, naye aonyeshe imani kwao kwa kusimamia maslahi ya wananchi wa Tunduru yote. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Juma Nkumba na Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Dkt. Kayombo wajiandae.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze tu kwa kuishauri Serikali juu ya uwiano mbaya wa matumizi ya kawaida na fedha zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti yetu; bajeti kubwa na vilevile bajeti za Wizara unaona ni namna gani Serikali haijajielekeza kutoa ufumbuzi wa matatizo ya wananchi, kwa sababu matatizo ya wananchi yatatuliwa kwa kutenga fedha nyingi sana za miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, unakuta fedha nyingi sana zinatengwa kwa ajili ya kuwalipa hawa mishahara na posho kwa watumishi lakini wale watumishi hawawezeshwi kazi ya kwenda kufanya kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kuona namna gani sasa Serikali inajielekeza kwa kasi kubwa sana kutenga fedha nyingi zaidi kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, limezungumzwa hapa suala la ununuzi wa tumbaku kwa dola. Nataka niiulize Serikali, hili jambo tumelisema kwa muda mwingi na Serikali kila wakati inasisitiza hapa kwamba biashara ya aina yoyote ndani ya nchi itafanyika kwa fedha za Tanzania. Sasa nataka niulize huu ni mradi wa nani? Maana kila tunapozungumza, Serikali inaziba masio, haitekelezi jambo hili. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie ni namna gani basi inalifanyia kazi na kulitafutia ufumbuzi suala hili ambalo wananchi wengi hawalihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ruzuku kwenye baadhi ya mazao, lakini zao ambalo linaingizia nchi yetu fedha nyingi za kigeni, kwa mfano, zao la tumbaku; hakuna ruzuku yoyote kwenye pembejeo zake. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, kama tunaweza kuwa na fedha zinazotengwa kwa ajili ya ruzuku, hata fedha zile za ndani, kama zile za nje zina masharti basi tujitahidi sana kuwapunguzia mzigo wakulima wetu ili waweze kulima vizuri zao hili na kupata tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la uhaba wa wateuzi wa tumbaku. Suala hili na lenyewe tumelizungumza sana mwaka uliopita na miaka miwili iliyopita. Lakini Serikali na yenyewe sasa kwenye jambo hili inaamua tu kutafuta fedha kwa sababu amesema Mheshimiwa Kawawa hapa, tuna fedha karibu Shilingi bilioni na kitu zinaingizwa kupitia tumbaku. Lakini namna gani basi zao hili linaimarishwa katika suala la uteuzi; katika suala la kuwaimarisha wateuzi na vilevile suala la ugani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa lugha yao ya Kikwere huko, huwa anatuambia kila siku, ukitaka kula na wewe lazima uliwe. Lakini sasa inaonekana Serikali inataka fedha tu, lakini kwa namna moja ama nyingine kuhakikisha zao hili linaendelea kuwa sasa zao la uhakika, hakuna fedha zozote zinazotolewa. Kwa

hiyo, naomba sana Serikali ijitahidi sana kuhakikisha kwamba zao hili na lenyewe linapata fedha za kutosha ili wakulima waweze kulima kwa wakati lakini vilevile kujitahidi sana kuhakikisha kwamba kwa namna moja ama nyingine wanapata fedha zao kwa uhakika lakini zao lao likiwa kwenye hali nzuri baada ya kununuliwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kwa namna moja ama nyingine kuipongeza sana Wizara kwa kufanya kazi kwa wakati mgumu maana fedha zinazopelekwa kwenye Wizara hii ni ndogo mno ukilinganisha majukumu makubwa sana ya Wizara. Lakini kwa namna moja ama nyingine, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wake wamejitahidi kujibana na kufanya kazi zao katika kutekeleza jambo hili kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba vile vile kwamba yale maelezo ambayo yametolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ya kuendelea kuimarisha ushirika wetu, ya kuhakikisha kwamba wabadhirifu wote wanaowaibia wanaushirika wanachukuliwa hatua, basi hatua zichukuliwe kwa haraka. Yako malalamiko mpaka sasa, baadhi ya wezi, wabadhirifu waliowaibia wakulima, walioibia wana ushirika, hawachukuliwi hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa nilikuwa namtania Mheshimiwa Waziri, nikamwambia hivi kesi za watu waliowaibia, zinachukua muda gani? Kuna watu wengine wanaiba Sh. 100,000/=, Sh. 200,000/= au Sh. 50,000/=, kuna watu wanaiba kuku; leo anaiba, kesho yuko Mahakamani. Hao wanaowaibia watu mabilioni ya fedha, wanachukua muda gani? Kuna uchunguzi gani dhidi ya taarifa ya CAG? Kuna uchunguzi gani dhidi ya taarifa mbalimbali zilizotolewa na ukaguzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonyesha wazi kabisa, wizi upo. Kuna kesi zinachukuliwa kwa muda mfupi na watu wanachukuliwa hatua, wengine wanafungwa, wengine wanaachiwa huru. Lakini wale ambao wanaiba fedha nyingi kwa kuwaiba wakulima mpaka leo hii uchunguzi bado unaendelea. Hili jambo linaendelea kuwakatisha tamaa wakulima na wanaushirika. Kwa hiyo, nalo hili nilikuwa naomba Serikali ichukue hatua za haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba nichukue fursa hii kusema kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kayombo na Mheshimiwa Matiko na Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda wajiandae.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kutupa nafasi ya kuweza kujadili Wizara hii ya Kilimo; Wizara muhimu sana katika Taifa letu na inagusa watu wengi sana.

Napenda pia kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Uongozi mzima katika Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya na inadhihirishwa na mambo mengi ambayo yameandikwa katika kitabu hiki. Lakini hii haina maana kwamba kazi hii ni kamilifu, kuna upungufu kadhaa ambao tutauonyesha hapo mbele kidogo, lakini kwa ujumla wanajitahidi sana kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kuzungumzia hasa madeni. Wizara hii inadaiwa na wakulima, ambao kipato chao ni kidogo sana kuliko Serikali yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Hesabu za Serikali *(PAC)*, tuliwahi kujadili hesabu za Mkoa mmoja ambako Mkandarasi alilipwa riba ya Shilingi milioni 300 kwa sababu Serikali hawakumlipa mapema. Sasa hawa wakulima ambao wanacheleweshwa namna hii malipo yao: Je, Serikali itawalipa kwa riba pia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wakulima waliouza mahindi, bado wanaidai Serikali; wako wafanyabiashara wadogo wadogo na wakubwa pia ambao walitoa pembejeo miaka miwili, mitatu iliyopita; bado hawajalipwa. Mimi nadhani hii siyo jambo jema kwa nchi yetu na siyo jambo jema mbele za Mungu pia kuwadhulumu watu wadogo na wanyonge kama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa umahiri wa Waziri wa Kilimo na Naibu wake wafanye kila linalowezekana watu hawa walipwe mapema; kwa sababu mabenki yanawadai, na inawatishia kuwapeleka Mahakamani na kuwanyang'anya vitu vyao. Wataadhirika kwa sababu wametoa huduma kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa habari ya Mbinga, kuna Chama cha Ushirika cha MBIKU nacho kinadai ambapo Serikali iliahidi kulipa Shilingi milioni 223. Sasa ni zaidi ya miaka kumi ahadi hii haijatekelezwa. Mheshimiwa Rais alipofika aliahidi kwamba watalipwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri hawa wakulima ingefaa wafikiriwe kulipwa kama ambavyo madeni mengine yanalipwa.

Pia taasisi ndani ya Wizara, yaani *NFRA*, nayo inadaiwa na Halmashauri ya Mbinga, zaidi ya Shilingi milioni 400 na Halmashauri ya Mbinga unavyoona mtiririko wa fedha unavyokwenda ni kidogo, fedha hizi wakizipata zitawasaidia sana. Kwa hiyo, ningeomba utusaidie kuwaambia *NFRA* wailipe Mbinga haraka inavyowezekana ili waweze kutimiza malengo waliyonayo kule Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia juu ya Ushirika. Naamini kwamba wakulima wetu bila ushirika hawataweza kukombolewa kama vile tunavyotegemea. Lakini kitabu hiki, ushirika ina kurasa mbili tu; na Wizara ni ya Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini kurasa zake ni mbili tu zinaongelea habari za ushirika. Lakini naamini mambo yaliyofanywa katika ushirika ni makubwa. Kule Mbinga mwaka 2014 Vyama vya Msingi tumekopesha Ushirika; na ninavyoongea sasa *NSSF* wamesha-*approve* mkopo wa Shilingi bilioni mbili na bado kama Shilingi bilioni tano ambazo ziliko kwenye *process*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi kubwa ambayo Watanzania wanapaswa waifahamu, ni ukombozi mkubwa kwa wakulima na kama jambo hili litakwenda nchi nzima, tunaweza tukabadilisha maisha ya wakulima hawa yakawa bora zaidi kwa kutumia taasisi zetu hizi kama *NSSF*. Kwa namna ya pekee napenda sana kuwashukuru viongozi wa *NSSF* kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa ajili ya Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni usindikaji. Tunauza mahindi bila kutengeneza unga, tunauza korosho ghafi, tunauza kahawa ghafi; nafikiri ifike wakati tuweke sera kwamba baada ya kipindi cha miaka mitatu au minne hatutaagiza unga nje, hatutaagiza mafuta ya kupikia kutoka nje, tutakula vitu ambavyo tunavitengeneza humu ndani. Hii itasaidia sana kujenga uwezo wa wajasiriamali na wananchi wetu. Bila kufanya hivyo hatuwezi kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1980 tuliagiza magari ya Chai Maharage kutoka Korea. Yalikuwa ni magari ambayo yalikuwa duni na ulikuwa ukipanda lile gari hujisikii vizuri. Lakini ukiona yale magari sasa, yameboreshwa, ni mazuri mno. Kwa hivyo, tusipoanza kutengeneza vya kwetu na kuvijali, kwa uhakika tutaendelea kuvishangaa vitu vya wenzetu na kutumia fedha za kigeni nyingi sana kuagiza vitu kutoka nje; kuagiza mafuta na unga kutoka nje. Jambo hili linaweza likawekewa ukomo; nami napendekeza pengine ukomo wa miaka mitatu unatosha kuifanya nchi hii kwamba baada ya hapo tusiagize mafuta yoyote ya kula kutoka nje, wala unga, wala aina yoyote ya vyakula kutoka nje na hili litatusaidia sana kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Jambo lingine ambalo ningependa kuongelea ni kuhusu zao la mahindi na mazao mengine mchanganyiko. Mwaka 2014 kule Mbinga tumepata taabu sana, tumebakiwa na mahindi kwa muda mrefu mno na mpaka sasa bado wananchi wanayo, hayakunuliwa yote. Idara ya masoko nayo haikutusaidia sana. Nimeongea na Naibu Waziri na Waziri wa Viwanda kuhusu masoko ya mahindi. Kwa kweli sielewi kwanini yale mahindi hayakunuliwa. Kama tungeweza kutumia tu kile chombo, yaani ile Bodi ya Mazao Mchanganyiko

ambayo naamini kwa muundo wake ingeweza ikakopa ikanunua mazao ya wakulima na kuyaweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nchi nyingi hapa duniani zinalia njaa, haya mahindi yangeweza kuwasaidia hao wananchi wa nchi nyingine na hao wananchi wetu wangekuwa wamepata fedha ya kuweza kumudu mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi nyingine ni ya Kahawa. Hii Bodi inafanya kazi nzuri lakini haisaidii wakulima wa kahawa kwa maana ya masoko. Mbinga kule mwaka 2014 tulikuwa na tani kama 780 za wanaushirika, lakini Bodi ya Kahawa haikutusaidia sana kutafuta masoko mazuri zaidi ya ule mnanda wa kuuza ile kahawa.

Kwa hiyo, naomba kwa sababu namwamini Mtendaji Mkuu wa *TCB* wa sasa, ana uwezo huo, atusaidie katika huu ili kahawa hii isiuzwe tu Tanzania, iuzwe nchi za nje ambako tutapata fedha zaidi na hivyo kuinua pato la mkulima kule Mbinga, Mbozi kwa Naibu Waziri, Kigoma na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kwa Wizara hii, kule Mbinga tuna mto Mungaka, tuna Mto Ruhuhu, yote hii maji inapeleka kwenye Ziwa Nyasa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Matiko; Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda na Mheshimiwa Shibuda wajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijalia afya ingawa naumwa kidogo, lakini nitachangia japo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu na wananchi zaidi ya asilimia 75 maendeleo au uchumi wao upo kwenye kilimo.

Pia nataka kujua kwa sababu tunaenda kumalizia awamu ya nne, Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha aje aniambie uhalisia wa ile kauli mbiu ya Kilimo Kwanza na ni mafanikio gani tumeyapata. Kwa sababu nikakaa nikitafakari, nikiangalia kwa ukubwa wake, sioni dhana na mafanikio kwenye hii kauli mbiu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kuwa na kilimo chenye tija na tumekuwa tukiongea haya mara kwa mara na nitaendelea kuyaongea, Ukiangalia uhalisia wa mkulima, analima kilimo ni cha kizamani na siyo kilimo cha kisasa. Mpaka leo hii tunaongea, kuna Watanzania ambao wanaishi huko

vijiji wanatumia plau, hawatumiii matrekta ambayo wanasema. Kama matrekta yamegawiwa ni machache, labda ni kwa watu wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, huyu Mtanzania analima kwa shida sana, anapata hayo mazao, anaweza kuyafikisha vipi mjini? Barabara ni mbovu, miundombinu ya barabara ni mibovu. Anaweza kuyasindika vipi huko aliko vijijini wakati hakuna miundombinu ya umeme? Mtanzania huyu huyu anayelima kwa shida, hawezi akapata kipato kinachojionyesha, kwa sababu nimemsikia hata kaka yangu Mheshimiwa Kayombo aliyemaliza kuongea, anasema tuhakikishe hatuingizi bidhaa kutoka nje, tuwe na viwanda sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawezaje kuwa na viwanda wakati zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania hawana umeme; na hao watu ambao hawana umeme ndio wakilima? Ndiyo maana nikasema, hii kauli mbiu ya Kilimo Kwanza haina maana; yaani haijabeba uhalisia ya neno lenyewe. Neno ni zuri, lakini halitoi uhalisia wenyewe. Ili tuweze kufanikisha, tuweze kuwa na viwanda vinavyosindika, ni lazima tuwe na umeme, maji na miundombinu mizuri ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo huyu mkulima kwa mfano analima viazi kule Tarime, gunia linauzwa Sh. 10,000/= au Sh. 15,000/= kwa sababu barabara ni mbovu, magari hayaendi kuchukua yale mazao. Kwa hiyo, unakuta mkulima analima, anatumia fedha nyingi, mwisho wa siku, hapati kipato halisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, wamezungumza wengi sana kuhusu tumbaku; na bahati nzuri na Mkoa wa Mara tunalima tumbaku. Kuna baadhi ya Kata zinalima tumbaku katika Wilaya ya Tarime; Kata ya Susuni, Mwema, Legicheli, Pemba na Mbogi. Lakini wale hawauzi hata kwa dola mbili ambazo zimetajwa hapa; wanauza kati ya Sh. 800/= mpaka Sh. 1,500/= za Kitanzania ambazo ni chini ya dola moja. Sasa uangalie ni kwa kiasi gani inauzwa chini ya dola moja lakini tunaambiwa zinauzwa dola tatu; na huyu huyu Mtanzania anaambiwa achangie maabara kwa hicho hicho kipato anachokipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kule Tarime tunalima mahindi, chai, ndizi na kahawa lakini hatuna masoko. Kwa mfano, kwenye mahindi hatuna hata kiwanda ambacho kinaweza kikachakata na kutoa unga. Nakumbuka mwaka 2013 kulikuwa na sakata ya mahindi yamezuiwa kwenda Kenya, Mkuu wa Mkoa wa Mara akalazimisha Mahindi yaende Musoma maana ndiyo kuna Kiwanda. Usafirishaji uwe kwa wale watu walioko Tarime malori zaidi ya 30. Huu ni unyanyasaji wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuhusu iliyokuwa *Mara Corp.* ambayo iko pale Lebu. Wakulima wa kahawa wanauza kati ya Sh. 900/= mpaka Sh.

1,500/= lakini bei halisi ya kilo ni Sh. 5,000/= tena wanapelekewa pale pale Lebu, wanawauzia wale watu wanaitwa WAMAKU, nao wanamuuzia mtu anaitwa Amiri Hamza, kwa Sh. 5,000/=. Yaani wanachukua kwa mkulima kwa Sh. 800/= mpaka Sh. 1,500/= yaani hapo hapo *distance* ndogo, wao wanaenda wanauza kwa Sh. 5,000/=. Huu ni wizi na hii yote inatokea; nimetaja *Mara Cooperative Union* iliyochukuliwa na Mfilisi tangu mwaka 1994 mpaka mwaka 2000 watakuwa wamemaliza lile deni, wawarudishie. Mpaka leo wamekodisha, hawa watu wanateseka. Nataka Mheshimiwa Waziri aje atueleze na kwa sababu anatokea Mara, atakuwa analifahamu sana hili. Ni lini sasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzia)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ni zamu ya Mheshimiwa Dkt. Mponda na Mheshimiwa Shibuda ajiandae.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo. Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kuwa mwingi wa afya leo kusimama hapa mbele na kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana moja kwa moja na Taarifa ya Kamati ya Kilimo Mifugo na Maji kwamba bajeti hii ni finyu. Hii bajeti ni ndogo sana ndugu zangu. Wengi tunashuhudia kwamba Watanzania wengi karibu asilimia 75 wanajihusisha na kilimo. Sasa naiomba Serikali, kuna kipindi mtarejea, mtakaa na Kamati ya Bajeti. Kwa kweli hii bajeti haitoshelezi kabisa, tutaishia kila siku kusema sungura mdogo, matokeo yake wakulima wanaumia. Hawana ajira, hawana mishahara, sasa kama tusipowekeza bajeti ya kutosha kwenye kilimo, hatuwatendei haki wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pembejeo, nakubaliana na Serikali, wamegundua kwamba kuna changamoto kwa mfumo ambao wameanzisha mwaka 2014 na wamekuja wanarudi tena na mfumo wa vocha, lakini wanaelekeza zaidi vocha zile katika kilimo cha mpunga na mahindi, kwamba watawekeza asilimia 50 na asilimia nyingine inayobaki wakulima wenyewe watachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi tena kwa Serikali, hasa Wakulima wa Mpunga Mkoa wa Morogoro Wilaya ya Ulanga; Serikali hapa wanaelekeza kwamba watatoa pembejeo kwa mbolea na mbegu bora. Sisi watu wa Ulanga, changamoto ya mbolea siyo kubwa sana na ndiyo maana mnapotuletea mbolea, tunazirudisha kwa njia nyingine ya kinyemela au njia ya panya huko huko tena ambako watu wanahitaji mbolea. Wakulima hawanufaiki na mbolea kule Ulanga, tunachoomba Pembejeo hii itolewe kwa dawa za kuuwa magugu

na mbegu bora; ndiyo changamoto! Ndiyo matatizo ambayo wananchi wanayo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Mfuko wa Taifa wa Pembejeo. Ni kweli Serikali imekuwa na nia njema ya kuweza kusaidia wakulima hawa, lakini wale wakulima wadogo wadogo hasa wanaokaa vijijini hawana dhamana ya kupata mikopo kutoka kwenye mfuko huo. Maana dhamana inayozungumziwa, ni lazima uwe na hati *(title deed)* ya nyumba au shamba. Wakulima wengi hawana hivyo vitu.

Kwa hiyo, naomba masharti haya kama itawezekana na ninaomba iwe hivyo, iwezekane masharti yapunguzwe, basi wakulima hao kwa dhamana ya walichokuwanacho, wana mashamba na wengine wana hatimiliki za kimila, kwa nini dhamana hizi zisitumike kukopesha wakulima hawa ili waweze kuboresha kilimo chao kiwe na tija? Ndipo tutaweza kuwasaidia wakulima hawa kuliko tunaendelea na hizi *theories* au masharti haya ambayo kabisa wakulima hawa wanapata ugumu wa kupata hizo huduma za ruzuku ya kutumia mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro ni wakulima sana wa zao la mpunga hasa Wilaya ya Ulanga na Kilombero. Kwa miaka takriban kumi sasa tumetoa malalamiko ya ugonjwa ambao unashambulia zao la mpunga, wenyewe kule kienyeji wanaita *Kimyanga.*

*(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ya kwanza hiyo!

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa huu Serikali bado hawajatusaidia; hawajaja na jibu! Wanasema wanaendelea na utafiti, lakini tafiti zimeonyesha nchi nyingine kama walivyofanya Ethiopia Wachina, imeonyesha dawa zipo. Kwa hiyo, nawaelekeza Serikali, hebu watumie matokeo ya tafiti ya nchi nyingine watuletee ufumbuzi. Lakini la pili, suala la elimu kwa wananchi wafanye nini dhidi ya kinga ya huo ugonjwa wa mpunga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 ili kuongeza bei ya zao la mpunga, Serikali waliongeza hifadhi ya chakula ya Taifa ya zao la mpunga, lakini matokeo yake mpunga huo umenunuliwa maeneo machache tu ambapo tunajua Mkoa Morogoro ndiyo wanazalisha mpunga zaidi pamoja na Mkoa wa Mbeya. Sasa naiomba Serikali huu mfuko sasa hii hifadhi ya chakula ambayo wataendelea kununua mpunga, basi watukumbuke na sisi wakulima wa Ulanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni kilimo cha umwagiliaji. Kuna *scheme* inaendelea pale Idete imefikia asilimia 75 kumalizika lakini ina changamoto kwamba imetengenezwa ile mifereji mikubwa ya *cement* na mifereji ya kati, lakini mifereji midogo haina *cement*. Kwa hiyo, naomba warejee…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shibuda, jiandae Mheshimiwa Lulida.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata fursa hii nami nishauri machache katika Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia jambo lolote, naomba kutumia fursa hii nikiwa ni mlezi wa Chama cha Wakulima wa Pamba *TACOGA*, ambacho ni chama cha wakulima wadogo wadogo; nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Ndugu Wasira pamoja na Mheshimiwa *Eng.* Chiza kwa ushiriki wao mkubwa walioweza kuwa pamoja nasi katika kipindi cha msiba wa Mwenyekiti wetu kilichotufika tarehe 29 mwezi wa Nne.

Natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwani mlikuwa liwazo kubwa sana. Vilevile natoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge walioweza kushiriki; Mheshimiwa Andrew Chenge pamoja na Mheshimiwa John Cheyo.

Vilevile natoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioweza kushirikiana nasi katika kipindi hicho kigumu, ambao ni Mheshimiwa Abdallah wa *Alliance* pamoja na Meneja wake Ndugu Hogora pamoja na Mkurugenzi wa Kahama *Oil Mill* Ndugu Mhoja Ndegesera. Nawashukuru sana kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba ambalo Mheshimiwa Waziri ni mtoto aliyezaliwa pia katika zao la pamba, naomba kusema ya kwamba maendeleo ya zao la pamba yanategemea sana mazingira ya mvua. Uzalishaji wa pamba kutokuwa na uwezo wa kuendelea pale pembejeo zinapopatikana sambamba na mtawanyo wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamasisho la bei vilevile husaidia wakulima kujituma na kuongeza uzalishaji wa pamba pamoja na kutumia kanuni bora za kilimo. Wakulima sasa wanadai: Je, Ruzuku inayohitajika kwa ajili ya kuendeleza zao la pamba Serikali itatoa lini kwa mfano ule ule kama wanavyotoa kwenye mazao mengine? Zao la pamba limekuwa kwa kweli ni zao ambalo hata

Mheshimiwa Rais tulipoenda kupeleka kilio chetu alishangaa kwa nini zao la pamba halipati.

Sasa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa sababu na wewe ni Mbunge, ni mtoto na vilevile nakupongeza kwa kumaliza kifungo chako cha jela cha matumaini mema; kwa hiyo, naomba sasa ukiwa pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu, utuambie ni lini Serikali itatoa ruzuku kwa mserereko ule ule kama inaotoa kwenye mazao mengine kwenye zao la pamba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha mkataba. Wakulima wa pamba hawakatai kilimo cha mkataba, wanachodai ni kwamba kilimo cha mkataba kiwe na mkataba wa kutolewa pembejeo, lakini vivyo hivyo pawepo mkataba wa nguvu kazi inayozalisha katika upande wa kilimo cha pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Mheshimiwa Wasira unapomwambia mtu akalime shamba lako unamlipa pesa, lakini kwenye kilimo cha mkataba unampa mtu pembejeo nguvu kazi yake hutaki kumlipa. Naomba suala hili lieleweke kwamba kilimo cha mkataba hatukikatai, tunachodai ni thamani ya mkataba wa uzalishaji pamba. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itoe kauli elekezi hasa kuhusu suala la kilimo cha mkataba na kwa wale wasimamizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali naomba ituelekeze ni lini Mheshimiwa Waziri utahakikisha kwamba mfumo wa *Passbook* uliokuwa na takwimu za kupandisha kilimo cha pamba, mfumo wa *Passbook* ambao ulikuwa ndiyo kinga na kumbukumbu ya pesa anazokatazwa mkulima mdogo na mkubwa akajua kwamba pesa yake imemnunulia mbegu kiasi gani na viuadudu kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri, wakati ule ulikuwa Waziri wa Kilimo…

*(Hapa Kengele ya kwanza ililia kuashiria kwishakwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ya kwanza hiyo!

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Wakati ule ulikuwa Waziri wa Kilimo, ulikuwa Mjumbe wa Bodi ya Pamba. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, *Passbook* irejeshwe. Kwa kweli wakulima wanasikitika sana na hii ni agenda kubwa sana kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaomba *Passbook* ambayo ilidhihirisha kwamba ilikuwa ndiyo lindo la usalama kwa pesa za mkulima, hivi sasa mkulima hajui pesa zake zinazokatwa zinahifadhiwa katika mfumo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaomba kufahamu kwamba fedha za Halmashauri zinazodaiwa zilizokatwa kwa ajili ya kupandisha bei ya pamba, lini zitatolewa? Vilevile wakulima wanaomba pesa za utafiti kwenye zao la pamba zitolewe na Serikali ili mkulima bei yake ya pamba ipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wanashauri kwamba Serikali iwe inatoa ruzuku kwenye viwanda vya uchambuzi kuhusiana na masuala ya makato ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba utuondolee hodhi ya soko huria kwa sababu mkulima wa pamba pesa zake vilevile zinatumika katika kilimo cha mkataba. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atambue ya kwamba *Victoria Federation* iliwakomboa wakulima na mnyororo wa faida zilizotendeka wakati wa *Victoria Federation* wakati wa kudai uhuru wakulima walihakikishiwa kwamba manufaa yaliyokuwepo wakati wa *Victoria Federation* yataendelea. Nasikitika kusema kwamba hivi sasa hali sivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali sasa ituelekeze: Je, bado iko katika duru za ujamaa na kujitegemea?

*(Hapa Kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Shibuda. Sasa Waheshimiwa nina *control time* ya Kiti dakika 15 ambazo ni zangu. Nampa Mheshimiwa Lulida dakika tano, Mheshimiwa Lwanji tano; na Mheshimiwa Jafo, tano.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali yangu kwa kazi kubwa inayoifanya lakini vilevile nataka niishauri katika mazingira ambayo tukirekebisha haya mazingira tutaweza kufika katika mazingira makubwa na maendeleo makubwa katika kilimo. Tanzania ni nchi ya 11 duniani kwa kuwa na maeneo makubwa ya mito, maziwa na mabonde. Kwa maana moja, tuna uhakika wa kilimo kwa kiasi kikubwa, lakini uzalishaji wetu mpaka sasa hivi ni chini ya asilimia tano. Tusuridhike na hicho kusema tuna chakula cha kutosha wakati wanasema kuna mikoa mingine wana balaa la njaa. Tukizalisha vya kutosha, nchi itakuwa na maendeleo makubwa ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini masikitiko yangu ambayo nimezungumza karibu miaka kumi niliyokaa katika Bunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano, kuna maeneo makubwa yamechukuliwa na wajanja. Mashamba makubwa ya katani na chai, watu wanachukulia mikopo, Watanzania

wanapigana na kuchinjana kwa ajili ya kutafuta ardhi. Yale mashamba yanafanya kazi gani? Ni *Condemned area,* lakini yamechukuliwa na watu wanakwenda benki kuchukua mikopo, Mawaziri wapo, wanaingia na kutoka na wanayaona haya, hawayafanyii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Serikali ituambie, haya mashamba ni mapaka lini itakuwa ni kero kwa Watanzania ambao wanahangaika kutafuta ardhi, yakichukuliwa na wajanja kuchukulia mikopo benki? Hii ni dhuluma kwa Watanzania. Tuwe na uchungu na nchi yetu na tukomboe hii hali ya kuchukua ardhi kwa ajili ya mabenki. Nataka unipe orodha ya wajanja hawa wenye mashamba makubwa ambao wanachukua mikopo lakini Watanzania wanakosa ajira. Tanzania inashindwa kuzalisha chakula katika maeneo hayo badala yake wao wanachukua fedha na wanakwenda kufanya biashara kubwa, wanawaacha Watanzania wakiwa katika hali ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa ninapozungumza, Mkoa wa Lindi wanavuna ufuta, lakini ushirika haiko rafiki na wakulima. Leo unauzwa ufuta kwa Sh. 1,000/=, amefanya kazi kubwa, faida hakuna. Hii ni ujanja wa wachache wanaenda kuchukua ufuta kwa Sh.1,000/= lakini wanauza karibu dola nne. Huyu anafaidika na nini? Huu ni umaskini! Hatutaweza kumkomboa Mtanzania kama tutaendelea kumwacha auze ufuta, zao ambalo mafuta yake ni bora kwa Sh. 1,000/=. Tunaletewa mafuta kutoka nje ambayo ni mabovu, yanaleta kansa na Tanzania sasa hivi kansa imekuwa juu kwa kulishwa vitu vichafu wakati mafuta masafi yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na viwanda vya mafuta Ilulu, Nachingwea. Vile viwanda vimechukuliwa katika ubinafsishaji toka mwaka 1967. *Spare parts* zote zimeuzwa, vile viwanda havifanyi kazi, hakuna ajira kwa Mtanzania; matokeo yake unachukuliwa ufuta kwa Sh. 1,000/=. Tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho lilikuwa ni zao lililokuwa linailetea Tanzania *foreign currency* ya kwanza, lakini leo korosho ile imekaa inazagaa kwa wananchi. Viwanda vya korosho vya Nachingwe vimefungwa, tumekuta kama ni magereji tu wameweka vitu mbalimbali, hatujui mwisho wake; tukasema yale ni maeneo yanaweka pembe zetu. Kwa nini viwanda vile vimekaa, vimefungwa? Kunawekwa nini ndani ya vile viwanda? Naomba uchunguzi, tujue kunafanyika nini ndani ya viwanda vya korosho vya Nachingwea, Mtama na maeneo mengine katika Mkoa wa Lindi? Hii ni hasara!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaweka wananchi katika hali ngumu; wananchi masikini! Tunasikia kuna mfuko; mimi nasikia hapa leo kama kuna mfuko. Ule mfuko haujawatangazia wananchi; wanahitaji matrekta, pembejeo na mbolea, lakini bado tuko katika hali ngumu. Wizara imekuwa kama

imepigwa *stroke*. Maana yake, *Extension Officer* yuko chini ya TAMISEMI. Wizara inatengeneza fedha inaipeleka TAMISEMI. Wafanyakazi kule kilimo, fedha hazifanyi kazi, zinaliwa tu. Kwenye mabonde makubwa ambapo zinakwekwenda fedha ya umwagiliaji, zinaliwa tu, matokeo yake kinachozalishwa, hakionekani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa namwita Lwanji; na Mheshimiwa Jafo na ajiandae, halafu Serikali.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nami nafasi. Naunga mkono hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamelalamikia suala la masoko. Wizara hii ni hodari sana kuhimiza watu kulima, lakini watu wakishalima wakapata mazao wanatekelezwa. Sasa tusifanane na wale watu wanaobembeleza sana akina mama, wakishapata mimba, basi wanawatekeleza, wanawaacha solemba. Sasa hii siyo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na kitengo zamani kinaitwa *Marketing Development Bureau* katika Wizara hii. Kikaja kikafutwa, sasa kuna kitengo kinaitwa soko la mazao ya kilimo, hakisimamiwi ndani ya Wizara hii. Hiki kitengo kiko Wizara nyingine. Sasa nashindwa kuelewa, kwa sababu hatuuzi nguo hapa, hili suala la chakula ni *very sensitive,* lingekuwa katika Wizara inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kushauri, hili lichukuliwe, waliangalie walirekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo ajizi, hali ni mbaya sana katika mikoa ya kati. Mvua hazikunyesha na wakati ambako mvua zimekuja, muda umepita; suala la tabia nchi. Sasa hivi sijui Serikali imejipanga vipi kupeleka chakula katika maeneo husika! Sasa hivi tunaambiwa watu ndiyo wananza kufanya tathimini, sijui wapeleke takwimu, wafanye hivi. Suala sasa hivi ni la kupeleka chakula katika maeneo yanayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida na Dodoma hali ni mbaya sana. Naomba watueleze, wana mipango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ije basi na uataratibu wa kutunga sheria, maana hizi sheria ndogo ndogo za kuhimiza mazao yanayostahimili ukame, watu hawa hawafuati. Watu wanalima mazao ambayo hayafanani kabisa na mazingira yao. Sasa nafikiri tungefanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida unafahamika sana na ni hodari katika kulima mazao hayo yanayostahimili, kama mtama na uwele. Lakini cha ajabu mwaka huu, mazao yameishia shambani tena hayo, uwele na mtama wote umeliwa na ndege waharibifu, kweleakwelea. Tumepiga kelele sana kuhusu ndege, sijui tuseme ni *aeroplane* au nini, inayonyunyiza dawa ya wale ndege. Tunaambiwa ndege hii hakuna, iko Ethiopia, sijui iko wapi; nchi sijui saba zinatumia ndege moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli miaka yote tumepiga kelele hapa, miaka 10 sasa tunaomba Serikali ije na ndege yake; iwe na ndege inayopita kunyunyiza *then* ina-*complement* hata sera hiyo tunayosema kwamba watu wasikate tama. Mwaka huu hakuna uwele, hakuna mtama, yote imeangamizwa mashambani. Kwa hiyo, watueleze wana utaratibu gani wa kuweza kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Singida tunalima tumbaku, hasa katika Jimbo langu, lakini zao hili ni mtoto yatima. Mkoa hauna *interest* kabisa hata kufuatilia juu ya zao hili. Zao hili wanapokwenda kulalamika na nini, mpaka waende Tabora. Naomba Wizara hii iweze kuwaelekeza hao watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii benki ya wakulima iliyozungumzwa na Mbunge wa Solwa, ije na utaratibu wa kukubali hati za kimila, maana mabenki mengine yanakataa. Tungeshukuru sana kama wangeweza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kuomba kwamba elimu itolewe ya kutosha katika *management* ya hivi vyama vya msingi. Kweli hivi Vyama vya Msingi kila vikiibuka vinakufa. Vimerushwa na mambo mengine! Kwa hiyo, naomba Wizara ijaribu kukazia itusaidie kutoa elimu ya kutosha ili hawa watu waweze kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini namshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende katika mada. Jambo la kwanza, tukijadili Wizara ya Kilimo, Chakula la Ushirika, maana yake tunajadili uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwamini sana Mheshimiwa Wasira na Wizara yake, lakini na wataalam wote waliokuwa katika Wizara hii, wanafanya kazi

katika wakati mgumu, lakini wanafanya kazi kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nataka nijielekeze katika suala zima la kibajeti. Mimi sijapendezwa sana, leo hii tunapozungumza, tuko ndani ya mwezi wa tano, bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo, Chakula la Ushirika, iko chini ya asilimia 46, lakini *OC* iko chini ya asilimia 26. Ina maana *performance* ya Wizara ambayo tunatarajia ibadilishe uchumi wa nchi, hatujaiwezesha ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijafurahia katika hili, kama Tanzania tunataka tujielekeze katika nchi yenye uchumi wa kipato cha kati, leo hii bajeti ambayo tunaona kwamba tunazungumza Wizara ambayo ni nyeti katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, upelekaji wake wa fedha umekuwa ni wa kusuasua, napata mashaka katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuomba leo nikamate Shilingi ili nipate maelezo ya kutosha. Kwa sababu simwoni Waziri wa Fedha yeyote hapa. Lengo langu ni kwamba tunapozungumzia masuala nyeti ya nchi, lazima kama kuna *commitment* ya kifedha tuweze kumpata mtu, kwa nini Hazina haijatoa fedha katika Wizara ambayo tunapekeka uchumi wa nchi yetu mbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni suala zima la umwagiliaji. Napenda sana kuwashukuru wataalam wa Wizara na Wizara kwa ujumla kwamba mwaka 2014 tulitenga Shilingi bilioni nane kwa ajili ya umwagiliaji, mwaka huu tumetenga Shilingi bilioni 19. Mtazamo wangu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kufanya mchakato mkubwa kubadilisha kilimo chetu cha sasa, lakini katika hilo naomba tujielekeze vizuri. Kuna Mikoa mingine kila mwaka lazima ipelekewe chakula cha njaa. Sasa ikiwezekana katika maeneo hayo, badala ya kupeleka chakula cha njaa, twende kuweka mifumo mikubwa ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo tutaondoa gharama kubwa sana za kupeleka chakula cha njaa kila mwaka katika yale maeneo ambayo ya tatizo la mvua kila mwaka. Vile vile naomba niwaambie, pale Kisarawe sisi kuna eneo moja la Mafizi na Malui kule, linafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji. Naomba watalamu wa Wizara, mje Kisarawe mtembelee maeneo hayo, ni muhimu sana. Vile vile wataalam wetu mtusaidie, ukitoka Mkuranga mpaka Mtwara, hili bonde linafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji, kwa nini watalam hatuwekezi katika kilimo kikubwa cha umwagiliaji kubadilisha uchumi wa nchi yetu? *(Makofi)*

Ndugu zangu, tukilima kilimo cha chakula peke yake, inawezekana nchi yetu katika Afrika nzima tukaweza kusambaza chakula. Mnaona sehemu nyingi watu wanakuwa na shida sana ya chakula. Watani wangu hapa wasukuma wanalalamika kuhusu pamba yao; wakati kumbe sasa hivi dunia inatafuta chakula. Kumbe hata hao Wasukuma tungewapelekea mfumo mzuri, wangeweza hata kulima kilimo cha mahindi, wangeweza kupata manufaa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka nizungumze suala zima la *Training Institution*. Taasisi zetu zinafundisha vijana, lakini taasisi hizo ukiondoka huko utakuta wataalam wamechoka! Halikadhalika utakuta mitambo yao ambayo vile vijana wanaitumia, imechoka! Naomba tuiangalie! Ukienda pale Ilonga na sehemu mbalimbali, utakusa mitambo imechoka pale.

Naomba Wizara ijielekeze huko, jinsi gani wataweza kusaidia, *OC* zao zipatikane maana ni changamoto kubwa sana. Naomba tujielekeze huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna vijana ambao wamefundishwa hivi; vijana hawa wamefundishwa katika hivyo vyuo, sasa hivi wana mwaka wa pili, mwaka wa tatu wengine hawajapata ajira. Kwa nini Serikali haiwezi ikafanya programu maalumu, kama ile tuliyofanya katika elimu na katika afya; vijana wale wakitoka vyuoni moja kwa moja wapelekwe katika sehemu ambazo zitasaidia suala zima la agenda ya ugani iweze kuwafikia wananchi, kuliko vijana wanamaliza miaka miwili, mitatu wako Mtaani, hawajui hata *future* yao inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwisho nimalizie *GMO*. Leo hii ukienda Afrika Kusini, *Mauritius* na nchi yoyote, watu wanakula machungwa na vitu vya aina mbalimbali, vyakula vilivyozalishwa kwa *GMO*.

Leo hii ndugu zangu kule Wasukuma wanazalisha pamba kwa kutumia mbegu za kizamani; tulienda Burkina Faso tuliona maajabu makubwa sana; jinsi gani wakulima wa Burkina Faso wanazalisha pamba kwa kiwango kikubwa sana kwa kutumia *BT Cotton*. Lakini sisi Watanzania tumelogwa nini? Leo hii tunakula vyakula hata katika *supermarket* vimetoka kwa watu wenzetu ambao wananchi wao wanakwenda kwa uchumi wa mbali sana, sisi tumeshikilia agenda ambayo mwananchi wa Tanzania anakwenda kulalamika siku zote! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalamu wanafanya kazi kubwa sana, lakini sisi wanasiasa wakati mwingine hata tunafifisha kazi za watalamu wanavyofanya. Naomba sana Serikali iweze kuangalia jinsi gani tutafanya. Kama kuna mazao mengine ya kuweza kujielekeza kwa kutumia *GMO*, tuweze kufanya hivyo kwa ajili ya kubadilsiha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sisi Tanzania tunashangaa, wenzetu wanakwenda mbali katika matumizi ya *GMO* na hali ya uchumi wao inaweza kubadilika. Inawezekana tukajielekeza, kuna baadhi ya mazao tukaanza nayo hasa pamba na mazao mengine ya biashara. Nina imani tutafanya mabadiliko makubwa sana. Leo hii koti zetu na nguo zetu tulizovaa, zote... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye rehema na muweza wa mambo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuzungumzia suala zima la uingizaji wa sukari kutoka viwanda vya nje ya nchi. Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwamba Serikali imekuwa ikitoa vibali vya kuagiza sukari kutoka nje kinyume na utaratibu jambo ambalo limekuwa likizua mzozo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kwamba sukari hii inayoingizwa nchini huwa inaingizwa kinyemela, hailipiwi kodi stahiki na kupelekwa kuuzwa kwa bei ya chini na kuwa kikwazo kikubwa kwa sukari inayozalishwa kwenye viwanda vya ndani. Athari yake ni viwanda vyetu vya ndani kukosa nguvu za uzalishaji kwa mrundikano wa sukari inayokosa mauzo kutokana na kuingiliwa na sukari ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumeshuhudia mahojiano kati ya waandishi na Mkurugenzi wa Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa naye akithibitisha utoaji wa vibali upo na umekiathiri kiwanda chake kiasi kwamba wanashindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi na kununua miwa ya wakulima wadogo wadogo jambo ambalo limepelekea hata baadhi ya wakulima kubadili kilimo na kulima mazao mengine badala ya miwa.

Kama hivyo ndivyo, naishauri Serikali kudhibiti utoaji vibali vya ununuzi wa sukari ili kuwalinda wakulima wetu na viwanda vyetu ili pia kuwanusuru wafanyakazi wa viwandani ili wasije kupunguzwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mazao ya wakulima wetu yaweze kuwa na thamani, suala la masoko ni lazima. Hivyo ushauri wangu kwa Serikali ijali juhudi za wakulima kwa kuwatafutia masoko ya ndani na nje ya nchi. Serikali iwe na dhamana ya jambo hili na ihakikishe masoko kwa wakulima wadogowadogo siyo tatizo. Kwa kufanya hivi tutawapa moyo wakulima na kupata thamani ya mazao yao na kutimiza malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba ikiwa Serikali itayashughulikia masuala haya itawasaidia sana wakulima wetu.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuongelea ruzuku za pembejeo za kilimo. Utaratibu utaorejewa wa vocha kwa kilimo cha mpunga na mahindi, naomba suala la mbolea liangaliwe upya kwa wakulima wa mpunga Ulanga na Kilombero kwani mahitaji makubwa ya wakulima hawa ni mbegu, dawa za kuua magugu na siyo mbolea ambayo haitumiki kwa wakulima hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, naomba Serikali iangalie masharti ya mikopo kwa wakulima hasa kuhusiana na dhamana kwa kuwa wengi hawana hati za kimiliki nyumba au mashamba. Hivyo dhamana hata za *offer* za viwanja au hati miliki za kimila zikubaliwe kama dhamana katika kuomba mkopo katika mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ugonjwa unaoshambulia mazao ya mpunga ujulikanao kama '*rice yellow mottle virus*' umekuwa ukiongezeka kila mwaka na kuathiri sana kilimo cha mpunga. Naomba Serikali ije na mikakati ya kukabiliana na ugonjwa huu ambao unazidi kusambaa katika Mkoa wote wa Morogoro. Elimu zaidi pia itolewe kwa wakulima katika kujikinga na kutibu ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, skimu ya umwagiliaji ya Itete (Morogoro-Ulanga), mifereji ya pembezoni haijajengwa kwa simenti hivyo mradi huo hautadumu. Mifereji mikuu (*primary canals*) tu ndiyo imejengwa kwa simenti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, katika bajeti ya 2014/2015, Wizara ilikuwa inaendelea na upembuzi yakinifu katika mradi wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Lupiro - Ulanga, lakini katika bajeti hii Wizara imekuwa kimya. Je, mradi huu wa skimu ya Lupiro - Ulanga umesitishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, elimu itolewe kwa walengwa wakulima wadogowadogo kwa mradi wa *SAGCOT* katika Wilaya ya Ulanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mengi mazuri katika Hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Bajeti ya 2015/2016, nashindwa kuelewa ni vipi Wizara imeacha kabisa kutambua

mchango wa sekta ya kilimo katika maeneo yafuatayo katika Wilaya ya Muheza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa zao la matunda – machungwa. Wilaya ya Muheza inaongoza kwa kilimo cha machungwa ambapo husafirishwa pia nchi za nje hasa Kenya na katika masoko makuu Mikoani hasa Dar-es-Salaam, Tanga, Arusha na hapa Dodoma. Zao hili, halikutajwa kabisa katika hotuba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ya Wizara yangelenga mipango ifuatayo kwa zao hilo la matunda:-

(a) Kuboresha mpango wa uzalishaji wa mbegu bora za michungwa ambapo Wilaya ya Muheza imefanya jitihada hizo.

(b) Kujenga mwelekeo na ushauri wa kujenga kiwanda cha usindikaji wa matunda ili kupunguza usafirishaji wa machungwa nje ya nchi. Muheza ilianzisha kiwanda kidogo japo sasa hakifanyi kazi. Tumeiomba Wizara ya Viwanda na Biashara kusaidia kufufua kiwanda hicho kupitia *SIDO;* Wizara ya Kilimo isaidie ufuatiliaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umwagiliaji Misozwe – Muheza. Mradi huu upo na bwawa limejengwa kwa gharama kubwa wastani wa shilingi bilioni moja. Lina maji mengi sana na aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Injinia Chiza, alitembelea eneo hilo. Kazi iliyokuwa inaendelea ni ujenzi wa mifereji mikuu miwili ya umwagiliaji; mfereji wa Mlinga na Kwemingoji. Mfereji mmoja umekamilika na wa pili umekwama kwa kukosekana fedha kwa Mhandisi kuukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi una wanachama wastani 120 waliojiandikisha katika chama maalum. Mwezi Machi 2015, nilitoa taarifa ya hali ya mradi huo kwa barua maalum kwa Waziri wa Wizara hii na Mheshimiwa Naibu Waziri aliahidi kwenda kutembelea mradi huo lakini hakupata nafasi. Pamoja na taarifa hiyo kamilifu, inashangaza kuona hakuna mpango wowote katika Hotuba ya Bajeti 2015/2016 ya:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa mifereji hiyo ya umwagiliaji.

(b) Kuandaa mchoro wa skimu ya umwagiliaji ili wanachama hao wa mradi wa umwagiliaji Misozwe watambue maeneo yao waweze kuanza kulima mpunga bila kuingiliana.

(c) Kuandaa utaratibu rasmi wa uzinduzi wa mradi huo 2015/2016.

(d) Kutoa elimu kwa kikundi hicho cha umwagiliaji kuhusu soko la mpunga na miradi ya kukoboa mpunga huo karibu na maeneo yao ya uzalishaji (Misozwe) ambapo umeme upo tangu 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kupitia Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Kaskazini kutoa maelezo fasaha ya uendelezaji wa mradi huo wa umwagiliaji Misozwe, Muheza na kuongeza mpango wa utekelezaji katika bajeti hii ya 2015/2016.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wassira, Naibu Waziri, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi walioshika kurugenzi mbalimbali ndani ya Wizara hii akiwemo ndugu Walua anayefanya kazi kwa mazingira magumu kwa kutengewa fedha kidogo na kusababisha madeni mengi kwa wakulima waliouza mazao na hata wale wanaosafirisha. Mwisho niwapongeze Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wakulima. Napenda kuiomba Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kumaliza madeni yanayomkabili Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa, Ndugu Walua. Tatizo hili limempa wakati mgumu Mtendaji huyu na kumfanya kushindwa kufanya kazi zake vema. Nasubiri maelezo ya Serikali ili wakulima wasikie hata wale waliopewa tenda za kusafirisha mazao kupeleka kwenye maghala ya Serikali, ni lini madeni yao yatalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji. Napenda kuisihi Serikali yangu kuongeza fedha kwenye skimu za umwagiliaji kwani skimu nyingi hazijakamilika kwani hazina mabwawa ya kuhifadhi maji, ili maji hayo yafanye kazi ya kilimo cha kiangazi na kukarabati mifereji inapobomoka. Ninao mfano hai wa skimu za Wilaya ya Manyoni hazina bwawa la kutunza maji ya mvua wakati wa masika, matokeo yake yanapotea bure. Naomba Waziri atueleze Wanamanyoni kama tumetengewa fedha kujenga mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabonde yote kuwa skimu za umwagiliaji. Bado Serikali haijatumia kilimo cha umwagiliaji kuwa ni njia ambayo inaweza kuinua kipato cha Watanzania na Taifa kwa ujumla. Kuna maeneo mengi sana yanayofaa kujenga skimu za umwagiliaji lakini bado yapo tu ingawa Serikali ilikwishaainisha mabonde hayo yakiwemo ya Mkoa wa Singida. Nasubiri Kauli ya Serikali ni mabonde yapi Singida yametengewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya pembejeo kwa wakulima. Naipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya kurudisha utaratibu wake wa awali

wa kutoa 50% ya gharama na wakulima wanalipa 50% kwa mbolea na mbegu. Nachosisitiza hapa ni umakini wa Watendaji katika utekelezaji ili pembejeo hizi ziwe zinafika kwa wakati kupitia utoaji wa vocha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali iangalie namna bora ya kuwakopesha trekta wakulima kwa kudhaminiwa na Halmashauri zao, kwani ndiyo wanaowafahamu kwa karibu zaidi. Wakulima wakipata matrekta kilimo kitakua na uchumi wao na wa Taifa utaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha vyama vya ushirika. Bado kuna tatizo kubwa la ununuaji wa mazao kupitia vyama vya ushirika kwa sababu, vyama hivi havina fedha na vingi havikopesheki. Hivyo, naomba vyama hivyo viandaliwe vizuri na Serikali ividhamini vyama hivi ili mabenki yakubali kuvikopesha. Naomba maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali ipige marufuku walanguzi wa mazao kwenda kulangua mashambani bali waende kwenye magulio ili washindane kwa bei iliyo kwenye soko, wakulima wasiendelee kupunjwa. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwisho. Napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja nikiwa na matarajio ya kujibiwa wakati Waziri na Naibu Waziri watakapokuwa wanajibu hoja za Wabunge, hususan madeni ya wakulima ya shilingi bilioni 12.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya. Mheshimiwa Rais alipotembelea Jimbo la Mpwapwa siku za nyuma, aliagiza Wizara ya Kilimo kupitia kwa Katibu Mkuu (Mama Sophia Kaduma) kwamba ahakikishe kinga maji linajengwa kati ya vilima viwili viitavyo Nughuli na Mkurungo vilivyopo katika Kata ya Chunyu.

Kwa kuzingatia kuwa utafiti wa kazi hii ulishafanyika, kinga maji hili litaleta nafuu kupata maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya mpunga ya Msagali. Je, utekelezaji wa agizo na kazi hii umefikia wapi? Wananchi wa Jimbo la Mpwapwa hususan Kata ya Chunyu wangependa kusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaleta maombi yangu kupitia Katibu Mkuu (Mama Kaduma) na kupatiwa wakala au duka la pembejeo za kilimo katika maeneo ya Inzomvu na Matomondo. (Jimboni Mpwapwa). Je, ni lini Wizara itawezesha upatikanaji wa pembejeo za kilimo katika maeneo haya ya Inzomvu na Matomondo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kupeleka chakula cha njaa katika Jimbo la Mpwapwa ufanywe kwa haraka kwa sababu mwaka huu hali ya mvua haikuwa nzuri, tathmini ya hali ya njaa imeshafanyika na taarifa iko Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaunga mkono hoja hii kwa 100%.

Pili, Kilimo cha Umwagiliaji Jimboni Igalula: Mabwawa na Mifereji iimarishwe ili usalama wa chakula katika jimbo na ngazi ya kaya uimarishwe,

(a) Goweko Mlimani bwawa lijengwe, tangu 2010 *Environmental Impact Assessment (EIA)* tayari imekamilika.

(b) Bwawa la Nsololo limejengwa hakuna mifereji ya umwagiliaji, samaki *(fingerings)* hamna, ambacho ni chanzo cha protein na pato kijijini. Bwawa linanywesha mifugo tu. Mahindi, choroko na mpunga yanastawi katika eneo hili

(c) Bwawa la Lutende na mifereji iimarishwe, mbegu zisizoota zinauzwa huko kama mbegu bora. Msambazaji atafutwe kuwalipa fidia wakulima.

(d) Bwawa *(Diversion)* la Loya katika Mto Ngwali linahitaji Wizara ya Ujenzi washirikiane na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili daraja lijengwe na mazao na bidhaa ziende katika Wilaya mbili za Uyui (Igalula) na Igunga. Mifereji iimarishwe ili umwagiliaji ufanyike kwenye mashamba ya mpunga na mahindi ili mazao yapatikane kwa wingi na kukuza pato.

Tatu, viwanda vya kuongeza thamani ya mazao katika Mkoa wa Tabora:-

(a) Kiwanda cha kusindika tumbaku na kuwa sigara na bidhaa nyingine za Tumbaku kijengwe Tabora ili kuongeza ajira, *cess* na pato la mkoa.

(b) Kiwanda cha usindikaji matunda; embe, matikiti maji, machungwa, nyanya, ndizi. Kama tutalima kisasa kwa kutumia mbegu bora kutoka *SUA* na sehemu nyingine za utafiti.

(c) Viwanda vya kusindika alizeti ili kupata mafuta kwa kusambaza mbegu bora na kuleta wabia kutoka China na kwingineko. Pia kugawa mashine ndogo ndogo za kukamua mafuta na kuongeza thamani na kuuzia kiwanda mama mafuta ghafi ya kula kwa kuyachuja. Mashudu ni chakula cha kuku na mabwawa ya kufugia samaki.

(d) Mahindi na mpunga, viwanda vikoboe na kusaga na pia kupaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni Zao la Tumbaku katika Mikoa ya Tabora, Ruvuma, Katavi na Mara.

(a) Mbona kesi za wezi wa Vyama vya Msingi katika Mkoa wa Tabora hazijaamuliwa tangu Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete atoe agizo kwamba, watuhumiwa hao wakamatwe na kufikishwa Mahakamani? Kigugumizi kwa Polisi na Mahakama ni cha nini?

Tabora *Auditors*, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na *CAG* walibaini wizi wa shilingi bilioni 28. Wakulima wa Vyama vya Msingi walitapeliwa pembejeo isiyo na ruzuku wamebambikizwa na madeni ya mbolea ambayo hawakupokea. Benki ya *CRDB* na *NMB* zimelipa mbolea na madawa hewa kutoka *WETCO*. Kuna *syndication* (mtandao) wa wizi, vyombo husika vitoe hukumu na wakulima walipwe.

(b) *Classifiers* wanawakwamisha wakulima kwa kuwapa *grade* ya chini, kama hawatoi ushirikiano Wizara ichunguzeni.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni chombo muhimu ambacho kinaweza kupunguza sana umaskini endapo Serikali itaweza kuweka kipaumbele katika mambo yafuatayo:-

Dhana ya kilimo; mikopo nafuu kwa wakulima wadogo; elimu bora ya kilimo (utaalam); vijana; wakulima kupata elimu ya ufundi stadi katika zana za kilimo; ardhi ya kutosha; masoko ya mazao na bei za kumudu gharama za uzalishaji; elimu ya ubora wa mazao; na maghala ya kutosheleza kuhifadhi mazao hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipandisha kiwango cha hifadhi ya chakula ili kununua tani nyingi zinazoweza kumudu kulisha Watanzania miaka miwili au zaidi endapo mvua hazitanyesha. Tutumie neema ya mvua inayokuwepo kuliko kuwa na matumaini ya mvua za mbele ambazo hatuna uhakika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa kutilia mkazo Miradi ya Umwagiliaji iliyokwishaianzisha, kwani imegharimu fedha nyingi sana lakini bado haijamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu kwa Mradi mkubwa wa Umwagiliaji wa Sakalilo ambao umetumia fedha nyingi lakini haujamalizika.

Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imeomba maombi maalum ya shilingi 30,000,000 ili kumaliza sehemu iliyoharibiwa na mafuriko ya mvua. Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaongezewa umaskini na Serikali kwa kuwakopa mazao yao na kuchelewa kuwalipa. Naomba Serikali itoe tamko ni lini itamaliza kulipa wakulima ambao bado wanaidai Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uingizaji wa chakula nchini kiholela bila kujua kiasi cha chakula kilichopo husababisha wananchi kukosa soko la mazao yao.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa Hotuba nzuri na Mipango mizuri, tatizo ninaloliona ni utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja ili warekebishe kasoro mbili ambazo miaka yote nikichangia Wizara hii huwa naeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka Wizara hii imekuwa ikiajiri Mabwana Shamba ambao wamepewa jukumu la kupeleka huduma za ugani kwa wananchi.

Pili, ningeshauri Serikali ijipange vizuri katika ununuzi uende kwa wakulima wenyewe badala ya kutumia mawakala. Kutumia mawakala kunawavunja wakulima kupata bei vizuri inayolipwa na serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, itoe ushauri kwa wakulima kuanza kulima mazao mengine ya biashara. Hivi sasa karibu mikoa kumi inalima Zao la Mahindi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na kutokuwepo mifumo ya uhakika wa mvua nchini na kuathiri sana kilimo kwa ujumla wake; hivyo, njia pekee ya kuendeleza ustawi wetu kama Taifa ni muhimu sana wataalamu wetu kuangalia njia bora ya kuhifadhi maji ya mvua kwa kujenga mabwawa na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Hata hivyo, inasikitisha sana, licha ya kushauri mara kwa mara juu ya kuendeleza Miradi michache kwa ukamilifu badala ya kuwa na orodha ndefu ya Miradi ambayo haikamiliki kutokana na mtiririko wa fedha na uwezo wa Taifa kuhimili kuendeleleza Miradi hiyo ya Maendeleo. Hivyo basi, ni bora Miradi ambayo inaweza kuchangia ongezeko la uzalishaji ikiwemo Mkoa wa Katavi, Mradi wa Kakese na Mwamkulu katika Jimbo langu kutokamilika. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuimarisha vituo vya utafiti kwa ujumla wake na kupewa fedha za kutosha ni dhahiri kabisa Serikali haioni umuhimu wa kuondoka tulipo kwa kuwekeza katika utafiti hivyo kulifanya Taifa hili kuwa tegemezi kwa uzalishaji wa mbegu na kuacha kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SAGCOT*, pamoja na nia njema na maelezo mazuri ya matumaini kwa wakulima wadogo kuingia katika kilimo cha biashara, Mpango huu ni wa muda mrefu sana na kuonekana katika nyaraka mbalimbali, lakini haujawasaidia wakulima wadogo katika maeneo yaliyokusudiwa.

Mpango huu ni mahususi kwa wawekezaji, wakulima wakubwa, kupata mikopo ya ndani badala ya fedha hizo kuwabadilisha wakulima wetu na kuwa wakulima na kibiashara wa kati na wakubwa. Hivyo basi, Mpango huu uwe shirikishi ili wanaotaka kuwekeza katika kilimo na kurahisisha upatikanaji wa fedha kupitia *SAGCOT* kwa wakulima wadogo, waweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningependa kujua kama sasa Wilaya ya Mpanda inaweza kulima pamba baada ya kuzuiliwa takribani miaka 45 iliyopita kutokana na athari ya funza wekundu. Je, bado hali ipo vile vile maana Mpanda zao la biashara ni tumbaku pekee? Kama pamba haitawezekana ni mazao yapi ya kibiashara yanaweza kustawi na kuendelezwa ili kuboresha maisha ya wananchi baada ya kutegemea zao moja tu la tumbaku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii katika suala zima la miundombinu yenye kuleta kilimo chenye tija. Kaulimbiu ya KILIMO KWANZA ni dhahiri inabaki kuwa nadharia tu bila matendo wala mafanikio ambayo ni halisia kwa Watanzania wengi, ambapo kwa zaidi ya 70% wanategemea kilimo katika kuendesha shughuli zao. Kwa masikitiko makubwa, kilimo chao kimeendelea kuwa cha kutumia teknolojia ya kizamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na kilimo chenye tija kwa wakulima ilhali Karne ya 21 wakulima wanalima kwa jembe la mkono au plau. Karne hii wakulima wanategemea misimu ya mvua ambazo hazitabiriki. Leo hii Karne ya 21 tunaendelea kushuhudia viwanda vingi vikitelekezwa au kubinafsishwa. Bado viwanda vyenye kusindika mazao ya kilimo hamna kabisa na kama vipo ni vya kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na kilimo cha kisasa lazima tufanye *modernisation agriculture*. Ili *supply chain value* iweze kuwa *realistic,* lazima tuboreshe miundombinu ya barabara, umeme, ili tuweze kuchakata na kusindika mazao yatokanayo na kilimo. Lazima tufanye kilimo cha umwagiliaji, lazima tutafute masoko ya mazao yetu ndani na nje ya nchi. Lazima tuwe na

viwanda vingi vya ndani kuliko ilivyo sasa hivi ambapo mazao mengi husafirishwa kwenda nchi jirani, halafu wanaleta bidhaa zitokanazo na mazao ambayo tumelima sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwa mfano, Wilaya ya Tarime ni Wilaya yenye udongo unaokubali mazao mbalimbali kama tumbaku, kahawa, chai, viazi, mahindi, mihogo, ulezi, mtama, kahawa, ndizi na kadhalika, lakini haya mazao yote hayatoi tija kwa mkulima. Hii leo Tarime tumbaku inauzwa kilo moja kwa 300/= hadi 500/=; hii haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo ilihamasisha Wananchi wa Tarime kuleta mimea mingine na kupanda chai, ila hadi leo hawajawaona wale waliowahamasisha wapande chai, kuja kuwaonesha ni wapi wachakate na kusindika chai yao.

Vilevile mashirika ya kahawa hasa Mumba Tarime yameingiliwa na ukiritimba na hata *Mara Coffee* sasa imebaki bila tija. Kahawa sasa inakatwa ili wapande mazao mengine! Suala hili lazima lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo viazi vinatolewa Tarime na kupelekwa Kenya kwa sababu Tanzania hamna masoko kwa maana ya viwanda vya kuweza ku-*process* mazao haya na kutoa bidhaa kwa mfano *biscuits* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ili tuwe na tija kwenye kilimo na uchumi wetu kukua, lazima tuwekeze kwenye kilimo kwa vitendo na si maneno ya kwenye vitabu tu. Tuwe na *modernization agriculture* kwa maana zana za kisasa za kulimia, kuvunia, kuchakata, viwanda vya kusindikia na kadhalika. Tuwe na miundombinu ya umeme hasa vijijini, ili tuweze kusindika mazao yetu. Miundombinu ya barabara iwe imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni miezi kumi na moja baadhi ya Wakulima wa Mkoa Rukwa na pia hata Halmashauri zetu, hazijalipwa ushuru wake. Wanaahidiwa tu eti deni limesalia bilioni kumi na saba. Nataka kujua tarehe ya mwisho ya kulipwa wakulima waliosalia pamoja na tarehe ya mwisho wa ushuru.

Baadhi ya mawakala wa mbolea na *transporters* wanaodai hifadhi ya Taifa na pembejeo, mawakala hawajalipwa. Je, msimu ujao nani atafanya kazi hiyo wakati hawajalipwa pesa zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Umwagiliaji ya Lwati ipo na hata Naibu Waziri Mheshimiwa Zambi alifika na aliahidi kusaidia fedha ili kumalizia skimu hiyo isaidie wakulima zaidi ya elfu tatu wa kilimo cha mpunga na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Waziri kuhusu Skimu hiyo ya Lwati.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri kwa kuja na mpango mzuri wa bajeti ya mwaka 2015/2016 na utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2014/2015. Nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2015/2016

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati asimilia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo, bado wakulima hawana masoko ya uhakika kwa mazao yao ya biashara na hata ya chakula. inashangaza kuona Kitengo cha Soko la Mazao ya Kilimo kinasimamiwa na Wizara nyingine ya Viwanda na Biashara. Nashauri kitengo hiki kiwe chini ya Wizara ya Kilimo kama ambavyo zamani kitengo cha *Marketing Development Bureau (MDB)* kilivyokuwa chini ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, Mikoa ya Kanda ya Kati ihimizwe kulima mazao yanayostahimili ukame (walazimishe) ikibidi Serikali itunge sheria itakayowabana wakulima wa maeneo haya kulima mazao hayo.

Aidha, Serikali inunue ndege yake ya kunyunyiza, kukabiliana tatiza la ndege waharibifu kweleakwelea. Wakulima wanakata tamaa wanapolima na mazao yanavyostahimili ukame yanaishia kumalizwa shambani na kweleakwelea. Mwaka huu Mkoa wa Singida hususan Wilaya ya Manyoni imeathirika sana na tatizo hili na wakulima wamekata tamaa na wanakabiliwa na njaa kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali mbaya ya hewa na tatizo la kweleakwelea, hakuna chakula Mkoa wa Singida na Dodoma. Serikali ijiandae kupeleka chakula cha kutosha maeneo yanayokabiliwa na njaa muda huu na siyo kusubiri. Nashauri utaratibu wa kupeleka chakula kutoka maghala ya chakula *(NFRA)* urahisishwe ili kuondoa urasimu watu wapate chakula mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida ni yatima. Mkoa haushughulikii sana matatizo ya zao hili. Naishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ishughulikie matatizo ya zao hili. Nashauri Serikali kupitia Wizara ya kilimo, ishuhulikie matatizo ya zao hili kuhusu bei na Menejimenti ya Vyama vya Msingi na wizi wa fedha na pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba elimu ya kutosha ya jinsi ya ku-*manage* na kusimamia Vyama vya Msingi itolewe kusaidia uendeshaji wa hivi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Benki ya Kilimo ikubali hati za kimila. Nawasilisha.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukame uliotokea katika mikoa mbalimbali unapelekea mazao mengi kuharibika na kukauka kabisa. Lakini wakulima walikopa fedha benki na waliweka dhamana nyumba zao, hivyo kutokana na yaliyotokea ni wazi wakulima hawatakuwa na uwezo wa kulipa fedha benki. Hivyo ni vyema mabenki yakaangalia upya utaratibu wa kuwaongezea muda wakulima kuweza kulipa na angalau wapewe muda wa mwaka mmoja yaani mwishoni mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo busara mabenki kuanza kuuliza nyumba za wakulima, kwani kilichotokea, yako nje ya uwezo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na wizi, ubadhirifu na ufisadi katika Vyama vya Ushirika ambapo Watendaji wasio waaminifu wanadhoofisha vyama hivi. Lakini cha kushangaza, Serikali bado haijawa na mkakati madhubuti wa kuwachukulia hatua mafisadi hao. Hivyo, napenda kujua ni vyama vingapi vya msingi na ngazi nyingine vimekufa kutokana na ufisadi? Watendaji wangapi wa Vyama vya Ushirika wamechukuliwa hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la korosho bado halijapewa nafasi kwa wakulima kuboresha maisha yao kwani ni viwanda vya korosho vimeuzwa kwa vigogo na haviendelezwi na inapelekea wakulima wa korosho kuuza korosho ghafi.

Hivyo, napenda kuelewa viwanda vyote vya korosho vya Mikoa ya Lindi na Mtwara vilivyobinafsishwa waliomilikishwa ni akina nani (kwa majina).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kulinda wakulima wadogo na wakubwa wa kilimo cha miwa na Viwanda vya Sukari umekuwa kizungumkuti kwani Serikali ilisema haitoi vibali vya kuingiza sukari toka nje, lakini sukari inaingizwa na Serikali inatoa vibali. Hivyo wakulima na viwanda vya ndani ni manung'uniko; umasikini na kupelekea viwanda hivyo kufungwa. Hivyo naomba kujua mkakati wa Serikali juu ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Mkoa wa Rukwa zinaidai *NFRA* jumla ya Sh. 2,588,389,586/= ikiwa ni ushuru wa mauzo ya mahindi katika msimu wa mwaka 2013/2014 na 2014/2015 ambacho ni chanzo kikuu cha mapato ya ndani ya Halmashauri hizi.

Kila wakati Mkoa umekuwa ukikumbushia deni hili kwa maandishi bila mafanikio kwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; Katibu Mkuu, Kilimo; Katibu Mkuu, Wizara ya fedha; na Hazina.

Je, Serikali ina kauli gani juu ya kulipwa kwa deni hili kwa maendeleo ya Mkoa wa Rukwa?

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wengine katika Wizara hii.

Naomba kuchangia hoja hii kwa kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

Je, mazao ya wakulima kama vile mahindi, korosho, kahawa, pamba na kadhalika yanasaidiaje kuinua kipato kwa wakulima? Je, soko lake likoje?

Je, Serikali inasaidiaje kuwatafutia wakulima soko nje ya nchi? Je, kwa nini Serikali haianzishi viwanda vya kuongeza thamani ya mazao?

Je, Serikali imejipanga vipi kuanzisha makambi ya kilimo kwa kila mkoa ili kuwezesha vijana kupata ajira ya kudumu? Je, Serikali haioni ni busara kutumia makambi ya JKT ili kuanzisha makambi hayo?

Serikali ina mpano gani wa kujenga maghala ya kuhifadhia chakula kwa kila mkoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maghala ya kuhifadhia chakula yaliuzwa kwa watu binafsi: Je, Serikali ina mpango gani wa kuyarudisha maghala hayo kwa ajili ya matumizi ya kuhifadhia chakula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti ni suala nyeti kwa ajili ya maendeleo ya kilimo hapa nchini. Je, Serikali imefanya tafiti ngapi kwa ajili ya mazao mengine ya biashara katika nchi hii? Je, tafiti hizo zimeleta faida gani? Watafiti wetu wa mazao mbalimbali wamewezeshwaje na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja!

**MHE. ZARINA S. MABABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa sera nzuri ya Kilimo Kwanza ambayo imepata mwitikio mzuri na pia kuzaa matunda mema. Lakini

sera hii imegeuka kuwa mwiba kwa wakulima kukosa masoko ya uhakika kwa mazao yao.

Je, Serikali ina sera gani ya kuhakikisha masoko ya wakulima ya uhakika? Sasa hivi wakulima wanakata tamaa kwa kutokuwa na masoko kwa mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wamehamasika kutumia zana bora za kilimo, lakini mpaka sasa wengi bado wanatumia kilimo cha jembe la mkono na wachache sana wanatumia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania bado ina mabonde mengi ya rutuba, lakini kilimo kinatumia zana duni na ukitilia maanani mabadiliko ya hali ya hewa ambayo huleta aidha mafuriko au ukame, hii inapelekea wakulima kutokuwa na uhakika wa kuvuna na kumfanya asijitosheleze na/au hata mwenyewe asithubutu kujaribu kukopa.

Je, ni jinsi gani Serikali imejipanga kuwasaidia; njia ya mkulima wa kawaida kutumia zana za kisasa na kulima kwa umwagiliaji badala ya hali ya sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia inatambua, Afrika inatambua na Tanzania inatambua kuwa ardhi na kilimo ndiyo utajiri wa mbele dunia inakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rekodi zinasema kwa asilimia 60 ya ardhi Afrika na Tanzania bado ni ardhi yenye rutuba ambayo bado haijatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 60 ya watu wake ni vijana ambao wengi hawana kazi/ajira. Serikali ingeweza kuwakusanya vijana ikawasaidia kuandaa ardhi, mbegu na pembejeo nyingine kwa misingi ya mkopo na kuwapa utaalamu. Mkopo huu wangeweza kuulipa kutegemea mazao watakayovuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani kuwasaidia vijana kujiajiri kwa kutumia ardhi yetu ambayo inaweza kutoa ajira kwa mamilioni? Hii itasaidia siyo tu kutoa ajira kwa vijana lakini pia itainua mauzo ya nje ya nchi na kupandisha hali ya uwezo wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kilio kikubwa kutoka kwa wakulima juu ya kodi kubwa ya ardhi. Wengi wao wanashindwa kulipa. Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza Kodi ya Ardhi na hivyo kuwezesha Serikali kukusanya kodi lakini pia kuwezesha wakulima ku-*register* mashamba yao na kuweza kuyatumia kukopa kwenye vyombo vya fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maofisa Kilimo hawapo vijijini kuwasaidia ushauri wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya madawa yasiyofanya kazi ni mbaya, Serikali iongeze ufuatiliaji wa suala hilo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yake ili tuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti; pamoja na kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu na asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima, bado Serikali haijaweza kutoa kipaumbele kwa kutenga bajeti ya kutosha ili kukuza uchumi na kuwainua wananchi kupitia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo; ni lini Benki ya Kilimo itaanza rasmi na kufunguliwa matawi katika Mikoa au Ukanda unaoshughulika zaidi kama Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwemo Mkoa wa Iringa. Wakulima wengi wamekuwa hawalimi kilimo cha kisasa, tatizo hawana nyenzo na hawana mitaji ya kutosha kuweza kulima kisasa ili kiweze kuwatoa katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchi za wenzetu walizoendelea kama China na kadhalika, kuna mabenki mengi ya kilimo yanafunguliwa ili kuwapatia mikopo ya kuwezesha kilimo kiweze kusaidia uchumi, lakini wakulima wa nchi hii bado benki hazijawatambua, hawakopesheki sababu hawana dhamana za kuweka ili wapatiwe mikopo. Je, Serikali inasemaje kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Kilimo; bado wakulima wa Tanzania wanalima bila kuwa na elimu ya kutosha na kusababisha kulima kilimo kisicho na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa katika hotuba Serikali imekiri kutoa elimu kwa baadhi ya maeneo, je, ni vigezo gani vinatumika ili kuanza kufikisha elimu hiyo kwa wakulima kwa sababu vijana wetu wengi wa Iringa wanaishi kwa kutegemea kilimo cha nyanya na vitunguu na matunda. Pia Vijana wameanza hata kulima kilimo cha maua, lakini hawana elimu ya kutosha kuweza kulima ili kilimo kiweze kuwasaidia. Pia hawana elimu ya kupata masoko ya biashara na elimu ya usindikaji, naomba Serikali itueleze vigezo vinavyotumika au nini kifanyike ili elimu hii iweze kuwafikia wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika; Serikali ilitilia mkazo katika kuanzisha Vyama vya Kuweka na Kukopa ili viweze kutoa umaskini na kuwa suluhisho la mitaji, lakini bado Vyama hivi vinaanzishwa na vinakuwa havidumu

sababu viongozi wengi walio kwenye vyama hivi hawana elimu ya kutosha kuendesha vyama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ni vema ikaweka utaratibu katika Vyama wa kuwapata viongozi wenye elimu ya kutosha au viongozi wa vyama wapate elimu baada ya kuchaguliwa. Je, ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya elimu kwa viongozi wa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii adimu kumshukuru na kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake nzuri iliyojaa matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yetu kupitia Wizara hii iwaambie Watanzania kuhusu programu ya miradi juu ya utekelezaji wake katika maeneo mbalimbali ya kilimo hapa nchini.

Katika Jimbo langu la Dole nilipangiwa kujengewa barabara tatu zinazopita maeneo ya kilimo Bumbwisudi, Kizimbani na Mwera. Hadi sasa hakuna hata barabara moja imejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kupitia program hii ilipangwa kuchimbwa kisima kikubwa katika bonde la kilimo lililopo Shehia ya Kianga Unguja ili kiwasaidie wananchi kulima kwa njia ya umwagiliaji. Kwa masikitiko makubwa hadi sasa hakuna kilichofanyika. Pia katika Shehia ya Mtofani pajengwe soko la mazao mbalimbali ili kuwapa fursa wakulima kuuza mazao yao. Hadi sasa hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu kwani zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wamejiajiri kupitia sekta hii. Pamoja na ukweli huu huduma za utafiti na ugani bado hazijawafikiwa wakulima wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukisikia wimbo mtamu kuhusu Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambayo imekuwa sawa na ndoto ya mchana. Naiomba Serikali iwaambie Watanzania ni lini hasa benki hii itaanza ili iwawezeshe wakulima kupata zana na pembejeo mbalimbali za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itoe kipaumbele kwa mazao ambayo yanaiingizia nchi yetu fedha nyingi za kigeni. Mazao ya tumbaku,

pamba, kahawa, chai, tangawizi na sukari yamepata masoko ya uhakika na bei nzuri ili kuwawezesha wakulima kunufaika na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuwalinda kwa dhati wakulima wa ndani kwa kuzuia uingizaji wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini, mfano, Serikali iwe macho na wafanyabiashara wasio waadilifu wanaoingiza sukari, kahawa, chai na mazao mengine yanayozalishwa kwa wingi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kupitia MKUKUTA, *MDGs, BRN,* sekta ya kilimo imepewa umuhimu mkubwa ili kuwa na uhakika wa chakula *(food security)*. Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya kila program ya Kilimo Kwanza ili kuweza kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa program hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za karibuni tumejionea Mikoa inayoteseka kwa wananchi wake kuwa na tatizo la utapiamlo pamoja na ukweli kwamba hiyo inayozalisha mazao mbalimbali. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha tatizo hili linaondoka na hivyo kuwasaidia wananchi hasa watoto katika Mikoa hiyo kuondokana kabisa na tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha maua ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Je, Serikali imejipanga vipi kuhamasisha kilimo cha maua hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Wizara ikaweka wazi malengo makuu yanayohitajika kufikiwa katika kila eneo na kupima ufanisi wake. Kwa mfano, kiambatisho namba sita, skimu 20 za umwagiliaji *(PHRD)* hakielezei ni tani ngapi kwa hekta zinazozalishwa na hakielezi tumeongeza hekta ngapi katika mpango mkuu wa umwagiliaji ili tujue itatuchukua muda gani kufikia malengo makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa sukari; hadi leo uzalishaji wa sukari ni MT. 300,858.00, hii ni aibu, Serikali lazima ilinde viwanda vya ndani na Serikali ieleze ni lini tutafikia lengo la kufikia MT. 600,000 za uzalishaji wa sukari ili kuzuia uagizaji na kuifanya sekta ya sukari kukua, kuchangia pato la Taifa na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya chakula kuwa ya biashara; yapo mazao ya chakula ambayo yangeweza kuwa ya biashara kama kuna mpango mkakati wa kufanya hivyo. Kwa mfano, zao la muhogo, mpunga, mahindi, mtama na kadhalika kama kuna mpango wa kuanzisha viwanda vinavyo-*process* mazao haya ili viongeze thamani na kusafirisha nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi kama Thailand, Vietnam zinatuuzia mchele na kuuza nje, lakini vipo viwanda vinavyofanya *packing* na kusafirisha. Kuna haja Wizara ya Kilimo, Viwanda na sekta binafsi kukaa pamoja na kufanya mkakati wa pamoja wa angalau mazao mawili ili tupunguze uzalishaji usio na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao makuu ya asili; kutokana na taarifa ya Wizara *page* 79 ni mazao matatu tu makubwa ya asili ambayo kidogo yamefanya vizuri, kahawa, tumbaku na korosho pamoja na kwamba yamesafirishwa ghafi kwa kiwango kikubwa. Hii si hali nzuri, je, ni kwa nini mazao mengine hayakufanya vizuri? Je, kuna mpango gani wa kuongeza thamani ya mazao haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vinavyoagiza malighafi za kilimo; viwanda vya ngano na mafuta ya kula bado vinaagiza malighafi ngano na mawese kutoka nje. Viwanda vya ngano huagiza ngano wastani wa MT. 1,000,000 kwa mwaka na vya mafuta MT. 500,000 za mawese kwa mwaka. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wenye viwanda hivi kupata malighafi ya ngano na mawese?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tulizonazo ni kwamba wenye viwanda vya ngano wameomba ardhi lakini hawajapatiwa hadi leo, je, upo mpango mahsusi wa kutumia bidhaa zetu za kilimo kwa viwanda vya ngano na mafuta ya kula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zana za kilimo; ni vyema Wizara ikaeleza ni matrekta na zana zipi nyingine zinazohitajika na ngapi zimeagizwa na upungufu unachukuliwa hatua gani, ikiwa ni pamoja na kuimarisha viwanda vya kuunganisha zana hizo? Ni aibu hata mapanga tunaagiza kutoka nje. Serikali kwa pamoja ina mkakati gani wa kuzalisha zana zetu kama enzi ya *UFI*?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uingizaji wa sukari nchini; bidhaa hii ya sukari ni miongoni mwa bidhaa muhimu katika nchi yetu ambayo kila mtu anatumia; maskini na tajiri wote wanauhitaji wa sukari sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na tatizo la uingizaji wa sukari kinyume na utaratibu unavyotakiwa na hili jambo limedidimiza viwanda vyetu vya ndani ambavyo vimekuwa na matatizo ya kupata soko la kutosha, matokeo yake viwanda vimeamua kusitisha uzalishaji hasa kwa kununua miwa ya wakulima wa nje wanaoitwa *outgrowers*. Wakulima hawa wa miwa walihamasishwa wakalima, walikopa fedha, lakini leo wako hatarini kunyang'anywa mali zao walizoweka rehani na hata kuuziwa nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuruhusu sukari kwa kutoa vibali kimesababisha viwanda kushindwa kuendelea na utaratibu wao, wakizalisha na kuchukua miwa ya wakulima wa nje na hii imesababisha hasara kubwa kwa viwanda hasa Kiwanda cha Kagera *Sugar* mpaka kufikia mabenki yaliyowakopesha kutaka kutaifisha kiwanda hicho.

Hivyo, sasa hivi wanataka kupunguza wafanyakazi karibu 1,500 na hata hawajawalipa wakulima wa miwa wa nje *(outgrowers)* kwa sababu ya hasara kubwa waliyoipata. Hii imesababisha mashamba ya *(outgrowers)* wakulima wa miwa kuwa kama mapori na kusababisha hasara kubwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Misenyi ni Wilaya inayotegemea kahawa kama zao kuu la biashara, lakini ni muda mrefu sasa zao hili limekosa soko na matokeo yake limerudisha nyuma sana maendeleo ya wana-Misenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kukosa soko kwa kahawa inashangaza sana kuona wangauzi wa kahawa wanaotoka Uganda *(kilogram)* moja wananunua Sh. 1,500 wakati hapa nchini kupitia ushirika wananunua Sh. 950. Swali, hawa watu wa Uganda soko wanapata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anamalizia anieleze lini kahawa itanufaisha mkulima kwa kupata bei kama wanayonunulia watu wa Uganda ili watu wanufaike kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja mbele kumalizia, aje na majibu lini Serikali itaacha kuagiza sukari nje na kulazimisha viwanda kuzalisha kiasi kinachotosha ili kuondoa utata wa kuagiza sukari nje ya nchi?

**MHE. DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji, tunaomba Serikali isaidie kukamilisha ujenzi wa bwawa la Kimkakati kwa ajili ya kuzuia mafuriko, kupata maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, maji kwa ajili ya mifugo na ufugaji wa samaki kwenye mto Themi, eneo la Themi ya Simba, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali isaidie ujenzi wa malambo kwenye mabonde ya Mwandet, Musa, Kisongo na Kigongoni ili pamoja na kuzuia mafuriko yanayosababisha maafa na hasara kwa uharibifu mkubwa wa mali na kupata maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 kikundi cha vijana cha ushirika wa Meiting-Aikata waliwasilisha maombi ya sh.150,000,000/= kwa Mfuko wa Tanzania – Japan kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji wa matone *(Green House drip irrigation)* ili waongeze wingi na ubora wa mboga wanazozalisha, lakini hadi leo hawajajibiwa kama imeidhinishwa au la na hivyo kuwakatisha tamaa. Naomba Waziri atujulishe ni lini watapa msaada huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya pembejeo, vijana katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha wanaanza kukata tamaa ya kujikwamua na umaskini utokanao na kukosa ajira na kuaminika kutokana na maombi yao ya mikopo ya pembejeo kukataliwa kwa sababu dhamana yao ya hatimiliki ya kimila haiaminiwi/haikubaliki. Mmoja wa vijana hao Bwana Kaisanwa Nduruma amewasilisha malalamiko kwangu kuwa Serikali inakataa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aingilie kati suala hili ili kuwawezesha vijana kujiajiri kupitia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Wasira kwa hotuba nzuri. Nimpongeze pia Naibu Waziri na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Soika, katika hotuba hii kuna mambo muhimu ningependa Serikali iyaangalie. Kilimo cha umwagiliaji Kanda ya Ziwa; nimepitia kitabu cha bajeti na sijaona mkakati wa kilimo cha umwagiliaji Kanda ya Ziwa. Mikoa ya Kanda ya Ziwa imezungukwa na Ziwa Victoria kama ilivyo kwa nchi kama Sudan ambazo zinanufaika kupitia kilimo cha umwagiliaji kutokana na maji ya Mto Nile. Tunaomba Serikali ione utaratibu wa kusaidia wakulima wa Kanda ya Ziwa kwa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa pembejeo kwa zao la pamba: Kilimo cha pamba katika Mkoa wa Geita kimekumbwa na changamoto za upatikanaji wa pembejeo. Wakati mwingine pembejeo zinazoletwa zinakuwa hazitoshelezi mahitaji. Mfano, upatikanaji wa dawa na mbegu umekuwa ni tatizo.

Mwaka 2012/2013 mbegu hazikuota, hivyo, wakulima wa pamba wa Mkoa wa Geita wanahitaji kulipwa fidia. Wakati wa majumuisho ningependa kujua kwamba ni lini sasa wakulima wa pamba watalipwa fidia. Ajira kwa Mafisa Ugani: Kuna upungufu mkubwa wa maafisa ugani. Nchi hii zaidi 70% ya Watanzania wanategemea kilimo. Ni vema tukawekeza katika sekta hii muhimu kwa kuajiri wataalamu watakaoweza kutoa elimu ya kilimo bora. Tunaomba

ajira za maafisa ugani ziwe na utaratibu wa kuajiri moja kwa moja kwani wahitimu wapo wengi na hawajapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ione umuhimu wa kuzifanyia kazi changamoto nilizotaja ili kuimarisha sekta ya kilimo kwa Watanzania wote kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naunga mkono hoja.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja na naomba niishauri Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwenye masuala kadhaa ya kilimo na ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa utaratibu wa mwaka 2014/2015 wa kuvipatia vikundi vya wakulima na Vyama vya Ushirika kwa kupitia taasisi za fedha, umeshindwa kuleta tija kwa wakulima kama inavyoonekana katika utekelezaji wake kwa vikundi vilivyosajiliwa 4,990, hadi Machi, 2015 ni vikundi 712 vilikidhi masharti ya kukopesheka kupitia benki ikiwa ni 24% tu. Naomba utaratibu wa zamani urudishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa stakabadhi ghalani ni mzuri kwa zao la korosho endapo fedha za wakulima zitalipwa kwa wakulima bila tozo zozote kama vile za usafirishaji, magunia na riba ya mabenki. Naishauri Serikali kuongeza nguvu ya kuwaelimisha wananchi kupeleka korosho na kusubiria ziuzwe kwa vyama vya msingi wasipewe mkopo ambao riba zake zinaumiza wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya fidia kwa waendesha maghala iangaliwe upya, wakithibitika kupoteza mzigo wa wakulima au kubadilisha mzigo, walipe gharama za mzigo na fidia juu, badala ya sasa wamewekewa kiwango maalumu cha faini ambacho wakati mwingine hakikidhi gharama ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ugawaji wa pembejeo za mazao mchanganyiko hasa mahindi na mpunga kwa mfumo mpya umefeli, hakuna mkulima aliyepata pembejeo msimu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mfumo wa zamani urudishwe.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iangalie wakulima wa miwa Mvomero wapate kulipwa fedha zao. Wakulima wamefikia wakati wameacha kulima miwa na wameanza kulima mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa Vijana: Nashauri vijana wapatiwe mikopo na ikiwezekana wakopeshwe pembejeo pia na matrekta chini ya masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hakitaweza kubadilika sana ikiwa tutaendelea na bajeti hii. Ifike wakati kilimo kipewe kipaumbele namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji; wakulima kwa kusaidiana na Serikali wapate elimu ya uvunaji wa maji kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, wahitimu wa fani ya kilimo kuajiriwa mara moja baada ya kumaliza masomo yao, hivyo tutatimiza sera ya afisa kilimo kwa kila kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia maandishi nachangia hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kahawa: Naunga mkono jitihada za Serikali za kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa. Aidha, maeneo mawili yanapaswa kuangaliwa ili kuongeza uzalishaji wa zao hili ambalo ni moja ya mazao yanayoongoza katika kulipatia taifa letu fedha za kigeni. Moja; ni mfumo wa soko, uhakika wa soko ikiwemo bei stahiki ambayo ni kivutio muhimu cha uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipitie upya vyombo vya ununuzi kwa lengo la kuondoa ukiritimba na unyonyaji wa wakulima. Inapobidi utaratibu wa kutafuta wateja wa moja kwa moja toka kwa wakulima utafutwe/ufuatwe *(niche markets)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na soko, Serikali ibuni mipango na mikakati ya kuwasukuma wananchi kulima kahawa. Historia inaonesha wazi kuwa ustawi wa zao hili pamoja na sababu nyingine ulichangiwa na msukumo wa Serikali. Serikali iwasukume wananchi kulima kahawa kwa maeneo husika na iwalinde dhidi ya wanyonyaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha miwa: Sekta hii ni njia mbadala ya kuwaongezea wananchi kipato kwa kuwapa zao mbadala – *out growers*. Ili kutumia fursa hii lazima viwanda na mashamba makubwa yalindwe. Tishio la kilimo cha miwa ni kudhibiti sukari itolewayo nje ya nchi. Sukari ya ziada iingizwe kwa pamoja kutokana na ukweli kuwa bei ya nje ni chini ya ile ya gharama za

ndani, sukari ya nje ifidie gharama za uzalishaji nchini *(cross subsidization)*. Kitengo maalum mithili ya kile cha mafuta *PICL* kifanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao: Narudia tena kushauri Serikali iwekeze katika kuzalisha chakula maeneo ya Kanda ya Ziwa. Mipango ya umwagiliaji kwa eneo hili itawezesha au kupunguza gharama za Serikali kupeleka chakula eneo hili. Tunapoelekea tutumie mitambo ya kisasa kumwagilia pale inapobidi ili tuzalishe chakula lakini pia kuwapa ajira vijana na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya chakula: Naishauri Serikali iendeleze kwa kasi mipango ya kujenga hifadhi za mazao za kisasa *(silos)* chini ya utaratibu maalum na kwa kutazamia mahitaji ya hapa nchini na nchi jirani, tunaweza kuendesha mtandao wa hifadhi kwa kukopa au kutumia huduma za kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali na hasa kuikumbusha juu ya umuhimu wa kupambana na magonjwa ya mazao. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa mwaka tunaomaliza imeshindwa kupambana na ugonjwa wa migomba ukilinganisha na wenzetu wa Uganda na Rwanda. Zao la ndizi ni chakula na chanzo cha mapato kwa wakulima na wananchi wa Kagera. Naomba na kuishauri Wizara hii kuzingatia mpango niliowasilisha kwao katika kupambana na ugonjwa huu. Uwezeshaji wa Chuo cha Maruku nayo ni njia mojawapo ya kuongeza kasi ya kupambana na hatimaye kufuta kabisa ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena na kuiomba na kuishauri Serikali juu ya kuajiri maofisa wagani wa kilimo. Vijana wote wenye fani hizi waajiriwe pindi wamalizapo masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutoa ajira, Serikali ipitie upya mfumo wa utumiaji wa watendaji hawa. Kimsingi Watendaji hawa kwa wale waliopata ajira hawatumiki kikamilifu. Kada hii kutokana na mfumo wa usimamiaji muda mwingi hawafanyi kazi kwa tija ikiwemo kufundisha au kushauri wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti hii ipite.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa bajeti. Pamoja na pongezi hizi ninao ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji: Nimesoma kurasa za 48 – 51 zinazofafanua kuhusu shughuli hizi za umwagiliaji. Ushauri ni kwamba, juhudi

hizi bado hazijaelekezwa kwenye maeneo kame. Maeneo haya yakipata skimu za umwagiliaji yana uwezo wa kuzalisha kiasi kikubwa cha mazao ya chakula na biashara na kuondoa tatizo la njaa inayotokea mara kwa mara na hivyo kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Manyoni ikiwa ni moja katika maeneo kame umebuniwa mradi wa bwawa la Mbwasa ambalo litahudumia skimu 4 za umwagiliaji ambazo tayari zina miundombinu ya mabanio na mifereji, lakini hakuna chanzo cha maji (bwawa). Kwa sasa skimu hizo zinategemea mvua. Bado Wizara inasisitiziwa kutafuta fedha za kujenga bwawa la Mbwasa kwani usanifu umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wakulima wa mahindi: Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imekiri kwamba bado Serikali kupitia *NFRA* inadaiwa shilingi bilioni 12, na kwamba deni hili litalipwa wakati wowote. Kwa kuwa ahadi kama hii imetolewa mara nyingi, ilifaa Serikali iseme kwa uhakika ni lini hasa deni hili litamaliziwa kwani malalamiko juu ya suala hili ni mengi na yanazidi kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri, dakika 10.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha hadi leo kuwa na afya njema na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Nambozi ambao wameendelea kuwa na imani nami kunichagua kuwa Mbunge wao. Naomba niwaeleze kwamba bado nina nguvu, nina akili timamu za kuweza kuendelea kuwatumikia katika nafasi ya Ubunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwaambie kwa kututumia Bunge lako Tukufu kwamba na mwaka huu ikimpendeza Mungu basi nitakwenda kwao ili niwaombe ridhaa niendelee kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kuishukuru sana familia yangu kwa kuendelea kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu. Namshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Mzee Wasira, kwamba nimeweza kushirikiana naye kwa kipindi kifupi alichokuja Wizarani, lakini pia na mtangulizi wake Mheshimiwa Chiza ambaye pia nilifanya kazi naye kazi kwa takribani kipindi cha mwaka mmoja vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba nizungumze masuala mawili tu, halafu nimwache Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja aweze kuzungumza hoja nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la umwagiliaji kwanza. Katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, tuliandika bayana kabisa kwamba tunataka chakula kinachozalishwa nchini, angalau asilimia 25 itokane na kilimo cha umwagiliaji. Leo mbele ya Bunge lako napenda kuwaarifu Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, kwamba mpaka sasa tumezalisha asilimia 24 ya chakula tunachozalisha kutokana na kilimo cha umwagiliaji.

Kwa hiyo, malengo tuliyoweka ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, kimsingi ni kama vile tumeyakamilisha. Kwa hiyo, siyo jambo dogo, ni kubwa, pamoja na kile kinachozungumzwa kwamba ndiyo tuna eneo kubwa linalofaa kwa umwagiliaji, zaidi ya ekari milioni 29, lakini kwa kiwango na lengo ambalo tulijipangia kutokana na uwezo wa Serikali, hicho tumejitahidi kwa sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge na hili jambo nimelisema sana hapa Bungeni nikijibu maswali, kwamba liko tatizo, nami niseme labda kwenye Halimashauri zetu. Tumeibua miradi mingi sana ya umwagiliaji. Hata katika Halmashauri nyingi nilizopita, namshukuru Mungu nimepita zaidi ya mikoa 20 nikiangalia shughuli mbalimbali za Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini pia na shughuli ya umwagiliaji, Halmashauri zimeibua miradi mingi mno ambayo utekelezaji wake, unaanza sehemu (a), haufiki mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano tu, nimekwenda Shinyanga kwa rafiki yangu Mheshimiwa Ahmed; Mkoa wa Shinyanga una *schemes* karibu 71. Mkoa wa Shiynyanga kama ulivyo vile, miradi ya umwagiliaji 71; vyovyote vile na kwa *resources* tulizonazo, ni ngumu sana kukamilisha miradi yote au *schemes* zote 71. Ni kweli iko *commitment* ya Serikali kwenye baadhi ya miradi na hii ndiyo tunakwenda nayo kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme na niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge, amesema Mheshimiwa Jafo hapa kwamba mwaka huu tumetenga Shilingi bilioni 19 na mwaka jana tulikuwa na Shilingi bilioni nane. Kama tunazungumza fedha zote ambazo zilikwenda kwenye umwagiliaji, basi mwaka 2014 zilikuwa ni karibu Shilingi bilioni 33.9, ndizo zilizokuwa zimepangwa. Mwaka huu zilizo kwenye bajeti yetu kwa Fungu Na. 5 - Maendeleo, zimepangwa karibu Shilingi bilioni 54.3 ndiyo tunategemea ziende kwenye shughuli zote zile za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba Waheshimiwa Wabunge waende kwenye kitabu chetu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, akianzia ukurasa wa 97, kwenye kiambatanisho Na. 2, pale tunazungumzia *schemes* zilizotekelezwa mwaka 2014/2015, kupitia mfumo wa *BRN*. Jedwali Na. 3, linazungumzia *schemes* zitakazofanyiwa usanifu kupitia mfumo wa *BRN*, mwaka 2015. Lakini ukienda jedwali Na. 4, tunazungumzia *schemes* zitakazokarabatiwa kupitia mfumo wa *BRN* mwaka 2015/2016 na jedwali Na. 5 tunazungumzia orodha ya miradi ya umwagiliiji inayotekelezwa kwa fedha za *DIDF* kwa mwaka 2014/2015, lakini pia kiambatanisho Na. 6, tunazaungumzia *schemes* 20 za umwagiliaji zitakazotekelezwa chini ya mradi wa Japan ambao tunauita *PHRD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu siyo rahisi kupitia na kutaja mradi mmoja mmoja. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ambao wangependa kujua Wizara tunafanya nini katika umwagiliajia, basi wapitie miradi hiyo kwenye kitabu chetu kama ambavyo nimekwishasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye umwagiliaji, wamezungumza labda kwa ufupi, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Chibulunje, amezungumza ndugu yangu Mheshimiwa Ahmed, Mbunge wa Solwa, ndugu yangu Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Dkt. Nkya, Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda na wengine wengi ambao pengine kwa sababu ya muda siwezi kuwataja wote, hawa wote wame-*address issue* ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kama nilivyosema, Wizarani tunajipanga tuhakikishe kwamba angalau miradi ile ambayo tunadhani inaweza ikatuletea chakula kingi kwa wakati mmoja, hiyo ndiyo tuhakikishe tunaendelea nayo kwa ajili ya uzalishaji mzuri zaidi. Lakini mkumbuke kama nilivyowaeleza wakati ule, nadhani tulifanya makosa mahali, tukaanzisha miradi mingi sana ambayo hatuwezi kuihudumia yote kwa wakati mmoja.

Wizarani tumeelezana kwamba lazima tuwe na utaratibu, tupange miradi yetu ipi tuanze kuiendeleza na ipi angalau iwe inakwenda hatua kwa hatua kadri ya upatikanaji wa fedha huku Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naziomba Halmashauri, utaratibu wa kuibua miradi pale ambapo hatuna uhakika wa upatikanaji fedha; na yenyewe pia haiwezi kutusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze suala la ushirika kwa kifupi sana kwa sababu ya muda. Kama Walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge, ushirika ndicho chombo pekee ambacho kinaweza kikamtoa Mtanzania wa kawaida, masikini, kutoka kwenye umasikini angalau kumpeleka kwenye kipato

cha kawaida na kipato cha kati, ambacho kinaweza kikafanya maisha yake na familia yake yawe mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu kama mnavyojua mwaka 2014 tulibadilisha sheria, tumeanza na kutumia Sheria mpya Na. 6 ya mwaka 2014, ambayo sasa tumerekebisha baadhi ya vifungu ili kufanya ushirika wenyewe uweze kufanya kazi vizuri; tukabiliane na wezi, wale ambao walikuwa wanaudumaza ushirika, walifikiri ushirika ni sehemu ambayo mtu anaweza akafanya kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria ile imeweka adhabu mbalimbali, lakini pia na namna ambavyo wanaushirika wenyewe wanaweza wakauendesha ushirika wao. Tumezungumzia pia suala la elimu kwenye sheria hiyo ili wananchi wajue namna ambavyo ushirika wao unaweza ukaendeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako matatizo mbalimbali kwenye ushirika ambayo sasa kuja kwa Tume ya Ushirika kunatufanya tukabiliane na matatizo mengi ambayo yako kwenye ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nizungumzie kwa kifupi sana na kwa sababu ya muda kama ulivyosema, suala la *KNCU*. Ndugu yangu Selasini amezungumza sana suala la *KNCU*. Suala hili ni moja ya maswali mengi katika ushirika na siyo *KNCU* ambayo ina matatizo peke yake, vyama vingi vina matatizo lakini ambayo tunaendelea kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *KNCU* ni kweli ina deni karibu la Shilingi bilioni nne kwenye Benki ya *CRDB* na hakuna namna yoyote; na ninaomba niwaeleze wana-*KNCU*, labda hapa niseme, ushirika ni mali ya wananchi. Serikali inashughulika na sera ya kusimamia maendeleo ya ushirika nchini, lakini ushrika wenyewe ni wa wanachama na hili lazima tuwaeleze kwamba wenyewe wasimamie ushirika wao vizuri kama wanataka uwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uuzwaji wa mali za *KNCU*, ili kulipan deni lile la Shilingi bilioni nne *CRDB*, hawana namna! Ni lazima waangalie wanatokaje pale, kwa sababu ziko sababu mbalimbali, ambapo kwa sababu ya muda sitaelezea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda Moshi karibu mara mbili, mara tatu, kwa ajili ya kushughulika na suala la *KNCU;* niseme kwamba, kama hatuwezi kuwa na hatua za dharura kwa wanaushirika wenyewe, ni hatari *KNCU* kama alivyosema Mheshimiwa Selasini, ushirika utakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna namna nyingine, ni lazima wachague. Walichagua kuuza shamba lao la Gararagua ambalo linakisiwa kuwa na

thamani kati ya Shilingi bilioni 10 na 14 na kwa sababu wenyewe waliomba, ni kwa ardhi yao na Serikali tulisharidhia waendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaomba wakae vizuri, waangalie taratibu nzuri zitakazowafanya wauze lile shamba ili waweze kulipa deni lile la benki ambalo ni karibu kama nilivyosema Shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kadri tunavyochelewa, lile deni linaedelea kukua, na nina hakika kama hatuwezi kulilipa mwaka huu, deni hili baada ya mwaka ujao linaweza likafika Shilingi bilioni tano, kwa sababu kila mwaka lina riba karibu ya Shilingi milioni 550.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita mtoa hoja, dakika 30.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja niliyoiwasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yaliyosemwa hapa ni mengi na kwa namna yoyote ile kwa dakika thelathini siwezi kutegemewa kuyajibu yote, lakini nataka kutoa ahadi kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba yote tuliyoyapokea, tutayaandikia majibu na kila Mbunge atapata nafasi ya kujua majibu yake yanastahili kuwa yapi. Kwa hiyo, nitafanya hivyo ili kuhakikisha kwamba tunapata majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa kuwashukuru wote waliosema, wako Waheshimiwa Wabunge 18 wamepata nafasi ya kuongea moja kwa moja na wako Waheshimiwa Wabunge 32 ambao wameandika na hoja zao za maandishi tunazo. Vile vile wako Wabunge 31 ambao walitoa hoja zinazohusiana na kilimo wakati wa mjadala wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaambia kwamba Serikali haipotezi *record*, kila kilichosemwa tutakizingatia na tutahakikisha kwamba utekelezaji wetu unafuata ushauri ule ambao unatekelezeka. Narudia maana kuna mengine magumu, mengine unasikiliza mpaka unashangaa kama na hili nalo kweli linatekelezeka au ni kweli au si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru sana Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushauri wao walioutoa katika hotuba, kwa sababu hotuba ile imetokana na mashauriano ambayo tulifanya sisi Wizara

tukiwa tunatoa taarifa kwenye Kamati. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia Kamati kwamba tutazingatia ushauri wote uliotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja kwamba Mfuko wa Taifa wa Pembejeo haufahamiki kwa wakulima, basi nalichukua suala hili na nitataka Mfuko ule uanzishe programu ya kujitangaza wenyewe kwa wananchi ili wanaotaka kukopa kwao wajue wapo na wanaweza kukopesha. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa ushauri huu nilioupata kutoka kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa niseme tu kwamba, wale wote ambao wamezungumza juu ya udogo wa bajeti, kwamba bajeti ya kilimo ni ndogo, nakubaliana nao, lakini mimi na wao hatuna namna ya kufanya, kwa sababu sisi wote Bunge hili ndiyo tunatoa bajeti. Tunaleta Bajeti ya Serikali na wakati mwingine lazima ushone nguo inayolingana na saizi yako na miaka mingi imepita tumekuwa na wahisani wanasema tu wataleta hela haziji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri Watanzania lazima tujifunze kujitegemea, lazima tutengeneze bajeti ambayo kweli inatekelezeka na inatokana na uwezo wetu. Tukiendelea tu kukaa tunalala tunasubiri mjomba, wajomba wenyewe wanaonekana kama hawana nia njema, wanasema tutawapa hiki, kila siku masharti. Sasa unajua ukiishi uko kwako una jirani kila siku anakwambia fanya hivi ama sivyo utakiona cha mtema kuni, siku nyingine unachoka unasema basi mimi sili kwako, mimi nitakula kwangu, hata kama kwa mlenda. Kwa hiyo, nadhani kwa mambo ya Bajeti lazima tujifunze kujitegemea, hakuna namna. Mapato yetu yakiongezeka bajeti itaongezeka, uchumi wetu ukikua bajeti itaongezeka na kilimo kitapewa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango ujao wa maendeleo wa miaka mitano ambao unaanza mwakani tulikubaliana kwamba sasa miundombinu tunaipa kipaumbele katika kipindi hiki, lakini sekta zinazozalisha mazao, sekta ya kilimo na sekta ya viwanda tutaipa nafasi kubwa zaidi katika mpango ujao kwa ajili ya kusaidia kuinua kipato cha wananchi na kupambana na umaskini na kutafuta ajira kwa vijana wengi ambao wanataka ajira. Kwa hiyo, nadhani hili jambo litaanza kutekelezwa na naamini bajeti ya kilimo itaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niseme tu, hata ukifanya Bajeti ya Kilimo ifike asilimia zaidi ya kumi, bado yako mambo yanayotekelezwa na Bajeti ya Serikali na yako mambo mengine ambayo yanatakiwa yatekelezwe kwa njia za mikopo. Mambo ya utafiti, mambo ya ugani, mambo ya miundombinu ya umwagiliaji na kadhalika, haya yatasimamiwa zaidi na bajeti ya Serikali. lakini mambo ya zana, mikopo ya pembejeo itabidi benki, ambayo tumeianzisha ifanye kazi ya kuwapa wakulima pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulikuwa tumeanza mwaka huu kufikiri hivyo, lakini haikufanya kazi vizuri sana, ndiyo maana mwaka huu tumerudi kwenye mfumo wa vocha ili tupate muda wa kupita wakati tunajiandaa kwa mikopo, basi tuwe kwanza tunawawezesha wakulima kupata pembejeo wakati mikopo bado inaandaliwa. Kwa hiyo, nafikiri suala hili tutalipa nafasi muhimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, rafiki yangu Opulukwa nadhani alikuwa anasema kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, lakini nataka kumshauri tu kwamba, siku nyingine wakikutuma hawa kusema, wafanye utafiti vizuri ili wakupe habari za kweli, maana unaposema hapa Watanzania wote wanakusikia. Sasa ni vizuri uwaambie maneno ambayo ni ya kweli, usipowaambia hivyo halafu unaandika tu, unasema Serikali imechoka, UKAWA tutachukua, hamuwezi kuchukua kwa kusema uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kabisa kwamba kuchukua mpaka Watanzania wawaamini. Kwa bahati nzuri kwa CCM, Watanzania bado hawawaamini maana wanaona mnatangatanga sana, kwa hiyo hamtaweza kufika huko kwa sasa. Hivyo, tunawatakia heri mwendelee kuwa wapinzani ambao watatusaidia kutuonesha kitu gani hatujafanya ili tufanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimwambie ndugu kwanza, kwa sababu moja katika vitu ambavyo amesema kwa nini *Quoton* si taasisi ya Serikali ipewe jukumu la kuzalisha mbegu. Kuzalisha mbegu ni utaalam, huo utaalam kama uko Serikalini sawa, kama unaweza ukafanywa na *private* na sisi tumesema sekta binafsi lazima ichangie katika maendeleo. Sasa *Quton* hatuipi fedha ya Serikali, haiwezi kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa sababu inatumia pesa zake, inazalisha mbegu na inapokwenda kwa mkulima kumweleza namna ya kupanda inamfundisha na inafanya kazi yake ya *marketing*, hakuna tatizo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui sera ya CHADEMA yenyewe inasemaje juu ya sekta binafsi, maana sisi tunasema sekta binafsi ni injini ya uchumi. Hapa *Quton* ni sekta binafsi na sisi tuko tayari kushirikiana nao, hatuwapi hela, lakini tunawaambia lima mashamba, shirikiana na utafiti, toa mbegu inayofaa kwa ajili ya manufaa ya zao la pamba. Sioni hoja hapo kwa kweli, nadhani hata ndugu yangu Opulukwa naye haoni hoja kwa sababu tulikuwa wote Mwanza wakati ule wa mkutano wa pamba, tuliyazungumza mambo haya vizuri

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema kwa nini kazi ya kuelimisha wakulima ifanywe na *Quton*, kwa nini isifanye? Hata kapuni binafsi inaweza ikafanya. Nafikiri tungewashukuru kampuni binafsi zinazoacha kazi zao na kuwaelimisha wakulima ili waweze kulima kisasa zaidi. Sasa hilo nalo tukihoji kana kwamba ni kosa hapo nitakuwa sielewi, nitasema sina jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja pia kwa nini Serikali isianzishe Mfuko kwa ajili ya kuzalisha mbegu, kama kupitia *TOSCI*. *TOSCI* ni kampuni inayosimamia ubora. Iko kampuni inaitwa, *ASC (Agricultural Seed Company)* ndiyo inayoshughulika na kuzalisha mbegu na inafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na vituo ya utafiti pamoja na wazalishaji binafsi wakiwemo na makampuni kama Suma JKT na Magereza. Yote hiyo tumefanya maana wale watafiti wanatoa mbegu mama *ASC* inaongeza ubora wa hizo mbegu na makampuni mengine baadaye yanazalisha ili mbegu zile ziwe *multiplied*, ziwafikie wakulima. Kwa hiyo, sikuona tena hapa napo kama kuna hoja ambayo inaleta shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufunga mkataba na bei ya pamba. Hili tumelieleza mara nyingi, hata mimi nakubaliana na niliwahi kumwambia hata yule bwana anayetusaidia, yule wa London, kwamba mkataba utaendelea kuwepo tu, lakini kwa sababu bei yenyewe ya pamba haifahamiki wakati mkataba unaposainiwa, kinachotakiwa kujua mkulima huyu ajue bei ya pembejeo anayopewa na thamani yake, akubali au akatae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia ndugu yangu Shibuda anazungumza juu ya *pass book* na nilikwishaiagiza Bodi ya Pamba iangalie mfumo wa kufikishia pembejeo wakulima, maana wako wakulima walio kwenye mkataba na wako ambao hawapo, lakini wote ni wakulima na wote wanachangia kwenye ule Mfuko wa Wakfu. Kwa hiyo, tutengeneze mfumo ambao utahakikisha kwamba walio katika mkataba wanafaidi na wasiokuwemo maana wote ni wakulima, mbele ya Serikali wote wana haki sawasawa. Nadhani hilo ndilo jambo la msingi ambalo tunaweza tukalishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tuliuza viwanda vya korosho, ni sera tu, tulidhani watafanya, wakishindwa tunawauliza kwa nini hamfanyi. Sasa ukiniuliza kwa nini tuliuza kwa sababu tulikuwa tunaiondoa Serikali katika biashara. Sasa ukimuuzia mwingine halafu akafilisika unamuuliza kwa nini ulifilisika na kwa nini ulinunua. Sasa tunazungumza nao tunaona kama hawafanyi kazi tuliyowatuma. Kwa hiyo, itabidi turudi tuzungumze namna ya kuvirudisha vile viwanda, labda tuvipe watu ambao wana uwezo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunataka kuongeza kabisa ubanguaji wa korosho, kwa sababu kwa kweli katika siku zinazokuja hatuwezi kuendelea kuuza korosho za maganda mpaka India, tuna-*export* kazi zetu. Sisi tuna vijana hawana kazi, tuna wanawake kule Mtwara hawana kazi, halafu tunapeleka India, akinamamma wa kihindi ndio wanakwenda kutengeneza. Nakubaliana na wote wanaosema tuwekeze katika kubangua ili korosho zetu ziweze kutupa thamani inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini korosho inasafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam, ndiyo nimeisikia leo hii hoja, tutafuatilia tujue kwa nini, labda kuna matatizo Mtwara, lakini kama hayapo hakuna hoja. Kwa nini tusafirishe kupitia bandari ile pale na Bandari iko pale, kwa hiyo, hili tutalifuatilia na tutakupa majibu ambayo ni sahihi. Wakulima wa zao la korosho nchini wako hatarini kupoteza soko duniani, hakuna hatari hiyo, tutabangua na tutauza. Korosho zina soko zuri ukibangua, usipobangua utakuwa na mnunuzi mmoja tu anaitwa India. Kwa hiyo, tunataka kuondokana na hiyo twende kwenye uuzaji wa nanihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watu wameiba hela, aliniambia hili hata rafiki yangu Mbunge wa Sikonge, Mheshimiwa Said Nkumba, nikamwambia lakini jamani hapa kwa kweli mtakuwa mnanionea, mimi ni Waziri wa Kilimo, sitaki kuibiwa na mimi ndiye nimeibiwa kupitia vyama vile. Sasa tushirikiane na wenzetu wa *Home Affairs*, tumeshawakabidhi ile ripoti, CAG amekagua, ameshamkabidhi *IGP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri jana ndipo tungemuuliza *IGP* maana alikuwepo hapa ili atuambie amefika wapi, lakini kwa sababu ameondoka, nitasaidia kuuliza, ili kwa kweli kama kuna mtu ameviibia Vyama vya Ushirika kule Tabora afikishwe kwenye Mahakama, akajitetee na ionekane kama ana hatia au hana hatia, hiyo ndiyo hoja. Hakuna mtu anaweza kuungana na wezi na nitakuwa mtu wa mwisho kuunga mkono wezi, ndiyo maana katika *record* yangu sijapata kuiba, wala sina mpango wa kuiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengine ambayo yamesemwa juu ya pembejeo. Pembejeo inazungumzwa kwamba mpango wetu haukufikisha pembejeo kwa wakulima. Tumekiri katika hotuba yetu kwamba kumekuwepo na udhaifu katika hili. Tumesema nini, tumesema kwa nia njema, tulidhani sasa tuanze safari ya kutoa mikopo, lakini mabenki yanayotoa mikopo hasa ya biashara haya hayakukubali kutoa mikopo kwa vikundi vingi sana. *NBC* haikutoa, imetoa kwa watu wachache sana, *NMB* nayo haikutoa na *CRDB* haikutoa. Kwa hiyo, waliotolewa ni wale ambao nimewaandika kwenye hotuba yangu. Hata hivyo, tunadhani turudi kwenye vocha ili tuwape vocha, wakati tunafanya maandalizi mazuri zaidi juu ya kufikisha utaratibu wa kukopesha wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo ipo imeanza, itaanza Julai na Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema isikae Dar es Salaam, lakini hata ikikaa Morogoro vile vile haitakuwa imefika kila Mkoa. Nadhani la maana hapa ni kwamba benki ile iwe na utaratibu wa kuanza kujitanua itakapokuwa na uwezo ili tuanze kwenda kwenye kanda, halafu baadaye twende kwenye mikoa na ikiwezekana twende Wilayani kule ambako wanaishi wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipotembelea Vietnam niliona inafanya kazi hiyo. Iko Makao Makuu ya nchi yao lakini ina *branch* katika kila Wilaya na inakopesha. Nadhani hilo ndilo jambo ambalo tungelihimiza huko tuendako ili wakulima waanze kupata mikopo. Hilo limezungumzwa na Wabunge wengi, Mheshimiwa Magdalena alisema sana, Mheshimiwa Vita Kawawa, Clara Mwatuka wote walizungumzia suala linalohusiana na pembejeo.

Sasa suala la tumbaku kwamba hakuna tija kwenye masoko, na fedha zimekosa za kuhudumia, hili nimelishughulikia. Ni kweli tuna *problem* ya bajeti, lakini tumezungumza na wadau wa zao hili, wakiwemo Vyama vya Ushirika na wanunuzi wa zao hili, wote tumekubaliana kwamba katika jukumu la wadau ni pamoja na kuchangia maendeleo ya zao lenyewe. Wamekubali kuchangia na tatizo hili la bajeti kwa kipindi hiki linalohusu soko la tumbaku, halitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niseme hapa kwamba, ziko fedha, tulivunja hapa, Bunge lilipitisha sheria ikavunja ile iliyokuwa inaitwa *Apex*. *Apex* ilikuwa inalipwa fedha nyingi, katika mfumo wa ushirika ule wa kuanzia *Apex* kwenda chini. Nimetoa maelekezo kwa wote wanaohusika, kwamba ile fedha iliyokuwa inakwenda *Apex* sasa irudishwe kwa wakulima ili iongeze bei kwa sababu ukiondoa *Apex* unaondoa gharama, sasa nani alikuwa anamiliki *Apex*, ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ile fedha iliyokuwa inakwenda *Apex* sasa iko kwenye makampuni ya wanunuzi na naijua kila kampuni ina fedha kiasi gani. Izipeleke, iziingize katika mfumo wa bei ili kuondoa gharama ya *Apex* kuwe na maana kwa mzalishaji wa tumbaku. Maelekezo nimetoa na nitafuatilia kuhakikisha yanafanyika. Kutokana na hiyo wakulima vile vile wanaweza kuchangia mfumo kwa sababu na wao ni wadau. Sehemu ndogo inaweza kwenda kwenye hiyo kazi ambayo tumesema ianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matumizi ya Dola, kwamba tunanunua kwa Dola. Hili suala la bei kwa Dola, kuna kitu kinatwa *Tobacco Council of* Tanzania. Huwa wanakutana, wakulima kupitia Vyama vya Ushirika na wanunuzi, ndiyo wanaokutana na kutazama bei ya soko na halafu wanaamua wananunua tumbaku hiyo kwa bei gani kwa Dola.

Wakati mwingine unaweza ukawa unagombana na Dola kumbe ungeshukuru, kwa mfano, sasa hivi thamani ya Dola ina-*fetch* Shilingi nyingi sana kwenye *exchange rate*. Kwa hiyo unaweza vile vile ukamwambia mpe shilingi halafu ukampa kidogo zaidi kuliko zile ambazo angepata kama *exchange rate* ingempa dola zaidi. Kwa hiyo, ni jambo linalozungumzika, tuone ukimlipa kwa dola anapata manufaa zaidi au ukimlipa kwa shilingi anapata nafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunaweza tukalizungumza na wadau na ndugu yangu Nkumba ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku na Bodi nitaizindua, tutataka watupe ushauri, kabla hatujasema Dola hakuna, basi watuambie tufanye nini. Nadhani hilo ni jambo ambalo linazungumzika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upangaji wa bei ya tumbaku nimeueleza. Serikali kushindwa kugharamia Bodi ya Shughuli za Masoko ni kweli, tunayo matatizo ya kibajeti, lakini tunatafuta kila njia kuhakikisha kwamba tunapata. Katika bajeti hii pamoja na udogo wa bajeti mwakani tutajaribu kuona jinsi ya kusaidia Bodi za mazao haya ili ziweze kufanya kazi vizuri kwa sababu ndiyo mikono ya Wizara ya Kilimo katika kuhudumia mazao makuu ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu muda ni mdogo labda niseme habari ya sukari. Maana kuna watu wanasema kwa nini tunatoa vibali vya sukari. Sukari tamu lakini kila siku ina maswali, mimi sijui tatizo ni nini hasa. Sukari tunayozalisha hapa nchini ni tani laki tatu na nne elfu, nimeisema kwenye hotuba yangu na mahitaji ya sukari hapa nchini ni tani mia nne na ishirini elfu, halafu mahitaji ya tani ya sukari kwa ajili ya viwanda ni laki moja na sabini elfu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wewe unazalisha tani laki tatu na nne elfu kwa mwaka na mahitaji yako ni laki nne na ishirini elfu ongeza laki moja na sabini elfu, sasa utaagiza nje na viwanda hivi huwa vinafika wakati vinafunga shughuli zao kwa muda. Sasa hivi viwanda vile havizalishi sukari kwa sasa. Kwa hiyo, katika kipindi hiki huwa kuna makubaliano, tena na wao wa viwanda wanashiriki, kwamba kuna kitu kinaitwa *gap sugar*, yaani tofauti kati ya uzalishaji na mahitaji, ndiyo yanayofanya tuagize na mwaka huu tumeona tofauti ya mahitaji na uzalishaji ni tani laki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hiki kitu ni *transparent* kabisa, kuna Kamati inaamua halafu inatangaza wanaotaka kuagiza sukari, makampuni 25, yalijitokeza mengi zaidi 25 yakapewa mengine hayakupewa, lakini sukari inayokuja hapa ni kwa ajili ya kupunguza tofauti kati ya mahitaji na uzalishaji. Nadhani ni jambo la kawaida, lakini wanasema kwa nini mnaagiza. Sasa tukiacha kuagiza halafu bei ya sukari ikapanda kwa sababu kuna upungufu wa sukari katika soko, tena Waheshimiwa Wabunge mtarudi mtauliza kwa nini bei ya sukari imepanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wasemaji wa wananchi, lakini wananchi vile vile wanataka sukari, lakini wanaitaka kwa bei ambayo wanaiweza. Kwa hiyo, tutazame pande zote mbili tutetee wanaozalisha na tutetee walaji maana ndiyo kazi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme vile vile kwamba wakati kumekuwa na maneno mengi sana juu ya sukari na kwamba soko linaharibika, Serikali

imechukua hatua kali. Tumezua sana hiyo *transit sugar* na iliyokuwepo ya mwisho tukasema isiende ilikokuwa inakwenda maana ilikuwa imekaa hapo, tukasema iingie kwenye soko halafu tuanze utaratibu wa kuhakikisha kwamba, *transit sugar* yoyote inayoingia bandarini, tunahakikisha kwamba, imevuka mpaka imekwenda. Tumeweka Kamati mahsusi inasimamiwa na *TRA* ambayo kazi yake ni hiyo ya kuhakikisha kwamba, sukari inayokuja hapa nchini inasindikizwa kwenda inakokwenda katika nchi nyingine na isibaki hapa na kuvuruga soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, wakati mwingine watu wanalalamika wakati ukienda kufanya utafiti sana unakuta hamna kitu. Kwa mfano, wakati kulipokuwa na hoja *hot* kabisa kwamba, sukari imejaa kwenye viwanda, niliwaita wenye Viwanda hapo Dar es Salaam nikawambia "Wewe niambie una kiasi gani". Yule wa *TPC* akasema ana 20,000 *tones*. Enhe, nikamuuliza haina soko? Akasema soko lipo, Kaskazini kote yeye ndiye anagawa. Nikamuuliza yule wa Kilombero akaniambia ana tani 17,000 na anatakiwa agawe mpaka Nyanda za Juu Kusini ambako hafiki na kule wanatumia sukari ya Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikamuuliza wa Mtibwa, wewe una kiasi gani? Akasema ana *zero*, yaani siku hiyo hakuwa hata na kilo moja. Sasa nikamuuliza unasema soko lina matatizo, mbona una kilo sifuri? Sasa unauza sifuri? Nikamuuliza yule wa Kagera wewe una kiasi gani, wakati huo alikuwa nayo tani 5000, ndiye analisha Lake *Zone*. Unajua wakati mwingine tuwe wakweli tu, tufanye utafiti, tuwe na uhakika na kile tunachokisema kwa sababu unaweza ukasema sana na mmoja alikwenda mpaka *Clouds FM*, sukari, soko la ndani! Aliona aibu sana nilipomuuliza una kilo ngapi, akasema mimi sina na wakati ule amechukua miwa ya wakulima ameshatengeneza sukari hajawalipa wakulima wala wafanyakazi wake. Tarehe 25 nakwenda Mtibwa kwa ajili ya kuzungumza na wafanyakazi na wakulima wadogo na yeye ili tuelewane kuhakikisha kwamba, wanalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwaambie Watanzania hawa ukweli ili waujue. Unasema tumeagiza Sukari, ndiyo tumeagiza sukari kwa sababu tusipofanya hivyo bei itapanda mpaka huko juu. Wanasiasa huwa wanageuka geuka sana, kesho hawa wanaotwambia tumeagiza sukari watakwenda watasema wananchi mnaona CCM hii imepandisha bei ya sukari, tena mtasema uongo, kwamba imepandisha ili ipate fedha za uchaguzi. Tunajua sana, ni lazima tuwaambie ukweli hapa, tuache kuwadanganya Watanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nizungumzie juu ya hali ya chakula na madeni ya *NFRA*. Hali ya chakula nimeieleza vizuri katika hotuba. Kuna mikoa haikupata mvua, kama Dodoma, Singida, ambayo kwa kawaida

ilikuwa inapata chakula cha kujitosheleza kila mwaka, lakini Mkoa kama Tabora hasa maeneo ya Igunga na Nzega ambayo ni makame, Mkoa wa Shinyanga hasa katika Wilaya ya Kishapu, kule ni pakame sana, Meatu, Mara kule Rorya, Bunda na Butiama, zile Wilaya zote zina matatizo. Hata hivyo, nataka kuwahakikishia kwamba, tunayo akiba ya chakula, wala hatuwalaumu kwa sababu hawakupata mvua za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunazo tani 400,000 za chakula na maombi yote ambayo yatakuja yatahudumiwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu njaa ni maafa, tutawapatia chakula. Nimesema mahali pengine jana kwamba, katika historia yetu miaka 10 iliyopita mwaka ambao tumewahi kutumia tani 150,000 ni mwaka 2005, lakini miaka mingine tumekuwa na upungufu na tulikuwa tunapeleka kidogo sana. Kwa hiyo, kwa sababu katika maghala yetu tuna tani 400,000 tutawahudumia Watanzania hawa mpaka hapo watakapopata mvua waanze kuvuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kwamba, Julai mpaka Septemba mvua zikinyesha, ni hadi Desemba ndiyo wanaweza kuvuna mavuno ya vuli ikiwa mvua zitanyesha wakati huo. Kama hali itakuwa ni mbaya hivi basi itakuwa *disaster*, lakini naamini Mungu hawezi kututupa mkono kiasi hicho. Nafikiri mwaka unaokuja wa kilimo tutapata mvua na tutarudi kule kwenye hali ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari inayohusiana na umwagiliaji nadhani Naibu Waziri ameieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni, maana wanasema kwa nini mmewakopa wakulima. Nasema wala Serikali haina sera ya kuwakopa wakulima, isipokuwa ilikuwa ni matatizo yaliyotokana na neema kwamba, tulizalisha chakula kwa wingi. Mvua zilikuwa nzuri tukapata chakula tani za nafaka milioni tisa, ndiyo mara ya kwanza tumefikia tani milioni tisa za nafaka. Sasa wakati *NFRA* inanunua, wananchi hawa wakiwa na mazao yao waliyaleta kwenye vituo vya *NFRA,* wakati bajeti iliyokuwa imetolewa na Serikali ilikuwa kidogo zaidi haiwezi kununua mahindi yote yale. Kwa hiyo, walipoyaleta, Serikali ya CCM ikasema hamuwezi kuwarudisha wakulima hao na mahindi yao, yatakwenda kuoza, ni bora myachukue tuyahifadhi kwenye ghala ili yapone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kweli kwamba ukiyahifadhi unalipa, ila Serikali inafanya huruma halafu inagharamika kwa huruma yake na tunakubali gharama ya huruma. Kweli tunadaiwa na tulikuwa tunadaiwa shilingi bilioni 89, lakini kuanzia mwisho wa mwezi Januari nadhani ilikuwa Februari mpaka leo pamoja na matatizo ya kupata fedha Hazina lakini tumewalipa wakulima shilingi bilioni 77 katika muda wa miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya! Sasa ninadhani kwa hilo mngetupongeza kwa kuwalipa shilingi bilioni 77 kwa gharama ya huruma ya Serikali na zimebaki shilingi bilioni 12 tutalipa, kwani ukiweza 77 huwezi kushindwa 12. Kwa hiyo, tutalipa mwisho wa mwezi au wiki ya pili ya mwezi ujao. Kabla ya hili Bunge halijatoka hapa tutakuwa tumeshawalipa na nataka wakulima wote ambao wanatudai wajue kwamba, wanaidai Serikali ambayo inajua madeni yake na inawajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine nilikuwa nao pale ofisini juzi, nikawaeleza kwamba, tutawalipa na wameamini kwamba, tutawalipa. Kweli wanaamini kwa sababu tumelipa na tulianza na wakulima wadogo wadogo kabisa, tumemaliza karibu wote. Waliobakia ni makampuni yale yaliyokuwa na fedha nyingi kidogo, ndiyo maana *twelve billions* zitakwenda kumaliza deni lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunawaambia nini wakulima wa Tanzania katika msimu unaokuja. Tutaendelea kununua mazao yao. *NFRA* itaendelea kununua na lile Shirika la Mazao Mchanganyiko litaanza kuingia sokoni. Hata hivyo, tunataka tuwahakikishie kwamba, Serikali itasimamia suala la masoko kwa mazao yao. Wasiwe na wasiwasi wala wasibabaishwe na watu wenye kusema huko maneno mengi bila masoko. Wangoje sisi tutaweka utaratibu ambao utanunua mazao yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, bado dakika moja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tumetoa ushauri wa kutosha na tumepokea ushauri mzuri. Masuala ya Tumbaku nimeeleza na pembejeo nimeeleza. Sijui ni kitu gani ambacho bado, kwani nadhani nimesema yote niliyoweza. Mengine ambayo sikuweza kuyasema ndiyo ambayo nitayaandika na kila Mheshimiwa Mbunge atapata nakala ili ajue Serikali inafanya nini na ina majibu gani kwa hayo yaliyosemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, Katibu!

*(Vifungu vilivyotaja hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 5 - Bodi ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resources Management… … …Sh. 187,780,000/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kibona!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa ajili ya kunipa nafasi hii. Nipo kwenye *subvote 1001*, kuhusiana na mambo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kuhusu neema tuliyoipata mwaka jana ya kuzalisha chakula kwa wingi kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu. Sasa yapo mabonde mengi ya umwagiliaji ambayo mwaka jana tulikuwa hatuna fedha za kutosha...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kibona, huu siyo mshahara wa Waziri.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuliweka vizuri kwamba, nataka nijue…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kibona, sasa subiri ukija mshahara wake utaliweka vizuri.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Haya!

**MWENYEKITI:** Subiri mshahara wake ndiyo utapata nafasi nzuri ya kuchangia na kupata majibu sahihi.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nashukuru.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts… … …* Sh. 11, 500,000/=
Kif. 1003 - *Planning Monitoring and Evaluation… … … … … … …*Sh. 34, 850,000/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit … … … … … … … … …*Sh. 3, 500,000/=

Kif. 1005 - *Procurement Management Unit… … … … … … … … …* Sh. 4,570, 000/=
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit… … … … …* Sh. 13,050,000/=
Kif. 1007 - *Information Communication Technology… … … … … … …* Sh. 6,400,000/=
Kif. 1008 - *Legal Service Unit… … … … …* Sh. 11,000,000/=
Kif. 1009 - *Environmental and Social Management… … … … … …* Sh. 5,100, 000/=
Kif. 2001 - *Irrigation Planning Design and Private… … … … … … … …* Sh. 5,871,000/=
Kif. 2002 - *Irrigation Infrastructure Development… … … … … …* Sh. 34,970,000/=
Kif. 2003 - *Irrigation Research and Technology Promo… … … … …*Sh. 38,900,000/=

*(Vifungu vilivyotaja hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2004 - *Irrigation Operations and Support Services… … … … ……*Sh. 15, 495, 000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Item 221000, Travel in Country*. Nauliza swali moja kwa Mheshimiwa Waziri, kiasi cha fedha ambacho nimeona kimetengwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kinapungua kwa sh. 8,200,000/= kutoka sh. 14,100,000/= na tunafahamu kwamba suala la kuimarisha kilimo kupitia miradi ya umwagiliaji ni la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ambayo tumeshuhudia katika baadhi ya maeneo hapa nchini imejengwa chini ya kiwango na pia kwa kusuasua. Kuna sababu gani zimeifanya Wizara ipunguze kiwango cha fedha ili watu hawa wasiweze kusafiri kadiri inavyowezekana kwa lengo la kufanya *monitoring* na *evaluation* kwenye miradi ya umwagiliaji. Ni kwa nini fedha zimepungua wakati ni eneo ambalo ni muhimu sana?

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeeleweka. Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Machali, kifungu hiki ni kwa ajili ya kuwawezesha Wataalam wetu kusafiri ndani ya nchi ili waweze kufanya kazi zao, lakini kimepungua kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ya Serikali.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2005 - *Irrigation Compliance and Quality Insurance… … … … …* Sh. 10, 700,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resources Management Division… … …* Sh. 3,106,417,400/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts… … …* Sh. 111,588,000/=
Kif. 1003 - *Planning Monitoring and Evaluation… … … … … … …*Sh. 210,470,000/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit… … … … … … … … …*Sh. 26, 500,000/=
Kif. 1005 - *Legal Service Unit… … … … …* Sh. 31,720, 000/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit… … … … … … … … …* Sh. 75,983,000/=
Kif. 1007 - *Information Communication Technology… … … … … … …* Sh. 50,480,000/=
Kif. 1008 - *Internal Audit Unit… … … … …*Sh. 39, 640,000/=
Kif. 1009 - *Research and Training Unit… …* Sh. 31,820, 000/=
Kif. 4001 - *Cooperative Promotion & Coordination… … … … … …* Sh. 357,100,000/=
Kif. 4002 - *Cooperative Micro Finance Section… … … … … … … …*Sh. 318,280,000/=
Kif. 4003 - *Regional Cooperative Offices… … … … … … … …* Sh. 284,273,000/=
Kif. 4004 - *Cooperative Marketing & Investment Section… … … …* Sh 125,113,000/=
Kif. 4005 - *Registration Service Section… …* Sh. 293,180, 000/=

*(Vifungu vilivyotaja hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4006 - *Inspection and Supervision Services Section... ... ... ... ... ... ... ...* Sh. 2,565,425,600/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Item 410600, Acquisition of Office and General Equipment,* nina swali moja hapo

wanisaidie. Kuna uongezekaji wa fedha wa kiwango kikubwa kutoka sh. 3,500,000/= kwenda sh. 26,000,000 kwenye *item* hiyo. Naomba ufafanuzi ni kwa nini kuna nyongeza kubwa namna hiyo? Tatizo ni nini, ina maana miaka yote waliacha mpaka vitu vimeharibika na sasa hivi ndiyo wanakuja kununua kwa mkupuo? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, subiri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ofisi kama vile tarikishi, kompyuta mpakato na kadhalika, ambapo pia kifungu kimeongezeka kutokana na ongezeko la Watumishi. Pia tujue kwamba, kimsingi hii ni Tume mpya hivyo ni lazima tuiwezeshe kuwa na vifaa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU – 43 WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resources Management*… … Sh. 5,146, 992,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kwa utaratibu wa Kanuni na tulivyokubaliana, tuna majina kutoka kwenye Vyama na kutokana na muda nitapanga kutokana na uwiano wa majina yale niliyoletewa na Vyama. Tutaanza na Mheshimiwa Opulukwa!

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka niongelee suala la pamba. Zao la Pamba inavyoonekana limeshindwa kupata ufumbuzi wa matatizo yanayoikabili sekta hii ndogo kwa muda wa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yanayoleta matatizo kwenye zao la pamba ni pamoja na kilimo cha mkataba na katika kilimo hiki cha mkataba unakuta mkulima kwa sababu naamini kuna mikataba ya aina mbili, kuna mkataba wa pembejeo kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyosema, lakini pia ni lazima tutambue kuwa kuna mkataba ambao unahusisha gharama za uzalishaji ikiwa ni pamoja na nguvu kazi ya mkulima anayotumia kuzalisha pamba yenyewe anayolima .

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mikataba hii unakuta pamoja na kwamba ni mkataba wa pembejeo, lakini mkulima analazimishwa kuuza pamba yake kwa mtu au kwa mnunuzi ambaye amemuuzia pembejeo hizi na hii imepelekea, kwa mfano, mwaka jana baada ya kuwa bei ya pamba

imeshuka na ikawa inauzwa kwa sh. 750/= kwa kilo, alitokea mnunuzi kutoka China ambaye alikuja na bei ya sh. 1,200/= kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu ya kilimo cha mkataba kwamba wakulima hawa wanalazimika kuuza pamba yao kwa mtu aliyewauzia pembejeo, kwa hiyo, wakawa wamelazimishwa kwamba, haiwezekani wakauza pamba yao kwa huyu mnunuzi kutoka China, lazima wauze kwa wafanyabiashara hawa ambao wanafanya nao biashara ya pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, yuko tayari kwa mikataba hii inayoanza kuanzia sasa katika msimu wa uuzaji wa mwaka huu ambao tunakwenda kuuza pamba, yuko tayari sasa kuwalazimisha au kuwashinikiza wafanyabiashara wa pamba, ili angalau mikataba hii wanayoingia iweze kuendana na bei ya pamba ambayo mkulima wa pamba anaweza kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata majibu ya kutosha nakusudia kutoa shilingi hadi hapo Mheshimiwa Waziri atakanipa majibu ya kutosha.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja anayoisema ndugu yangu Opulukwa ni ya mkataba, mikataba ambayo iko katika zao la pamba ni ya makampuni yaani *ginneries* ndiyo wanaotoa pembejeo kwa mkulima, halafu pembejeo zile zinamwezesha yule mkulima kwa makubaliano lakini, kwa hiyo neno lazima hapa ni lazima aliondoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba ule hauwezi kuwa ni wa lazima, ndiyo maana kuna wakulima ambao wako ndani ya mkataba na wengine ambao hawako kwenye mkataba. Kama ingekuwa ni lazima hiyo ingefanywa na nani maana Serikali peke yake ndiyo inaweza ikafanya lazima, kwa hiyo, wakulima wote wangekuwa kwenye mkataba. Wakulima waliokubali mkataba ule kwa vikundi wakipewa pembejeo wanatakiwa kurejesha gharama za pembejeo na namna peke yake ni ya kwenda kumuuzia yule walioingia naye mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwamba kuna gharama ya kuzalisha, gharama ya kuzalisha haiwezi kuingizwa kwenye mkataba kwa sababu bei hii haipangwi na yule anayenunua na wala haipangwi na Serikali, tunatazama soko na sisi Serikali huwa tunazungumza nao ili kusema bei ya chini iwe ni shilingi ngapi baada ya kujua bei ya soko. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali halisi.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa, nilichokiongelea ni kwamba mkataba ambao mkulima anaingia na *ginners.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Opulukwa unatoa shilingi au hutoi?

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa.

Mkataba huu ambao *Ginneries* wanaingia na mkulima kama nilivyosema mwanzo ni mkataba ambao hauelezei ni kiasi gani cha fedha ambayo mkulima atapata atakapouza pamba yake kwa huyu *ginners*. Nataka labda na wenzangu waweze kuchangia ili kunisadia kwa sababu tayari nimeshatoa shilingi.

Kama Serikali itakubali sasa kukaa na hao wafanyabiashara ambao *ginner* hao wanapoingia mkataba na wakulima basi ile bei iweze kujulikana kwamba kwa mwaka x wakati wanakwenda kuuza pamba yao watapewa shilingi ngapi, lakini iwe kwenye mkataba badala ya kutumika ule mkataba wa pembejeo kuwa ndiyo mkataba wa kuuzia pamba.

**MWENYEKITI:** Mheshimikwa Opulukwa, lakini huu ni Mkataba kati ya mkulima na mtu wa *ginnery,* Serikali ni *custodian* wa vitu vyote hivi, Serikali haiingilii mikataba hii, ni kati ya mkulima na yule anayempa pembejeo hizo. Nafikiri, sasa ni nafasi yako wewe na wanasiasa kusaidia wakulima hawa wasije wakadhulumiwa haki zao

Mheshimiwa Shibuda!

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo cha mkataba kwa wakulima wa pamba linaeleweka zaidi kwa sisi wakulima wa pamba kuliko linavyotafsirika na kutambulika nje ya mkulima wa pamba. Kwa hiyo, ningeomba hili lieleweke na uwe na subira anapozungumza Mheshimiwa Opulukwa kuhusu utata wa kilimo cha pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha mkataba Mheshimiwa Waziri anatambua vizuri sana kasoro zinazozungumzwa kwa sababu Bodi ya Pamba ambayo ndiyo msimamizi wa Sheria za masuala ya kilimo cha Mkataba na ndiyo Mhamasishaji na ndiyo mhimili mkubwa na Wakuu wa Mikoa wamekuwa wakilazimisha, nashukuru yeye baada ya kuja kuna ulegevu Fulani, lakini kasoro ya kilimo cha mkataba Mheshimiwa Waziri unaitambua.

(a) Kilimo cha mkataba ambacho kinatekelezeka hivi sasa kinatumia pesa za Mfuko wa Wakfu ambazo anakatwa mkulima. Kwa hiyo, mkulima *indirectly* pesa alizokatwa yeye zinakwenda kutumika tena kununulia pembejeo anaambiwa jikopeshe kutokana na peza zako.

(b) Sasa kasoro hiyo inatambulisha kwamba kilimo cha mkataba kihuruwishwe, kiwe huru dhidi ya kutumia Mfuko wa Wakfu. Hivyo, Serikali inapaswa sasa ituambie itatoa mwongozo wa kusema kwamba, pesa za Mfuko

wa Wakfu anazokatwa mkulima ambazo zamani zilikuwa kwenye kitabu cha *pass book* ambacho leo pesa hizo hazitambuliki ziko kwenye…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shibuda umeeleweka, Mheshimiwa Waziri *plead* yao umeiona Mheshimiwa Waziri?

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba uwe na wakati nakamilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shibuda tuna Kanuni hapa za dakika tatu, zima kipaza sauti chako.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimemwelewa Shibuda zaidi kuliko mtoa hoja, kwa sababu suala hili kama ni hili analolisema Shibuda, tumelifanyia uamuzi Mwanza, tumesema hivi kama kuna *ginner* anataka kufanya mkataba na wakulima wa kuwapa pembejeo awape kwa hela zake, asitumie hela za Mfuko wa Wakfu, hilo tumekubaliana na najua kuna makampuni matano yanajiita *UMWAPA,* yanafanya kazi katika Wilaya 27 za pamba na yamesema na tumehakikisha kwamba yanatumia pesa zao, siyo fedha inayotokana na mchango wa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo ndiyo hoja, nilikwenda Mwanza, nilizungumza na Wadau na tulifanyia uamuzi palepale. Nikawaambia Bodi ya Pamba, ikae ituletee utaratibu gani fedha za Wakfu zitatumika, kama tutarudi kwenye *passbook* tutarudi kwenye *passbook,* hili tumeshalimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii anayoisema Mheshimiwa Opulukwa, napata tabu kumwelewa, kwa sababu Mkataba huu ni wa hiari, halafu Mkataba huu haufanywi wakati wa msimu wa kununua, unafanywa kabla ya msimu wakati bei ya soko haijajulikana. Kwa hiyo, ni vigumu sana kuweza kufanya hilo likawa kwenye mkataba.

**MHE. MIESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeyasikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri, basi ningependa kumrudishia shilingi yake na nipende kumwamini au kuiamini Wizara kwamba itaweza kufanya yale ambayo wakulima wanatarajia kutoka katika Serikali hii pamoja na Wizara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud!

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni miaka kadhaa sasa Serikali imesema ina mkakati wa kuthaminisha zao la korosho na inaachana na aibu ya kuuza korosho ghafi nchini India na hata leo

Mheshimiwa Waziri hapa wakati anafanya majumuisho alisema, ili wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na walio Pwani ambao ni wakulima wa korosho waweze kupata kipato cha ziada na kuondokana na umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 hata Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Kigoda naye pia alisema hivyo hivyo kwamba tatizo kubwa la kuthaminisha zao la korosho na umasikini uliopo katika Mikoa ya Lindi na Mtwara na Pwani ni suala zima la viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo haviendelezwi hadi leo na akasema atawaita ili kujua tatizo liko wapi, waweze kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itueleze na kama sikupata majibu ya kuridhisha nitatoa shilingi. Naomba Serikali itueleze hasa, viwanda vyote vya Mtwara, kule Mtama, Lindi Mjini, Nachingwea, vilivyobinafsishwa vilivyochukuliwa na Vigogo wa Serikali na kwa sababu Serikali ilikwishaahidi itawaita ili ijue hatima yake. Naomba maelezo ya kina Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuthaminisha zao la korosho kwa wakulima?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshalijibu hili swali wakati wa majibu ya hoja kwamba tunataka kuhakikisha kwamba korosho zinabanguliwa. Pia kuna hoja ya viwanda nimeijibu kwamba, kweli tuliuza viwanda lakini siyo vya korosho peke yake vipo na vingine ambavyo vinataka kuanza sasa kuchukua hatua ili hao waliovinunua wavitumie, vifanye kazi au kama hawawezi, basi wapishe tuvikabidhi kwa watu wengine. Nadhani hilo ndiyo jibu ambalo naweza kui-*commit* Serikali, zaidi ya hapo sijui Mheshimiwa Mbunge angependa niseme nini.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa shilingi, kwa sababu Mheshimiwa Waziri anasema kwamba waliochukua viwanda vile na Serikali ilikwishaahidi kwamba mtawaita ni miaka mitatu sasa, ina maana kwamba kwa sababu waliochukua viwanda vile ni Vigogo wa Serikali, hoja ni hiyo tu hamuwezi kuwaita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama ni hivyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge waunge mkono tuweze kujua nini hatima yake. Maana maelezo ni haya haya na ahadi zimekuwa nyingi viwanda hivi vimechukuliwa kwa muda mrefu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud umeshatoa shilingi kaa chini watu wachangie, Mheshimiwa Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mheshimiwa Masoud amesema kwamba vigogo wa Serikali wamechukua viwanda au waliuziwa viwanda. Kusema uongo Bungeni ni kosa, ataje hata

kiongozi mmoja tu wa Serikali ambaye amemilikishwa Kiwanda cha Korosho mmoja tu siyo wawili atutajie hapa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niridhike na michango yote ya Mheshimiwa Masoud, lakini pia Mheshimiwa Waziri alivyofanya *clarification* hapo, nadhani kama Taifa itabidi tujieleze zaidi, natoa ushauri kwamba sasa hivi tuangalie ni jinsi gani tutawawezesha watu wa kawaida hata kuanzisha viwanda vidogo ili mradi kuhakikisha usindikaji wa korosho unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika eneo hilo katika kuunga kwangu hoja ni kwamba, Tanzania *Investment Bank* iangalie ni kwa jinsi gani itawezesha vikundi vidogo vidogo kupeleka mafungu katika vikundi vidogo vidogo katika Ukanda huu wa Pwani, licha ya kuwa na viwanda vikubwa zaidi maana yake hatuwezi kusema kwamba Serikali itajenga viwanda hivi leo, maana yake sasa hivi tunasema kuwa tuna *private sector* ndiyo ifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi ambao wameji-o*rganise* vizuri, sasa ni jinsi gani tutafanya na *Tanzania Investment Bank?* Tuwawezeshe wananchi hawa katika vikundi waweze kuweka viwanda vidogo vidogo vya kusindika korosho, jambo hili tutasababisha korosho za Pwani zitapata thamani zaidi na tutaondoa suala zima la kupeleka korosho ghafi nje. Inawezekana tukitegemea kupata *structure* kubwa ya jengo kubwa la kiwanda inaweza kuwa ni changamoto kubwa. Mchango wangu ni huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri *concern* ya Wabunge ni kwamba, Serikali ina wajibu ya kuwawezesha wananchi kuanzisha viwanda, hizi korosho zikienda India zinabanguliwa kwenye nyumba za watu kwa mitambo midogo tu. Sasa hoja tunasema ili ku-*add value* kwenye *product* hii ya korosho badala ya kuhangaika na masoko, kuhangaika kuwa wanalima na hawapati bei nzuri, Serikali itakuwa na mpango gani sasa, wanataka *commitment* na *comfort,* je, sasa Serikali, sisi tunaona kilio hiki cha wananchi tunawaahidi na tunaji-*commit,* tutaanza kuwatafutia viwanda vidogo vidogo tutaweka kwa pamoja ili muweze kupata bei kubwa kutokana na kubangua korosho *within the country,* Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kutusaidia kutuelezea jambo hili. Nimeshasema na nataka nirudie ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba badala ya kuendelea kuuza korosho ghafi, tuanze kuuza korosho zilizobanguliwa, hoja ya ndugu yangu pale anazungumza vigogo, nasema kigogo ndiyo kitu gani kwa sababu hata mimi

nikimaliza Uwaziri naweza kufanya biashara ya korosho, sasa huwezi kusema huo ni mwiko, unaweza kunilaumu kama nimechukua kiwanda na sifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba ni kigogo au kitu gani, hiyo siyo hoja kubwa, hoja ni hii aliyoitoa Jafo kwamba tusaidie wakulima wadogo wadogo katika kuanzisha viwanda vidogo vidogo na naiagiza Bodi ya Korosho kuanza kutazama ni wapi ambapo tunaweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud!

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza majibu kwa kina sana, lakini pia nataka kusema kwamba hoja ya kusema kwamba ni vigogo isipuuzwe na amesisitiza pale katika malumbano...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Ni lini viwanda hivyo…

**MWENYEKITI:** Hiyo ndiyo hoja, hili jambo la vigogo lina toka wapi? Waziri ameshaji-*commit* anaiagiza Bodi, Bodi iandae utaratibu wa sasa kuanzisha viwanda vidogo vidogo kuhamasisha na kuwasaidia wakulima wadogo ndiyo *commitment* ya Serikali, hili la vigogo achana nalo.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Nakushukuru umenielewa. Najua umenielewa maana ningetaja sasa hivi…

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud usiende huko, wewe malizia tu, mrudishie shilingi yake tuendelee na biashara.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia. Naomba *commitment* ya Serikali kama Bodi amesha…

**MWENYEKITI:** Serikali imesha–*commit,* ameshasema hapa na kwenye *Hansard* imeingia, ameiagiza Bodi ya Korosho iandae utaratibu sasa wa kutazama ni namna gani, viwanda vidogo vidogo vinavyotumika India sasa vitumike Tanzania amesema na iko kwenye *Hansard*.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema mengi na umechombeza sana, narudisha shilingi lakini naomba...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mshama!

**MHE. ASUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi, lakini nianze tu kwa kusikitishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa suala la Viwanda vya Sukari, niseme hivi pointi mbili ambazo nitazisimamia ambazo ameziongea, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba walipokwenda kwenye viwanda walikuta hakuna sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumweleza Mheshimiwa Waziri, nilikwenda kwenye viwanda nilikuta sukari na tulipokuta sukari mpaka kufikia wewe Waziri kuchukua nafasi ya Waziri aliyekuwepo ilikuwa ni zaidi ya miezi minane kilio kinasika na walishindwa kuchukua miwa ya wananchi tena kuweza kusindika kwa sababu Sera ilikuwa haijaeleweka. Mheshimiwa Waziri naomba kuna hasara imepatikana na matokeo yake wananchi wa Misenyi na kwingine hawajalipwa, siyo kwamba viwanda havitaki kuwalipa lakini walipata hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kujua ni lini Serikali itatoa msimamo mmoja wa kuweza kusaidia viwanda vyetu vilivyoko ndani, viweze kufanya kazi na wananchi wetu, matokeo yake huu mwezi wa Nane wanakwenda kuondoa watu 1,500 kwenye Kiwanda cha Kagera *Sugar*. Tumefunga viwanda sasa hivi siyo kwa sababu eti hawataki kuzalisha, ni mvua. Kwa hiyo, kuna kipindi wanazalisha sana, wanaweka *stock* halafu wanafunga. Kwa hiyo, hamjawatendea haki watu wa viwanda vya sukari kwa namna ambavyo mnaendesha Sera ya Sukari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ni lini tutaweka Sera nzuri ilinde viwanda na iwepo sukari kwa kuweka viwanda zaidi. Walitaka kuweka kiwanda kingine hapa nchini wamekipeleka Ghana kwa sababu ya *Bureaucracy* zilizoko hapa nchini na wana uwezo wa kuzalisha kama tutawawekea Sera zinazolinda viwanda vya ndani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilifikiri utasema ni lini mtakwenda wote na Mheshimiwa Waziri mtakwenda wote mkakague huko kwenye nini. Kumbe unataka Sera, haya Mheshimiwa Waziri ni lini mnaweka Sera?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ipo, kilichokuwa kinalalamikiwa na ambacho Mheshimiwa Mshama anazungumzia ilikuwa ni hiyo historia ya kusema kulikuwa na *transit sugar* inaingia nchini badala ya kwenda inakokwenda inaingia sokoni, hiyo ndiyo Serikali tumechukua hatua na kwa kweli nimebadili na nime-*sign* Kanuni mpya ambazo zinasimamia uagizaji wa sukari. Kwa hiyo, kwa sasa hakuna sukari ambayo itaagizwa kwa jina la *transit* halafu ikauzwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka Kamati mahususi ya kusimamia kuwa ile sukari itakuwa inakwenda. Nilichokuwa nasema ni kwamba, wakati nilipowaita wazalishaji walikuwa hawana sukari ingawa manung'uniko yalikuwa yanaendelea hata baada ya Serikali kuchukua hatua hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninaloweza kusema ni kwamba kule Kagera pamoja na Mtibwa ambapo mwekezaji wake ni mmoja, mpaka hapa mwishoni walikuwa hawana sukari, tulipotoa vibali vya kuagiza sukari tumewapa waagize wao Mtibwa na Kagera tani 32,000. Kwa hiyo, kama kuna hasara yoyo te ambayo walipata na kama kuna matatizo ya kulipa wakulima, wauze hiyo sukari wawalipe wakulima.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso! Mheshimiwa Kakoso, hayupo, Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jambo langu lipo katika suala zima la kibajeti. Ukisoma kitabu cha Waziri inazungumza kwamba *flow* ya pesa ina changamoto kubwa, lakini ukija kwenye *analysis* ya Kamati inakuonesha kwamba matumizi ya kawaida yalifika asilimia 24 mpaka tarehe 22 Aprili, lakini hali kadhalika miradi ya maendeleo asilimia 46.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia suala zima la kilimo tunazungumzia uchumi wa nchi hii. Tuna changamoto na tatizo kubwa tulilokuwa nalo la kushuka kwa thamani ya shilingi. Inashuka kwa sababu hatu-*export* ukilinganisha na jinsi ambavyo tunavyo- *import*. Kwa hiyo, ina maana kwamba kama tusipokazania katika suala la kilimo na kama Wizara ya Kilimo haitopewa nguvu ya kutosha maana yake tunakuja kuondoa kabisa uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie kwamba, katika Wizara ya Kilimo, leo hii *flow* ya pesa ikienda chini, maana yake Idara ya *Research* haifanyi kazi, *irrigation* haifanyi kazi, *training institution* zote hazifanyi kazi. Ina maana mfumo mzima ume-*stuck*. Uki-*stuck* mfumo mzima maana yake umeharibu uchumi mzima wa nchi. Kwa hiyo, nataka nipate *commitment* ya Serikali na nisipopata maelezo ya kutosha katika Serikali kwa kweli nitatoa shilingi katika hili, kwa sababu hatuwezi kupitisha bajeti ambayo inakuwa haiwezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nipate *commitment* ya Serikali, ni jinsi gani itafanya katika kipindi hiki kilichokuwepo na namwona Naibu Waziri wa Fedha yupo hapa, kwamba jinsi gani Serikali itahakikisha kwamba Wizara ya Kilimo inapata fedha kama tulivyokusudia kwa ajili ya kuokoa uchumi wa nchi hii. Hatuwezi kupitisha bajeti hapa ambayo mwisho wa siku wananchi wote ambao ni wakulima asilimia themanini, Taifa lina-*stuck* hatuwezi kupitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata maelezo ya kutosha na *commitment* ya Serikali nakusudia kutoa shilingi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge anasema, wekeni pesa, mzalishe pesa! *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane moja kwa moja na kumshukuru Mheshimiwa Jafo aliyoyasema yote yapo sawa, labda lile la kushuka kwa thamani ya shilingi kidogo lina mgogoro, lakini kwa hii *element* nyingine nadhani Serikali inaji-*commit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema mwaka huu katika masuala ya kifedha kidogo ulikuwa ni mwaka mgumu kulingana na makusanyo na kadhalika. Moja ya mambo ambayo tumefanya kwa kushirikiana na kilimo ni yale aliyokuwa anasema Waziri wakati wa kuchangia, kujaribu kuweka bajeti ya kilimo ambayo ni halisia, lakini lazima tutambue kwenye upande mwingine kilimo kinakabiliwa na changamoto kubwa ya kununua mazao ya wananchi ambayo sisi hatuna *function* ya soko, tuna *function* ya kuhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme kwamba Serikali imeji-*commit,* Wizara ya Fedha, Hazina imeji-*commit* hasa katika miradi ya maendeleo; ya umwagiliaji, *research* na hasa kwenye kutoa fedha za ugani *extension,* Serikali itatenga haya kama ni maeneo mahsusi na maeneo ya pembejeo ili wakulima waweze kuzalisha zaidi na pia kwenye maeneo ya masoko.

**MWENYEKITI:** Unasikia Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, nchi hii inaweza kulisha Afrika nzima kama tutakuwa na *commitment*, tutakuwa *serious* katika kuwekeza kwenye kilimo. Bajeti ya Kilimo mwaka jana *disbursement* ilikuwa *percent* ngapi?

Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumza hapa maana yake tunazungumza uchumi wa nchi. Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza hapa, lakini naomba Serikali katika *commitment* iliyosema kwa sababu *budget process* tunaanza na Wizara na mwishowe tunamalizia na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni imani yangu kwamba *commitment* hii iliyofanywa na Serikali, kwa sababu tunachozungumza hapa ni uchumi wa nchi yetu. Nina imani kwamba tutakapofika katika eneo hilo, tutaweza kupata taarifa rasmi kutoka Serikalini kwamba *commitment* hiyo imetekelezeka vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nairudisha shilingi ya Mheshimiwa Waziri pale, tukijua kwamba kuna siku ya mwisho tutakuja kukamatana na Wizara ya Fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Raya!

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ningependa kujua Serikali ina mkakati gani ambao mmeuweka au mtauweka katika kuhakikisha utoaji wa mbolea zinafika kwa wakati kwa wakulima. Kwa sababu tunaona kwamba pamoja na kuwa kuna utaratibu ambao umewekwa wa *SACCOS,* yaani mbolea zinapitia kwenye *SACCOS* wakulima wazipate, lakini bado mpango huu unasuasua na bado mbolea inachelewa kufika kwa wakati kwa wakulima. Sasa ningependa kujua, Serikali ina mkakati gani katika kuboresha hili na kufikisha mbolea kwa wakati kwa wakulima? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshafanya mashauriano na makampuni yanayoagiza na yanayouza mbolea hapa nchini na tumefanya makubaliano kwamba mbolea ile ipelekwe katika maeneo ya wakulima ifikapo Julai, kuhakikisha kwamba ipo kule kule na siyo tena ya kufuata Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeanzisha mfumo wa vocha ambao utawafikishia mbolea wakulima familia milioni moja kwa mwaka unaokuja wa kilimo kuhakikisha kwamba zinafika na wanalipa asilimia hamsini ya bei na asilimia hamsini inalipwa na Serikali! Hizo ndizo hatua tulizokwishazichukua mpaka sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu nilipozungumza hapa Bungeni, nilizungumzia baadhi ya matatizo machache tu ya zao la tumbaku hapa nchini. Nikazungumzia mawili tu! Yapo lukuki, lakini kwa sababu ya muda nikazungumzia mawili tu. Suala la bei, kuendelea kuwa ndogo na suala la pili ni suala la matumizi ya dola kwenye ununuzi wa tumbaku na kusambaziwa mbolea kwa wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amejaribu kueleza kwamba bei inatokana na kikao cha wadau na pia alijaribu kusema kwamba, suala la matumizi ya dola inawezekana wakulima wananufaika nalo.

Nitangulie kusema kwamba, naomba majibu ya kueleweka na ya kuwatia moyo wakulima wa tumbaku, vinginevyo nitatoa shilingi kwenye suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka yote wakulima wananunua tumbaku kwa dola na hata ile dola halisi ya siku hiyo hawaambiwi. Mheshimiwa Waziri atueleze mkulima wa kule Kaliua kijijini anajua dola leo ni shilingi ngapi, hivi tunavyozungumza? Leo dola imepanda kutoka 1800 ama 1900 mpaka 2100. mkulima kule anajua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ulaghai mkubwa wa hali ya juu wanavyokwenda kule wenye makampuni hawasemi hata bei ya dola halali. Ndiyo maana tunasema wanazidi kuonewa miaka yote wanakwenda kudanganywa, lakini suala la bei, hiv vikao vya wadau wanasema wanapanga, Bodi ya Tumbaku, baadhi ya wakulima na sehemu ya Serikali. Wanapanga wakijua kwamba bei inawaumiza wakulima. Ndiyo maana nikasema Serikali iingilie kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hapa ninavyozungumza, miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2011 mpaka 2015, dola bei ilikuwa kilo moja Dola 2.13. Kikao kilichokaa sasa hivi kwa kupitisha bei ya mwaka huu, wamesema ni dola 2.06, imeshuka! Kwa 0.19. hatuwezi kuendelea kuishi katika maisha haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu kwamba nini suala bei, Serikali inaingiliaje kikao cha juzi cha wadau kilikwenda kuwakandamiza wakulima wa tumbaku kwa sababu badala ya kupandisha bei wamekwenda kushusha bei.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya! Umeshajieleza na umeshafahamika. Sasa muda unaotumia na naingia kwenye *guillotine* sasa hivi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitaridhika nitashika shilingi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bei za mazao ya kilimo, siyo kwa tumbaku lakini kwa mazao mengi, huwa zinalalamikiwa kwa sababu Serikali siyo inayopanga bei, isipokuwa Serikali inawaunganisha wale wadau baada ya kujua kiwango cha bei ya soko la dunia. Ndiyo maana kwenye tumbaku kuna kitu kinaitwa *Tobacco Council of Tanzania* ambayo ndiyo hii inawaunganisha wakulima na wanunuzi na kufanya makubaliano.

Serikali hatukai kimya tunapoona makubaliano yale hayana maslahi kwa mkulima, kwa sababu kazi yetu hiyo. Kwa hiyo, ilipomalizika ndiyo ikatoka bei ya dola 2.6.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaingia kwenye *guillotine*!

**MHE. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa kwenye orodha ya Chama changu cha CCM lakini naona…

**MWENYEKITI:** Tunaingia kwenye *guillotine* Mheshimiwa Salum. Twende!

**MHE. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jana niliomba sijapewa na leo sijapewa, nadhani sijatendewa haki na si jambo la busara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum mimi napewa jina na Chama chako. Jina lako halipo humu.

**MHE. SALUM:** Nilikuwa wa kwanza kuorodheshwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum onana na viongozi wa Chama chako.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts… … …* Sh. 1,784,414,100/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning… … …* Sh. 1,863,930,520/=
Kif. 1004 - *Agriculture Training Institute… … … … … … …* Sh. 9,406,299,410/=
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit… … … … …*Sh. 379,449,400/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit… … … … … … … …* Sh. 890,553,900/=
Kif. 1007 - *Government Communication Unit… … … … … … … …* Sh. 278,190,100/=
Kif. 1008 - *Legal Unit… … … … … … …* Sh. 415,097,530/=
Kif. 1009 - *Management Information Systems Unit… … … … … …* Sh. 459,002,400/=
Kif. 1010 - *Environmental Management Unit… … … … … … … … ...*Sh. 332,077,600/=
Kif. 2001 - *Crop Development… … …* Sh. 145,776,792,230/=
Kif. 2002 *Agriculture Mechanization… … …*Sh. 936,149,100/=
Kif. 2003 - *Agriculture Land Use and Management… … … … … …*Sh. 913,190,100/=
Kif. 2004 - *Plant Breeders Unit… … … …* Sh. 236,378,800/=

Kif. 2005 - *Irrigation and Technical Services… … … … … … …* Sh. 4,804,551,000/=
Kif. 3001 - *Research Development… …* Sh. 21,334,315,600/=
Kif. 5001 - *National Food Security… …* ...Sh. 54,794,166,210/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 5 - Bodi ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kif. 1002 - *Finance and Accounts… … … … … … ...* Sh. 0
Kif. 1003 - *Planning Monitoring and Evaluation… … … … … …* Sh. 1,235,954,000/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit… … … … … … … … … … … …* Sh. 0
Kif. 1007 - *Information Communication Technology… … … … … … ..*Sh. 130,000,000/=
Kif. 1008 - *Legal Services Unit… … … … … … … …*Sh. 0
Kif. 1009 - *Environmental and Social Management… … … … … …*Sh. 200,000,000/=
Kif. 2001 - *Irrigation Planning Design and Private … … … … … …*Sh. 20,468,989,000/=
Kif. 2002 - *Irrigation Infrastructure Development … … … … …* Sh. 30,868,143,000/=
Kif. 2003 - *Irrigation Research and Technology Promo… … … … …*Sh. 200,000,000/=
Kif. 2004 - *Irrigation and Support Services… … … … … … …* Sh. 1,291,488,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

*Kif. 1003 - Policy and Planning … … …* Sh. 9,512,622,000/=
*Kif. 1004 - Agriculture Training Institute… … … … … … …* Sh. 1,069,691,500/=
*Kif. 1009 - Management Information Systems Unit… … … … … …* Sh. 100,000,000/=
*Kif. 1010 - Environmental Management Unit… … … … … … … … … … … …* Sh. 0
*Kif. 2001 - Crop Development… … … …* Sh. 4,042,066,000/=

*Kif. 2002 - Agricultural Mechanization… ..Sh. 2,155,827,800/=*
*Kif. 2003 - Agriculture Land Use Planning*
*and Management… … … … Sh. 7,941,000,000/=*
*Kif. 2005 - Irrigation and Technical*
*Services… … … … … … … … … … … Sh. 0*
*Kif. 3001 - Research and Development… Sh. 3,442,900,000/=*
*Kif. 5001 - National Food Security… … …Sh. 12,728,965,700/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Mtoa hoja, taarifa!

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imepitia Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika - Fungu 43, Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24 na Tume ya Umwagiliaji- Fungu 5, kifungu kwa kifungu bila ya mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2015/2016 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakupongeza, lakini *concern* hizi, Mheshimiwa Waziri msianze kupeana mikono, *concern* hizi za Wabunge ni *genuine*. Ni kanuni tu hizi zinatupeleka kama tunavyokwenda, lakini suala la korosho, suala la Serikali kusimamia masoko si kwenye korosho tu, Serikali lazima iwe na kitengo maalum cha *research* kutafuta masoko ya wakulima ili hawa wakulima sasa waone namna gani na wao wanathaminiwa na Wizara pamoja na Serikali yao. Wizara zote zinazohusika, iwe Mawaziri mkisafiri kwenda nje, mwende kutafuta masoko na si kwenda tu kufanya shughuli zingine. Nawapongeza bajeti yenu imepita, nawapongeza watendaji wenu. Mna wataalam wazuri sana, watumieni wataalam, wawezesheni waweze kuwashauri.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.51 mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 25 Mei, 2015, Saa Tatu Asubuhi)*